# MAFUNDISHO NA MAZOEZI YA MAISHA MATAKATIFU

Dr. Randall McElwain

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki © 2019 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Pili la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa. Isipokuwa kwa kurasa za majaribio, hakuna sehemu yeyote katika kitabu hiki itakayotengenezwa au kutawanywa kwa njia yeyote ile ya – elektroniki, mbinu za utunzi mfupi, kunakili, kurekodi au vinginevyo- bila kibali kutoka Shepherds Global Classroom (SGC). Kila linaponunuliwa toleo la mtalaa wetu wa SGC Kiswahili au Kiingereza kunatusaidia kufanya tafsiri kwa lugha nyingi ili kuvigawa kwa Viongozi wa Kikristo duniani kote. Kwa kuwasiliana na SGC au kuchangia katika maono haya ya kuvutia sana, ingia kwenye tovuti yetu: www.shepherdsglobal.org.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB)."

Usanifu wa jalada: Shane Muir

Tafsiri ya chapisho la Kiingereza kwenda katika Kiswahili imefanywa na:
Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,
Arusha, Tanzania, East Africa.
E-mail: revwangowi@gmail.com

# Yaliyomo

Muhtasari wa Kozi ........ 5
(1) Uzuri wa Utakatifu ........ 7
(2) Utakatifu ni Mahusiano ........ 23
(3) Utakatifu ni Sura ya Mungu ndani ya mtu. ........ 33
(4) Utakatifu ni Kutengwa ........ 47
(5) Utakatifu ni Moyo Usiogawanyika ........ 69
(6) Utakatifu ni Haki na Uadilifu ........ 81
(7) Utakatifu ni Kumpenda Mungu ........ 97
(8) Utakatifu ni kumpenda jirani yako ........ 117
(9) Maisha matakatifu ni kuishi katika ukamilifu wa Roho ........ 141
(10) Utakatifu ni Kumfanania Kristo ........ 159
(11) Utakatifu ni Ushirika usiovunjika na Mungu ........ 185
(12) Je, Maisha Matakatifu yanawezekana? ........ 199
Mpangokazi wa Mwisho ........ 217
Vyanzo Vilivyopendekezwa ........ 218
Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa ........ 219

# Muhtasari wa Kozi

**Ufafanuzi Kuhusiana na Kozi**

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

**Maelezo na maelekezo kwa viongozi wa madarasa.**

Kozi hii inapima Imani na uzoefu wa maisha ya utakatifu. Unapaswa uratibu dakika 90-120 kwa kila kikao cha darasa, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi wanazopewa nje ya darasa.

Alama ► inaashiria **swali linalopaswa kujadiliwa**. Wakati wowote unapokuja katika hayo, uliza hayo maswali yanayokuja mbele yake, na uwaachie wanafunzi wajadili jibu lake. Jitahidi kuhakikisha kwamba wanafunzi wote darasani wanahusika katika majadiliano. Ikiwa ni lazima, waite wanafunzi kwa majina yao.

Kila tanbihi chini ya ukurasa inarejea **andiko** la Biblia. Kama aya haijatolewa au hazijatolewa kutoka kwenye fungu, tafadhali wafanye wanafunzi waziangalie na wazisome wakati wa kipindi darasani. Labda iwe imeelekezwa vinginevyo, nukuu ya maandiko yanatoka katika Biblia ya English Standard Version (ESV).

Kila somo litakuwa na **kazi za kufanya** mbili:

(1) **Insha fupi** ya mada maalumu itakayotolewa. Kwa utashi wa kiongozi wa darasa, insha hii inaweza kuwa ni ya kuandikwa au inayoweza kuwakilishwa kwa mdomo.

(2) Kazi ya **kukariri maandiko**. Haya yatakuwa yanapitiwa katika kila kipindi darasani. Itakapofikia mwisho wa kozi, wanafunzi watatakiwa wawe wamenukuu aya zote ziizokaririwa kwa kipindi chote cha kozi.

Kusudio mojawapo la kozi hii ni kuwaandaa wanafunzi kuwa waalimu. Kiongozi wa darasa anapaswa awape wanafunzi **nafasi za kukuza vipawa vyao vya ufundishaji**. Kwa mfano, kiongozi wa darasa mara moja moja anapaswa ampe mwanafunzi nafasi ya kufundisha sehemu fupi ya somo darasani.

Kila mwanafunzi ataandaa **mpango kazi wa mwisho** wa somo. Mpango kazi huu utahusisha mahubiri au masomo matatu kuhusiana na maisha ya utakatifu. Haya yanaweza kuelekezwa aidha kwenye uhalisia wa kibiblia au wa vitendo halisi vya maisha ya utakatifu. Ikiwezekana, kila mwanafunzi atapaswa kuwakilisha kila hubiri au somo alilolifanya na kuweka kumbukumbu kwa ajili ya kiongozi wa darasa.

Kama mwanafunzi atataka apewe cheti cha kuhitimu **Shepherds Global Classroom**, ni lazima ahudhurie vipindi vyote na akamilishe kazi zote za kufanya. Fomu itatolewa kila mwisho wa kozi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi zote zilizomalizika.

# Somo la 1
# Uzuri wa Utakatifu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Akubaliane na uzuri wa utakatifu wa Mungu na mpango wake wa kutufanya tuwe watakatifu.

(2) Akatae mitazamo inayopotosha kuhusiana na utakatifu, na akubaliane na mitazamo ya kibiblia inayohusiana na utakatifu.

(3) Aimarishwe katika kuweza kumfafanulia mwamini mpya ni nini maana ya kuwa mtakatifu.

(4) Kukariri 1 Petro 1:14-16.

## Utambulisho wa Kozi

Utakatifu ni mojawapo ya dhamira kuu ya Biblia. Katika maandiko, Mungu alituonyesha yeye ni nani: kwamba ni Mungu aliye Mtakatifu. Kisha, Mungu akatuonyesha tunawezaje kuwa kwa neema yake: tunaweza kuwa watu watakatifu.

Kwa kila mwamini wa kweli, kuna kiu ya utakatifu. Kama watoto wa Mungu, tunatamani sana kuwa kama yeye. Kwa masikitiko, wengi katika kanisa la wakati huu wa sasa wamekubaliana na mawazo potofu kwamba utakatifu hauwezekani. Badala ya kutafuta kuwa kama Kristo, Wakristo wengi wanakubaliana na kushindwa katika kuishi maisha ya dhambi. Badala ya maisha ya Kikristo yenye ushindi, Wakristo wengi wamejilazimisha kuwa chini ya "utawala wa dhambi."

Zaidi ya miaka mia moja iliyopita, John Hyde. Mmishenari maarufu kwa ajili ya India, alisema, "Tunachohitaji kwa sasa ni uamsho wa utakatifu." Kama ndivyo ilivyokuwa, basi ni ukweli usiopingika katika ulimwengu wa dhambi wa karne ya ishirini na moja.

Kama utakatifu ni muhimu sana kwa Mungu, ni lazima tujiulize, "Inamaanisha nini kuwa mtakatifu?" Kama utakatifu umeamriwa katika maandiko matakatifu, tunapaswa tujiulize, "Je inawezekana kuishi maisha ya utakatifu?"

Katika kozi hi, tutajifunza anachomaanisha Mungu anaposema "Kuweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu." Kama tunavyoelewa ujumbe wa utakatifu katika Biblia, tutaona kwamba maisha ya utakatifu yanawezekana kwa kila Mkristo. Kila somo litahusisha mambo matatu:

1. Tutajificha maana za maneno ya Biblia kama "utakatifu", "utakaso", na "ukamilifu". Hii ni sehemu ya theolojia ya Biblia inayohusiana na utakatifu.

2. Tutajifunza mitazamo ya vitendo halisi vya maisha ya utakatifu, moyo ulio safi, na roho inayomfanania Kristo.
3. Tutayaangalia maisha ya Mkristo anayedhihirisha maana ya kuwa mtakatifu. Tutaangalia ni kwa jinsi gani mtu mtakatifu anatenda katika maisha yake ya kila siku.

**Maandiko ya Kusoma na Kujadili**

Kabla ya kuendelea na somo, soma maandiko yafuatayo kwa uangalifu na jadili maswali yaliyopo. Hii itatambulisha baadhi ya mada tutakazojifunza katika masomo haya.[1]

► Soma Mambo ya Walawi 19:2. Kutokana na kifungu hiki, Kwanini Israel walitakiwa kuwa watakatifu?

► Soma 1 Petro 1:15-16. Waamini wanatakiwa kuwa na tabia gani?

► Soma Waebrania 12:14. Kutokana na kifungu hiki, ni sifa gani kuu mbili ambazo Wakorintho wanapaswa kuzifanyia kazi kama watataka kumwona Bwana?

► Soma 1 Wathesalonike 4:3-8. Mungu anamwita kila mwamini kukaa mbali na dhambi gani? Mungu amewaita watu wake kwenye nini?

► Soma Ufunuo 20:6. Kuna tabia gani ya kiroho inayoonekana kwa wale wote watakaokuwepo katika unyakuo wa kwanza?

## Uzuri wa Utakatifu

► Unaposikia mtu akitambulishwa kama "mtakatifu" ni wazo gani linakujia kwenye ufahamu wako? Je wazo lako ni hasi au chanya? Kwa nini?

Mmishenari mmoja wakati fulani alimtembelea chifu wa zamani wa Kiafrika. Chifu alimwuiza, "Mkristo ni nani?" Mmishenari akajibu, "Mkristo hawezi kuiba ng'ombe wa adui yake. Mkristo hawezi kutembea na mke wa adui yake. Mkristo hawezi kuua."

Chifu akasema, "Nimeelewa. Kuwa Mkristo ni sawa na kuwa mtu mzee! Nilipokuwa kijana, nilimpiga adui yangu, nikamwibia ng'ombe wake na nikatembea na mke wake. Kwa sasa mimi ni mzee sana kuweza kumshambulia adui yangu; mimi ni Mkristo!"

Kwa masikitiko, hivi ndivyo watu wengi wanavyofikiri kuhusiana na ujumbe wa maisha ya utakatifu. Wanafikiri kwamba utakatifu siyo zaidi ya orodha ya majina ya dhambi za kukwepa. Wanakosa uzuri wa Utakatifu kama unavyofundishwa katika neno la Mungu.

### Mawazo potofu kuhusu utakatifu

Mungu ni Mtatakatifu. Watu wa Mungu ni lazima wawe watakatifu. Huu ni ujumbe mkuu sana katika Biblia. Hata hivyo, bado kuna imani nyingi potofu kuhusiana na utakatifu.

[1] Maswali haya yamekusanywa na Mchungaji Timothy Keep.

1. **Watu wengine wanaamini kwamba ni watu wachache tu wanaweza kuwa watakatifu**. Wanawagawa Wakristo katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni Wakristo katika imani zao ambao wamemwamini Kristo kama Bwana na Mwokozi wao, lakini hawamtii Mungu kwa uaminifu katika matendo na tabia zao. Kundi la pili linatokana na Wakristo waliofikia kiwango cha juu zaidi wakiwemo- wahubiri, wachungaji, na watu wema sana. Kwa mujibu wa mtazamo huu, ni Wakristo wachache sana walio watakatifu.

2. **Watu wengine wanaamini kwamba tunakuwa watakatifu kwa kujitenga na watu wengine.** Miaka mingi iliyopita, baadhi ya "watu watakatifu" walikwenda kuishi jangwani. Mtu mmoja aliishi huko kwa miaka thelathini na saba juu ya jukwaa lilioinuliwa sana juu ya ardhi. Aliamini kwamba tunafanyika watakatifu kwa kujitenga na watu wengine.

3. **Watu wengine wanaamini kwamba tunakuwa watakatifu tu tukishafariki.** Wanaamini kwamba kamwe hatuwezi kutimiza makusudi ya Mungu katika maisha haya, lakini tutafanywa watakatifu tukishafariki. Kwa imani hii, kifo siyo adui yetu bali rafiki. Katika kifo, hatimaye tunalipata kusudi la Mungu kwa watu wake.

4. **Watu wengine wanaamini kwamba tunakuwa watakatifu kwa kufuata sheria.** Wanaamini kwamba tunakuwa watakatifu kwa kuvaa aina fulani ya mavazi, au kwa kufuata orodha ya vitu vya "kufanya au kutofanya". Wanaamini kwamba utakatifu ni kwa mambo ya nje tu lakini siyo kubadilishwa kabisa kwa moyo.

5. **Watu wengine wanaamini kwamba ushahidi wa mtu mtakatifu ni pale anapokuwa na karama ya kunena kwa lugha na kufanya miujiza.** Wanaupima utakatifu kwamba siyo katika maisha ya utakatifu, bali katika matendo ya ishara na miujiza.

6. **Mwisho, watu wengine wanaamini kwamba utakatifu hauwezekani!** Wanaamini kwamba utakatifu ni dhana tu Mungu alioiweka kwetu ili kutupa changamoto ya kufanya mambo mazuri, lakini siyo jambo la uhalisia katika ulimwengu huu. Kwa imani hii, hakuna hata mtu mmoja anayeweza kushika agizo la Mungu la "Iweni watakatifu".

Hata hivyo, agizo la Mungu la "Iweni watakatifu" ni agizo analotuka sisi tulitii. Mungu ni Baba mwema; kamwe hawezi kutuamuru tufanye jambo lolote ambalo haliwezekani ndani ya neema yake. Kuwa watakatifu ni kuwa katika ile hali Mungu aliyotuumba tuwe nayo. Kwa nguvu zetu wenyewe, haiwezekani kuwa na moyo wa utakatifu, lakini kwa uweza wa Mungu moyo wa utakatifu unawezekana kwa kila mwamini. Utakatifu huja kupitia neema ya Mungu, na siyo kwa nguvu zetu wenyewe.

► Katika haya mawazo potofu yote kuhusiana na utakatifu, ni lipi limekithiri kwenye eneo lako unalohudumu? Je, utakataifu unaonekana kuwa ni mzuri miongoni mwa Wakristo katika jamii yako?

### Picha ya Biblia kuhusu utakatifu

Kinyume na mawazo hasi yaliyoorodheshwa hapo juu kuhusiana na utakatifu, Biblia inaonyesha utakatifu kama uwezekano mzuri kwa watoto wa Mungu. Jaribu kufikiria mambo yanayoitwa matakatifu ndani ya Biblia. Hakuna hata moja lilil0 baya au lisilovutia; yote ni mazuri na yanayovutia. Asili ya Mungu ya utakatifu ni nzuri na inayovutia.

- Asili ya Mungu ya utakatifu ni nzuri na yenye utukufu.
- Vitu vyote vilivyokuwa kwenye hekalu vilikuwa vitakatifu na vinapendeza.
- Israeli iliitwa kuwa taifa takatifu litakalowavuta watu wengine kuja kwa Mungu. Utakatifu wake uliwavutia watu, haukuwafukuza kutoka kwao.[2]
- Kanisa linaitwa liwe watu watakatifu. Ndiye atakayekuwa bibi harusi mzuri kwa ajili ya Bwana harusi.

Kila picha hapa inavutia. Biblia inaonesha kwamba utakatifu wa kweli siyo mchafu au wa kuogopesha. Badala yake ni kipawa cha Baba yetu wa Mbinguni. Kama tutauona utakatafu kama ulivyo tutakuwa na kiu ya moyo mtakatifu na maisha matakatifu. Kama tutafundisha utakatifu kama Biblia inavyofudisha watu wetu watakuwa na kiu ya moyo safi na maisha matakatifu. Utakatifu ni kipawa kizuri kutoka kwa Baba mwenye upendo

## Uzuri wa utakatifu unaonekana katika uumbaji wa asili wa Mungu

### Aliumba dunia iliyokamilika

Tuanzie kwenye bustani nzuri ya Eden. Fikiria kuhusu matunda matamu ambayo umewahi kula, tunda katika Eden lilikuwa tamu zaidi. Fikiri kuhusu maua mazuri sana ambayo hujawahi kuyaona; maua ya bustani ya Eden yalikuwa mazuri zaidi. Mungu aliumba dunia iliyokamilika, ambayo ilikuwa haina madhara ya dhambi. Aliumba ulimwengu usiokuwa na maumivu, machozi au kifo.

Muhimu kuliko yote, Mungu aliumba ulimwengu wenye urafiki wa ndani kati ya Mungu na mwanadamu. Hakuna kilichomtenganisha mwanadamu na Mungu. Kila siku Mungu alimtembelea Adamu na Hawa. Hakuna kiumbe yeyote aliyekuwa na upendeleo kama huu. Mungu alimwumba mwanadamu kwa ajili ya uhusiano maalumu na yeye. Katika bustani ya Eden, kulikuwa na amani iliyokamilika kati ya Mungu na mwanadamu.

### Shetani aliiharibu dunia ya Mungu iliyokuwa Kamilifu

Shetani alitaka aiharibu hii dunia iliyokamilika. Shetani alichukia kila kitu Mungu alichoumba. Juu ya yote, Shetani alichukia urafiki wa karibu uliokuweko kati ya Mungu na mwanadamu. Alikusudia kusambaratisha uhusiano huu wa upendo na uaminifu.

---

[2] Unaweza ukasema. "Lakini vipi kuhusu Mafarisayo? Walikusudiwa wawe watu "watakatifu", lakini waliwafungia wengine nje." Tutaona katika masomo haya kwamba "utakatifu" wa Mafarisayo haukuwa wa kweli, Kwao haki ilikuwa ni ukiri wa nje tu na siyo utakatifu wa kweli.

Shetani hakuweza kumharibu mwanadamu moja kwa moja, kwahiyo alidhamiria kuusambaratisha uhusiano uliokuwepo kati ya Mungu na mwanadamu. Shetani alijua kwamba Mungu ni mtakatifu na kwamba alimwumba mwanadamu kwa mfano wake. Shetani alitaka aharibu ule mfano mtakatifu ndani ya mwanadamu. Mungu mtakatifu na mwanadamu mtakatifu wangekuwa na uhusiano usiovunjika, lakini Shetani akaweza kuuharibu uhusiano huu kwa kumdanganya mwanadamu atende dhambi.

Shetani alikuja kwa Hawa kwa sura ya nyoka. Nyoka alihoji amri ya Mungu. Akauliza, "Je ni kweli Mungu alisema 'Msile matunda ya miti yote ya bustani'?" Alitaka amsababishe Hawa awe na mashaka dhidi ya uzuri wa Mungu. Hawa akamjibu, "Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, 'Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.'"[3]

Nyoka alimlaumu Mungu kwa kuwafanyia mema Adam na Hawa. Nyoka akamwambia mwanamke, "Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." Nyoka akamwingiza Hawa kwenye kiburi: "Mtakuwa kama Mungu."

Hawa akala lile tunda, akampa na Adam, akala. Adam na Hawa walijitambua kwamba wamevunja sheria ya Mungu. Mungu alipofika bustanini, waliona aibu wakajificha asiwaone. Uhusiano wa karibu uliokuwepo kati ya Mungu na mwanadamu ukavunjika.

**Mungu hakuvunjika moyo na uumbaji wake**

Kutokana na dhambi yao, Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa kutoka katika bustani ya Eden. Dhambi ilivunja uhusiano wa karibu kati ya Mungu na mwanadamu. Dhambi iliharibu mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu. Lakini kwa sababu ya upendo wake, Mungu hakumwacha mwanadamu katika hali hii ya kutisha. Mungu angeweza kusema, "Adamu, umesababisha balaa hili lote, ni tatizo lako! Mimi ninaondoka." Badala yake, Mungu wa upendo akafanyika sehemu ya ulimwengu wetu akatoa tiba kwa ajili ya dhambi zetu.

Tiba hii ilihusisha njia ya kuelekea msamaha. Mungu akatoa njia ya kurejesha uhusiano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu aliyeanguka. Kanisa limekuwa kila wakati likihubiri kwamba, "Wenye dhambi wanaweza kuhesabiwa haki na Mungu." Kupitia msalaba, tunaweza kusamehewa dhambi.

Hizi ni habari njema sana! Lakini wakati mwingine Kanisa limesahau upande mwingine wa tiba ya Mungu. Tiba ya Mungu kwa dhambi siyo tu njia ya msamaha bali pia njia ya urejesho. Mungu alitoa njia ya kurejesha sura yake ndani ya mwanadamu.

Mungu hakuridhishwa na kusema, "Mtakuwa huru kutokana na adhabu ya dhambi, lakini kamwe hamtakuwa huru kutokanana nguvu ya dhambi." Hapana! Mungu alitoa njia ambayo itaweza kumfanya mwanadamu awe mtakatifu. Mungu alitembea bustanini akiwa

[3] Mwanzo 3:1-6

na watu watakatifu; hawezi kutembea na watu wenye dhambi.  Mungu anataka uhusiano na watu wake, kwa hiyo alitoa njia ya kutufanya watakatifu.

Katika maandiko yote, tunamwona Mungu akiwa na kazi ya kuwafanya watu wawe watakatifu ili aweze kuwa na uhusiano nao. Mungu hawezi kusema, "Najua wewe ni mdhambi, lakini nitafunga macho yangu, nisizione dhambi zenu, nijifanye nyie ni wenye haki."  Badala yake Mungu anaahidi kuwafanya watu wake watakatifu.

> Bwana atakuweka uwe taifa takatifu kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia zake.[4]

Mungu anataka awafanye watu kuwa watakatifu. Hili ndilo kusudi la Mungu kwa watu wake. Mungu anaahidi kwamba, "watawaita, Watu watakatifu, Waliokombolewa na Bwana."[5]

## Uzuri wa utakatifu unaonekana katika asili ya Mungu

Kutokana na anguko, mwanadamu hakuwa mtakatifu tena. Kwa haraka tunasahau asili ya Mungu ya utakatifu.  Mungu alituumba "kwa mfano wake". Kwa sasa tumejiumbia miungu midogo katika mifano yetu - wivu, chuki, na kiburi.

Wababeli walielezea habari za Marduk aliyekuwa chifu wa mungu kwa kumuua mama yake. Wagiriki walielezea habari za Zeu aliyekuwa anamiliki vimada wengi. Warumi walielezea habari za Bacchu, mungu wa ulevi na ufisadi.

Miungu hii haikuwa mitakatifu. Watu walioiabudu miungu hii walifanana na miungu hii pia. Watu walisema uongo, waliiba, na walidanganywa sawa na miungu yao ilivyosema uongo, ilivyoiba na kudanganywa. Watu waovu walitengeneza miungu waovu. Kinyume chake, miungu hii ikawaruhusu wanadamu kuendelea katika dhambi zetu. Tukawa kama miungu tuliyoiabudu.

Yehova hafanani na hii miungu ya uongo. Mungu ni mtakatifu. Kwa kurudia – rudia, maandiko yameshuhudia utakatifu wa Mungu. Baada ya kuvuka Bahari ya Shamu, watu wa Israeli walimsifu Mungu wao aliye Mtakatifu. Waliimba, "Ee Bwana, katika miungu ni nani aliye kama wewe? Ni nani aliye kama wewe, mtukufu katika utakatifu, Mwenye kuogopwa katika sifa zako, mfanya maajabu?"[6]

Mtunga Zaburi aliimba, "Na Wewe U Mtakatifu, Uketiye juu ya sifa za Israeli."[7] Isareli ilimsifu Mungu kwa ajili ya utakatifu wake. Muimba Zaburi, walimwita Mungu, "Mtakatifu, Mungu wa Israeli."[8]

Manabii walishuhudia kwamba Mungu ni mtakatifu. Sawa na mtunga Zaburi, walimwita Mungu, "Mungu mmoja Mtakatifu wa Israeli."[9] Isaya akamwita Mungu, "Mtakatifu wa

[4] Kumbukumbu la Torati 28:9
[5] Isaya 62:12
[6] Kutoka 15:11
[7] Zaburi 22:3
[8] Zaburi 71:22; 78:41; 89:18

Israeli" mara ishirini na sita. Isaya alimheshimu, "Yeye aliye juu ya vyote na aliyeinuliwa juu, anayeishi milele, ambaye jina lake ni mtakatifu."[10] Utakatifu ni sehemu kubwa sana ya tabia ya Mungu kwamba hata kuweza kuapa kwa "utakatifu wake" ilikuwa sawa na kuapa kwa "jina kake mwenyewe."[11] Habakuki alimshuhudia Mungu, "Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu, wewe usiyeweza kutazama ukaidi."[12] Manabii walijua kwamba Mungu ni Mtakatifu.

Huko mbinguni, kumwabudu Mungu kunasherehekea utakatifu wake. Malaika Maserafi waliimba, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake."[13] Yohana mwona maono aliona viumbe wanne wakimsifu Mungu wakisema, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja!"[14] Mungu ni Mtakatifu.

**Uzuri wa utakatifu unaonekana katika mpango wa Mungu kwa watu wake**

Mungu Mtakatifu alimuumba mwanadamu kwa ajili ya uhusiano na yeye, lakini dhambi zetu zilitutenganisha na yeye. Hata hivyo, Mungu alikusudia kuurejesha uhusiano huo na watu wake. Kwa kuwa ni watu watakatifu tu wanaoweza kusimama mbele ya uwepo wa Mungu Mtakatifu, alitengeneza njia ya kutufanya sisi watakatifu. Mungu alifundisha maana ya kuwa mtakatifu kwa watu wake ambao hawakuwa watakatifu. Kuna maeneo mawili katika hatua hii:

1. Mungu alimfundisha mwanadamu asili ya utakatifu wa Mungu. Marduk, Zeu, na Bacchu walikuwa na nguvu lakini wasio na maadili. Mungu alijidhihirisha mwenyewe kuwa mwenye nguvu na mtakatifu.

2. Mungu alimfundisha mwanadamu asili ya watu watakatifu. Mungu alisema, "Mtakuwa watakatifu; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu."[15] Kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu, watu wake ni lazima nao wawe watakatifu.

Isaya alihubiri katika taifa la watenda maovu. Dhambi ilikuwa imeharibu kabisa uzuri wa watu wa Mungu. Kutoka kuwa watu waliochaguliwa na Mungu, Israeli ilikuwa imeangukia katika hali ya aibu ya watu walioshindwa na kupelekwa utumwani; walikuwa watumwa waliofedheheshwa. Lakini Isaya aliona katika maono siku ambayo "Haki ya Israeli itakapokwenda kung'aa." Katika siku hiyo, Israeli "itakuwa taji ya uzuri katika mkono wa Bwana."[16]

Watu wanaoshindwa kuelewa ujumbe wa utakatifu katika Biblia mara nyingi wanauonesha utakatifu kama sheria, sheria ngumu, na sura za ukali. Huu siyo mtazamo wa kibiblia

---

[9] Isaya 5:19; 10:20; Yeremia 50:29; 51:5; Ezekieli 39:7
[10] Isaya 57:15
[11] Amosi 4:2; 6:8
[12] Habakuki 1:13
[13] Isaya 6:3
[14] Ufunuo 4:8
[15] Mambo ya Walawi 19:2
[16] Isaya 62:2-3

kuhusiana na utakatifu. Badala yake, kuwa mtakatifu ni kuonyesha uzuri wa utakatifu wa Mungu mwenyewe. Kuwa mtakatifu kunatoa uhuru wa furaha wa kuishi ndani ya uhusiano na Mungu Mtakatifu. Katika Biblia, utakatifu siyo neno la huzuni bali la furaha na uzuri!

Katika Biblia, Mungu anadhihirisha asili yake ya utakatifu. Kisha, Mungu anawafundisha watu wake jinsi ya kuishi maisha matakatifu. Kwa umuhimu mkubwa kabisa, Mungu anaonyesha kwamba atawapa watu nguvu za kuwawezesha kuwa kama yeye anavyotaka wawe. Kupitia neema yake, Mungu anaweza kuwafanya watu wawe watakatifu. Mungu hapuuzi dhambi zilizoko ndani ya watoto wake; badala yake anatufanya tuwe watakatifu. Mungu wa utakatifu anapendelea ushirikiano na watu watakatifu.

### Inamaanisha nini kuwa Mtakatifu?

Kupitia Neno lake, Mungu amewafundisha watu wake ni nini maana ya kuwa mtakatifu. Wakati Mungu alipoanza kuwafundisha watu wake, hawakujua lolote kuhusu utakatifu. Hawajawahi kumwona Mungu aliye mtakatifu au watu watakatifu. Mungu alifundisha sana kuhusa utakatifu zaidi ya tunapofundisha lugha kwa mtoto.

Tunapomfundisha mtoto mdogo tunanyoosha kidole kueleka kiti na kusema "Kiti". Tunanyoosha kwenye gari na kusema, "Gari". Hatua kwa hatua mtoto anajikuta anajifunza maana za maneno. Mtoto huanza kujifunza maana ya neno "upendo" kwa uzoefu wa upendo anaoupata kutoka kwa mama yake. Mtoto anajifunza maana ya neno "haki" wakati mama yake anapomwadhibu kwa kosa la kukosa utii.

Mungu alifundisha maana ya utakatifu kwa njia hiyo hiyo. Tukiwa watu tuliokuwa tumeanguka, hatukujua ni nini maana ya kuwa mtakatifu. Hatua kwa hatua, Mungu akawa anafunua maana ya utakatifu kwa watu wake kupitia maandiko na picha zinazoonyesha ni nini maana ya kuwa mtakatifu.  Tunapotafuta maana ya neno Utakatifu ndani ya Biblia tunaona mambo yafuatayo:

1. **Kuwa mtakatifu ni kuwa na ushirika wa karibu na Mungu**. Watu watakatifu katika kitabu cha Mwanzo (kama Henoko na Abrahamu) walikuwa ni watu waliokuwa na uhusino wa karibu sana Mungu. Walitembea na Mungu. Kwa kuonesha maisha ya watu watakatifu, Mungu alijifunua kwamba mtu mtakatifu ni yule aliye katika ushirika na Mungu.

2. **Kuwa mtakatifu ni kuakisi mfano na sura ya Mungu**. Utakatifu siyo tabia ya asili ya mwanadamu. Utakatifu ni sifa ya Mungu pekee. Israeli walitakiwa wawe watakatifu, "Mtakuwa watakatifu; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu."[17] Kuwa Mtakatifu maana yake ni kuakisi mfano na sura ya Mungu.

3. **Kuwa mtakatifu maana yake ni kufanana na Mungu**. Kwa mara ya kwanza neno "Utakatifu" lianze kwenye Biblia, lilirejea siku ambayo imetengwa kwa makusudi maalumu kwa ajili ya Mungu. Siku ya Sabato ilikuwa takatifu; ilikuwa

[17] Mambo ya Walawi 19:2

imetengwa kutoka zile siku nyingine sita. Kama mtoto anayejifunza maana ya "kiti," Mungu aliilenga siku ya saba na kusema "Ni takatifu."

4. **Kuwa mtakatifu ni kuwa na moya usiogawanyika**. Katika vitabu vya historia, Mungu alitumia neno "ukamilifu" kwa watu ambao "hawana moyo wa kugawanyika." Kuwa mtakatifu kunamaanisha kuwa na uamuzi usiokuwa na kusitasista katika msimamo wetu na Mungu. Moyo wa utakatifu humpenda Mungu bila mgawanyiko.

5. **Kuwa mtakatifu ni kuishi maisha ya haki**. Manabii walihubiri kwa watu waliofikiria tu kwamba, "Tunaenda kuabudu hekaluni na kutoa zaka zetu, kwa hiyo ni watakatifu." Manabii walionesha wazi kwamba haitoshi tu kufuata matambiko. Kuwa mtakatifu inamaanisha kuishi maisha ya uadilifu kwa ajili ya Bwana na watu wengine. Watu watakatifu "wanatenda haki, wanapenda huruma na wanaenenda kwa unyenyekevu pamoja na Mungu."[18]

6. **Kuwa watakatifu ni kuwa na upendo kamili kwa Mungu na kwa jirani yetu**. Vitabu vya Injili vinaonyesha ufunuo kamili wa utakatifu wa maisha ya Yesu Kristo. Yesu alikuwa na moyo wa utakatifu uliokuwa umejitoa kabisa kwa ajili ya mapenzi ya Baba. Yesu alikuwa na mikono ya utakatifu iliyotenda kwa upendo halisi dhidi ya watu wengine. Yesu alionyesha kuwa kuwa mtakatifu inamaanisha kumpenda Mungu, kumpenda jirani yetu kama tunavyojipenda wenyewe.

7. **Kuwa watakatifu ni kuishi katika utimilifu wa Roho Mtakatifu**. Katika kitabu cha Matendo, tunaona mfano wa Wakristo waliokuwa wanajazwa na Roho wa Mungu. Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, waliyaishi maisha matakatifu. Tunakuwa watakatifu tunapoendelea kuishi katika utimilifu wa Roho Mtakatifu.

8. **Kuwa Mtakatifu ni kumfanania Kristo**. Yesu alikuwa mfano halisi wa utakatifu wa moyo na mikono. Nyaraka za Mitume katika Agano Jipya zinaonesha kwamba inawezekana kabisa kwa Wakristo wa kawaida kufuata mfano wa Yesu Kristo. Nyaraka hizi hutoa mwongozo wa vitendo wa jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu kila siku. Nyaraka hizi zinatufundisha jinsi ya kuishi kama watu tunaomfanania Kristo.

> "Ni lazima tuwe watakatifu, kwa sababu hii ndio sababu kuu ya msingi iliyomfanya Yesu kuja duniani. Kuzungumza na watu waokoke kutoka kwenye hatia ya dhambi bila kuokolewa kutoka utawala wa dhambi ndani ya mioyo yao ni kujichanganya kwa ushuhuda wote wa Maandiko. Yesu ni mkombozi kamili. Haondoi tu hatia ya dhambi; bali huivunja nguvu yake."
> - Nukuu kutoka kwa Askofu J.C. Ryle

9. **Utakatifu hutuandaa kumwona Mungu**. Bustanini Eden, Mungu aliandaa bustani ambayo watu watakatifu wangeishi wakiwa katika ushirika na Baba. Kwa sababu ya dhambi tulifukuzwa kutoka katika ile bustani. Lakini Mungu hakuachana na mpango wake. Katika kitabu cha Ufunuo, tunaona kwamba watu wa Mungu siku moja watauona uso wa Mungu. Hakuna mwenye dhambi atakayeweza kuuona uso wa

[18] Mika 6:8

> Mungu, lakini Mungu anawaandaa watu watakatifu watakaoishi kwenye umilele pamoja naye. Huu ni mpango wa Mungu kwa ajili ya watu wake.

### Hitimisho: Mungu Mtakatifu anawaita watu wake wawe Watakatifu

Dr. John Stott alikuwa mmoja wa Wainjilisti maarufu sana wa karne ya ishirini. Katika moja ya mahubiri yake ya mwisho, Dr. Stott alizungumza kuhusu mpango wa Mungu kwa watu wake.[19] Tumekombolewa kwa neema kupitia imani; tumetolewa mautini hadi kwenye uzima. Kwa nini? Kusudi la Mungu la kutukomboa ni ili tuwe kama Kristo. Dr. Stott alisema, "Kufanana na Kristo ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya watu wa Mungu."

Maandiko matatu katika Agano Jipya yanatuonyesha kukua kwetu katika mfano wa Kristo hapa duniani kunatuandaa tukaishi na Mungu. Maandiko haya yanatuonyesha umuhimu wa utakatifu katika maisha ya mwamini.

**Warumi 8:29 inarejea wakati uliopita na inaonyesha kusudi la Mungu la umilele kwa watoto wake.**

> Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

Mpango wa Mungu wa umilele ni kwamba, "tufanane katika sura ya Mwana wake." Tangu mwanzo mpango wa Mungu ni kutufanya tuwe kama Kristo. Warumi 8:28 inatoka ahadi kwamba, "katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema." Ahadi hii "ni kwa ajili ya wale wote walioitwa kwa ajili ya kusudi lake." Kusudi lake ni nini? Kusudi la Mungu tangulizi ni kuwafanya wana wa Mungu katika sura ya mwanae. Mungu alitukomboa ili atufanye watakatifu.

> "Mungu anao mpango mmoja wa hatima ya mwisho ya mwanadamu– utakatifu. Kusudi lake moja ni kuzalisha watakatifu. Alikuja kuwakomboa wanadamu kwa sababu aliwaumba ili wawe watakatifu."
> - Oswald Chambers

Paulo aliwakumbusha Wakristo wa Kolosai juu ya mabadiliko makubwa ambayo Mungu ameyafanya katika maisha yao. "Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake," Kupitia kifo cha Yesu, hawa watu ambao walikuwa "maadui" kwa Mungu, sasa walikuwa wamepatanishwa na yeye. Kisha Paulo akawakumbusha hawa waamini kuhusu kusudi la Mungu la kuwapatanisha wao na yeye. "ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama."[20]

Paulo hasemi tu, "Umepatanishwa na Mungu ili ukautumie umilele wako mbinguni." Hizo ni habari njema, lakini siyo habari njema zilizokamilika. Paulo anasema, "Umepatanishwa na Mungu ili uweze kuwa Mtakatifu." Lengo la Mungu ni kuwafanya watoto wake wawe watakatifu wasiokuwa na lawama."

---

[19] Hotuba ya John Stott huko Keswick. (June 20, 2014). Imechkuliwa kutoka https://www.leightonfordministries.org/2014/06/20/john-stott-address-at-keswick/ Desemba 20, 2019.
[20] Colossians 1:21-22

**2 Wakorintho 3:18 inarejea wakati uliopo na kuonyesha jinsi kusudi hili linavyotimia leo katika maisha ya muumini:**

> Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano huo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.

Kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, "tunabadilishwa kutoka kiwango kimoja cha utukufu hadi kingine." Kusudi la Mungu linatimizwa katika mabadiliko ya watoto wake kupitia nguvu za Roho Mtakatifu. Siku hadi siku tunafanywa ili tufanane na Kristo.

**1 Yohana 3:2 inarejea katika wakati ujao na kuonyesha ukamilikaji wa mwisho wa kusudi la Mungu:**

> Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.

Kitabu cha ufunuo kinalenga kwenye siku ambayo tunaweza kumwona Mungu uso kwa uso. Siku hiyo tutafanana na yeye. Kusudi la Mungu litakuwa limetimizwa kabisa na hata milele. John Stott anahitimisha kwamba, "Tutakuwa pamoja na Kristo, kama Kristo, milele."

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Maliza, kisha, tufanyie uumbaji upya;
ulio safi, usiokuwa na doa ili tuwe hivyo.
Tunaomba tuuone wokovu wako mkuu kwa ukamilifu
ukirejeshwa tena ndani yetu kwa Jina lako:
Tukibadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu mwingine
mpaka mbinguni tutakapochukua nafasi zetu.
Tuimbe na tutupe taji zetu mbele yako Bwana, kwa
mshangao, upendo na sifa."

- Charles Wesley

Kama Wakristo, kutafuta kwetu maisha ya utakatifu kunatuandaa kwa ajili ya siku ambayo tutamwona Mungu na kusudi lake katika maisha yetu likiwa linatimia. Hii itatufanya sisi tuwe na bidii katika ukuaji wetu wa utakatifu. Kila siku tunabadilishwa zaidi na zaidi katika sura yake.


Utakatifu siyo wazo la mtu fulani; bali ni tabia ya Mungu. Uelewa wetu kuhusu utakatifu unaendana zaidi na tabia ya Mungu ya Utakatifu tunayoipata katika Biblia. Jinsi tunavyotafuta kuwa kama yeye zaidi na zaidi, tukishirikiana na Mungu katika kusudi la umilele. Utakatifu ni kusudio la Mungu la uzima wa milele kwa kila mwamini. Kama watoto wa Mungu, tunapaswa tuwe na uchu wa kuona kwamba hili kusudi linatimizwa ndani ya mioyo na maisha yetu.

## Aliipata Siri - Samweli Kaboo Morris

Mwaka 1873, Samweli Morris[21] alizaliwa Liberia, Afrika Magharibi kama Mwana wa mfalme Kaboo, mtoto wa chifu wa kabila. Baba yake aliposhindwa kwenye mapigano, Kaboo

[21] Image: "Samuel Morris", Samuel Morris: A Spirit Filled Life (1921), retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:JORDAN-READ-MERITT(1921)_Samuel_Morris._A_Spirit_Filled_Life.jpg, public domain.

alikamatwa kwa ajili ya kutolewa kama fidia. Siku moja, Kaboo akaona mwanga uking'aa na akasikia sauti kutoka mbinguni ikimwambia aondoke akimbie. Kamba zilizokuwa zimemfunga mikononi zilifunguka zikaanguka, na Kaboo akakimbilia jangwani.



Alitembea kwenye jangwa kwa siku kadhaa hadi alipofika katika jiji la Monrovia. Akiwa kwenye lile jiji, kijana mmoja akamwalika aende kanisani kwake. Wakati Kaboo alipotembelea lile kanisa, mmishenari alikuwa anaelezea historia ya jinsi Paulo alivyobadilishwa. Alipokuwa akielezea kuhusu mwanga na sauti kutoka mbinguni, Kaboo alitambua kwamba hii ni ile ile sauti aliyoisikia jangwani. Bila kukawia, alimkubali Kristo kama Bwana na Mkombozi wake na akabatizwa kwa jina la Samweli Morris.

Baada ya miaka miwili, Samweli Morris alianza kufanya kazi ya kupaka rangi ili ajipatie kipato cha kuendesha maisha huku akiendelea kujifunza Biblia. Alikuwa anapenda kujifunza zaidi kuhusu Roho Mtakatifu na maisha ya nguvu za Roho. Baada ya mmishenari kumweleza kwamba amefundisha yote aliyojua, Morris alimwuliza, "Je mwalimu wako alikuwa nani"? Akamwlezea kuhusu mhubiri mmoja mtakatifu wa Amerika aitwaye Stephen Merritt. Akiwa hana fedha au usafiri, Morris akajongea karibu na bandari kutafuta meli ya kuzamia ili aende Amerika. Alikuwa amekusudia kujifunza Zaidi kuhusu kuishi katika Roho.

Alilala ufukweni akingojea apate meli. Wakati meli ilipofika, Morris akamwomba kapteni wa meli ampeleke Amerika. Kapteni alikataa, lakini baada ya muda mfupi, mabaharia wake wawili wakatoroka kazi wakakimbia. Kapteni akamwambia Morris kwamba anaweza akamsaidia kufanya kazi kwa kubadilishana na yeye kumpeleka New York. Wakati wa safari, alinyanyaswa vibaya na wale mabaharia wengine, ikiwa ni pamoja na kupewa kazi nzito za kwenye meli. Hata hivyo, Samweli alionyesha moyo wa upendo kwa wale mabaharia waliomsulubu hadi meli ilipokaribia New York, kapteni na baadhi ya mabaharia wakawa wamebadilishwa (wameokoka).

Wakati Morris alipowasili New York, alikutana na Stephen Merritt na akamwelezea shahuku yake ya kutaka kujifunza zaidi kuhusu Roho Mtakatifu. Bwana Merritt alikuwa akahudhurie kikao mahali pengine, lakini akamwacha Morris kwenye misheni yake kwa ajili ya jioni. Aliporejea, alimkuta Samweli akiongoza kipindi cha maombi. Katika usiku wa kwanza nchini Amerika, Samweli Morris aliwaongoza karibu watu ishirini kumpokea Kristo.

Stephen Merritt alimsaidia Samweli Morris kujiunga na Chuo Kikuu cha Taylor kwa ajili ya maandalizi ya kwenda kufanya Uinjilisti katika nchi Liberia. Morris aliwasili chuoni Indiana bila fedha, lakini akiwa na imani kubwa kwamba Mungu atatoa. Alimwomba raisi wa wanafunzi, "Naomba unipe chumba ambacho hakuna mtu mwingine yeyote anayekitaka." Usiku ule wanafunzi wenzake walimsikia "akizungumza na Baba yake." Umahiri wake wa kumwamini kabisa Mungu uliwavutia wengi katika chuo na hata kwenye makanisa ya jirani.

Ingawaje Morris alipanga kurudi Liberia, Mungu alikuwa na mpango mwingine juu yake. Katika kipindi cha miaka miwili cha kuwepo katika chuo kikuu cha Taylor, Samuel Morris

alikufa kwa ugonjwa wa nimonia. Alikuwa na umri wa miaka ishirini tu, lakini alikuwa na amani kwa kuwa kwenye mpango wa Mungu. Samweli alikuwa amemwambia raisi wa chuo, "Siyo kazi yangu. Ni kazi ya Bwana. Nimeimaliza kazi yangu. Mungu atawatuma watu wengine wazuri kuliko mimi kuifanya kazi hii katika Afrika."

Maisha ya Morris yalikuwa yamegusa watu wengi sana kiasi kwamba wakati wa mazishi yake mamia ya watu walipangana barabani kwa ajili ya kuhudhuria mazishi yake. Baadhi ya wanafunzi wenzake walikwenda Afrika kama wamishenari, wakitumika kwa "kumkumbuka mtoto wa mfalme Kaboo" Raisi wa chuo kikuu cha Taylor akasema, "Samweli Morris alikuwa mjumbe wa Mungu kwenye chuo kikuu cha Taylor. Alifikiria kwamba alikuja hapa ili kujiandaa mwenyewe kwa ajili ya huduma ya umisheni, lakini badala yake Mungu alikuwa amemtuma kuja kukiandaa chuo kikuu cha Taylor kwa ajili ya umisheni wa dunia nzima. Wote aliokutana nao walivutiwa na utakatifu wake, lakini pia na urahisi wa imani yake kwa Mungu."

Kwa sasa, mnara wa kumbukumbu kwenye kaburi la Samweli Morris lililoko Fort Wayne, Indiana linasomeka kama ifuatavyo:

Samweli Morris; 1873-1893
Mtoto wa Mfalme Kaboo
Raia wa Afrika Magharibi
Mchaji maarufu wa Ukristo
Mtume wa Imani rahisi
Mwakilishi wa Maisha yaliyojazwa Roho.

Maisha mafupi ya Samweli Morris yanadhihirisha kwamba kila mwamini anaweza kuishi katika uwezo wa nguvu ya Roho Mtakatifu. Moyo wa utakatifu na maisha ya utakatifu ndio kusudi la Mungu kwa kila mwamini.

**Tafakuri ya Somo la 1**

(1) Uzuri wa utakatifu unaonekana katika uumbaji wa Mungu wa asili. Mungu aliuumba ulimwengu ukiwa mkamilifu na bila dhambi.

(2) Uzuri wa utakatifu unaonekana unaonekana katika asili ya Mungu. Mungu ni Mungu Mtakatifu.

(3) Uzuri wa utakatifu unaonekana kwenye mpango wa Mungu kwa wanadamu. Ingawaje dhambi ilivuruga asili ya mwanadamu, Mungu hakuachana na mpango wake wa watu watakatifu. Kurejesha uhusiano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu aliyeanguka dhambini, Mungu alifundisha:

- Mungu mtakatifu yukoje
- Mtu mtakatifu yukoje.

(4) Kuna dhana nyingi potofu kuhusiana na utakatifu. Hizi ni pamoja na:

- Ni watu wachache tu wanaweza kuwa watakatifu.
- Tunakuwa watakatifu kwa kujitenga na watu wengine.
- Tunakuwa watakuwa tukishakufa.
- Tunakuwa watakatifu kwa kufuata sheria maalumu.
- Ushahidi kwamba mtu ni mtakatifu unaonekana katika vipawa maalumu vya kunena kwa lugha na matendo ya miujiza.
- Utakatifu hauwezekani.

(5) Ukweli kuhusu Utakatifu ni rahisi. Ifuatayo ni maana halisi ya kuwa mtakatifu:

- Kuwa mtakatifu ni kudumisha uhusiano wa karibu na Mungu.
- Kuwa mtakatifu ni kuakisi mfano na sura ya Mungu.
- Kuwa mtakatifu ni kutengwa kwa ajili ya Mungu.
- Kuwa mtakatifu ni kuwa na moyo usiogawanyika.
- Kuwa mtakatifu ni kuishi maisha ya haki.
- Kuwa mtakatifu ni kuwa na upendo kamili kwa Mngu na jirani zetu.
- Kuwa mtakatifu ni kuishi katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu.
- Kuwa mtakatifu ni kumfanania Kristo.
- Utakatifu hutuandaa sisi kumwona Mungu.

(6) Maandiko matatu katika Agano Jipya yanatuonyesha umuhimu wa utakatifu katika maisha ya mwamini:

- Warumi 8:29 inarejea wakati uliopita na inaonyesha kusudi la Mungu la umilele kwa watoto wake.
- 2 Wakorintho 3:18 inarejea wakati uliopo na kuonyesha jinsi kusudi hili linavyotimia leo katika maisha ya muumini.

- 1 John 3:2 inarejea katika wakati ujao na kuonyesha ukamilikaji wa mwisho wa kusudi la Mungu.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Hebu fikiria Mkristo mpya anakuambia, "Nilisoma katika Biblia kwamba Mungu ametuita tuwe watakatifu kama yeye alivyo mtakatifu. Hilo haliwezekani! Inamaanisha nini kuwa mtakatifu?" Andika ukurasa mmoja wa majibu kwa ajili ya huyu mwamini mpya. Kwenye kikao kinachofuata cha darasa, kila mwanafunzi asome majibu yake. Jipeni muda wa kujadili haya majibu kama darasa.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu 1 Petro 1:14-16.

(3) Kozi hii imeambatanishwa na Mradi wa Mwisho ambao utatakiwa urejeshwe siku ya mwisho ya darasa. Unatakiwa uanze kuufanyia kazi sasa. Fungua ukurasa wa 221 wa kozi hii kwa maelezo zaidi na ya kina kuhusiana na mradi huo.

# Somo la 2
# Utakatifu ni Mahusiano - "Kutembea na Mungu"

## Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Akubaliane na mpango wa Mungu anayewezesha mahusiano ya kila siku kwa watu wake.

(2) Atambue kwamba sisi ni watakatifu kupitia mahusiano yetu na Mungu, na siyo kwa jitihada za kibinadamu.

(3) Ajikabidhi kabisa katika kutumia muda wake wa ila siku kujenga mahusiano na Mungu.

(4) Ajazwe uwezo wa kuwasaidia waamini wengine kukua katika mahusiano na Mungu

(5) Kukariri 1 Yohana 1:6-7.

## Ibrahimu: Mtu aliyetembea na Mungu

Fikria kwamba wewe ni mtu wa umri wa miaka 75 unayeishi katika taifa la watu wanaoabudu sanamu mara ghafla unasikia sauti ya Mungu ikiongea. Utajibuje?

Mungu akamwambia Ibrahimu, "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha;"[22] "Acha kila kitu na unifuate!" Mungu hakuwambia Ibrahimu aende wapi. Alisema tu, "nifuate."

Ibrahim alimwamini Mungu na akamfuata kutoka nchi ya Uru hadi Harani, na kutoka Harani hadi Kaanani. Ibrahimu alitembea zaidi maili 1,000 kwa ajili ya kutii amri ya Mungu.

Ibrahimu aliziamini ahadi ambazo zilionekana kama ni jambo lisilowezekana kabisa. Aliamini kwamba Mungu atampa mtoto, ingawaje Sara alikuwa ameshapitiliza umri wake wa kuweza kupata mtoto. Aliamini kwamba Mungu ataenda kumpa

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Bwana,
Ninaachilia mipango na makusudi yangu mwenyewe,
Matamanio na mategemeo yangu yote,
Na ninakubaliana na mapenzi yako kwa maisha yangu.
Ninatoa kwako maisha yangu,
na kila kinachohusiana nami kabisa
navitoa kwako viwe vyako daima.
Nijaze na unizingire kwa Roho wako Mtakatifu,
Nitumie sawasawa na mapenzi yako,
nitume popote unapotaka,
Yatimize mapenzi yako yote ndani ya maisha yangu,
kwa gharama yeyote, sasa na hata milele."

- Betty Stam
(Mfiadini China)

---

[22] Mwanzo 12:1

nchi ya ahadi, ingawaje hakuwa na ardhi yeyote aliyokuwa ameimiliki katika nchi ya Kaanani. Aliamini kwamba Mungu atamfanya awe Taifa kubwa, ingawaje hakuwa na watoto." Ibrahimu, mtu aliyetoka katika jamii ya kipagani, aliitwa rafiki wa Mungu.[23] Alitembea na Mungu.

► Waulize watu watatu katika darasa lako watoe ushuhuda wa jinsi walivyotembea na Mungu hadi sasa. Kutembea na Mungu kulianza lini? Umejifunza masomo gani wakati huo?

## Utakatifu katika vitabu vitano vya kwanza vya biblia- Kutembea na Mungu

Watu watakatifu hutembea na Mungu; wanautumia muda wao na Mungu. Wanapokuwa wanatembea na Mungu, wanakua na kufana na yeye. **Kuwa matakatifu ina maana ya kujenga uhusiano wa ndani sana na Mungu**.

Mungu alitembea na Adamu na Hawa katika Bustani ya Eden. Baada ya dhambi kuvunja mahusiano wao na Mungu, Adamu na Hawa walijificha kutoka uso wa Mungu. Dhambi ikawatenganisha na Mungu.

Dhambi huvunja mahusiano na Mungu; huvunja mahusiano kati ya wanadamu; Adamu alimlaumu Hawa. Adamu na Hawa walishirikiana katika dhambi, lakini dhambi pia ikawaharibia mahusiano yao wenyewe. Malengo ya Mungu ni kwa watoto wake kutembea kwa amani pamoja naye na watu wengine. Malengo ya Shetani ni kuharibu mahusiano yetu na Mungu pamoja na watu wengine.

Dhambi iliharibu mahusiano kati ya Mungu na wanadamu, lakini Mungu alitafuta njia mbadala ya kurejesha uhusiano huo. Dhabihu zilitumika kudumisha mahusiano na Mungu mtakatifu. Hatuwezi kuwa watakatifu kwa juhudi za wanadamu; tunakuwa watakatifu kupitia mahusiano na Mungu mtakatifu.

Katika Agano la Kale lote, tunaona mifano halisi ya watu waliotembea na Mungu. Hawatembei tena na Mungu katika ile bustani nzuri. Kwa sababu ya dhambi, wanadamu sasa wanatembea na Mungu katika ulimwengu wa Dhambi wa giza. Lakini bado hata katika ulimwengu wa dhambi, inawezekana kutembea na Mungu. Huu ni utakatifu.

### Kutembea na Mungu kunahitaji nidhamu-binafsi

Kutembea kwa ukaribu na Mungu kunahitaji nidhamu binafsi ya kuweza kusema hapana kwa matamanio ya dhambi. Kwenye nyakati za giza kabla ya Mafuriko, Henoko "alitembea na Mungu."[24] Henoko alijiweka katika nidhamu mwenyewe ya kusema "Hapana" kwenye majaribu.

Henoko alizungukwa na majaribu yale yale kama majirani zake, lakini mahusiano yake na Mungu yalidhibiti mwitikio wake kwenye mambo ya dhambi. Watu wengine husema, "Raha hii ni nzuri sana, acha niifurahie." Henoko alisema, "Raha hii inaonekana ni nzuri

[23] Yakobo 2:23
[24] Mwanzo 5:24

katika mwili, lakini inaonekana ni uovu kwa Mungu wangu. Sitajeruhi mahusiano yangu na Mungu kwa sababu ya tamaa za kimwili."

"Hatupati" utakatifu kwa kuwa na nidhamu-binafsi. Ni kwa neema ya Mungu pekee inayotufanya tuwe watakatifu. Tumeokolewa kwa neema, na tunafanywa watakatifu kwa neema. Hata hivyo, haimaanishi kwamba nidhamu-bianafsi siyo muhimu.

Dallas Willard aliandika, "neema haipingwi na juhudi, neema hupingwa na tunavyopata."[25] Kutembea kunahusisha juhudi, lakini hata juhudi hiyo huja kama matokeo ya neema ya Mungu. Juhudi zetu haziwezi kutupatia neema ya Mungu; juhudi zetu ni mwitikio wa furaha ya neemayake. Kama watoto wa Mungu hatuupati upendeleo wa Mungu kwa juhudi zetu wenyewe, bali tunatambua hitaji la nidhamu-binafsi.

**Kutembea na Mungu kunahitaji utii**

Mungu alimwita Ibrahhimu kwenda mahali ambapo hajawahi kupaona, "Basi Abramu akaenda, kama Bwana alivyomwamuru..."[26] Ibrahimu alitembea na Mungu katika maisha ya utii. Maisha ya utakatifu ni moyo wenye kutii:

> Kwa Imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.[27]

> "Sheria ya kuyaelewa mambo ya kiroho siyo uwezo wa kufikiri, bali utii."
> - Oswald Chambers

Mungu hakuwa amempa Ibrahimu ramani ya nchi ya Kaanani. Hakumpa Ibrahimu maelezo yeyote ya safari anayotakiwa kwenda. Alimtaka tu Ibrahimu aondoke-na akatii. Kutembea na Mungu kunahitaji utii. Maisha ya utakatifu yanahitaji utii.

**Kutembea na Mungu kunahitaji Imani inayokua**

Wakati Ibrahimu alipoondoka nyumbani hakukuwa na ushahidi wowote wa ahadi za Mungu. Ibrahimu alitembea na Mungu katika maisha ya utakatifu. Tunapokuwa tunatembea na Mungu, tunajifunza kumwamini kabisa. Imani yetu inaongezeka kila tunapoutumia muda wetu na yeye. Hii ilikuwa ni muhimu sana kwa Ibrahimu kwa sababu alikabiliwa na jaribu kubwa zito kuliko lile la kuondoka nyumbani kwake.

Akiwa kule Kaanani, Mungu alimwita Ibrahimu na kumtaka amtoe mwanae Isaka awe dhabihu. Mungu alishamwahidi Ibrahimu kwamba atamfanya awe baba wa mataifa yote. Baada ya miaka mingi, Ibrahimu na Sara wakapata mtoto. Ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu amtoe mtoto wake awe dhabihu ya kuteketezwa. Mwandishi wa Waebrania anasema, "Kwa Imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu."[28]

Kwa kuwa Ibrahimu alitembea na Mungu, alimtegemea Mungu. Ibrahimu alikuwa akitembea na Mungu, kwa hiyo aliweza kumwamini Mungu hata pale alipokuwa hajaelewa

---

[25] Dallas Willard, *Hearing God* (Westmont: InterVarsity Press, 2012), 254
[26] Mwanzo 12:4
[27] Waebrania 11:8
[28] Waebrania 11:17

kwa ukamilifu maagizo ya Mungu. Ibrahimu alitembea na Mungu katika mahusiano ya kukua kwa imani yake.

Kutembea na Mungu kunahitaji kwamba tumwamini yeye. Tunapotembea na Yesu, tunamwamini yeye hata pale tunapokuwa katika maeneo magumu. Tunamruhusu Mungu afanye lile analoliona kwamba ni jema katika maisha yetu.

Kanuni hii inaonekana katika maandiko yote. Katika majaribu yasiyofikirika, Ayubu alijifunza kwamba anaweza kumwamini Mungu. Akiwa uhamishoni, Yeremia alileta ahadi za Mungu za kuleta mema katika maeneo ya mateso makali.[29] Akiwa kwenye maumivu makali yaliyofanyika miiba kwenye mwili wake, Paulo anajifunza neema ya Mungu, "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu."[30]

Historia ya Ibrahimu na taarifa za watu wengine wa Mungu kupitia historia zao zinatufundisha kwamba kutembea na Mungu kunahusisha utii kamili katika maagizo yake na uaminifu kabisa katika amri zake. Kadri tunavyotembea naye, imani yetu kwake inakua zaidi.

**Kutembea na Mungu ni mahusiano yaliyojitenga**

Sura ya kutembea ni ya kawaida sana katika maandiko. Kwa masikitiko, Israeli mara nyingi ilitembea na dhambi badala ya kutembea na Mungu. Wafalme wengi wa Israeli "walitembea katika dhambi." Walijenga mahusiano na dhambi. "Abiya alifanya dhambi zote ambazo baba yake alifanya kabla yake."[31] Wafalme wengine "walitembea katika njia za baba" zao kuliko kutembea na Mungu. Walijenga mahusiano na dhambi; hawakutembea na Mungu.

> "Kama nitatembea na dunia, siwezi nikatembea na Mungu."
> - Dwight L. Moody

Kutembea na Mungu ni mahusiano yaliyojitenga. Mungu ni Mungu mwenye wivu.[32] Huwezi kutembea kwa wakati mmoja na Mungu na wakati huohuo na dhambi. Mtunga Zaburi aliuliza, "Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima chako kitakatifu?" Ni nini mahitaji ya kuishi katika uwepo wa Mungu?

> Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, Wala hakumsengenya jirani yake.[33]

Malaki sema, "Mmemchokesha Bwana kwa maneno yenu," Waisraeli wakauliza, "Tumemchokesha kwa maneno gani?" Malaki akajibu, "Kwa kuwa mwasema, Kila atendaye mabaya ni mwema machoni pa Bwana, naye huwafurahia watu hao,"[34] Wana wa

---

[29] Yeremia 29:10-14
[30] 2 Wakorintho 12:9
[31] 1 Wafalme 15:3
[32] Kutoka 34:14;  Kumbukumbu la Torati 4:24; Yoshua 24:19
[33] Zaburi 15:1-3
[34] Malaki 2:17

Israeli walitaka kuwa marafiki wa Mungu wakati wakiwa wanaendeleana dhambi za makusudi. Badala yake Malaki aliwaonya kwamba siku ya hukumu inakuja, inawaka kama tanuru. Katika siku hiyo, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi.[35] Mungu mtakatifu hawezi kuacha kushughulikia dhambi.

Mungu aliwashutumu wana wa Israeli kwa kutenda dhambi za mataifa badala ya kuishi maisha ya utii kwa amri za Mungu, "kwa maana hamuendi katika amri zangu, wala hamkuzishika hukumu zangu, bali mmetenda mambo kama hukumu za mataifa wanaowazunguka."[36] Wana wa Israeli hawakuweza kutembea na Mungu wakati walikuwa wanatembea katika dhambi. Wana wa Israeli hawakuweza kutembea katika njia za Bwana na wakati huo huo katika njia za dhambi. Ingawaje walikuwa ni taifa lililokuwa limeteuliwa na Mungu, Mungu aliwaadhibu kwa dhambi zao. Haingewezekana kutembea na Mungu na huku wanatembea na dhambi.

**Utakatifu katika matendo: Kutembea na Mungu ni mahusiano endelevu**

Tunapokuwa tunatembea na Mungu, tunakua katika mahusiano yetu na yeye. Katika Kumbukumbu la Torati 6, Musa alitoa picha ya nini maana ya kutembea na Mungu. Alisema kwamba watu wa Israeli wanapaswa kuwafundisha watoto wao sheria. Ni Wakati gani? Wakati wote:

> Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.[37]

Mtu anayetembea na Mungu anadumisha uhusiano usiokatika kati yake na Mungu. Hakuna tofauti kati ya "maisha ya kawaida" na "maisha ya kanisani". Watu watakatifu siyo "Wakristo wa Jumapili tu" ambao wanamtumika Mungu wawapo kanisani tu. Watu watakatifu hutamani kuwa na mahusiano na Mungu yanayoendelea na yanayokua.

Wakati wana wa Israeli waliposhindwa kutunza ukuaji wa kila siku wa mahusiano yao na Mungu, waligeukia kwenye miungu mingine. Wakati mfalme Sulemani alipofanya uzembe katika mahusiano yake na Mungu, alijikuta amevutwa kwenye miungu ya uongo ya wake zake.

Hata Kanisa la mwanzo lilikutana na hatari hii. Kanisa la Efeso lilianzishwa na Paulo kwa uamsho wa kuvutia sana. Mtume Yohana alitumika kama mchungaji wao kwa muda. Mariamu, mama wa Yesu, aliishi Efeso. Walikuwa watu waliotangulia kupata ufahamu wa ukweli kuhusu Injili. Lakini katika kizazi kimoja tu, Yohana akaja na onyo hili:

> Nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza.[38]

[35] Malaki 4:1
[36] Ezekieli 11:12
[37] Kumbukumbu la Torati 6:7
[38] Ufunuo 2:4-5

Ni nini kilichotokea? Kwa sababu walishindwa kutunza hisia zao za upendo wa zamani, na kwa sababu walishindwa kuendelea kukua katika mahusiano yao na Mungu, upendo wao ukawa baridi.

Tunayaona haya katika mahusiano ya wanadamu. Je, unaweza kumfikiria mwanamume aliyemwoa mwanamke mzuri sana, anatundika cheti cha ndoa ukutani, lakini hana muda wa kushirikana naye? Je, ndoa yao hii ina afya? Hapana! Inachukua zaidi ya kuwa na cheti cha ndoa ili kuijenga ndoa yenye afya. Ndoa yenye afya hukua hatua kwa hatua kwa miaka wakati watu hawa wawili wakiendelea kukua katika upendo na mwenzake.

Kwa njia hiyo hiyo, tunaitwa tuendelee kukua katika upendo kwa ajili ya Mungu. Kutembea na Mungu ina maana ya kuendelea kuutumia muda pamoja na yeye. Kutembea na Mungu ina maana yakuendelea kukua katika mahusiano na yeye. Hii ndiyo maana ya kuwa mtakatifu.

Kutembea ni kitendo endelevu. Kinaashiria uhusiano unaoendelea na kukua. Mtu mtakatifu anaendelea kukua katika mahusiano yake na Mungu. Kipindi cha kujisalimisha kwa Yesu siyo mwisho wa njia. Maisha ya utakatifu yanahusisha kuendelea kutembea na Mungu. Kutembea kwetu na Mungu kunaanzia pale tunapozaliwa na kuendelea mpaka kumwona Mungu uso kwa oso. Maisha ya utakatifu ni mahusiano endelevu.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwamba maisha ya kiroho yanategemea kabisa kudumisha mahusiano na yeye mwenyewe:

> Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.[39]

Baadhi ya Wakristo huufikiria uhusiano wao na Mungu kama "Sala ya mwenye dhambi" ikifuatiwa na maisha yaliyobadilishwa kidogo sana. Picha ya Kibiblia ya mahusiano na Mungu iko tofauti. Maisha ya Kikristo yameunganishwa na mzabibu.[40] Maisha yetu ya kiroho yameimarishwa kupitia mahusiano yetu ya kila siku na mzabibu. Ikimaanisha kwamba, tawi lililotenganishwa na mzabibu halichukui muda kufa. Mkristo aliyetenganishwa na mzabibu hufa haraka sana.

Kutembea na Mungu kunatuhitaji tutumie muda wetu na yeye. Haiwezekani ukatembea na mtu ambaye hujatumia muda na yeye. Watakatifu hutumia muda wao na Mungu. Mara nyingine wanasalimisha nafasi za biashara na starehe ili tu waweze kuutumia muda wao na Mungu. Wanaelewa kwamba hakuna jambo la muhimu kama mahusiano yao na Mungu. Kama Mariamu alivyoketi kwenye miguu ya Yesu, kadhalika watu watakatifu wanajua kwamba "jambo moja muhimu" ni muda wao pamoja na Mungu.[41]

---

[39] Yohana 15:4-5
[40] Yohana 15:1-17
[41] Luka 10:41


Watu watakatifu huupa kipaumbele muda wao na Mungu. Wanajua kwamba maombi na maandiko ni muhimu sana kuliko shughuli nyingine zozote-hata kuliko huduma. Hukumbuka kwamba Yesu mara nyingi "alikuwa akiamka mapema sana" kwa ajili ya kumuomba Baba yake, kwa hiyo walijenga tabia ya kutumia muda wao ili kuwa naye katika maombi.

Watu watakatifu wanaelewa kwamba kutembea na Mungu inamaanisha kufuata maelekezo. Wako makini na uongozi wake. Hawaulizi tu kwamba, "Je, shughuli hii ni dhambi?" bali wanauliza "Je, jambo hili litanisogeza karibu na Mungu?" Wanataka wampendezeshe Mungu katika kila uamuzi, kwa sababu wana mioyo mitakatifu na wako makini kuwa mbali na dhambi. Wanaelewa kwamba kuwa na mahusiano na Mungu kunahitaji kutenganishwa na chochote cha kumchukiza yeye.

► Ni njia gani za kivitendo zinazohitajika kukuza uhusiano wa ndani na Mzabibu?

► Kuna changamoto tatu zinazozuia mahusiano yetu na Mungu. Ni zipi?

### Aliipata Siri - Frances Ridley Havergal



Baba yake na Frances Havergal[42] (1836-1879) alikuwa mtumishi katika Kanisa la Uingereza.[43] Akiwa na umri wa miaka 14, Frances aliyatoa maisha yake kwa Kristo. Katika maisha yake yote, Frances aliwekeza nia ya kutembea karibu na Yesu. Aliandika, "Oh, nifanye niwe chombo kilichotakaswa na kilicho tayari kutumiwa na Bwana! Kuna nyakati nyingine ninausikia sana upendo kwa ajili yake kwamba sina maneno ya kuweza kuulezea… lakini bado nahitaji kuwa karibu. Siyo tu kuijua Imani, lakini kuwa pamoja naye ndiyo itakalowezesha hili." Kwa kutembea na Mungu, alikuwa karibu sana na yeye.

Mwaka 1873, Havergal alishuhudia kwamba "ametakaswa na dhambi zake zote na kufanywa mtakatifu kutokana na utakaso endelevu wa Roho wa Mungu." Hakuna kilichoweza kumzuia katika kutembea kwake na Mungu. Maombi yake ya kujitoa kwa ajili ya Mungu ndio ukawa wimbo wake, "Chukua maisha yangu na uniweke wakfu Bwana, kwa ajili yako wewe."

Havergal alisalimisha kila kitu kwa Mungu. Hii ndio maana ya kutembea na Mungu. Ni kuwa karibu sana na yeye kiasi kwamba kila kitu ni mali yake. Baada ya kitambo kirefu cha maisha ya kutembea na Mungu, maneno ya mwisho ya Harvegal yalikuwa, "Uzuri, utukufu wa kuwa karibu na malango ya mbinguni! Pumziko la Baraka!" Kaka yake aliandika kwamba uso wake, "ulikuwa na furaha sana, kana kwamba alikuwa anazungumza na yeye (Yesu)."

[42] Image: "Frances Ridley Havergal", Christmas Sunshine with Love and Light for the New Year (1886), retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Frances_Ridley_Havergal.jpg, public domain.
[43] Kisa hiki cha Frances Havergal kimenukuliwa kutoka Wesley L. Duewel, *Heroes of the Holy Life* (Grand Rapids: Zondervan, 2002), 80-89.

Dada Havergal alitembea na Mungu; alikuwa mtu mtakatifu. Kutembea na Mungu siyo kwa watu walioishi katika nyakati za Biblia tu. Unaweza kutembea na Yesu leo; unaweza kuwa mtakatifu.

**Chukua maisha yangu na ifanyike hivyo – Frances Havegal**

Chukua maisha yangu na uniweke wakfu Bwana, kwa ajili yako wewe.
Chukua nyakati na siku zangu – zifurike bila kikomo na sifa isiyoisha.

Chukua mikono yangu na uaichie itembee kwa upendo wa Bwana,
Chukua miguu yangu na uifanye iwe miepesi na mizuri kwa ajili ya Bwana

Chukua sauti yangu na uniwezeshe niweze kuimba kwa mfalme wangu tu.
Chukua mdomo wangu - na uujaze ujumbe kutoka kwa Bwana.

Chukua shaba na dhahabu yangu— hata kitu kidogo sitaweza kuzuia
Chukua akili zangu na tumia kwa uwezo wote kama Bwana utakavyoamua.

Chukua mapenzi yangu na uyafanye yako mwenyewe— hayatakuwa yangu tena.
Chukua moyo wangu, na nafsi yangu mwenyewe—viwe vyako katika ufalme wako

Chukua upendo wangu, Bwana wangu, ninaumimina miguuni pako kwenye hazina yako
Nichukue mimi mwenyewe, nitakuwa wako na kwa ajili yako tu.

## Tafakuri ya Somo la 2

(1) Kuwa mtakatifu ina maana ya kudumisha mahusiano na Mungu. Utakatifu ni kutembea na Mungu.

(2) Kutembea na Mungu kunahitaji nidhamu ya kibinafsi ya kusema "hapana: kwa ajili ya tamaa mbaya.

(3) Nidhamu ya binafsi haikatai nguvu ya neema. Tunaokolewa kwa neema, tunafanywa watakatifu kwa neema.

(4) Kutembea na Mungu kunahitaji uaminifu kamili katika amri za Mungu. Hatuwezi kutembea na Mungu pamoja dhambi kwa wakati mmoja.

(5) Kutembea na Mungu kunahitaji utii kamili kwenye ahadi za Mungu.

(6) Kutembea na Mungu inamaanisha kujenga uthabiti wa kila siku wa mahusiano na Mungu.

(7) Maisha ya utakatifu yanahitaji mahusiano ya kila siku na mzabibu. Maisha yetu ya kiroho yanategemea kabisa uhusiano wetu na Mungu.

## Kazi ya Kufanya

(1) Fikiria kwamba Mwamini mpya Mkristo anakuambia, "Nataka niwe na mahusiano ya ndani sana na Mungu. Nampenda Mungu, lakini ni vigumu kwangu kukua kwenye mahusiano na yeye. Siwezi kumwona Mungu kwa sababu inaonekana anakaa mbali sana. Nifanye nini?" Andika ukurasa mmoja juu ya jinsi utakavyoweza kumsaidia huyu mwamini mpya kuelewa jinsi ya kukua katika mahusiano yake na Mungu. Kwenye kipindi cha darasa kinachofuata, kila mwanafunzi asome majibu yake na kuwepo na muda wakuyajadili haya majibu.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu 1 Yohana 1:6-7.

# Somo la 3
# Utakatifu ni Sura ya Mungu ndani ya Mtu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kutambua vyema mpango wa Mungu wa kurejesha sura ya Mungu kwa mwanadamu.

(2) Kufahamu utaratibu anaoutumia Mungu katika kurejesha sura yake ndani ya mwanadamu.

(3) Aruhusu Mungu autimize mpango wake wa kila siku wa mabadiliko ili kufikia sura na Mfano wake.

(4) Kukariri 2 Wakorintho 3:17-18.

## Musa: Mwanamume wa sura ya kung'aa

Ilikuwa ni siku kubwa kwa maisha ya Musa.[44] Alikuwa amekulia katika kasri la mfalme Farao. Alikuwa amekutana na watu wenye nguvu sana duniani. Lakini leo, Musa anakutana na mtu mwingine mwenye nguvu kuliko Farao. Anakutana na Yehova, Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo

Musa alikuwa amezungumza na Mungu katika kichaka kinachowaka moto. Aliwahi kumwona Mungu akiliangamiza jeshi lote la Farao katika Bahari ya Shamu. Musa anaenda kumwona Mungu kwa ukaribu zaidi kuliko kwenye kichaka kinachowaka moto au Bahari ya Shamu.

Leo, Musa alikuwa mbele ya uwepo wa Yehova. Musa alikuwa na ombi moja tu, "Nionyeshe utukufu wako." Mungu alimwambia Musa kwamba hiyo kamwe haiwezekani. "Huwezi ukauona uso wangu, kwa sababu mwanadamu akiniona uso wangu atakufa." Lakini Mngu akampa Musa upendeleo mwingine:

> Bwana akasema, "Tazama, hapa pana mahali karibu nami, nawe utasimama juu ya mwamba; kisha itakuwa wakati unapopita utukufu wangu, nitakutia katika ufa wa ule mwamba, na kukufunika kwa mkono wangu hata nitakapokuwa nimekwisha kupita; nami nitaondoa mkono wangu, nawe utaniona nyuma yangu, bali uso wangu hautaonekana."[45]

---

[44] Kutoka 33:17-23
[45] Kutoka 33:21-23

Musa alikuwa ameona sehemu ndogo tu ya utukufu wa Mungu, lakini aliporejea kambini, uso wake ulikuwa unang’aa. Kila wakati Musa alipokuwa mbele ya uwepo wa Mungu, “ngozi ya uso wake Musa iling'aa; naye Musa akautia utaji juu ya uso wake tena, hata alipoingia kusema naye.”[46] Uso wa Musa uliakisi utukufu wa Mungu. Musa akawa mtu mwenye uso wa kung’aa.

Tuliumbwa katika sura na mfano wa Mungu; tuliumbwa ili tuudhihirishe utukufu wa Mungu. Ingawaje dhambi iliharibu sura ya Mungu ndani ya mwanadamu, Mungu anatafuta sana kuirejesha sura yake ndani ya kila mwamini. Kuwa watakatifu ni kuwa kama alivyo Baba yetu wa mbinguni. Kusudi la Mungu ni kurejesha sura yake kwa watu wake.

## Utakatifu ni Sura ya Mungu ndani ya Mwanadamu

► Fikiria juu ya Mkristo anayeonesha utakatifu na kuwa mfano kwa wengine. Ni tabia gani za Baba yetu wa Mbinguni unazoweza kuziona katika maisha ya huyu mtu?

Vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia vinaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu, na anawataka watu wake wawe watakatifu. Tulitakiwa tufanane na Baba yetu wa mbinguni; tuliumbwa tuwe watakatifu. Lengo la Mungu ni kuwafanya watoto wake wawe katika sura yake.

Kuwa katika sura ya mtu fulani, inamaanisha kufanana na huyo mtu. Tuliumbwa katika sura ya Mungu. Kama vile kioo kinavyoakisi sura ya mtu, tuliumbwa ili tuakisi sura ya Mungu. Hii haimaanishi kwamba Mungu ana uso unaofanana na sisi; bali roho zetu zilifanywa kamilifu katika asili ya Mungu. Tuliumbwa tuwe mfano wa sura ya Mungu. Kama vile kioo kinavyoakisi sura ya mtu, nasi tumeumbwa ili tuakisi sura ya Mungu.

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

“Bwana, ifanye roho yangu
ikufananie wewe,
inga’e kama wewe peke yako
ndani yangu,
ili watu waweze kuuona upendo
wako na neema yako…”
- Blanche Mary Kelly

Tuliumbwa tuwe wasafi sana na watakatifu kama Mungu alivyo msafi sana na mtakatifu. **Kuwa mtakatifu ina maana ya kuakisi Sura ya Mungu.** Mungu anawaamuru watu wake, “Mtakuwa watakatifu.” Kwa nini? “Kwa kuwa mimi ni mtakatifu. Mtafanana na mimi.”[47] Tumeumbwa ili tuwe watakatifu; tuliumbwa ili tufanane na Baba yetu wa mbinguni.

### Tumeumbwa katika Sura ya Mungu

Kilele cha historia ya uumbaji kilikuwa pale uumbaji wa mwanadamu ulipotimizwa “kwa kufanywa katika mfano wa Mungu.”[48] Vyote alivyoumba Mungu vilikuwa vizuri, lakini

[46] Kutoka 34:35
[47] Mambo ya Walawi 11:45; 1 Petro 1:16
[48] Mwanzo 1:27

mwanadamu peke yake aliumbwa kwa sura ya Mungu. Mungu alimwumba Mwanadamu ili afanane na yeye mwenyewe. Mungu "akamvalisha taji la utukufu na heshima."[49]

Mwanadamu ana uthamani usioisha kwa sababu ameumbwa kwa sura ya Mungu. Paulo anaandika, "kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu."[50] Tuliumbwa kuakisi utukufu wa Mungu.

**Sura ya Mungu ndani ya mwanadamu iliharibiwa na anguko la dhambi**

Dhambi iliharibu kabisa sura ya Mungu ndani ya mwanadamu. Katika Mwanzo 1, mwanadamu aliumbwa "kwa Mfano wa Mungu;" Katika Mwanzo 6, "kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani."[51] Mwanadamu alijiondoa mapema kwenye mpango wa Mungu kiasi kwamba "kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote."[52]

Utukufu aliokuwa amepewa mwanadamu wakati wa uumbaji ulibadilika ukawa aibu. Paulo anaweka bayana kile kilichomfanya mwanadamu alichopoteza kutokana na kumuasi Mungu na kugeukia miungu mingine. Kutokana na anguko, wanadamu "wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu…" matokeo yake, Mungu:

- Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao na unajisi.
- Aliwaacha katika hisia zao kali zisizoweza kuwaletea heshima.
- Aliwaacha na ufahamu pungufu.[53]

Yote haya ni matokeo ya anguko. Kwa sababu ya dhambi utukufu wa Mungu ulifanyika kuwa ni aibu kabisa. Sura ya Mungu iliharibiwa; mwanadamu hakufanana tena na Muumba wake.

**Sura ya Mungu inarejeshwa ndani ya watu wake**

Hata hivyo, Mungu hakumwacha mwanadamu mwenyewe. Dhabihu zilikuwa ni njia ya kuthibitisha adhabu ya dhambi na kurejesha mahusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Lakini kusudi la Mungu linaenda mbali zaidi kuliko kulipa adhabu ya dhambi zetu. Mungu anatafuta kumfanya mwanadamu awe mtakatifu kama yeye alivyo matakatifu.

Kusudi la Mungu ni kuturejesha katika sura yake.[54] Sura yake ikisharejea ndani yetu, aibu ya dhambi inafutwa na kwa mara nyingine tena tunauonesha utukufu wa Mungu. Hii ndiyo mojawapo ya dhamira kuu ya Biblia:

---

[49] Psalm 8:5
[50] 1 Wakorintho 11:7
[51] Mwanzo 6:12
[52] Mwanzo 6:5
[53] Warumi 1:23-28
[54] Warumi 8:29

- Tulifanywa katika sura ya Mungu (Mwanzo 1-2)
- Kupitia dhambi, sura ya Mungu kwa mwanadamu iliharibiwa (Mwanzo 3)
- Kuanza na ahadi ya Masihi katika Mwanzo 3:15 na kilele kitakapofikia mbinguni, Mungu anarejesha sura yake kwa mwanadamu.

Yohana aliahidi kwamba kama tutakaa ndani yake, "tuwe na ujasiri, wala tusiaibike mbele zake katika kuja kwake."[55] Tutakapokuwa tunabadilishwa katika sura yake, tunaurejesha tena utukufu uliokuwa umepotea kwenye anguko la dhambi. Aibu yetu imefutwa, na tunangojea ujio wake kwa matumaini. Tutakapoendelea kukua katika sura ya Mungu tunafanywa watakatifu. Kama Mungu alivyo mtakatifu, watu wake pia wanafanywa kuwa watakatifu.

**Israeli walitakiwa kudhihirisha Sura ya Mungu**

Mungu aliwaita Israeli kuwa watu watakatifu. Kusudi lake lilikuwa kurejesha sura yake kwa Israeli. Mungu aliwateua Israeli kama mwakilishi wake maalumu kwa mataifa mengine. Aliwatenga Israeli kama wateule wake ambao wangeuonesha utakatifu wake kwa mataifa mengine.

Mungu aliwaita Israeli kuwa "ufalme wa makuhani." "Nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu."[56] Jukumu la kuhani lilikuwa ni kumwakilisha Mungu kwa watu. Kazi maalumu kwa Israeli ilikua kumwakilisha Mungu kwenye mataifa yote. Mungu aliwaita Israeli kudhihirisha asili ya utakatifu wake kwa mataifa mengine. Ili kufanikisha umisheni huo, Israeli alipaswa awe mtakatifu.

Wakati Israeli ilipokuwa mwaminifu kwa Mungu, ilidhihirisha asili ya utakatifu wa Mungu; alifanyika kioo cha Mungu cha utakatifu. Wakati Israeli ilipogeukia miungu, ilidhihirisha asili ya dhambi ya miungu, na alifanyika kioo cha dhambi kwa miungu. Wakati Israeli iliposhindwa kufanana na Mungu, alishindwa katika umisheni wake kwa ulimwengu.

**Kanisa linatakiwa kudhihirisha Sura ya Mungu**

Katika Agano Jipya, Kanisa linaitwa liwe watu wa Mungu watakatifu. Kanisa linaitwa kuwa "ukuhani wa kifalme" unaomwakilisha Mungu kwa ulimwengu.

> Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.[57]

Kama vile Mungu alivyoichagua Isreli kuonesha sura yake kwa mataifa, vivyo hivyo ameliteua Kanisa "kuwaeleza wengine jinsi Mungu alivyowaita kutoka katika dhambi kuingia kwenye nuru yake kuu." Mungu alilichagua Kanisa kuwakilisha asili yake kwa wale

[55] 1 Yohana 2:28
[56] Kutoka 19:6
[57] 1 Petro 2:9

ambao walikuwa hawajamjua. Kufanya hivyo, Kanisa lazima lidhihirishe sura ya Mungu. Kukamilisha umisheni huu, kanisa ni lazima liwe takatifu.


Wakati Kanisa linapokuwa mwaminifu kwa Mungu; linawakilisha asili ya utakatifu ya Mungu. Wakati kanisa linapogeukia miungu ya umaarufu, utajiri, nguvu na mengineyo, linafanana na miungu hiyo; na linadhihirisha asili ya dhambi ya miungu hiyo batili. Kanisa linaposhindwa kufanana na Mungu, limeshindwa pia katika umisheni wake kwa ulimwengu.

**Sura ya Mungu ni kurejeshwa tena kwa kila mwamini**

Tuliumbwa tufanane na Baba yetu wa mbinguni. Tuliumbwa katika sura ya Mungu, lakini sura hii iliharibiwa wakati wa anguko la dhambi. Sura ya Mungu bado iko pale,[58] lakini bado imefichwa na dhambi.

Jaribu kufikiria mtu anayechimba kitu kule China kisha akakuta kitu cha kale cha thamani kubwa. Mwanzoni, hakitaonekana na uzuri wowote kwani kitakuwa kimefunikwa kwa udongo na matope. Mtu mwingine anayekiangalia anaweza kusema, "Kitupe mbali, hakina thamani yeyote!" Lakini mtu mjuzi anajua kwamba chini ya huo uchafu kuna tunu nzuri sana.

Sura ya Mungu kwa mwanadamu iliharibiwa na anguko la dhambi. Sura ya Mungu ilifunikwa na udongo na tope la dhambi, lakini Mungu anafanya urejesho wa sura yake kwetu. "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake..."[59] Kama vile Yesu alivyofanana na Baba yake, tunapaswa kufanana na Mungu wetu. Utakatifu ni "mfano wa Mungu"; utakatifu ni urejesho wa sura ya Mungu kwa mwanadamu.



Michelangelo, mchongaji wa kinyago kilichoitwa *Pieta*[60] ni mmoja wa watu maarufu sana wa Sanaa ya uchongaji nchini Italia. Mwaka 1972, mwanamume mmoja kichaa alichukua nyundo akavunja kinyago chake. Wachongaji walichukua miezi kadhaa kukifanyia marekebisho kwenye uharibifu uliofanyika. Kwa sababu kinyango hicho kilikuwa cha thamani sana, walifanya kazi kwa uangalifu mkubwa ili kukirudisha katika sura yake ya awali. Leo hii, huwezi ukaona mahali popote palipoharibika katika kinyago hicho. Mchongaji alirejesha *Pieta* katika uzuri wake wa asili.

[58] Mwanzo 9:6
[59] Warumi 8:29
[60] Image: "Michelangelo's Pieta 5450 cut out black" taken by Stanislav Traykov on December 4, 2005, edited by Niabot, retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Michelangelo%27s_Pieta_5450_cut_out_black.jpg, licensed under CC BY 2.5, desaturated from the original.

Kwenye anguko, dhambi ilichafua sana uumbaji mkuu wa Mungu. Dhambi iliharibu sura ya Mungu kwa mwanadamu. Kwa kuwa mwanadamu ni wa thamani sana kwa Mungu, alianza kurejesha sura yake ndani yetu. Kuanzia wakati wa anguko hadi sasa, Mungu amekuwa akifanya kazi kwa neema yake kurejesha wanadamu kwenye uzuri wetu wa asili. Kusudi la Mungu ni kuturejesha katika uzuri wa sura yake.

Wetu wengi sana wana uelewa usiokamilika kuhusu Injili. Mtazamo wao kuhusiana na Injili ni:

1. Nilikuwa mwenye dhambi.
2. Mungu akaniokoa.
3. Sasa ninaweza kwenda mbinguni.

Hizi ni habari njema – lakini siyo Injili yote. Habari njema za Injili zinatambua kusudi la Mungu la umilele:

1. Nilikuwa mtenda dhambi.
2. Mungu akaniokoa.
3. Sasa Mungu anarejesha sura yake ndani yangu.
4. Mbinguni, "nitakuwa kama yeye, kwa sababu nitamwona kama alivyo."[61] Kusudi la Mungu kwa watu wake litakuwa limetimia.

Je, hii haishangazi? Mungu amekuokoa wewe *ili uwe kama yeye.* Huu ndiyo uzuri wa maisha ya utakatifu. Kama watakatifu, tunarejeshwa kwenye sura ya Mungu.

> "Ushahidi unaovuma sana wa Roho Mtakatifu katika maisha ya mtu ni ule uwazi wa usio na mashaka wa mfanano wa kifamilia na Yesu, na uhuru kutoka kwa kila kitu ambacho hakifanani na yeye."
> - Oswald Chambers

Mungu aliwaokoa wana wa Israeli kutoka Misri ili kwamba aweze kuishi pamoja nao katika mahusiano ya upendo. Mungu hakuwakomboa wana wa Israeli ili waje waishi kama Wakanaani. Aliwaweka huru ili waweze kuwa kama yeye.

Kwa njia hiyo hiyo, tumeokolewa tuishi katika uhusiano wa karibu sana na Mungu na tubadilishwe kabisa katika sura yake. Mungu alituokoa katika dhambi zetu ili tuweze kuwa watakatifu kama yeye alivyo mtakatifu. Tuliumbwa tuudhihirishe utukufu wake.

### Utakatifu katika Matendo - Utakatifu na Hulka za Watu

Watu wengine wanaamini kwamba mtu mtakatifu atakuwa na aina fulani ya tabia na hisia zake. Fikiria nyuma kwenye majibu yako ya mwanzo wa somo hili: "Fikiria juu ya Mkristo anayeonesha utakatifu na kuwa mfano kwa wengine. Ni tabia gani za Baba yetu wa Mbinguni unazoweza kuziona katika maisha ya huyu mtu?" Je, umezielezea kimsingi katika tabia au hisia za mtu? Mara nyingi tunafanya!

[61] 1 Yohana 3:2

Hata hivyo, tunaposoma vitabu vya Agano Jipya, tunaona kwamba aina zote za hulka za watu ziliwakilishwa wakati wa Pentekoste. Watu wa aina mbalimbali walijazwa na nguvu za Roho. Baada ya Pentekoste, wanafunzi hawakubadilika ghafla kuwa watu wa aina nyingine. Badala yake, Mungu alifanya kazi nao kupitia tabia na hisia zao za asili kufanikisha malengo yake kwa njia mpya.

Tomaso hakufanyika mara moja mtu mwenye ufahamu na mwenye matumaini. Hadi kufikia kifo chake, Tomaso labda alikuwa mkimya na wa kujifkiria. Simoni Petro hakuwa kwa ghafla mtu mpole akikaa bila kujulikana na watu kwenye kona. Hata baada ya Pentekoste, Petro alikuwa mmojawapo aliyesema kwa kujiamini, "Hasha, Bwana!"[62]

Mungu alimuumba kila mmoja wetu na hulka ya kipekee. Utakaso hauharibu hizi hulka. Badala yake, jinsi sisi wenyewe tunavyojisalimisha kwa Mungu, sura yake inazidi kung'aa ndani yetu kupitia hulka zetu.

**Je, inawezekana Sura ya Mungu ikang'ara kupitia Hulka zetu?**

Hii itaonekanaje katika maisha ya kila siku? Mtu "A" mshindani. Mchangamfu ambaye amejisalimisha kabisa kwa Mungu ataendelea kuwa na tabia na hisia za mtu "A". Mtu mwenye aibu anayeepuka makundi ya watu ataendelea kuwa kuwa na aibu. Hata hivyo, katika hali zote mbili, mtu alitetakaswa humruhusu Mungu "kusakafia maeneo korofi" ya tabia na hisia zake pale inapoonekana kuna maeneo ambayo hayaakisi sura ya Mungu.

Nitatoa mfano: Wachungaji Greg na Mark walikuwa wenye tabia na hisia zenye nguvu sana. Wote walikuwa na msimamo imara. Wote walikuwa "wasemaji" wazuri waliokuwa na uwezo wa kushindana kwa hoja. Wote walikuwa katika nafasi za uongozi. Kwa sababu ya msimamo wao imara, wote mara nyingine waliweza kulaumiana kwa maneno yao.

Nilimjua Mchungaji Greg alipokuwa anakaribia mwisho wa maisha yake. Aliniambia, "Huwa siombi msamaha. Haijalishi watu wanafikiria nini katika yale ninayoyasema. Ni makosa yao kama wakishindwa kunielewa. Ninajua moyo wangu uko sahihi!" Ingawaje moyo wa Greg ungeweza kuwa wa kweli, watu katika makanisa aliyokuwa akihudumia walikuwa mara nyingi wanaumizwa na maneno yake. Alikuwa hajaweza kujifunza kwa ukamilifu jinsi ya kuachilia sura ya Mungu ing'are kwenye tabia na hisia zake.

Mchungaji Mark pia alikuwa kiongozi mwenye nguvu. Hata hivyo Mchungaji Mark alijifunza inamaanisha nini kuakisi sura ya Mungu. Alijifunza kusema, "Samahani. Nimezungumza kwa hisia kali sana." Alijifunza kuonesha huruma na kutenda haki. Wafuasi wake walikuwa wanasema, "Mchungaji wetu alitutendea kama Yesu."

Utakatifu haubadilishi aina yako ya tabia na hisia; Utakatifu unakufanya uwe msikivu kwa sauti ya Roho Mtakatifu wakati anaposema, "Unahitajika kuomba msamaha. Ulikuwa na hisia kali sana."

---

[62] Matendo ya Mitume 11:8

Kama una tabia na hisia ya kuepuka macho ya watu hadharani, utakatifu haukufanyi ugeuke uwe mchangamfu unayependa kujitokeza mbele ya watu. Hata hivyo, utakatifu unakufanya uwe tayari kuweka pembeni mashaka yako anaposema, "Ninakutaka utoke ukaongoze katika mazingira haya."

Everett Cattell anatoa mifano mitatu kuonyesha ni kwa jinsi gani Shetani anapenda kupindisha mwelekeo wetu wa asili katika kupiga vita sura ya Mungu katika maisha yetu.[63]

**Mfano wa 1: Kula**

Njaa ni hamu ya asili. Inawezekana kula "kwa ajili ya utukufu wa Mungu."[64] Hakuna hata mmoja atakayetafuta uzoefu wa kiroho wa kuharibu njaa.

Kwa watu wengi, hata hivyo, Shetani ameharibu hii hamu ya asili kuifanya ulafi. Badala ya kula ili kutosheleza hitaji la kawaida na la asili, kula kumekuwa ni njia ya kufurahisha tamaa za binafsi.

Suluhisho la kuzuia hivi vita siyo kuondoa kabisa hamu ya kula. Suluhisho ni kujithibiti mwenyewe kunakozuia hamu ya asili isipindishwe kuwa kitu kingine cha hatari na hata cha dhambi.

**Mfano wa 2: Wepesi katika kuhisi:**

Everett Cattell anatoa tena mfano mwingine mgumu zaidi. Mtu yeyote mwenye mhemuko wa kawaida ana kiwango fulani cha wepesi wa kuhisi maumivu au mateso. Hii ni kawaida na siyo dhambi. Hata hivyo, kama tutaruhusu huu wepesi wa kuhisi ukue kufikia kiwango cha kujihurumia kupita kiasi, inakuwa ni tabia ya kujifikira mwenyewe tu ambayo inazuia uwezo wetu wa kumtumika Mungu kikamilifu na kuakisi sura ya Mungu kwa wengine.

Hapa tena, suluhisho siyo kuondoa mihemuko ya kawaida au wepesi wa kuhisi na kukosa huruma kwa maneno na vitendo vya watu wengine. Badala yake, tunapaswa tujifunze kusalimisha huu wepesi wa kuhisi kwa Mungu na tumruhusu aongoze na kutawala mwitikio wetu kwa mambo yanayoumiza.

**Mfano wa 3: Ulimi:**

Inawezekana huu ni mfano mgumu zaidi. Sisi sote ni lazima tutumie ulimi. Hatuwezi kuomba, "Mungu, nakuomba ng'oa ulimi wangu." Hata hivyo, ulimi hauwezi kuruhusiwa utoke nje ya kujitawala.

Cattell anatoa mfano wa mmishenari aliyekuwa mara kwa mara sahihi katika maoni yake, lakini akiumiza wengine kwa hisia zake kali. Kwenye maisha ya mabadiliko ya kiroho,

---

[63] Everett L. Cattell, *The Spirit of Holiness* (Newberg: Barclay Press, 2015), 30-35

[64] 1 Wakorintho 10:31

alisema maneno ya kuwaumiza watu wake aliowahudumia. Usiku ule, Mungu akamwonesha yule mmishenari kwamba ana makosa ya ulimi wake kuumiza watu wengine.

Mmishenari aliomba kisha akaenda kwenye mkusanyiko wa asubuhi. Akawaambia watu kwenye ule mkusanyiko, "Kama tatizo langu lingehusiana na pombe, ingekuwa rahisi sana kwangu. Ningeachana nayo kabisa na tatizo lingeisha. Lakini tatizo langu kubwa ni ulimi wangu. Siwezi nikaukata nikautupa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Lakini nimeukabidhi ulimi wangu kwa Mungu, ninaamini kwamba Roho Mtakatifu atanisaidia niutumie kwa ajili ya utukufu wake."

Mchungaji Cattell anaonyesha makosa mawili yanayofanana na ya ulimi:

1. Kusema kwamba, "Mimi ni mwenye dhambi lakini siwezi kuutawala ulimi wangu. Nitaendelea kutenda dhambi, kwa sababu neema ya Mungu haina uwezo wa kuondoa tatizo langu."
2. Kusema kwamba, "Nimeomba ili Mungu anifanye mimi kuwa mtakatifu. Kwa hiyo, atautawala ulimi wangu. Sihitajiki kufanya lolote kujiweka katika nidhamu mwenyewe. Nitamwamini Mungu tu.

Tabia iliyo sahihi inasema, "Nimeusalimisha moyo wangu –na ulimi wangu – kwa Bwana. Moyo wangu ni msafi, lakini natambua kwamba napaswa kutiisha matumizi ya ulimi wangu. Nitachukua muda kufikiri kabla kabla ya kuongea. Nitachukua muda wa kuomba kwanza kabla ya kuongea. Na kama ninazungumza sana, nitajishusha mwenyewe na kutubu." Mtu mtakatifu atakuwa mwepesi kumwendea mtu aliyemkwaza au kumkosea kwa toba ya unyenyekevu.[65]

► Ni sehemu gani yenye hatari kwako? Fikiria tamaa za asili zinazoweza kukuingiza kwenye mitazamo na tabia za dhambi. Toa mfano ni kwa jinsi gani hii hamu mara nyingine imekusababishia matatizo. Kisha toa mfano wa jinsi Mungu alivyokusaidia katika kutiisha hamu hii.

### Je, ni kwa jinsi gani Mungu hutengeneza tabia na hisia za mtu mtakatifu?

Tunapotafuta kuakisi sura ya Mungu katika maisha yetu, Mungu hufanya kazi kwa njia nyingi kututengeneza tuwe watu anaotaka yeye. Kama mwana akiolojia atafutaye sanamu za zamani kule China, na kwa uangalifu mkubwa akakipaka polishi hadi kikang'aa, Mungu kwa utaratibu huwapaka watoto wake polishi hadi wakang'aa na kudhihirisha sura yake.

Ni njia gani Mungu hutumia katika kuwatengeneza watu wake kurejea katika sura yake? Mwanzoni mwa somo hili, tuliona ni kwa jinsi gani Musa aliakisi sura ya Mungu.

[65] Mathayo 5:23-24

Tunapoangalia maisha ya Musa, kunatupa vielelezo vya jinsi Mungu anavyotutengeneza sisi katika sura yake.

Mwanzoni mwa maisha yake, Musa hakuwa anaakisi sura ya Mungu kila wakati. Hasira yake ilimfanya akaua mtu, na hii ikatishia kumweka nje kabisa kwa ajili ya kutumika kwenye ufalme wa Mungu.[66] Hata hivyo, Mungu alimtengeneza Musa katika hali ya kuwa, "mnyenyekevu zaidi kuliko watu wote waliokuwa chini ya uso wa dunia."[67] Musa alikuwa mwepesi kukata tamaa,[68] lakini Mungu alimtengeneza kuwa mtu mwaminifu wa kuwaongoza watu wake kwa miaka arobaini jangwani. Je, ni kwa jinsi gani Mungu alibadilisha tabia ya Musa?

***(1) Mungu hutumia neno lake kutengeneza watoto wake kuwa katika sura yake***.

Moja ya kifaa muhimu sana anachokitumia Mungu ni Neno lake. Tuanapoliweka Neno la Mungu ndani ya mioyo yetu, hulitumia katika kutuongoza.[69] Kitendo cha Musa kupokea sheria za Mungu moja kwa moja kutoka mikononi mwa Mungu, kulitengeneza uelewa wake na tabia yake.

Watu watakatifu ni watu wa duniani. Wanajua katika Neno la Mungu wataiona asili ya Mungu. Wanajua kwamba kwenye Neno la Mungu watajifunza jinsi ambavyo tabia zao zitaakisi tabia ya Mungu. Simjui Mkristo yeyote maarufu katika historia ambaye hajawahi kuwa mwanafunzi wa dunia.

***(2) Mungu hutumia mazingira magumu kuwatengeneza watoto wake katika sura yake***.

Kwa sababu ya mauaji ya Mmisri, Musa alitumia miaka arobaini jangwani. Mara nyingi, alikuwa anaweza kufikiria, "Nimepoteza nafasi yangu. Siwezi nikafanya jambo lolote la ziada zaidi ya kuchunga kondoo." Lakini Mungu aliitumia miaka ile arobaini katika kumtengeneza Musa awe kiongozi.

Moja kati ya aya zinazotia moyo katika maisha ya mtume Petro ni wakati Yesu alipotabiri kuhusu anguko lake wakati wa mateso yake. Yesu alimwonya Petro, "Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano;…" Akamtia moyo, "lakini nimekuombea wewe ili Imani yako isitindike." Kisha baadaye, akaahidi kwamba kutokana na anguko la kushindwa kwa Petro (kwa muda), Mungu atafanya jambo jema. "Nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako."[70] Mungu alitumia hata mazingira ya uharibifu ya kushindwa kwa Petro kumfanya awe wa kufaa zaidi.

---

[66] Kutoka 2:11-15
[67] Hesabu 12:3
[68] Kutoka 5:22-23
[69] Zaburi 119:9-11
[70] Luka 22:31-32

Watu watakatifu huamini utoaji wa Mungu katika nyakati za matatizo. Wanaamini katika Warumi 8:28 kwa sababu wanataka waiishi Warumi 8:29. Mungu anaahidi, "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake." Kisha, anatuambia sisi "kusudi" la Mungu ni kuleta ndani yetu maisha ya mtoto wake: "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake."

Siyo kila jambo linalofanyika kwa mtu mtakatifu ni jema! Lakini yote yanayotendeka "hufanya kazi pamoja" katika kutimiza kusudi la Mungu – kututengeneza katika sura ya Mwana wake.

***(3) Mungu hutumia watu kutengeneza watoto wake kwa sura yake***.

Hii inaweza kuwa ni ngumu zaidi katika zote tatu. Mungu hutumia watu – mara nyingi watu wenye matatizo - ili kututengeneza sisi kuwa katika sura yake. Wakati Musa alipokuwa karibu kuvunjika moyo kutokana na majukumu mazito ya uongozi aliyokuwa nayo, Mungu alimtumia baba mkwe Yethro (ambaye hata hakuwa Mwisraeli) kumpa Musa ushauri uliomfanya awajibike kwa ufanisi zaidi.[71]

Tunaweza kumwangalia tena Simoni Petro. Kupitia kukutana kwake na Yohana, na baadaye kupitia makabiliano yake na Paulo, Petro alitengenezwa zaidi na zaidi katika Sura ya Mungu. Paulo "alikabiliana naye uso kwa uso" kutokana na Petro kushindwa kuishi kwenye mafundisho aliyokuwa amefundishwa na Roho Mtakatifu kuhusu kula pamoja na mataifa.[72] Akiwa ni mtume aliyemtangulia, hii ilitosha kumfanya Petro ajisikie kufedheheshwa sana. Alikuwa anamfuata Kristo wakati Paulo alikuwa bado anawauwa Wakristo! Lakini Petro aliruhusu Mungu aendelee kufanya kazi ndani yake ili kumleta karibu na kile ambacho Mungu alikuwa amemkusudia Petro awe.

Watu watakatifu huruhusu Mungu kufanya kazi kupitia watu wengine ili kutengeneza tabia zao katika Sura ya Mungu. Mithali anasema, "Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake."[73] Sehemu ya makali ya shoka hupata makali yake kutokana na kunolewa na chuma kingine. Kwa njia hiyo hiyo, watu wanapokutana na watu wengine, ustadi wao unanolewa zaidi.

Maisha ya utakatifu ni zaidi ya kipindi kimoja cha mgogoro. Ni maisha ya kubadilishwa kila siku katika sura ya Mungu. Kila tunapojikabidhi kwa kazi ya Bwana katika maisha yetu, anatutengeneza hatua kwa hatua katika sura yake. Haya ni maisha ya vitendo ya utakatifu.

---

[71] Kutoka 18:1-27
[72] Wagalatia 2:11
[73] Mithali 27:17

## Aliipata Siri - Frank Crossley

Moyo wa utakatifu haujawekwa kwa ajili ya wachungaji na wamishenari. Mungu anataka ambadilishe kila Mkristo katika sura yake. Frank Crossley alionesha sura ya Mungu katika maisha ya kawaida sana. Frank Crossley hakuwa mwalimu; alikuwa mmiliki wa injini za Crossley. Hakuishi kwenye pango lililofichwa na majaribu: aliishi Manchester, katika jiji kubwa la viwanda.

Frank Crossley alikuwa mfanya biashara tajiri mkubwa Uingerza katika karne ya 19. Mara tu baada ya kuokoka kwake, Crossley alimsikia msichana mdogo akiimba kutoka Jeshi la Wokovu akishudia kuhusiana na nguvu ya kubadilisha ya Roho Mtakatu. Crossley akamwambia mke wake, "Ninataka nimfahamu Mungu kama yule msichana anavyomjua Mungu." Alirudi usiku unaofuata na akaanza kutafuta moyo safi.

Baada ya Mungu kutakasa moyo wake kupitia Imani, Crossley alitaka kufanya zaidi kuliko kutafuta fedha. Aliamua kuwa mhubiri. Aliwasiliana na Jenerali William Booth wa Jeshi la Wokovu, lakini Booth kwa hekima alimshauri Bwana Crossley aendelee na kazi yake ya biashara. Jenereali Booth aliamini kwamba Frank Crossley angekuwa wa ufanisi zaidi katika kumtumikia Mungu kupitia biashara zake.

Bwana Crossley aliuliza, "Ninawezaje kuonyesha sura ya Mungu katika maisha yangu? Ni kwa jinsi gani Yesu anaweza kuwatendea wafanyakazi wangu?" Alihamishia kiwanda chake kwenye eneo lililokuwa maskini sana la jiji ili kuwasaidia wahitaji. Aliwachukulia wafanyakazi wake kama ndugu zake wa Kikristo.

Frank Crossley alidhihirisha moyo wa utakatifu kupitia tabia iliyomfanania Kristo. Siku hadi siku, bwana Crossley aliiakisi sura ya Mungu katika kuhudumia watu wengine. Wakati fulani mfanyabiashara mpinzani akakutana na Bwana Crossley kuhusiana na mkataba mgumu. Baadaye alisema, "Bwana Crossley alinitendea kama ambavyo Yesu Kristo angefanya." Mfanyabiashara mwenzake aliiona Sura ya Mungu ndani ya Frank Crossley.

Kwa Frank Crossley, swali muhimu sana kwake halikuwa, "Nitawezaje kupata fedha zaidi?" Swali muhimu sana alilokuwa nalo ni, "Je, ninafanana na baba yangu wa Mbinguni?" Kwa sababu ya hiyo, Bwana Crossley aliudhihirisha uso wa Mungu kwa wale waliokuwa wamemzunguka. Huu ndio utakatifu.

## Oh! Kwa ajili ya kumsifu Mungu wangu - Charles Wesley

Oh! kwa ajili ya kumsifu Mungu wangu, moyo kutoka dhambini umewekwa huru.
Moyo ambao unaihisi damu yake ikimwagwa bure kwa ajili yangu.

Moyo uliokubali, mnyenyekevu, mpole, kiti cha enzi cha mkombozi wangu mkuu,
Mahali ambapo Kristo peke yake husikika akisema, mahali ambapo Kristo peke yake anatawala.

Moyo, mnyenyekevu, ulioshuka, uliopondeka, unaoamini, mkweli na msafi,
Ambapo aidha uhai au kifo haviwezi kuutengana na Kristo ambaye anakaa ndani yake.

Moyo katika fikra zote uliofanywa upya na uliojaa upendo wa Mungu.
**Uliokamilika na sahihi na safi na nzuri — nakili, Bwana, wa nafsi yako mwenyewe.**

## Tafakuri ya Somo la 3

(1) Kuwa mtakatifu inamaanisha kuakisi sura ya Mungu.

(2) Sura ya Mungu kwa wanadamu iliharibiwa katika anguko.

(3) Mojawapo ya dhamira kuu ya Biblia ni kurejesha sura ya Mungu kwa mwanadamu.

(4) Kusudi la Mungu la umilele ni kuturejesha katika sura yake

(5) Wakati Israel ilipokuwa mwaminifu kwa Mungu, ilionyesha sura yake kwa mataifa.

(6) Kanisa tunapokuwa na uaminifu kwa Mungu, tunaudhirisha uso wa Mungu kwa ulimwengu unaotuzunguka.

(7) Sura ya Mungu ndani yetu imeharibiwa na dhambi. Hata hivyo, Mungu anafanya kazi ndani ya kila mwamini ili kutufanya tufanane naye zaidi na zaidi.

(8) Habari njema za Injili ni kwamba:

- Nilikuwa mwenye dhambi.
- Mungu akaniokoa.
- Sasa ninaweza kwenda mbinguni.
- Mbinguni, nitafanana na yeye kwa sababu nitamwona kama alivyo.

(9) Mungu yuko kazini akiwatengeneza watoto wake katika sura yake. Bila kujali tabia na hisia zetu, anataka kujidhihirisha mwenyewe kwetu. Mungu hulitumia neno lake, mazingira ya maisha, na watu wengine katika kututengeneza katika sura yake.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Andika insha ya kurasa 2-3 yenye kichwa cha habari: "Sura ya Mungu ndani yangu." Jibu mawali manne:

- Kama watu wa familia yangu wakiniangalia, je, wataiona sura ya Mungu ndani yangu?
- Watu wa familia yangu wataona nini watakapoona kwamba hakuna kinachofanana na sura ya Mungu ndani yangu?
- Ni hatua gani tatu za vitendo nitakazoweza kuchukua ili kuakisi sura ya Mungu katika maisha yangu?
- Ni mazingira gani au watu ambao Mungu huwatumia kunitengeneza katika sura yake kwa sasa hivi?

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu 2 Wakorintho 3:17-18.

# Somo la 4
# Utakatifu ni Kutengwa

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Atambue umuhimu wa kila Mkristo kutengwa kutoka kwenye dhambi.

(2) Afahamu faida kubwa iliyopo katika kutengwa kwa ajili ya Mungu.

(3) Aweze kukuza kanuni za kivitendo za ufahamu wa kibiblia za kutengwa.

(4) Kukariri 2 Wakorintho 6:16-18.

## Musa: Mwanamume aliyesimama katika Ardhi Takatifu

Alipokuwa akichunga kondoo jangwani, Musa aliona kijiti kilichokuwa kinawaka lakini hakiteketei. Wakati Musa alipokuwa akisogea karibu na eneo hili la ajabu, alimsikia Mungu akiita, "Musa, Musa!" Musa akasema, "Mimi hapa." Mungu akamwonya, "Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu."[74]

Katika ulimwengu wa zamani, kutembea miguu mitupu kuliwakilisha unyenyekevu na heshima kuu. Hakuna mtu ambaye angeweza kuvaa kanda mbili mbele ya Farao. Musa alikuwa mbele ya aliyekuwa mkuu kuliko Farao. Alikuwa mbele ya Mungu mwenye mamlaka yote. Musa alikuwa kwenye nchi takatifu.

Kulikuwa na kitu gani maalumu kuhusiana na eneo alilosimama Musa? Nini kilipafanya pawe patakatifu? Je, kulikuwa na uzio uliokuwa umebandikwa ishara ya "Nchi Takatifu"? Hapana. Kuna mtu yeyote aliyeandaa sherehe za kidini kuashiria kwamba nchi hiyo ni takatifu? Hapana.

Ardhi hiyo ilikuwa takatifu **kwa sababu** tu ni mali ya Mungu. Mungu alikitenganisha kipande hiki cha ardhi kutoka katika eneo lote la jangwa na kutangaza kuwa ni takatifu; Mungu "aliitakasa" hiyo ardhi. Hii inatoa kielelezo muhimu sana kuhusiana na utakatifu. Ardhi hii ilikuwa takatifu kwa sababu Mungu aliitenga. Kile kilichokuwa kitakatifu kiliwekwa pembeni, kikatengwa na Mungu.

> **Sala kwa ajili ya Utakatifu**
>
> "Mungu mwenye nguvu zote,
> Umetuweka sisi kwa ajili yako
> mwenyewe, na mioyo yetu
> haitapumzika hadi ipate
> pumziko kutoka kwako.
> Tupe usafi wa moyo na nguvu
> za kusudi lako, na kwamba
> hakuna hisia za binafsi
> zitakazotuzuia kuyajua
> mapenzi yako, na hakuna
> madhaifu yatakayotuzuia
> kuyafanya."
>
> - Augustine wa Hippo

[74] Kutoka 3:5

Miaka mingi baadaye, Mungu akakutana na Musa kwenye mlima Sinai. Hapa tena, Mungu akaweka pembeni kipande cha ardhi kama kitakatifu. Musa aliwaambia watu wakae mbali na ule mlima. Hawakutakiwa kuukwea mlima huo au kugusa chochote kilichokuwa karibu kwa sababu ulikuwa takatifu. Uwepo wa Mungu mlimani ulikuwa na nguvu sana hata ikabidi Musa awaonye watu kwamba yeyote atakayeugusa mlima ule "atauawa."[75] Mlima ni mali ya Mungu. Musa alisimama kwenye nchi takatifu.

## Utakatifu ni Kutengwa

Utakatifu ni tabia ya Mungu. Katika maandiko, neno "utakatifu" linarejea kwamba ni Mungu au chochote ambacho ni mali ya Mungu. Katika kisa cha cha Musa na kichaka kilichowaka moto, ardhi ilikuwa takatifu kwa sababu ilikuwa ni mali ya Mungu. **Kuwa mtakatifu inamaanisha kutengwa kwa ajili ya Mungu.** Mifano mingi kutoka katika vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia inaonyesha kwamba vitu "vitakatifu" hutengwa pembeni na vitu vingine vya kawaida.

### Siku takatifu

Kwa mara kwanza neno "utakatifu" kuonekana kwenye Biblia halikuwa limemrejelea kwa mtu bali siku. Katika mwisho wa siku sita za uumbaji. Mungu aliitenga siku ya saba pembeni na zile siku sita.

> Kwahiyo Mungu akaitakasa siku ya saba na kuifanya takatifu, kwa sababu katika hiyo Mungu alipumzika kutokana na kazi zote alizozifanya wakati wa uumbaji.[76]

Siku ya saba ilikuwa takatifu kwa sababu ilitengwa kwa ajili ya Mungu; haikuwa ya kawaida tena. Isaya alisema Sabato ilitengwa kutoka katika siku nyingine zote. Siku hii siyo kwa ajili ya "njia zenu wenyewe" au "anasa zenu wenyewe"; ni mali ya Mungu.[77] Sabato ilitengwa na Mungu kwa ajili ya kuabudu.

Uaminifu wa Isareli kwa ajili ya Sabato ulionyesha uaminifu wake kwa Mungu. Mungu aliyeitenga Sabato pia aliitenga Israeli.

> Bwana akasema na Musa, na kumwambia, "Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Hakika mtazishika Sabato zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana niwatakasaye ninyi.'"[78]

Kuwa mtakatifu ni kutengwa **na** Mungu na kwa **ajili** ya Mungu. Mungu aliitakasa Sabato; Mungu anawatakasa watu wake.

---

[75] Kutoka 19:12
[76] Mwanzo 2:3
[77] Isaya 58:13
[78] Kutoka 31:12-13

## Vitu vitakatifu

Kipande cha ardhi kilichotengwa pembeni kutoka katika ardhi nyingine kilikuwa kitakatifu; ni mali ya Mungu. Siku iliyokuwa imetengwa pembeni kutoka katika siku nyingine ilikuwa takatifu; ni mali ya Mungu. Chochote kinachotengwa kwa ajili ya Mungu kilikuwa kitakatifu.

**Mavazi** waliyokuwa wanavaa makuhani yalikuwa matakatifu.[79] Yalikuwa yanatengenezwa kwa maelekezo maalumu kutoka kwa Mungu na yalikuwa mali yake. **Sadaka** ambazo watu walizileta kwenye hema la kuabudia zilikuwa takatifu; zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya Mungu.[80] Makuhani walitumia mafuta maalumu wakati wa kuabudu. Mungu aliamuru, "Haya yatakuwa ni **mafuta** matakatifu **ya kutiwa** kwa ajili yangu mimi katika vizazi vyenu vyote."[81] Hakuna mtu mwingine yeyote ambaye angeweza kutumia mafuta haya; yalikuwa yametengwa pembeni kwa ajili ya matumizi ya Mungu.

Utoaji kwa ajili ya hema la kuabudia, Mungu alitaka kila mtu wa Israeli alipe kodi iliyoitwa "**shekel ya mahali patakatifu**."[82] Fedha hii haikutumika kwa matumizi ya kawaida. Wasomi wengi wanaamini kwamba hii ilikuwa ni sarafu nyingine tofauti kabisa na shekali ya kawaida. Ilikuwa takatifu; ilikuwa mali ya Mungu.

**Vitu vya samani** katika hekalu la kuabudia vilikuwa vitakatifu. Mungu alimwamuru Musa kutenganisha hizi samani kutoka katika vitu vingine vyote. "Nawe utavitakasa vitu hivyo, ili viwe vitakatifu sana; tena kila kivigusacho vyombo vile kitakuwa kitakatifu."[83]

Kila kitu kilikuwa aidha kitakatifu au cha kawaida.[84] Kuwa kawaida haikumaanisha kwamba kinahusika na dhambi; bali ilimaanisha kwamba hakikuwa kimetengwa pembeni kwa ajili ya matumizi ya Mungu. Kuna uwezekano wa mambo matatu yaliyoeleweka kwa Israeli kuhusiana na kila kitu:

1. **Kichafu** – hakuna ambaye angeweza kukitumia. Kilikuwa ni marufuku kwa wana wa Mungu.
2. **Kisafi** – Kilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
3. **Kitakatifu** – Kilichotengwa pembeni kwa ajili ya matumizi ya Mungu tu. Kilikuwa kinatumika *tu* kwenye ibada ya Mungu.

[79] Kutoka 28:2
[80] Kutoka 28:38
[81] Kutoka 30:31
[82] Kutoka 30:13, 24; 38:24-26; Mambo ya Walawi 5:15; 27:3, 25; Hesabu 3:47, 50; 7:13
[83] Kutoka 30:29
[84] Tafsiri nyingi hutumia neno "vya ulimwengu" badala ya "vya kawaida" kwenye vitu. Toleo la KJV linatumia "visivyo vitakatifu." Katika maneno yote hakuna linaloonyesha "kuwepo na dhambi." Maneno haya kiuhalisia yanamaanisha kwamba hicho chombo "hakijatengwa" kwa ajili ya matumizi ya mambo ya utakatifu.

Kabla Israeli haijaingia katika nchi ya Kaanani, Mungu alitoa maelekezo kwa ajili ya kupanda miti.

1. Kwa miaka mitatu ya kwanza, matunda yake "mmenyimwa" msiyatumie. Ni **"machafu"** kwa ibada.
2. "Katika mwaka wa nne matunda yake yote yatakuwa ni matakatifu, kwa ajili ya kumpa Bwana shukrani." Matunda ya mwaka wa nne yalitengwa pembeni na Mungu kwa ajili ya matumizi yake. Yalikuwa **"matakatifu"**
3. Kuanzia mwaka wa tano, "mtakula katika matunda yake." Miti sasa ni **"misafi"** kwa ajili ya matumizi yake.[85]

**Maeneo Matakatifu**

Hema ya kukutania ilikuwa takatifu kwa sababu ilikuwa imetengwa pembeni na Mungu. Kila kitu kwenye hema ya kukutania kilikuwa kimetengwa kwa matumizi ya Mungu. Sehemu ambayo Mungu alikuwa akikutana na kuhani mkuu paliitwa Mahali Patakatifu Pa-patakatifu.

Baadaye, hekalu la Yerusalemu lilikuwa takatifu kwa sababu lilitengwa maalumu kwa ajili ya kumwabudia Mungu. Hekalu lilikuwa takatifu tu kwa sababu ni mali ya Mungu. Kwa sababu ya dhambi ya Israeli, Ezekieli aliona maono ya utukufu wa Mungu ukiondoka katika Hekalu.[86]

Baada ya utukufu wa Mungu kuondoka, hekalu halikuwa takatifu tena. Mwaka 63 KK, Jenerali wa Kirumi aitwaye Pompey aliingia Patakatifu Pa-Patakatifu akakuta pako wazi hakuna chochote. Kwa sababu Mungu hakuwa akiishi tena pale, hekaluni.

**Kabila Takatifu**

Kabila la Walawi lilitengwa maalumu na Mungu. Katika usiku ambao Israeli walikuwa bado hawajaondoka, kila mzaliwa wa kwanza katika kila Mmisri aliuawa. Wazaliwa wa kwanza wa Israeli waliokolewa kwa sababu walitii amri ya Mungu ya kunyunyiza damu juu ya miimo ya milango ya kila nyumba.

Israeli ilikumbuka ukombozi wao kutoka Misri kwa njia mbili. Kwanza, kila familia ya Mwisraeli ilishiriki "Chakula cha Pasaka" kila mwaka. Chakula hiki kilisherehesha ukombozi wa Israeli kutoka Misri

Njia ya pili ambayo Israeli inakumbuka ukombozi wao ni ya kuvutia zaidi. Kuwakumbukusha Israeli kwamba amewakomboa wazaliwa wao wa kwanza wote, Mungu aliamrisha:

[85] Mambo ya Walawi 19:23-25
[86] Ezekieli 10

> Nitakasie mimi wazaliwa wa kwanza wote. Kila afunguaye tumbo katika wana wa Israeli, wa binadamu na wa mnyama; ni wangu huyo.[87]

Neno "nitakasie" linatokana na neno la Kiebrania "takasa" au "iliyotengwa pembeni." Kila mzaliwa wa kwanza ni mali ya Mungu. Mungu alilichagua kabila la Walawi kuwakilisha wazaliwa wa kwanza wa Israeli yote. Kabila hili lilitumika badala ya taifa lote.

> Mimi, tazama, nimewatwaa Walawi na kuwatoa kati ya wana wa Israeli badala ya wazaliwa wa kwanza wote wafunguao tumbo katika wana wa Israeli; na hao Walawi watakuwa wangu; kwa kuwa hao wazaliwa wa kwanza wote ni wangu; katika siku ile niliyowapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri nikajiwekea wakfu wazaliwa wa kwanza wote wa Israeli, wa wanadamu na wa wanyama; Watakuwa wangu; Mimi ndimi BWANA.[88]

Katika kitabu cha Kutoka 29, Mungu aliagiza jinsi ya kutakasa makuhani. Jina "utakatifu" linatumika mara tisa katika sura hii. Walawi walitakaswa mahali pa wazaliwa wote wa kwanza; kabila lote lilikuwa ni mali ya Mungu kabisa.

► Kwa nini ilikuwa ni muhimu sana Mungu aweke msisitizo katika ujumbe wa kutengwa kwa Israeli? Kwa nini Paulo awekee msisitizo ujumbe huu kwa makanisa katika Korintho (2 Wakorintho 6:14-7:1) na Thesalonike (1 Wathesalonike 4-5)? Kwa nini ujumbe huu ni muhimu hadi leo?

Mifano hii (siku takatifu, maeneo takatifu, n.k.) inaonyesha kwamba kuwa mtakatifu ni kutengwa kwa ajili ya Mungu. Hii inatusaidia tuelewe maana ya maisha ya utakatifu kwa sasa. Mtu mtakatifu moja kwa moja ni wa Mungu. Ametengwa kwa ajili ya makusudi ya Mungu. Kuwa mtakatifu ni kutengwa kutoka ***katika dhambi*** na kutengwa ***kwa ajili ya Mungu*****.**

## Kuwa Mtakatifu ni kutengwa kutoka katika dhambi

Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, watu wake ni lazima wawe watakatifu. Watu wenye dhambi hawawezi wakawa na mahusiano na Mungu aliye mtakatifu. Watu watakatifu hujitenga wenyewe na chochote kinachomchukiza Mungu.

### Mungu Mtakatifu anachukia dhambi

***(1) Mungu aliudhihirisha utakatifu wake katika gharika***.

Dunia iliyoumbwa na Mungu ilikuwa "nzuri sana," lakini dhambi ikauharibu uumbaji. Mungu alipomwangalia mwanadamu, aliouna uovu ndani ya moyo wake.

---

[87] Kutoka 13:2
[88] Hesabu 3:12-13

> Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote. Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo.[89]

Nuhu na familia yake waliokolewa kwa sababu waliishi maisha ya utakatifu. "Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu."[90] Alibakia akiwa ametengwa kutoka katika dhambi.

***(2) Mungu alidhihirisha utakatifu wake kwenye maamuzi yake juu ya Nadabu na Abihu***.

Watoto wakubwa wa Haruni walitengwa kwa ajili ya huduma kwa Mungu. Walipokiuka utakatifu wa hema ya kuabudia, "moto ukatoka hapo mbele za Bwana, nao ukawala, nao wakafa mbele za Bwana."[91] Kitabu cha Mambo ya Walawi hakikuelezea kumbukumbu za ndani kuhusu dhambi ya Nadabu na Abihu, lakini Mungu alisema, "Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote."[92] Makuhani wa Mungu wanapaswa kuitendea hema ya kuabudia kama takatifu. Nadabu na Abihu walifikiri wangeweza kuutendea utakatifu kama yalivyo mambo mengine ya kawaida.

***(3) Mungu alidhihirisha utakatifu wake kwenye maamuzi yake juu ya Musa na Haruni***.

Musa na Haruni hawakuingizwa katika Nchi ya Ahadi kwa sababu "hamkuniamini mimi, (Mungu) kama mtakatifu ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa Israeli."[93] Baada ya Mungu kumwamrisha Musa auambie mwamba utoe maji, Musa aliupiga mwamba. Mungu alimhukumu Musa kwa sababu hakumheshimu Mungu kabla ya watu.

Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kupuuzia dhambi. Mara kumi katika vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia, dhambi inaitwa "machukizo mno kwa Mungu," Jambo ambalo Mungu anachukia. Mungu mtakatifu anachukia dhambi.

**Watu Watakatifu wanachukia dhambi**

Mungu ni wa utakatifu na Mungu ni wa upendo. Dhambi ya mwanadamu ilisababisha tatizo kubwa. Ni kwa jinsi gani Mungu aliye mtakatifu anaweza kujenga mahusiano na mwanadamu mtenda dhambi? Ni kwa namna gani anaweza kuuonyesha upendo wake kwa mwanadamu na kuwa mkweli kwa utakatifu wake kwa wakati mmoja?

---

[89] Kutoka 6:5-6
[90] Mwanzo 6:9
[91] Mambo ya Walawi 10:2
[92] Mambo ya Walawi 10:3
[93] Hesabu 20:12

> "Yesu alikufa, siyo kuwapatanisha watu na dhambi, bali kuwakomboa kutoka dhambini."
> - R.E. Howard

Mungu alitoa Sheria yake kuwasaidia watu wake waweze kuishi kama watu watakatifu. Sheria haikutolewa ili kuyafanya maisha yawe magumu kwetu; ilitolewa ili itusaidie kuishi kwenye mahusiano sahihi na Mungu. Sheria iliwapa watu mfumo wa kuweza kujitenga na dhambi. Watu watakatifu wataichukia dhambi sawa na Mungu mtakatifu anavyoichukia dhambi.

Waandishi wa Agano Jipya walifundisha kwamba kujitenga kwa ajili ya Mungu kunahitaji kujitenga na dhambi. Yakobo alisema, "Hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu."[94] Haiwezekani ukawa rafiki wa Mungu na wa dhambi kwa wakati mmoja. Haiwezekani ukatembea na Mungu pamoja na dhambi kwa wakati mmoja. Maisha ya utakatifu yanahitaji kujitenga na dhambi.

Paulo aliandika kwa watu waliofikiri kwamba neema ya Mungu kwao inawaruhusu kuendelea katika kuikumbatia dhambi. Aliuliza, "Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema?"[95] Jibu la Paulo lilikuwa la kukazia sana, "Hasha! Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii?" Kuna chaguo la mambo mawili tu:

1. Kama utajitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi, mwisho wake ni kifo.
2. Kama utajitoa mwenyewe kwa Mungu, mwisho wake ni kuhesabiwa haki.[96]

Huwezi ukajitoa mwenyewe kwenye dhambi na kwa Mungu kwa wakati mmoja. Wakristo "baada ya kuwekwa huru mbali na dhambi, wamekuwa watumwa wa haki."[97] Kama watoto wa Mungu, tunapaswa tutengwe na dhambi.

Paulo aliyaweka haya katika maneno ya vitendo kuonyesha wajibu wetu wa kuepukana na dhambi za kujitakia. "Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa."[98]

Haiwezekani kuimarisha urafiki na dhambi wakati huo huo ukiishi na Mungu. Kutengwa kwa ajili ya Mungu, kunahitaji kutengwa kutokana na dhambi. Hatuwezi tukaendeleza urafiki na Mungu na dhambi kwa wakati mmoja. Baada ya Adamu na Hawa, kutenda dhambi, walijificha wenyewe kutoka katika uso wa Mungu kwenye miti iliyokuwa kwenye bustani hiyo.[99] Kuunganika na dhambi kumesababisha kutengwa mbali na Mungu.

---

[94] Yakobo 4:4
[95] Warumi 6:15
[96] Warumi 6:16
[97] Warumi 6:18
[98] Warumi 6:19
[99] Mwanzo 3:8

Wokovu hautufanyi tuwe huru katika kuendelea kutenda dhambi. Wokovu umetuweka huru na dhambi ili tuweze kuwa watakatifu. Lengo la wokovu ni kuwaleta watu wa Mungu kwenye utakatifu. Lengo la Mungu ni kututoa katika dhambi na kututenga kwa ajili ya mahusiano na yeye mwenyewe.[100]

Nilikuwa ninasafiri sehemu ya mlimani huko Taiwan. Mbele ya barabara kulikuwa na mwamba uliomeguka kwenda hadi chini sana kwenye mto. Unadhani niliweza kumwuliza dereva anionyeshe wakati anaendesha gari  na kwamba anaweza kuusogelea ule mwamba kwa ukaribu kiasi gani? Hapana! Nilikuwa nataka nikae mbali sana itakavyowezekana na mwamba huo. Vivyo hivyo, mtu mtakatifu hujiweka mbali na dhambi. Katika kila eneo la maisha, mtu mtakatifu huepuka kila aina ya mtindo wa maisha ya dhambi. Mtu mtakatifu anakaa mbali sana na dhambi na anakaa karibu sana na Mungu.

Mtume Petro analiweka jambo hili kama ifuatavyo: "ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu." Sisi tutafanyaje? Kwa kuishi maisha matakatifu. "Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. Muwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa."[101] Maisha ya utakatifu ya wana wa Mungu ni alama ya kumilikiwa. Watu watakatifu hukaa mbali na dhambi kwa sababu ni wa "milki yake mwenyewe," watu ambao ni mali ya Mungu. Mtu mtakatifu anataka awe mali ya Mungu kabisa.

Paulo aliwakumbusha watu wa Korintho kwamba "wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu." Anaorodhesha msururu wa baadhi ya watu ambao hawaturith: "Waasherati, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi hawataurithi ufalme wa Mungu." Kisha anawakumbusha, "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii" Wakristo wa kule Korintho walikuwa wamekulia katika mazingira ya maovu na walikuwa wamefanya matendo mengi ya dhambi.

Lakini Paulo anakataa kuwaacha Wakristo katika hali ile. Hajasema, "Sasa ninyi ni Wakristo – mnaoweza kuendelea kuwa waasherati, waabudu sanamu, wazinzi, wafiraji, walawiti, wevi, watamanio, walevi, watukanaji, wanyang'anyi na kadhalika." Badala yake, Paulo anasema. "**lakini mlioshwa**, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."[102]

Paulo anafurahia, "Hamko tena kama mlivyokuwa! Hamfungwi tena na zile dhambi. Mmetengwa kwenye dhambi na sasa ninyi ni mali ya Mungu." Kuwa mtakatifu ni kutengwa na dhambi ili tuweze kutengwa kwa ajiliya Mungu.

---

[100] John N. Oswalt, *Called to Be Holy: A Biblical Perspective* (Nappanee: Evangel Publishing House, 1999), 33
[101] 1 Petro 2:9-12
[102] 1 Wakorintho 6:9-11

## Kuwa mtakatifu ni kutengwa kwa ajili ya Mungu

Uzia alikuwa mfalme mzuri ambaye "alifanya yaliyo ya adili machoni pa Bwana… Akajitia nia amtafute Mungu… Mungu akamsaidia juu ya Wafilisti."[103] Uzia alifanikiwa kisiasa. Alilipanua eneo la utawala la Yuda na akaikomboa ardhi iliyokuwa imechukuliwa wakati wa utawala wa wafalme dhaifu. "Umaarufu wa jina lake ukaenea mpaka kuingia Misri; kwa kuwa aliongezeka nguvu mno."[104]

Uzia alikuwa mfalme mwenye nguvu sana, lakini kisa chake kilikuwa na mwisho mbaya. "Lakini alipokuwa na nguvu, moyo wake ulitukuka, hata akafanya maovu, akamwasi Bwana, Mungu wake."[105]

Ni nini kilicholeta hukumu kwa Uzia? Mfalme aliingia hekaluni kufukiza uvumba kwenye madhabahu. Alikiuka agizo la kutenganisha vitu vya kawaida na vile vitakatifu. Matokeo yake, Uzia alikuwa na "ukoma hata siku ya kufa kwake, na akiwa mkoma akawekwa katika nyumba ya pekee, kwa kuwa ni mwenye ukoma; maana alitengwa na nyumba ya Bwana."[106]

Mfalme Uzia hakuua, hakuiba, au hakufanya uzinzi. Hakuaudu sanamu au hakwenda kwa waganga. Uzia alitenda dhambi kwa kukiuka sheria ya Mungu ya kutenganisha. Kwa majivuno yake, mfalme Uzia aligusa madhahabu takatifu. "Akawa na majivuno… Hakuwa mwaminifu kwa Bwana Mungu wake."

Katika majivuno yake, mfalme Uzia alikiuka utakatifu wa hekalu. Sheria ilifundisha watu wa Mungu kwamba wanapaswa kujitenga na dhambi, ili waweze kuishi katika mahusiano sahihi na Mungu. Maisha matakatifu ni **Kutengwa kwa ajili ya Mungu.**

Vitabu vya historia vya Biblia, vinaelezea mifano ya watu na vitu vilivyokuwa vimetengwa kwa ajili ya Mungu. Kama ambavyo alifanya kwenye kichaka kilichokuwa kinawaka moto, Mungu alitenga sehemu ya **ardhi** iwe takatifu. "Amiri wa jeshi la Bwana alimwambia Yoshua, 'Vua viatu vyako miguuni mwako; kwa kuwa mahali hapo usimamapo ni patakatifu.'"[107]

Wakati Israeli walipoishambulia Yeriko, Mungu aliwaamuru waharibu kila kitu kilichokuwa "kimewekwa wakfu kwa Bwana kwa ajili ya uharibifu…. Lakini fedha yote, na dhahabu, na **vyombo** vya shaba, na chuma, ni vitakatifu kwa Bwana; vitaletwa katika hazina ya Bwana."[108] Kule Yeriko, vitu vyote hivi havikuwa takatifu; lakini vilikuwa takatifu tu wakati Bwana alipovitaka kwa ajili yake mwenyewe.

---

[103] 2 Mambo ya Nyakati 26:4-7
[104] 2 Mambo ya Nyakati 26:8
[105] 2 Mambo ya Nyakati 26:16
[106] 2 Mambo ya Nyakati 26:21
[107] Yoshua 5:15
[108] Yoshua 6:17, 19

Daudi aliwaamuru **Walawi**, "Jitakaseni, ninyi na ndugu zenu, ili mlipandishe sanduku la Bwana, Mungu wa Israeli, mpaka mahali pale nilipoliwekea tayari."[109] Kabla ya kulibeba Sanduku la Agano kulirudisha Yerusalemu, Walawi walijitoa wenyewe kwa ajili ya makusudi ya Mungu.

Kujitenga kutokana na dhambi siyo lengo la mwisho kwa watu watakatifu. Israeli ilikuwa imechaguliwa **kutoka miongoni** mwa mataifa maovu yaliyokuwa yameizunguka ili liweze kutengwa kwa **ajili ya Mungu** na kuwa milki yake.[110] Wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu, Sulemani aliomba. "Kwa maana uliwatenga na watu wote wa dunia, **wawe urithi wako**, kama ulivyonena kwa mdomo wa Musa, mtumishi wako, hapo ulipowatoa baba zetu katika Misri, Ee Bwana MUNGU."[111] Mungu aliitenga Israeli kutoka mataifa mengine ili iwe mali yake. Israeli ilikuwa na heshima ya kuwa "urithi" wa Mungu.

Akiwaonya Wakorintho kuhusiana kuwa na mahusiano na Mataifa, Paulo alimnukuu Isaya: "'Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao,' asema Bwana, 'Msiguse kitu kilicho kichafu.'"[112] Nikiwa kijana Mkristo, Ninakumbuka kusikia mahubiri kuhusu utakatifu na kutengwa yakimalizia na aya hii. Wahubiri wakiwahusia watu wa Mungu kwa kusema "jitengeni na mambo machafu."

Ujumbe wa kutengwa mara nyingi ulikuwa hasi (kinyume). Hata hivyo, aya inaendelea na ahadi nzuri sana! Tumetengwa kutoka kwenye dhambi ili kwamba tuweze kutengwa kwa ajili ya Mungu. Paulo anaendelea na ahadi kwamba; "Nitawakaribisha, Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi."


Kutengwa kutokana na chochote kile kichafu hakutunyang'anyi furaha yetu. Badala yake, tumetengwa kutoka dhambini **ili tuweze kuwa na furaha ya kutembea na Mungu.** Wakristo tunatengwa kutoka katika dhambi ili tuweze kuwa mali ya Mungu kikamilifu. Watu watakatifu kwa furaha hukaa mbali na dhambi kwa sababu wanajua kwamba kutengwa kutoka dhambini kunatoa fursa ya wao kutembea katika mahusiano ya ndani na Baba wa mbinguni.

Kanuni hii inaweza kuonekana katika sheria za chakula na mavazi. Kwa nini Mungu alisema, "Msile aina ya vyakula hivi" au "Msivae aina hizi za mavazi"? Sheria hizi zilikuwa ni mafundisho yaliyokusudiwa kuwafundisha Israeli kwamba ilikuwa ni lazima itengwe kwa ajili ya Mungu. Sheria hizi zilikua ni alama kwamba Israeli kama taifa ni mali ya Mungu. Mungu alisema kwa Israeli, "ulikuwa wa thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda."[113] Mawazo gani haya ya kufikirika! Israeli haikutengwa

[109] 1 Mambo ya Nyakati 15:12
[110] Mambo ya Walawi 20:26 na Kutoka 19:5
[111] 1 Wafalme 8:53
[112] 2 Wakorintho 6:17-18
[113] Isaya 43:4

kwa ajili ya Mungu kama adhabu; bali alitengwa kwa ajili ya heshima na upendo. Ilikuwa ni tunu kwake kuliko makabila yote ya watu.[114]

Wazo hili linaonekana katika kielezo cha hema ya kuabudia. Wale ambao kwa mujibu wa kawaida za dini walikuwa siyo wasafi walikaa "nje ya kambi." Wale ambao kwa mujibu wa kawaida za dini walikuwa safi walikaa "ndani ya Kambi." Katikati ya eneo la kambi, makuhani walikuwa wakitoa dhabihu "ndani ya hema ya kuabudia." Kuhani mkuu ndiye peke yake aliyeingia Patakatifu pa Patakatifu. Mpangilio huu uliwapa watu kumbukumbu ya kuona kiuhalisia jinsi kutengwa **kutoka katika dhambi** kunapotoa fursa ya sisi kutengwa kwa **ajili ya Mungu**. Hii iliwaonyesha watu ni nini maana ya kuwa karibu na uwepo wa utakatifu wa Mungu.




D = Nje ya Kambi (Siyo wasafi)
C = Ndani ya Kambi (Wasafi)
B = Hema ya kuabudia (Makuhani)
A = Patakatifu pa Patakatifu (Kuhani Mkuu)

Kwa jinsi ambavyo watu walikuwa wanafuata sheria za kutengwa, walijifunza kwamba ni lazima kuwa watakatifu katika kila eneo la maisha. Mungu anayo mamlaka juu ya maisha yote.

> "Hakuna lolote katika maisha yetu ambalo halina umuhimu wa kina kwa Mungu."
> - Oswald Chambers

Mambo ya Walawi 17-26 inaitwa "Kanuni ya Utakatifu." Kanuni ya Utakatifu iliifundisha Israeli jinsi ya kuishi kama taifa takatifu. Kutoka kwenye kila kitu kidogo hadi kwenye kanuni kubwa, hizi sheria zilipewa nguvu na utakatifu wa Mungu. Ziliwaonesha Israeli ni kwa jinsi gani wanaweza kuwa watakatifu katika ulimwengu wa dhambi. Israeli walifundishwa jinsi ya kutengwa kutoka katika dhambi. Kwa umuhimu zaidi, zilifundisha jinsi Israeli itakavyoweza kutengwa kwa ajili ya Mungu wao, "Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, niliyewatoa katika nchi ya Misri."[115]

Katika Mambo ya Walawi 20, Mungu alisema, "Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu mimi; kwa kuwa mimi Bwana ni mtakatifu nami nimewatenga ninyi na mataifa, ili kwamba mwe wangu."[116] "Nimewatenganisha ninyi na mataifa." Kwa nini? "ili muwe wangu." Hii ilikuwa ni kutengwa kwa **ajili ya Mungu**.

Neno la Kiebrania lililotafsiri "kutengwa" katika Mambo ya Walawi 20:26 linatumika katika Mwanzo 1:4 wakati Mungu "alipotenganisha" nuru kutoka giza. Huwezi kuchanganya nuru na giza pamoja; vinapingana. Mungu alikusudia kuwepo na kutengwa kabisa kwa Israeli dhidi ya mataifa yote maovu yaliyoizunguka Israeli.

[114] Kutoka 19:5
[115] Mambo ya Walawi 19:36
[116] Mambo ya Walawi 20:26

Mungu amewaita watu wake watengwe kabisa kutokana na dhambi. Kwa nini? **Ili waweze kuwa mali yake kabisa.** Hizi sheria zinaonesha kwamba mifumo ya maisha yote ni mali ya Mungu. Kwa watu watakatifu, mifumo yote ya maisha iko chini ya mamlaka yake. Kuwa mtakatifu inamaanisha kutengwa kwa ajili ya Mungu katika maeneo yote. Tumetengwa katika dhambi ili tuweze kuwa mali ya Mungu.

► Ni lipi linaloonekana kuwa ni ngumu zaidi – **kutenganishwa kutoka katika dhambi** au **kutengwa kwa ajili ya Mungu?** Kwa nini?

## Utakatifu katika Matendo: "Katika dunia, lakini siyo kwa ajili ya dunia"

### Utengwaji wa kibiblia unatoa ushuhuda kwa dunia

Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake wawepo ulimwenguni, lakini wasiwe sehemu yake. Danieli alikataa "kujitia unajisi kwa kula chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa."[117] Katika historia nzima, watu wa Mungu wamekuwa wakijitenga na dhambi katika maeneo yao wanayoishi. Hali hii imeruhusu watu wa Mungu kuwa mashuhuda kwa dunia yao.

Israeli iliitwa kuwa "taifa la makuhani," taifa takatifu lililoongoza mataifa mengine kwa Mungu.[118] Wakati Israeli ilipokuwa waaminifu kwa Mungu, ilikamilisha umisheni huu. Rahabu alisema, "hofu imetuangukia mbele yenu… mioyo yetu iliyeyuka, wala haukusalia ujasiri wo wote katika mtu awaye yote, kwa sababu yenu." Kwa nini? Kwa sababu Israeli ilikuwa taifa lenye nguvu na jeshi kubwa? Hapana! Bali ni kwa sababu, "Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini."[119] Wakati Israeli ilipotengwa kwa ajili ya Mungu, ilifanyika ushuhuda kwa mataifa yote.

Tunaiona kanuni hii kwenye maisha ya Yusufu. Kwa kuwa Yusufu alijitenga mwenyewe na dhambi za Wamisri, alikuwa ni ushuhuda kwa Farao. "Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?"[120] Kama Yusufu angekuwa ameishi kama Wamisri, isingewezekana kupatiwa nafasi kubwa kama hiyo ya kuwa shuhuda mbele ya Farao.

Yesu aliomba kwamba wafuasi wake wawe ndani ya ulimwengu, lakini siyo kwa ajili ya ulimwengu. Kifungu hiki mara nyingi kimekuwa hakieleweki kwa Wakristo wanaotaka kuishi maisha ya uangalifu na ya kimungu. Wanafanya makosa kwa kufikiri kwamba kuwepo "katika ulimwengu huu" ni uovu wa lazima ambao watu wa Mungu ni lazima wapitie katika safari ya kuelekea mbinguni.

Hata hivyo, baada ya kufurahia kwamba wafuasi wake "siyo wa ulimwengu huu," Yesu aliomba "Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao

---

[117] Danieli 1:8
[118] Kutoka 19:6
[119] Yoshua 2:9-11
[120] Mwanzo 41:38

ulimwenguni."[121] Yesu aliomba kwamba wafuasi wake watumike kwa ufanisi mkubwa **duniani.** Yesu aliomba tusiwe "watu wa dunia" wakati tumetumwa "tuenende duniani." Kwa kukaa tukiwa tumetengwa na dhambi, tunaweza kutimiza wito wetu wa kuibadilisha dunia. Kama watoto wa Mungu, tunaweza tukawa chumvi na nuru kwa ulimwengu wa dhambi.

Mitume walijua kwamba maisha ya utakatifu ni ushuhuda kwa dunia. Petro aliwataka waamini waishi maisha ya kumcha Mungu kama ushuhuda kwa wasioamini:

> Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.[122]

Paulo aliandika kwa Tito, kiongozi wa kanisa katika kisiwa cha Krete. Waumini hawa walizungukwa na wapagani. Paulo akamwambia Tito kwamba Wakristo "wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote."[123] Wakati Wakristo wakiyaishi maisha ya utakatifu, tabia zao "zitaipamba" Injili. Tabia za watu watakatifu zitaifanya Injili iwe kivutio kwa dunia.

Paulo aliwataka Wakristo wa Filipi kuishi maisha ya kumcha Mungu. Walitakiwa wabakie wakiwa wametengwa katika dhambi. Walitakiwa wawe "wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao **kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu**."[124]

Kama watu wa Mungu tunaoishi maisha ya utakatifu, "tunang'ara kama nuru ya dunia." Maisha ya watoto wa Mungu yanatakiwa yatoe ushuhuda unaong'aa kwa dunia iliyoko gizani. Kutengwa katika dhambi siyo jaribio la kisheria la "kupata wokovu." Kutengwa katika dhambi kunatuwezesha sisi kutimiza mwito wa Yesu wa kuwa "nuru ya ulimwengu" na "chumvi ya dunia."[125] Mikono mitakatifu ni ushuhuda wenye nguvu kwa dunia yetu.

### Kanuni za Kibiblia za Kutengwa

Kwa watu wengi "kutengwa kutokana na dunia" ni orodha ya "fanya" na "usifanye." Mara nyingi kutengwa kunafafanuliwa kwa msururu wa sheria nyingi. Watu wengi wanafafanua kutengwa kwa mlolongo wa mavazi wasiyotakiwa kuvaa, maeneo wasiyotaliwa kwenda, na sherehe wasizotakiwa kushiriki.

Ni ukweli usiopingika kwamba watu watakatifu hawataweza kuvaa nguo za aina fulani, au kwenda kila eneo la maisha. Mtu mtakatifu hupenda kumpendezesha Mungu katika kila

[121] Yohana 17:16-18
[122] 1 Petro 2:12
[123] Tito 2:10
[124] Wafilipi 2:15
[125] Mathayo 5:13-14

eneo la maisha yake. Hata hivyo, kutengwa katika dhambi na kutengwa kwa ajili ya Mungu ni zaidi ya msururu wa sheria.

Tatizo moja katika kufafanua kutengwa kwa njia ya msururu wa sheria ni kwamba sheria hizo hubadilika mara kwa mara, mara nyingi kwa maelezo machache sana. Kanisa moja litasimamia kutengwa kwa mfumo wa sheria zake; kanisa lingine nalo litasimamia kwa mfumo wa sheria nyingine. Njia nzuri ya mtazamo ni kufafanua kanuni za kibiblia ambazo ni za kweli **kwa nyakati zote** na kwa **mila zote.**

Kama Wakristo, aina ya maisha yetu ni lazima yalenge utii wetu kwa neno la Mungu na uongozi wa Roho Mtakatifu. Kama tutatafuta kuwa watu tuliotengwa kwa ajili ya Mungu kama "watu wa milki yake mwenyewe,"[126] kwa hiari tutayatii mafundisho ya neno lake.

Wakati Biblia haielekezi moja kwa moja mwelekeo wa maisha ya kisasa, inajenga kanuni ambazo zinaweza kutuongoza sisi. Ni kanuni gani zinazoweza kuongoza aina ya maisha ya mtu mtakatifu?

### *(1) Kanuni ya Staha*

Kanuni ya staha inathibitisha kwamba uvaaji na tabia zetu ni lazima zimpe Mungu heshima na lazima kujizuia na yale yote ambayo ni aibu mbele zake. Uvaaji wetu na tabia zetu zinaongozwa na matamanio yetu ya kumpa Mungu utukufu.

Ndani ya Biblia yote, **kutembea uchi** kulikuwa ni aibu sana. Baada ya kutenda dhambi, Adamu na Hawa waliona aibu kwa sababu "Walifumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi."[127] Kwa hiyo "wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo." Wakati Mungu alipokutana nao bustanini, aliwatengenezea "mavazi ya ngozi yaliyokuwa makamilifu zaidi akawavika."[128]

Kwa mujibu wa muendelezo wa maandiko yote, kukaa uchi ni tendo la aibu.[129] Manabii walitumia kutembea uchi kama ishara ya hukumu ya Mungu.[130] Kama watu wa Mungu, uvaaji wetu ni lazima uonyeshe kwamba tunaheshimu viwango vya Mungu vyenye staha. Tunapaswa tuone aibu kwa uvaaji uchi ambao ulikuwa ni ishara ya aibu kwa manabii wa Mungu. Uvaaji wetu uwe kweli ni uvaaji ambao unawakilisha watu wa Mungu watakatifu na wasafi.

---

[126] 1 Petro 2:9
[127] Mwanzo 3:7
[128] Mwanzo 3:21
[129] Kwa mfano, kukaa uchi kulikuwa ni ishara ya hukumu ya Mungu (Hosea 2:3; Ezekieli 23:29).
[130] Isaya 20:1-4; Hosea 2:3; Ezekieli 23:29

Ustaha katika Biblia ulihusisha **tofauti za jinsia.** Wakati Biblia haifafanui ni vitu gani maalumu vya mavazi vivaliwe na Waisraeli, Mungu anawaamrisha watu wake wazingatie tofauti za jinsia katika mavazi yao.[131]

Agano Jipya linafundisha kwamba **mapambo** yetu lazima yaonyeshe kwamba sisi ni wana wa Mungu. Paulo alilinganisha aina mbili za mapambo:

> Wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele,[132] wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu.[133]

Paulo anakataza mapambo yaliyo juu ya viwango vya kawaida ya kulinganisha mitindo ya nywele, vito vya mapambo, na mavazi. Wakati huo huo, anashauri mapambo "yenye mavazi ya heshima" ambayo ni sahihi kwa wanawake wanaokiri uungu. Haya ndiyo mapambo ya "kazi njema" ambayo Wakristo wanapaswa kutafuta.

Mafundisho ya Paulo yanaonyesha uhusiano uliopo kati ya mapambo ya nje na roho wa ndani. Katika sehemu hii ya barua ya Paulo kwa Timotheo, analenga kuhusu maombi katika kanisa. Anamwambia Timotheo jinsi Wakristo wanavyopaswa kuomba. Anaelekeza kwa kila jinsia.

Paulo anaandika kwamba wanaume wanapaswa waombe "bila ghadhabu au ugomvi." Hatupaswi kuingia mbele za Mungu na roho ya ghadhabu. Paulo anaandika kwamba wanawake wanapaswa kuomba kwa roho ya staha na unyenyekevu; ikiwa pia ni katika uvaaji na mapambo. Hatupaswi kwenda mbele ya uwepo wa Mungu kwa majivuno na utukufu wa binadamu. Watu watakatifu wanayo staha inayodhirika katika maeneo yote ya maisha.

Petro alitoa uhusiano unaofanana kati ya mwonekano wa nje na roho wa ndani.

> Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao....[134]

Kama Paulo, Petro anatambulisha aina mbili za mapambo. Anakataza mapambo ya **nje** yanayoonyesha mitindo ya nywele, mapambo ya dhahabu na mavazi. Kisha anaamrisha

---

[131] Kumbukumbu la Torati 22:5

[132] Neno "kusuka" mara nyingine huwachanganya wasomaji. Mitindo ya nywele ya kujivunia ya sikuya Paulo ilikuwa ni pamoja na almaria zilizopambwa. Kanuni yake ni "wanawake wanapaswa kujipamba kwa staha na siyo kwa makusudi ya kujionyesha au kujitangaza."

[133] 1 Timotheo 2:9-10

[134] 1 Petro 3:3-5

mapambo ya ndani "roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu." Watu watakatifu hujali zaidi katika kuwa wa "thamani mbele za Mungu" kuliko kuvutia na kupata uthibitisho wa dunia hii. Hivi ndivyo "wanawake watakatifu wanaomtegemea Mungu walivyojipamba wenyewe."

Kama Wakristo, **burudani** yetu lazima ionyeshe kwamba tumetengwa kwa ajili ya Mungu. Paulo anatuambia kwamba Wakristo tunapaswa kujaza fahamu zetu na mambo ambayo yatatufanya tufanane zaidi na Kristo.

> Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.[135]

Kama watu watakatifu, kila eneo la maisha linadhibitiwa na Mungu. Ukisoma mambo ya Walawi, utaona kwamba hakuna kitu chochote kidogo kinachoweza kuzuia umakini wa sifa njema ya Mungu. Kila kitu ni muhimu kwake! Hii **siyo** kwa sababu Mungu ni mjeuri anayetaka kutawala kila eneo la maisha. Ni kwa sababu Mungu ni Baba wa upendo anayejali kila kipengele cha maisha ya watoto wake. Baba yetu wa mbinguni hapendezwi watoto wake kuvaa mavazi ambayo yanadhalilisha miili aliyoiumba kwa upendo mkubwa. Baba yetu wa mbinguni hataki watoto wake wajazwe fahamu zao na burudani ambazo zinavutia mawazo ya dhambi na aibu. Sisi ni "watu wa milki yake mwenyewe," na anajali kila kipengele cha maisha yetu.

► Tumia kanuni ya staha katika mila yako. Ni maeneo gani (ya mavazi na mitindo ya maisha) ambayo ni changamoto katika kudumisha staha kwenye dunia yako?

### *(2) Kanuni ya Uwakili*

Kanuni ya uwakili inathibitisha kwamba kila kitu tulicho nacho ni mali ya Mungu. Kama watoto wa Mungu, tutatumia fedha na mali zetu kwa njia ambayo inamheshimu yeye.

Katika karne ya kumi na nane, baadhi ya Wakristo walifuata kanuni kali ya uvaaji. Walikataa kila aina ya nakshi kwenye mavazi yao. Hawakuvaa vifungo vya kung'ara katika nguo zao; wanaume hawakuvaa tai shingoni; walivaa nguo zilizotengenezwa kwa kitambaa cha kijivu. Inaonekana kwamba walikuwa watu wa kiasi sana.

Hata hivyo, John Wesley alihubiri somo kuhusu mavazi ambapo alilalamika kwamba huo muonekano wa staha ulikuwa wa nje tu. Wakati mavazi yalionekana ni ya kawaida tu, baadhi ya Wakristo walipuuzia kanuni ya uwakili. Walisafiri kutoka Uingereza hadi Paris kwenda kununua vitu vya gharama sana kwa ajili ya uvaaji wao. Ndiyo, walinunua tu

[135] Wafilipi 4:8

nguo za rangi ya kijivu – lakini walinunua nguo za gharama kuonyeshana utajiri wao. Walikuwa watu wa staha, lakini hawakuwa mawakili wazuri wa fedha za Mungu.[136]

Wesley aliweka mkazo kwamba kujitenga na dunia kulimaanisha kuwa wakili mzuri wa fedha Mungu anazotupa. Alihubiri kwamba watu watakatifu hawapaswi kupoteza fedha zao kwa fujo kupita kiasi katika nguo. Inawezekana kuvaa nguo zenye staha lakini tukawa ovyo kwenye chaguo la mavazi. Palo alisema kwamba mapambo yetu hayatakiwi yawe "mavazi ya gharama kubwa."[137]

Kanuni ya uwakili haimaanishi kwamba kila siku ni kununua vitu rahisi tu. Mara nyingine nguo za thamani zinazogharimu zaidi zinadumu muda mrefu zaidi. Baadhi ya makanisa hutumia $100 kufunga vitu rahisi – na baadaye hutumia mamia ya dola katika kufanya ukarabati wa maeneo yanayoharibika na kuvuja! Huu ni uwakili mbaya.

Kanuni ya uwakili inasema, "Sisi ni mawakili wa fedha ambazo Mungu ametukabidhi. Tunapaswa tuzitumie kwa busara. Sisi ni mawakili wa talanta ambayo Mungu ametupa, tunapaswa tuzitumie kwa utukufu wake. Kila tulifanyalo limpe yeye heshima."

► Tumia kanuni ya uwakili katika utamaduni wako. Ni kwa jinsi gani makanisa yenu yanaweza kuwa mawakili wazuri kwa rasilimali za Mungu?

### *(3) Kanuni ya Kuwa na Kiasi*

Kanuni ya kuwa na kiasi inathibitisha kwamba hatutaruhusu "vitu" (hata vizuri kiasi gani) vitawale maisha yetu.  Mojawapo ya changamoto ya kuishi "humo" lakini siyo "kwa ajili" ya dunia ni kwamba tuko duniani! Kuna vitu vingi sana katika dunia yetu ambavyo tunaweza kuvifurahia. Maisha ya utakatifu yanahitaji kuwa na kiasi hata kama mambo ni mazuri.

Chakula ni mfano. Njaa ni tamaa ya asili, siyo dhambi. Paulo aliandika kwamba tunapaswa kula "kwa utukufu wa Mungu."[138] Kula siyo dhambi. Hata hivyo, kama mimi ni mlafi ambaye siwezi kujithibiti, sitakuwa ninakula katika utukufu wa Mungu. Dunia inakula kwa kujiridhisha; kama sina kiasi katika tabia zangu za kula, mimi ni "wa dunia." Badala yake, napaswa kula "kwa ajili ya utukufu wa Mungu." Hii inamaanisha kwamba nitaimarisha kujithibiti wakati nafurahia chakula alichonipa Mungu.

Wakorintho walisisitiza kwamba, wangeweza kufanya zinaa kwa sababu wao walikuwa watoto wa kiroho wa Mungu haijalishi miili yao iko katika hali gani na inafanya nini. Walisema kwamba, "Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula." Walikuwa na msimamo wa mila yao kwamba mwili unaruhusiwa kupewa chochote unachotaka.

---

[136] John Wesley, "On Dress" from *The Works of John Wesley*, (Grand Rapids: Baker Books, 1996)
[137] 1 Timotheo 2:9
[138] 1 Wakorintho 10:31

Paulo aliwajibika kujibu kwa kunukuu mafundisho ya Wakorintho na kisha kukanusha kila mapokeo ya uongo kutoka katika mafundisho hayo. "'Vitu vyote ni halali kwangu,' **lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote**. 'Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula;' **lakini Mungu atavitowesha vyote viwili, tumbo na vyakula**."[139] Akaendelea, "Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo?" Kisha akahitimisha, "Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu."

Kanuni ya Paulo hapa ni hii – hata vile vitu ambavyo ni halali havipaswi vitutawale. Mungu anayo mamlaka katika nyanja zote za maisha ya Mkristo, ikiwa ni pamoja na miili yetu. **Kila kitu** tunachokifanya ni lazima kimletee Mungu heshima. Hii inatutaka tuishi maisha ya kiasi na kujithibiti.

Hii itaonekanaje katika maisha ya kila siku? Inamaaisha kujithibiti katika vile tunavyokula na kunywa. Inamaanisha kujitawala katika burudani zetu. Kama mtu mtakatifu "sitatawaliwa na chochote." Hata katika burudani ambazo kwazo ni safi na hazina lolote baya kwangu ni mbaya kama zitanitawala. Kanuni ya kuwa na kiasi inafundisha kujithibiti katika maeneo yote.

Nataka nitoe mfano mmoja. Elewa kwamba hii siyo sheria kwako! Ninatumia mfano huu kuonyesha ni jinsi gani kanuni hizi zinaweza kuhusiana na madhaifu binafsi na utu wa mtu.

Nilinunua kompyuta mpya iliyokuwa na mchezo unaoitwa "Tetris." Hakuna jambo lolote baya kuhusiana na mchezo huu. Siyo ya vurugu au ya kimwili. Ni chemsha bongo rahisi. Baadaye nikajigundua kwamba "nimeshatawaliwa" na ule mchezo. Nitakuwa ninafanya kazi – na kisha nitaanza kucheza mchezo. Kisha ninasema, "Nitachukua mapumziko kazini nikacheze Tetris." Dakika thelathini baadaye nitasema, "Nataka nimalizie mchezo mmoja zaidi." Baada ya saa moja, ninajikuta bado naendelea kucheza. Mwishoni, Mungu akanikumbusha kanuni ya kuwa na kiasi. "'Vitu vyote ni halali kwangu,' lakini sitatawaliwa na chochote."

Kwa sababu ya hili, nilijifunza kwamba ni lazima niufute mchezo wa Tetris kutoka kwenye kompyuta yangu. Je, hii ni kanuni ya kibiblia? Hapana! Biblia haijahusisha mchezo wa Tetris mahali popote! Lakini kwangu mimi kanuni ya kuwa na kiasi inamaanisha kuachana na mchezo unaoweza kunitawala mimi.

Kanuni ni pana kuliko sheria. Hakuna fundisho lolote katika Biblia linalohusiana na Tetris. Kama Tetrs ni mchezo pendwa wako, huhitaji kuachana nao kwa sababu yangu. Lakini **kwangu mimi,** kutokana na udhaifu wangu, Tetris ni mtego kwangu. Kama tunataka kuishi maisha matakatifu, tutamwuliza Mungu, "Niishije katika njia inayokupendeza wewe?"

---

[139] 1 Wakorintho 6:12-20

► Tumia kanuni ya kuwa na kiasi katika utamaduni wako. Ni maeneo gani yana changamoto ya kudumisha uwiano wa kibiblia katika maisha yako?

### *(4) Kanuni ya Stahili*

Wakati Timotheo, mtoto wa Baba wa Kigiriki na mama wa Kiyahudi, alipoungana na Paulo katika safari yao ya umishenari, Paulo alimtaka Timotheo atahiriwe kwa ajili ya huduma yenye ufanisi.[140] Mapema, Paulo alikuwa amekataa kumtahiri Tito, Mgiriki aliyeokoka.[141] Hali hizi mbili za mwitikio tofauti wa Paulo unafundisha kanuni muhimu katika huduma.

Katika suala la Tito, Paulo anasimama kwenye ukweli kwamba tunaokolewa kwa neema katika Imani. Kumtaka mtaifa aliyeokoka afuate sheria za Kiyahudi kungeshusha hadhi ya uhuru wa Mkristo. Paulo alisimama imara dhidi ya wale wote waliotaka Tito atahiriwe.[142] Katika Matendo 15, Kanisa la Yerusalemu lilikuwa linatambua wazi kwamba kutahiriwa kulikuwa hakuhitajiki kwa mataifa wanaookoka.

Katika Matendo 16, Paulo alimtaka Timotheo atahiriwe. Kwa nini? Siyo kwa sababu ya wokovu, bali ni kwa ajili ya ufanisi wa huduma kwenye masinagogi.

► Soma 1 Wakorintho 9:19-23.

Paulo alionyesha tena kanuni hii kwa Wakorintho. Kwa ajili ya Injili, Paulo alikuwa tayari kufanya dhabihu katika maeneo ambayo hayakuhusisha kanuni za kibiblia. Hakuelewana na hukumu za kibiblia, lakini alijitoa dhabihu uhuru wake kwa ajili ya huduma.

Hali hii inapendekeza kanuni muhimu sana kwa Wakristo. Kuna mambo yanayoweza kuonekana ni sahihi katika mazingira fulani, lakini yasionekane ni sahihi kwenye mazingira mengine. Kwa ajili ya ufanisi mzuri wa huduma, kiongozi anaweza kusalimisha sehemu ya "uhuru" wake katika maeneo ambayo hayataathiri maamuzi yake. Maeneo haya siyo yale yenye mafundisho ya Biblia, bali ni yale yenye hukumu za binafsi na mambo ya kitamaduni.

Gary ni mmishenari katika Afrika. Gary amefuga ndevu nyingi sana. Katika nchi yao, kufuga ndevu ni ishara ya umri na mamlaka. Chifu wa kabila siku zote anakuwa na ndevu ndefu. Ndevu za Gary zinampa heshima miongoni mwa watu anaojaribu kuwafikia kwa Injili. Amekubali kubeba ndevu nyingi kwa sababu ya kanuni ya Stahili.

Rick ni mmishenari katika Asia. Katika nchi ya Rick, kufuga ndevu kumefungamana na unyonge na muonekano wa unyonge wa mtu. Mara tu alipokwenda kwenye hii nchi, Rick akahisi kwamba ndevu zake zitakuwa ni kikwazo kwa ufanisi wake. Alinyoa ndevu zake kwa sababu ya kanuni ya stahili.

---

[140] Matendo 16:3
[141] Wagalatia 2:3
[142] Wagalatia 2:1-6

Kuwa na ndevu ni vibaya au vizuri? Wala! Wanaume wote walijifunza jinsi ya kufuata kanuni ya Stahili. Ni kitu gani kizuri katika mazingira ambayo Mungu ameniwekea?

► Umeshaona maeneo ambayo kanuni ya Stahili inakutaka wewe utoe dhabihu ya uhuru wako ilikuwafikia walio karibu nawe kwa ajili ya Kristo?

### *(5) Kanuni ya Uwajibikaji: Ninajibu kwa Nani?*

Mara nyingi huwa nawauliza wanafunzi wangu chuoni, "Je, mnapendelea sheria au kanuni kwa ajili ya kitabu chenu cha bwenini?" Kwa kawaida watasema, "Tunapendelea Kanuni."

Kisha nitauliza, "Ni kipi rahisi kutii: sheria inayosema, 'Taa zote ni lazima zizimwe usiku wa manane,' au kanuni inayosema, 'Unajiandaa kwa huduma. Kalale mapema upate mapumziko ya kutosha na uwe tayari kwa kazi ya darasani katika kipindi cha kwanza cha asubuhi.'? Wanafunzi wanatambua haraka kwamba kanuni inahitaji kufikiri zaidi kuliko sheria ya kawaida!

Kanuni zinaweza kuwa ngumu. Mojawapo ya ufunguo ni kutambua kwamba tunamjibu Mungu katika jambo la kutengwa. Huwezi kuwa na sheria inayosema, "_____ gramu za chakula kwa siku ni za kiasi. Zaidi ya hapo ni ulafi." Hiyo haiwezekani. Badala yake kumbuka kwamba ninawajibika kwa Mungu kwa ajili ya kijitawala.

Mtu mmoja atakuwa ofisini kwa kazi inayohitaji suti nzuri; lakini mtu mwingine atakuwa msimamizi maskini kama atanunua suti ya kuvaa shambani!

Mungu anaweza kutoa mitazamo tofauti kwa watu tofauti kutegemeana na muundo wa huduma zao; maisha ya nyuma; na hata dhambi zinazowakabili. Sisi wote hatufanani; na hatutafanana na mwingine. Kaka na dada zetu wanaweza kuwa na mitazamo tofauti ya aina za maisha. Ili mradi tofauti hizo hazipingani na mafundisho ya Maandiko, tofauti hizi zinaweza kuwa ndio uhuru wa kibiblia.

Kwa sababu hiyo, napaswa kukumbuka mambo mawili:

1. Sipaswi kuhukumu juu ya moyo wa mtu mwingine. Wanajibu kwa Mungu kwa kutengwa kwao na dunia.[143]

2. Nitauhukumu moyo wangu mwenyewe kwa uangalifu sana. Ninajibu kwa Mungu kwa kujitenga kwangu na dunia.

## Waliipata Siri - Count Zinzendorf na Wamoraviani

Katika karne ya kumi na nane, kundi la Wakristo lilikimbilia Ujerumani kukwepa mateso huko Monrovia. Walikaa katika shamba la Count Nikolaus von Zinzendorf,[144] akawa

---

[143] Warumi 14:4

[144] Image: "Portrait of Count Zinzendorf" by J. Archer, *The Life of Nicholas Lewis Count Zinzendorf* (1838), retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Portrait_of_Count_Zinzendorf.jpg, public domain.

kiongozi wao. Kwa miaka michache walikuwa zaidi ya Wamoraviani 300 wakiishi katika shamba hili eneo la Herrnhut.



Wamoraviani walikuwa wamejitoa kabisa kwa utakatifu wa kweli. Waliishi maisha ya wazi yalioongozwa na kanuni za Maandiko. Walijulikana kwa ustadi wao wa kujifunza Biblia na kwa ajili ya maombi. Mwaka 1727, Wamoraviani walianzisha kutaniko la maombi yaliyoendelea kwa masaa ishirini na nne kwa siku kwa zaidi ya miaka mia moja.

Wamoraviani walichagua kuwa wana wa Mungu kabisa. Kulikuwa na matokeo gani ya uwajibikaji huu wa maisha ya kutengwa? Mungu aliwatumia kwa njia ya nguvu sana.

Wamoraviani walikuwa na ushawishi sana juu ya Wakristo wengine. Mmishenari wa Kimoraviani, Peter Boehler, alikuwa ni muhimu sana katika kuokoka kwa John na Charles Wesley. Wiki chache baada uhakika wa wokovu wa John na Wesley kwenye kanisa la Moraviani, barabara ya Aldersgate, alisafiri hadi Herrnhut kujifunza zaidi kuhusu uzoefu wa kiroho wa waamini waliojitoa kabisa. Kutoka Kwa Wesley hadi William Carey, Wakristo waliojikabidhi kabisa walivutiwa na ufuatiliaji wa utakatifu wa Wamoraviani.

Wamoraviani walibeba ushuhuda mkubwa sana wa Uinjilisti duniani kote. Ndani ya kipindi cha miezi sita ya mikutano ya maombi iliyoanza mwaka 1727, vijana ishirini na sita wa Kimoraviani walishajitolea kwa ajili ya huduma ya kimishenari – wakati ambapo huduma za kimisheni za kigeni zilikua hazijulikani kabisa miongoni mwa makanisa ya Kiprotestanti. Kwenye karne ya kumi na nane, zaidi ya wamishenari 300 walikuwa wametumwa kutoka katika hivi vikundi vidogo vya Wakristo waliokuwa wametengwa. Baadhi ya wamishenari wa Kiprotestanti wa mwanzo kabisa walikuwa wametumwa na Wamoraviani. Wakristo waliotengwa kwa ajili ya Mungu wanaweza kutumiwa na Mungu kuibadilisha dunia.

Wimbo, "Nataka kanuni ndani yake" unatoa kanuni za ujumla za kutengwa zilizofundishwa na Wamoraviani. Mtu mtakatifu anadumisha dhamira ambayo ni nyeti kwa marudio ya Mungu.

**Nataka kanuni ndani yake - Charles Wesley**

Nataka kanuni ya ndani ya kukesha, hofu ya Mungu,
Ufahamu wa Mungu kuhusu dhambi, maumivu ya kuisikia kwa karibu.
Nataka mshiko wa kwanza uguse kiburi au matamanio mabaya,
Ukamate kutangatanga kwa nia yangu, na uzime moto unaowaka.

Kutoka kwa Bwana sitapotea tena, na hakuna huzuni tena katika wema wako.
Nipe hofu ya kifamilia, naomba, tabia na dhamira ya kutoa,
Haraka kama mboni ya jicho, Ee Mungu, itengeneze dhamira yangu;
Iamshe roho yangu wakati dhambi iko karibu, na uifanye bado imeamka.

## Tafakuri ya Somo la 4

(1) Kuwa mtakatifu inamaanisha kutengwa au kuwa wa Mungu. Mifano mingine:

- Siku takatifu
- Vitu vitakatifu
- Maeneo matakatifu
- Kabila takatifu

(2) Kuwa mtakatifu maana yake ni **kutengwa katika dhambi**. Kwa kuwa Mungu anachukia dhambi, Watu wa Mungu huchukia dhambi.

(3) Kuwa mtakatifu maana yake ni **kutengwa kwa ajili ya Mungu***.* Kusudi la kutengwa na dhambi ni ili kutengwa kwa ajili ya Mungu.

(4) Watu wa Mungu hukaa mbali na dhambi. Kuishi karibu na Mungu inamaanisha tunaishi mbali na dhambi.

(5) Maisha matakatifu yaliifanya Israeli iwe shuhuda kwa dunia yote. Maisha matakatifu yanawafanya Wakristo waweze kuushuhudia ulimwengu.

(6) Kutengwa Kibiblia kunaanzia moyoni.

(7) Kanuni za kutengwa na dunia ni pamoja na:

- Kanuni ya Staha
- Kanuni ya Uwakili
- Kanuni ya Kuwa na Kiasi
- Kanuni ya Stahili
- Kanuni ya Uwajibikaji

## Kazi ya Kufanya

(1) Chagua suala moja ambalo kutengwa ni tatizo la Wakristo katika jamii yako. Kutumia kanuni zilizopo katika sura hii, andika insha ya kurasa 1-2 ukipendekeza ni jinsi gani Wakristo wanaweza kutengwa na dhambi na kutengwa kwa ajili ya Mungu katika suala ulilochagua.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu 2 Wakorintho 6:16-18.

# Somo la 5
# Utakatifu ni Moyo Usiogawanyika – "Kuwa Mkamilifu"

## Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa kwamba neno "Kuwa Mkamilifu" kwenye Agano la Kale linamaanisaha moyo usiogawanyika.

(2) Kuelewa hatari ya kiroho iliyopo ya moyo uliogawanyika.

(3) Kujisalimisha kwa Mungu na "Ndiyo" isiyokuwa na masawli.

(4) Kukariri Zaburi 86:11-12.

## Kalebu: Mtu asiyekuwa na moyo wa kugawanyika

Watu wa Isareli walikuwa tayari kuingia nchi ya Kaanani. Mungu aliwaleta huko kote kupitia jangwani, na walikuwa wamebakiza umbali kidogo tu kutoka nchi ya ahadi. Musa aliwatuma wapelelezi kumi na wawili kwenda kuipeleleza nchi. Baada ya siku arobaini, wapelelezi walirudi na zabibu na taarifa za maajabu ya nchi ya Kaanani. Lakini, walisema, Wakaanani ni watu wenye nguvu sana wanaoishi katika miji. Tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi!

Wapelelezi wawili tu, Yoshua na Kalebu waliamini ahadi ya Mungu ya ushindi. Kalebu akasema, "Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka."[145] Yoshua na Kalebu waliiona ile nchi kama wapelelezi wengine. Waliiona miji na maboma makubwa sana. Waliwaona wapiganaji wenye nguvu sana.

Lakini Yoshua na Kalebu waliona kitu tofauti ambacho wapelelezi wengine hawakukiona – waliona kwamba Mungu aliyewatoa Israeli kutoka Misri atawaleta Israeli kuingia nchi ya Kaanani. Waliona kwamba Mungu aliyeharibu jeshi la Farao ataharibu na kuta za Yeriko. Waliona kwamba Mungu wa Ibrahimu alikuwa pia Mungu wa Musa. Mungu alisema, "lakini mtumishi wangu Kalebu, kwa kuwa alikuwa na roho nyingine ndani yake, naye ameniandama kwa moyo wote."[146]

Kwa kuwa hawakumwamini yeye, Mungu alikilaani kile kizazi cha watu wazima kifie jangwani. Miaka arobaini baadaye, Israeli ikaingia Kaanani, na ilikuwa ni wakati wa

[145] Hesabu 13:30
[146] Hesabu 14:24

kuigawa nchi. Kalebu alikuwa na zaidi ya miaka themanini. Akamwambia Yoshua, "Hata sasa mimi nina nguvu zangu hivi leo kama nilivyokuwa siku hiyo Musa aliyonituma…. Basi sasa unipe mlima huu." Ndiyo, kulikuwa na miji imara iliyokuwa na wapiganaji hodari sana. Lakini Kalebu alikuwa na Imani katika ahadi za Mungu. "Nami nitawafukuza watoke nje, kama Bwana alivyonena."[147]

Ni kitu gani kilimpa Kalebu Imani kubwa hivyo? Ni moyo usiogawanyika. Kalebu alisema, "Ila mimi nilimfuata Bwana, Mungu wangu, kwa utimilifu."[148] Kalebu alimwamini Mungu kwa moyo wake wote. Kalebu alikuwa na moyo usiogawanyika.

## Moyo Mkamilifu ni moyo usiogawanyika

Vitabu vya Historia vinaelezea anguko la kutisha la Israeli lilivyosababisha watu wake wasiwe kama Mungu alivyotaka wawe. Vitabu vya Hisoria vinaonyesha jinsi Israeli ilivyopotea njia kutoka katika mpango wa Mungu. Israeli ilikuwa imeitwa kumwakilisha Mungu kwa mataifa. Badala yake, ikageukia miungu ya uongo. Kutokana na kushindwa kwake, Israeli ilishindwa na kupelekwa utumwani. Utukufu wake uligeuka kuwa aibu.

Pamoja na picha ya kukosa uaminifu kabisa, Vitabu vya Historia vinaonyesha watu watakatifu waliomtumikia Mungu. Wakati wengi katika Israeli walikuwa siyo waaminifu tena kwa Mungu (Waamuzi), mjane mmoja mdogo Mmoabi alikuwa mwaminifu (Ruth). Hata wakiwa utumwani (2 Wafalme), binti mdogo wa Kiyahudi alikubali mwito wa Mungu akatumikia watu wake (Esta). Watu hawa walimheshimu Mungu kwa mioyo yao yote. Walikuwa watakatifu.

Vitabu vya Historia vinafundisha kwamba kuwa mtakatifu ina maana ya kumtumikia Mungu kwa uaminifu wote. Utakatifu haumaanishi utendaji kamili. Utakatifu unamaanisha kumtumikia Mungu kwa moyo usiogawanyika.

Tafsiri za zamani za Agano la Kale zimetumia neno "kamilifu" kutafsiri neno la Kiebrania *shalem*. *Shalem* inatafsiriwa "Kuwa mkamilifu." Kuwa mkamilifu ni kwamba umekamilika. Kuwa mtakatifu inamaanisha kwamba wewe ni mali ya Mungu kabisa.

*Shalem* inahusiana na neno la Kiebrania la amani, *shalom*. Kuwa mkamilifu mbele ya Mungu inamaanisha kuwa na amani na yeye ("mioyo iliyo kamili kwa BWANA").[149] Kuwa na "moyo mkamilifu" ni kuwa na moyo ambao "umekamilika" au "usiogawanyika," moyo ulio na uaminifu wa peke yake. Tuangalie mifano ya neno "mkamilifu" au "usiogawanyika" katika Vitabu vya Historia.

[147] Yoshua 14:11-12
[148] Yoshua 14:8
[149] 1 Wafalme 8:61

**Jeshi lenye kusudi lisilogawanyika**

Baada ya kifo cha Sauli, makabila ya kaskaini yalimtawaza Ishboshethi kuwa mfalme wakati Yuda ilimfuata Daudi. Kulikuwa na miaka miwili ya vita ambayo Daudi aliiongoza Yuda kupigana na makabila ya kaskazini. Baada ya miaka miwili, Ishboshethi aliuawa na makepteni wake mwenyewe. Majeshi yaliungana kumtawaza Daudi awe mfalme juu ya Israeli wote. Taifa likawa sasa liko chini ya utawala wa mfalme mmoja.

> Hao wote, watu wa vita, askari wastadi, wakaja Hebroni wenye moyo mkamilifu, ili kumtawaza Daudi awe mfalme juu ya Israeli wote; tena wote waliosalia wa Israeli nao walikuwa na moyo mmoja kwamba wamtawaze Daudi.[150]

Jeshi "likaja Hebroni **kwa moyo mmoja** (*shalem*) kumfanya Daudi awe mfalme." Tafsiri za zamani zinatumia maneno "pamoja na moyo makamilifu."[151] "Mkamilifu" haina maana kwamba hakukuwa na hata mtu mmoja aliyetenda dhambi. Inamaanisha hapa kwamba "taifa lote lilikuwa mwaminifu" kwa Daudi. Walikuwa wameunganishwa chini ya mfalme mmoja. Katika aya hii, *shalem* siyo neno la kidini; bali la kisiasa. *Shalem* ikimaanisha kuwa na uaminifu mmoja usiogawanyika kwa mfalme.

**Madhabahu iliyo na mawe yasiyochongwa**

Wakati Isaraeli ilipoingia katika Nchi ya Ahadi, Yoshua alijenga madhabahu katika mlima wa Ebali. Yoshua alijenga madhabahu ya "mawe yasiyochongwa (*shalem*) ambayo mtu hakutumia juu yake chombo cha chuma" (Yoshua 8:31). "Yasiyochongwa" ni neno lililo sawa na "yaliyo mazima" au "makamilifu." Kuwa *shalem* ni kutogawanyika.

**Moyo usiogawanyika**

Wakati wa kujitolea kulijenga hekalu, mfalme Sulemani aliwataka watu wa Israeli wamtumikie Mungu kwa mioyo isiyogawanyika.

> Mioyo yenu na iwe kamili (*shalem*) kwa Bwana, Mungu wetu, kuenenda katika sheria zake, na kuzishika amri zake, kama ilivyo leo.[152]

Hili ni neno lililo sawa na yaliyotumika kuelezea muungano wa jeshi moja chini ya Daudi. Ni neno hilo hilo limetumika kuelezea mawe yasiyochongwa. Sulemani aliwataka Israeli kuwa na uaminifu usiogawanyika kwa Mungu. Kama watu wa Israeli wangekuwa na moyo usiogawanyika, "wangetembea katika amri zake na kuzishika amri zake." Mtu aliye na moyo usiogawanyika kwa hiari yake humtii Mungu.

---

[150] 1 Mambo ya Nyakati 12:38
[151] *Toleo la King James (KJV)*
[152] 1 Wafalme 8:61

## Mioyo Iliyogawanyika na Mioyo Isiyogawanyika

Historia ya wafalme wa Israeli inaonyesha kwamba Mungu huwaita watu wamtumike kwa mioyo isiyogawanyika. Mungu anatafuta watu watakatifu. Mungu yuko katika kutafuta mioyo isiyogawanyika.

### Mfalme Sulemani: Moyo uliogawanyika

Wakati wa kujitolea kulijenga hekalu, Sulemani aliwataka watu wa Israeli wamtumikie Mungu kwa mioyo isiyogawanyika. Kwa masikitiko, Sulemani hakuutendea kazi ushauri wake mwenyewe. "Maana ikawa, Sulemani alipokuwa mzee, wake zake wakamgeuza moyo wake, afuate miungu mingine, wala moyo wake haukuwa mkamilifu (*shalem*) kwa Bwana, Mungu wake, kama moyo wa Daudi baba yake."[153]

Moyo wa Sulemani ulikuwa umegawanyika. Alitaka awe anaabudu Mungu wa Israeli na wakati huo huo aabudu miungu. Huwezi ukawa mwaminifu kwa Mungu na kwa miungu kwa wakati mmoja. Mwandishi wa kitabu cha 1 Wafalme hasemi kwamba Sulemani aliacha kumwabudu Yehova. Sulemani aliendela kutoa dhabihu kwenye Hekalu, lakini moyo wake ulikuwa umegawanyika. Alljaribu kumtumikia Mungu na moyo uliogawanyika.

### Mfalme Daudi: Moyo usiogawanyika

Katika 1 Wafalme 11:4, tunasoma mtazamo wa Mungu kuhusiana na moyo wa Daudi na Sulemani. Moyo wa Daudi haukugawanyika, lakini moyo wa Sulemani uligawanyika. Kwa mtazamo wa kibinadamu tunaweza kufikiria uzinzi na mauaji ya Daudi kama yaliyo mabaya sana kuliko kuasi kwa Sulemani. Kwanini mwandishi wa Wafalme aseme kwamba moyo wa Daudi "ulikuwa mkweli kabisa" kwa Bwana?

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Naomba nife mimi ili niweze
kuishi ndani yako;
Naomba unifanye mimi mtupu
ili niweze kuzidi ndani yako;
Naomba mimi nisiwe chochote
ili niwe ni yote kwako"
- Erasmus

Tofauti ni mwitikio wa Daudi kwenye dhambi. Wakati nabii alipokabiliana na Daudi, kwa haraka sana Daudi alitubu. Daudi hakujitetea mwenyewe. Badala yake, alikiri uovu wake kwa Mungu, "Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako."[154] Daudi alimtumikia Mungu na moyo usiogawanyika. Moyo wake ulikuwa *shalem*. Moyo wake haukugawanyika.

Zaburi 86 inaelezea njaa ya Daudi ya moyo usiogawanyika. Katika Zaburi ya 86, Daudi anaomba ukombozi kutokana na maadui zake wanaotafuta kumwua. Katikati ya maombi haya, Daudi analia, "Uunganishe moyo wangu katika kuhofia Jina lako."[155] Daudi anaomba

---

[153] 1 Wafalme 11:4
[154] Zaburi 51:4
[155] Zaburi 86:11

kwa ajili ya moyo usiogawanyika. Daudi alitafuta kumtumikia Mungu kwa ukamilifu wa moyo wake wote.

**Mfalme Asa: Moyo uliogawanyika**

Asa aliingia madarakani kuitawala Yuda mwaka wa 910 K.K. Alikuwa amejitoa kabisa kwa Mungu; aliharibu madhabahu zote za miungu ya uongo; alivunjavunja maashera yote yaliyotumika kwa ajili ya ibada za sanamu. Wakati jenerali wa Kushi alipoipiga Yuda na jeshi lake kubwa, Asa alimlilia Mungu kwa ajili ya ukombozi:

> …Bwana, hapana kuliko wewe aliye wa kusaidia, kati yake yeye aliye hodari, na yeye asiye na nguvu; utusaidie, Ee Bwana, Mungu wetu; kwa kuwa sisi twakutegemea wewe, na kwa jina lako tumekuja juu ya jamii kubwa hii. Ee Bwana, wewe ndiwe Mungu wetu, asikushinde mwanadamu.[156]

Mungu alijibu ombi la Asa. "Basi, Bwana akawapiga Wakushi mbele ya Asa, na mbele ya Yuda..."[157] Asa aliweka uaminifu wake wote kwa Mungu, na Mungu akampa ushindi mkubwa.

Miaka ishirini ilipita, Asa akakutana tena na jaribu lingine jipya. Wakati huu, Baasha, mfalme wa makabila ya kaskazini, aliitishia Yuda. Kwa hofu yake, Asa aliamua kuunda muungano wa kijeshi na taifa lingine. Alisaini mkataba na Ben-Hadad, mfalme wa Syria. Badala ya kumtumainia Mungu peke yake, Asa akaweka tumaini lake kwa mfalme wa kipagani.

Katika kujibu, nabii Hanani alimkumbusha Asa kuhusu ushindi wake mkubwa wa nyuma dhidi ya jeshi kubwa la Wakushi. Alimkumbusha Asa kwamba "wakati ulipomtegemea BWANA aliwaingiza mikononi mwako." Kwa nini Mungu afanye hivyo? Kwa sababu, "macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyo (*shalem*) kuelekea kwake."[158]

Wakati Asa alipomwamini Mungu kwa ukamilifu wote, Mungu alimpa ushindi mkubwa. Lakini sasa Asa anamtegemea mtawala wa Syria. Kwa sababu Asa hamwamini Mungu peke yake tena, Mungu hatamwokoa tena katika hatari yeyote. Hanani alimwonya Asa kwamba atakumbana na vita katika wakati wake wote wa utawala uliobakia.

Miaka ya mwisho ya kutawala kwa Asa ni kivuli tu cha wakati mzuri ujao wa miaka yake ya awali. Mwishoni mwa maisha, Asa akawa mgonjwa, lakini "hakumtafuta Bwana katika ugonjwa wake."[159]

---

[156] 2 Mambo ya Nyakati 14:11
[157] 2 Mambo ya Nyakati 14:12
[158] 2 Mambo ya Nyakati 16:9
[159] 2 Mambo ya Nyakati 16:12

Utawala wa Asa ulikuwa bora kuliko wa wafalme wengine wengi. Asa hakutelekeza kumsifu Yehova, lakini moyo wake ulikuwa umegawanyika dhidi ya Mungu. Alishindwa kumwamini Mungu kabisa. Asa hakuweza kufikia mafanikio mazuri ya Mungu.

Maisha ya Asa ni kielelezo cha nguvu cha hatari iliyoko katika moyo uliogawanyika. Katika kisa cha kwanza, Asa alimwamini Mungu kabisa. Katika kisa cha pili, aliendelea kutumika kama kiongozi wa watu wa Mungu, lakini moyo wake haukuwa mkamilifu. Badala ya kumtegemea Mungu kabisa, yeye alitengeneza muungano wa kijeshi na adui wa Mungu. Asa alikuwa na moyo uliogawanyika.

**Mfalme Amazia: Moyo uliogawanyika**

Amazia anaonyesha hatari ya moyo uliogawanyika. Utawala wa Amazia ulianza kwa nguvu kubwa: "Alifanya yaliyo mema machoni pa Bwana."[160] Kama ilivyokuwa kwa Asa, Amazia alianza vyema.

Hata hivyo, vitabu vyote viwili vya wafalme na Mambo ya Nyakati vinaonya kuhusu hatari iliyopo. Mwandishi wa kitabu cha Wafalme anasema Amazia alifanya yaliyo mema, "lakini siyo kama Daudi baba yake." Mwandishi wa kitabu cha Mambo ya Nyakati anasema kwamba Amazia alifanya yaliyo adili, "Lakini siyo kwa moyo mkamilifu." Hakuweza kubomoa "mahali pa juu." Kwa sababu ya hilo, watu waliendelea kutoa dhabihu zao kwa miungu ya uongo. Kiongozi mwenye moyo uliogawanyika hulipeleka taifa kwenye matatizo.

Kama Asa, Amazia aligundua kwamba kumtumikia Mungu kwa moyo uliogawanyika kunaleta matatizo. Ingawaje utawala wa Amazia ulianza vizuri, baadaye aliabudu miungu ya Edom. Katika hukumu, Mungu aliruhusu ufalme wa Kaskazini kumshinda Amazia. Ahadi ya mwanzo ya utawala wa Amazia kamwe haikutimia kwa sababu alikuwa na moyo uliogawanyika. Moyo wa Amazia haukuwa mkamilifu.

**Utakatifu katika vitendo: Utakatifu huanzia ndani ya Moyo**

Yesu alizungumza na viongozi wa dini waliokuwa waangalifu sana kuhusu muonekano wa nje, lakini wanafiki wa moyo.

> Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na Imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache. Viongozi vipofu, wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia![161]

Hawa wakuu wa dini walikuwa waangalifu sana katika kufuata sheria za dini, lakini hawakufuata sheria ya ndani iliyo muhimu. Yesu aliishutumu dini yao ya uongo.

[160] 2 Wafalme 14:3; 2 Mambo ya Nyakati 25:2
[161] Mathayo 23:23-24

"Unamchuja mbu (uko mwangalifu kwa mambo madogo tu), lakini unammeza ngamia (unadharau matatizo makubwa)." Utakatifu huanzia moyoni.

Kama tufikiria tu muonekano wa nje, tunaweza kusema:

- "Mimi ni mtakatifu kwa sababu sivai _______________."
- "Mimi ni mtakatifu kwa sababu siendi _______________."
- "Mimi ni mtakatifu kwa sababu siangalii _______________."

Tunapodai kuwa watakatifu kwa sababu ya mambo tunayoyatenda au tusiyoyatenda, Tunaweza kuwa kama Mafarisayo. Yesu alielezea kuhusu Farisayo aliyekuwa akiomba, "Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote."[162] Farisayo huyu aliufafanua utakatifu kwa matendo yake, "Mimi sidanganyi, ninafunga, ninatoa sadaka." Anadai kuwa mtakatifu, lakini moyo wake haukuwa mtakatifu.

Mafarisayo walikuwa wanajivunia kutengwa kwao na dunia, lakini mioyo yao haikuwa mitakatifu. Yesu alisema, "Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote."[163] Kwa nje, Mafarisayo walikuwa wametengwa; kwa ndani walikuwa wenye dhambi.

► Ni kipi kinaonekana rahisi kupima – muonekano wa nje au utakatifu wa ndani? Ni kipi rahisi kuigiza – muonekano wa nje au utakatifu wa ndani? Ni kipi tunapenda kuwekea mkazo sana – muonekano wa nje au utakatifu wa ndani?

**Mfano kutoka Hezekia**

Sheria ya kutengwa ilikuwa muhimu kwa kufundisha kwamba Mungu anahitaji watu watakatifu. Lakini Mungu alikuwa anahusika zaidi na mioyo ya watu wake kuliko ibada zao.

Masimulizi kutokana na uamsho wa Hezekia unaelezea kanuni hii. Baada ya hekalu kutakaswa, Hezekia aliirejesha Pasaka ya Wayahudi. Alilikaribisha taifa "kuja kwenye nyumba ya Bwana Yerusalemu ili kuiweka Pasaka kwa Bwana, Mungu wa Israeli." Wajumbe kutoka kwa Hezekia walisafiri nchi nzima wakiwakaribisha watu kwenye sherehe hii. Katika maeneo mengi, "watu waliwacheka kwa dharau na kuwadhihaki. Hata hivyo, watu Asheri, Manase, na Zabloni walijinyenyekeza wenyewe na kuja Yerusalemu."[164]

Walipoanza kuchinja kondoo wa Pasaka, "walikuwepo wengi ndani ya ukumbi ambao walikuwa bado hawajajiweka wakfu wenyewe." Kwa kuwa taifa lilishakaa muda mrefu sana bila kuwepo na ibada ya kuabudu hekaluni, watu walikuwa wamenajisika na

[162] Luka 18:11-12
[163] Mathayo 23:27
[164] 2 Mambo ya Nyakati 30:1, 10-11

hawakuwa tayari kushiriki Pasaka. Makuhani walipaswa wafanye nini? Mungu aliruhusu watu washiriki Pasaka kwa sababu mioyo yao ilimtaka Mungu, *ingawaje bado walikuwa hawajatakaswa.*

> Kwani wingi wa watu, naam, wengi wa Efraimu, na wa Manase, na wa Isakari, na wa Zabuloni, hawakujisafisha, lakini wakala pasaka, ila si kama ilivyoandikwa. Naye Hezekia alikuwa amewaombea, akisema, "Bwana mwema na amsamehe kila mtu, aukazaye moyo wake kumtafuta Mungu, Bwana, Mungu wa babaze, hata ikiwa si kwa utakaso wa patakatifu." Bwana akamsikia Hezekia, akawaponya watu.[165]

Mungu alikuwa anataka mioyo isiyogawanyika. Hata pale watu waliposhindwa kufuata ibada za kutengwa, Mungu aliangalia mioyo ambayo ilikuwa imejitenga kwa ajili ya kumtafuta Mungu.

**Watu watakatifu huitakasa mioyo yao kwa ajili ya Mungu**

Utakatifu **wakati wote** huanza na Mungu. Chochote kilicho kitakatifu ni mali yake. Mungu aliitakasa Sabato, ardhi kwenye kichaka kinachowaka, mzaliwa wa kwanza wa Israeli, Hema ya kuabudia, madhabahu, na Walawi. Mungu alifanya vyote hivi kwa ajili yake mwenyewe. Vilifanywa vitakatifu kwa uwepo wa Mungu.

Utakatifu unaanza na Mungu, lakini Mungu ametuita tujitakase kwa ajili yake. Kama tutaisoma aya ambayo Mungu anasema "Nitawatakasa," tunaweza tukaamua kwamba utakaso ni tendo la Mungu **peke yake**. Hata hivyo, Biblia inaonyesha kwamba, utakatifu unahitaji mwitikio kutoka kwa mtu mwenyewe.

Kutoka 19 kunatupa mfano. Mungu anamwagiza Musa, "Enenda kwa watu ukawatakase." "Kwahiyo, **Musa… alitakasa watu."** Musa aliwaweka watu kwa kusudi la Mungu. Baadaye Mungu alisema, "Makuhani nao, wamkaribiao Bwana, **na wajitakase**."[166] Makuhani waliagizwa kujiweka kando kwa ajili ya makusudi ya Mungu. Walipaswa wawe watakatifu; walipaswa wajitenge wenyewe kwa ajli ya Mungu.

Moyo usiogawanyika unahusisha masuala mawili:

1. Mungu aliahidi kuwatenga watu wake: "Mimi ndimi Bwana niwatakasaye ninyi."[167] Mungu huwafanya watu wake wawe watakatifu.

2. Mungu huwaagiza watu wake wajitenge kwa ajili yake. "Takaseni nafsi zenu basi; iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni Mtakatifu."[168]

[165] 2 Mambo ya Nyakati 30:18-20
[166] Kutoka 19:10-22
[167] Kutoka 31:13
[168] Mambo ya Walawi 11:44; 20:7

Tunajitakasa wenyewe **kama mwitikio wa neema ya Mungu**. Watu watakatifu kwa hiari yao wenyewe hujitakasa kwa Mungu. Wanajitoa wenyewe kwa Mungu **kwa moyo mkunjufu.**

Katika Walawi 20, **amri** hii "Jitakaseni wenyewe" inafuatiwa na **ahadi,** "Mimi ndimi Bwana niwatakasaye ninyi." Ni jina moja la Kiebrania linalofanana katika aya zote mbili. Zinaweza zikatafsiriwa kama ifuatavyo: "Jitengeni wenyewe… Mimi ni Mungu niwatengaye."[169]

Utakaso unahusisha **kwa pamoja** kazi ya Mungu na mwitikio wetu wenyewe. Hatufanyiki kuwa watakatifu kwa juhudi zetu wenyewe, wala hatusemi, "Kama Mungu akitaka niwe mtakatifu, atanifanya niwe mtakatifu bila ya mwitikio wangu." Tunaitikia neema ya Mungu kwa kujitakasa wenyewe kwa ajili yake. Moyo usiogawanyika unahitaji utakaso.

Utakatifu chimbuko lake ni Mungu mwenyewe. Hata hivyo, Mungu ametuita sisi tujitoe wenyewe kwake. Tunafanywa watakatifu tunapojitoa kwa ajili ya wito wa Mungu. Paulo aliandika, "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."[170] Paulo ametuita tujisalimishe kabisa kwa kusudi la Mungu. Kwa kuwa Mungu anaahidi kwamba atatufanya watakatifu, lazima tujisalimishe wenyewe. Utakatifu ni agizo ("jitakaseni wenyewe,") na ahadi ("nitawatakasa").

> "Tunaweza kutumiwa na Mungu peke yake baada ya kumruhusu atuonyeshe maeneo yaliyofichwa kwa undani ya tabia zetu. Hata hatutambui wivu, uvivu, au kiburi kati yetu tunapokiona. Lakini Yesu atatuonyesha kila kitu tulichoshikilia ndani yetu kabla neema yake haijaanza kufanya kazi."
> - Oswald Chambers

### Watu watakatifu wanasema "Ndio" iliyokamilika kwa Mungu

Maisha ya Sulemani, Asa, na Amazia yanaonyesha hatari ya moyo uliogawanyika. Moyo uliogawanyika siyo kusudi la Mungu kwa watu wake. Moyo mtakatifu ni moyo usiogawanyika. Kwa hiyo, inamaanisha nini kuwa na moyo usiogawanyika? Inamaanisha nini kuwa na moyo ambao ni *shalem* au "mkamilifu"?

Wakristo wanaitwa kuwa watumishi wa Mungu. Kazi ya mtumishi ni kufanya kile ambacho bwana wake humwagiza kufanya. Mtumishi mzuri haulizi, "Hiki ndicho nilichochagua?" Mtumishi mzuri hufanya kwa hiari kile ambacho bwana wake ameagiza kifanyike. Wajibu wa mtumishi ni kusema "ndiyo" iliyo kamili na isiyobadilika.

Kwa hali hiyo hiyo, mtu anayemtumikia Mungu kwa moyo usiogawanyika anaitikia "ndio" kwenye wito wa Mungu. Huu ni moyo usiogawanyika. Musa aliwataka Israeli wamtumikie Mungu kwa moyo usiogawanyika:

[169] Mambo ya Walawi 20:7-8, Tafsiri ya Biblia, *New Living*
[170] Warumi 12:1

> Na sasa, Israeli, Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia zake zote, na kumpenda, na **kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote**; kuzishika amri za Bwana na sheria zake, ninazokuamuru leo, upate uheri?[171]

> "Nimesema 'ndiyo' ya milele. Kamwe sitaangalia nyuma tena."
> - Elisabeth Elliot

Akiwa mwanafunzi wa chuo, Elisabeth Elliot aliandika kwenye kitabu chake cha kumbukumbu, "Bwana, nimesema 'ndiyo' ya milele. Kamwe, baada ya kuweka mkono wangu kwenye plau, nisiangalie nyuma. Ifanye inyooke njia ya msalaba mbele yangu. Nipe upendo, ambao hautatoa nafasi ya wazo la kurudi nyuma au hatua."[172] Elliot alikuwa na moyo usiogawanyika; alikuwa mkamilifu mbele ya macho ya Mungu.

Miaka iliyofuata baada ya maombi haya, Elizabeth Elliot alikutana na changamoto nyingi. Mume wake, Jim Elliot aliuawa mwaka 1956 alipokuwa akijaribu kufanya uinjilisti kwa kabila la Huaorani nchini Ecuador. Elizabeth baadaye alikuja kuwa mmishenari kwa watu waliomwua mume wake. Ni mtu tu aliyeweza kusema "ndiyo ya milele" anayeweza kwenda kama mmishenari kwa wauwaji wa mume wake.


Mtu mtakatifu humtumikia Mungu kwa moyo usiogawanyika. Mtu mtakatifu husema"ndio ya milele" kwa Mungu. Hii ina maana ya kujisalimisha kabisa kwa Mungu. Mtu mtakatifu anapoyajua mapenzi ya Mungu, kwa hiari hutii. Moyo wake haujagawanyika; ni wa Mungu kabisa. Mtu mtakatifu anasema "ndio" wakati wa kipindi cha kujisalimisha kabisa.

Mtu mtakatifu **huendelea kusema** "ndio" kila siku. Baada ya Elisabeth Elliot "kusema ndiyo ya milele" aliendelea kukutana na msongo wa maamuzi. Kulikuwa na nyakati nyingine anasema tena, "Ndiyo, Bwana". Wakristo wengi wanaamini kwamba "ndiyo ya mara moja tu" kutaondoa majaribu ya kujitoa kwako. Kujisalimisha ya mara moja tu ni jambo muhimu sana, lakini bado Shetani ataendelea kuleta majaribu kwenye kujitoa kwako. Zaidi na zaidi sana, utaendelea kusema, "Ndiyo Bwana. Maisha yangu ni yako wewe." Hii ni "ndiyo" Roho endelevu ya maisha.

---

171 Kumbukumbu la Torati 10:12-13
172 Elisabeth Elliot, *Passion and Purity* (Old Tappan: Fleming H. Revell Co., 1984), 25

## Aliipata Siri - George Muller



George Muller[173] alikuwa ni Mkristo aliyekuwa maarufu sana katika karne ya kumi na tisa.[174] Alijenga vituo vitano vya makazi ya watoto yatima na kuhudumia zaidi ya yatima 10,000. Muller alichangisha mamilioni ya dola kwa ajili ya kusaidia yatima na wamishenari wengine. Hadi wakati wa kifo chake, Muller alikuwa ametoa elimu kwa watoto 122,000, aligawa karibu Biblia 2,000,000, na zaidi ya vitabu na vipeperushi milioni 100. Alifanya hivi bila kuomba mchango wowote kutoka kwa mtu binafsi. Alidhamiria kumwomba Mungu tu kwa msaada.

Wakati Mungu alipomwita Muller kujenga makazi yake ya watoto, alikuwa na senti hamsini tu mfukoni mwake! Muller aliitikia wito huu wa Mungu akimtegemea Mungu kwa ufadhili wake wote. Muller alikuwa na senti hamsini tu – lakini aliitoa kwa Mungu na akamwamini Mungu katika mambo mengine yote yaliyosalia. Muller baadaye alikuja kutoa ushuhuda kwamba yatima wake hawakuwahi kukosa chakula; Mungu alitoa kila hitaji.

Muller aliishi maisha ya uovu akiwa kijana mdogo, akiwa ametumikia jela akiwa na umri wa miaka kumi na sita. Hata hivyo, akiwa na umri wa miaka ishirini, George Muller alimpa Yesu maisha yake. Kwa miaka kadhaa iliyofuata, Muller alikuwa na vipindi vya mafanikio ya kiroho, lakini pia akatambua maeneo ya mapambano. Mwishoni, akiwa na umri wa miaka ishirini na nne, Muller aliusalimisha kabisa moyo wake. "Nilijitoa kwa ukamilifu mwenyewe kwa Bwana."

Akiwa na miaka sabini, Muller alianza kusafiri nchi za nje kuhubiri. Katikati ya miaka sabini na themanini na saba, alikuwa amesafiri katika nchi arobaini na mbili na kuhubiria watu zaidi ya 3,000,000.

Mwishoni mwa maisha yake, George Muller aliulizwa siri ya maisha yake ya huduma. Alijibu, "Kuna siku ambayo nilikufa mwenyewe (mawazo na matamanio yangu), kwa dunia kuidhinisha au kutoidhinisha, na hata kwa kuidhinishwa au kulaumiwa na marafiki zangu. Nilichojali mimi ni kuidhinishwa na Mungu." George Muller alikuwa na moyo usiogawanyika. Alikuwa mkamilifu mbele ya macho ya Mungu.

[173] Image: "Mr George Muller" by Frank Holmes, *George Müller, The Modern Apostle of Faith* (1898), retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Mr_George_Muller.jpg, public domain.
[174] Kimenukuliwa kutoka Roger Steer, *Spiritual Secrets of George Muller* (PA: OMF Books, 1985) and J. Gilchrist Lawson, *Deeper Experiences of Famous Christians* (Anderson: Warner Press, 1911).

## Tafakuri ya Somo la 5

(1) Kuwa mtakatifu ni kuwa na moyo usiogawanyika.

(2) Neno *shalem* linamaanisha “isiyogawanyika.” Neno hili linalinganishwa na neno *shalom*, likimaanisha “amani.” Kuwa na “ukamilifu” au “kutogawanyika” moyo ni kuwa na moyo wenye uaminifu mmoja.

(3) Sulemani, Asa, na Amazia wanaonyesha hatari ya moyo uliogawanyika. Kila mmoja alishindwa kumpendeza Mungu kikamilifu kwa sababu mioyo yao ilikuwa imegawanyika.

(4) Utakatifu huanzia moyoni. Yesu aliwaangaliza wale wanaojali ibada ya nje bila ya moyo safi.

(5) Ni lazima tujiweke wakfu wenyewe kwa Mungu. Mungu huwatakasa watu wake. Mungu anawaita watu wake wajiweke wakfu wenyewe kama mwitikio wa neema yake.

(6) Watu watakatifu husema “ndio” iliyokamilika kwa Mungu. Kama mtumishi aliyejitoa, kwa hiari yao husema ndio kwa bwana wao.

(7) Baada ya kusema “ndiyo ya milele” ni lazima tuendelee kusema “ndiyo” kila siku.

## Kazi ya Kufanya

(1) Andaa fundisho kuhusu “Kuishi na Moyo Usiogawanyika.” Unaweza ukatengeneza muhtasari wako mwenyewe, au ukafuata muhtasari ufuatao:

A. Mfano wa kibiblia wa moyo uliogawanyika
B. Hatari za kuishi na moyo uliogawanyika
C. Tiba ya moyo uliogawanyika

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Zaburi 86:11-12.

# Somo la 6
# Utakatifu ni Haki na Uadilifu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Atambue kwamba uadilifu wa ndani ni lazima uonekane katika tabia ya nje.

(2) Kutumia kanuni za utakatifu katika maamuzi ya kimaadili kwa vitendo.

(3) Kutathmini maadili yake binafsi.

(4) Kukariri Mika 6:8.

## Ezekieli: Mtu aliyeuona mpango wa Mungu kwa ajili ya baadaye

Israeli haikuwa taifa takatifu tena. Iliabudu masanamu; Iligandamiza maskini, ilipuuzia Sabato. Katika hukumu, Mungu aliwapeleka watu wake uhamishoni. Mungu aliruhusu jeshi la Babeli kuipiga Yerusalemu na kuliharibu hekalu. Kwa kuwa watu wa Mungu hawakuwa watakatifu tena, hakuikubali tena ibada yao. Kwa kuwa watu wa Mungu hawakuwa tena wametengwa na dhambi, hakuikubali tena ibada yao.

Hata hivyo, bado Mungu alikuwa na kusudi na watu wake. Miaka kumi baada ya kuharibiwa kwa hekalu, Mungu alimpa maono Ezekieli, nabii aliyeishi kama mateka karibu na Babeli. Ezekieli aliyaona maono ya Mungu kwa ajili ya baadaye.

Katika maono ya Ezekieli, uhamisho umefika mwisho; Hukumu imemalizika; na uwepo wa Mungu umerudi. Hekalu limejazwa na utukufu wa Mungu. Mungu amewanyunyizia maji safi na kuwatakasa na uchafu wote wa nje wa ukosefu wa maadili. Ameondoa "moyo wa jiwe" na kuwapa "moyo mpya na roho mpya." Ametimiza ahadi yake kwamba, "Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda."[175] Israeli ni safi nje na ndani.

Ezekieli aliona hekalu lililobariki mataifa. Maji safi yakitiririka kutoka katika hekalu lililorejeshwa upya kuelekea Bahari Nyeusi. Miti ilitoa matunda kwa ajili ya chakula na majani kwa ajili ya tiba. Uzuri wa Edeni ulirejeshwa upya.

Sehemu ya kupendeza sana katika maono haya ni katika aya ya mwisho: "…na jina la mji huo tangu siku hiyo litakuwa hili, 'Bwana yupo hapa'" (Ezekiel 48:35). Kusudi la Mungu kwa watu wake limetimia: watu watakatifu wakiishi mbele ya Mungu mtakatifu!

[175] Ezekieli 36:25-27

► Jadili ushahidi mbalimbali wa nje kwamba mtu ni mtakatifu. Tutegemee matendo gani ya nje kutoka kwa mtu ambaye moyo wake ni mtakatifu?

## Matatizo ya Manabii: Israeli haikuwa na maadili

Manabii walileta mashitaka dhidi ya taifa ambalo lilikuwa limevunja agano. Katika Vitabu vya Manabii, kama ilivyo katika Vitabu Vitano vya Mwanzo vya Biblia, neno "mtakatifu" linarejea kitu ambacho ni mali ya Mungu na kilichotengwa kwa ajili ya Mungu. Yerusalemu na hekalu vilikuwa vitakatifu kwa sababu vilikuwa ni mali ya Mungu.

### Mungu ni Mtakatifu

Mara ishirini na moja, Isaya alizungumzia kuhusu "Mtakatifu wa Israeli." Maserafi waliimba: "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake!"[176]

Mungu ni ambaye "hujidhihirisha utakatifu wake katika haki."[177] Ezekieli aliiona siku ambayo Mungu ataudhihirisha utakatifu wake kwa mataifa yote. "Nami nitajitukuza, na kujitakasa, na kujidhihirisha, mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana."[178]

**Hukumu** za Mungu zinaonyesha asili yake ya utakatifu. Mika alionya kwamba, kutokana na dhambi ya Israeli, "Bwana anakuja akitoka mahali pake, naye atashuka, na kupakanyaga mahali pa dunia palipoinuka."[179] Mungu aliihukumu Israeli kwa sababu Mungu mtakatifu hawezi kuhurumia au kuachilia dhambi ipite bila kuadhibiwa.

**Ukombozi** wa Mungu kwa Israeli unaonyesha kwamba yeye ni mtakatifu. Mungu hakuikomboa Israeli kwa sababu alistahili kukombolewa, lakini ni kwa ajili ya jina lake takatifu miongoni mwa mataifa.

> …Bwana MUNGU asema hivi "Sitendi hili kwa ajili yenu, Ee nyumba ya Israeli, bali kwa ajili ya jina langu takatifu, mlilolitia unajisi katika mataifa mliyoyaendea. Nami nitalitakasa jina langu kuu, lililotiwa unajisi katika mataifa, mlilolitia unajisi kati yao…"[180]

Mungu asingeweza kukubali jina lake liaibishwe kwa sababu ya dhambi ya Israeli. Aliahidi kuirudisha Israeli katika ardhi yake kuonyesha utakatifu wake mbele ya mataifa mengine.

> Bwana MUNGU asema hivi: "Nitakapokuwa nimewakusanya nyumba ya Israeli, na kuwatoa katika watu ambao wametawanyika kati yao, na kutakasika kati yao

---

[176] Isaya 6:3
[177] Isaya 5:16
[178] Ezekieli 38:23
[179] Mika 1:2-3
[180] Ezekieli 36:22-23

> machoni pa mataifa, ndipo watakapokaa katika nchi yao wenyewe, niliyompa mtumishi wangu, Yakobo."[181]

Hii ni ahadi ya ajabu. Mungu aliahidi kuonyesha utakatifu wake kwa kuikomboa Isreli na kuirejesha nyumbani. Mungu aliahidi kuudhihirisha utukufu wake kwa watu wale wale alioamua kuwapeleka uhamishoni. Utakatifu ni wa Mungu.

**Israeli haikuwa Takatifu**

Kwa kuwa utakatifu ni wa Mungu, tunakuwa watakatifu pale tu tunapoishi kwenye mahusiano na Mungu mtakatifu. Manabii walitangaza kwamba Israeli siyo takatifu tena kwa sababu iliishi katika matamanio ya dhambi badala ya kuishi kwa utiifu na mahusiano ya upendo na Mungu.

Katika **Isaya**, Mungu alisema kwamba alikuwa ametengwa na Yuda kwa sababu ya dhambi yake. Mungu aliikataa Israeli kwa sababu haikukubali kuishi maisha ya haki na uadilifu.

> …kazi zao ni kazi za uovu, na vitendo vya udhalimu vimo mikononi mwao. Miguu yao hukimbilia mabaya, nao hufanya haraka kumwaga damu isiyo na hatia; mawazo yao ni mawazo ya uovu; ukiwa na uharibifu zaonekana katika njia kuu zao.[182]

Mungu alimwamuru **Yeremia** kuuficha mshipi wake. Kitani cheupe kilikuwa ni ishara ya usafi. Yeremia aliuficha ule mshipi hadi udongo na tope vikauharibu. Hii iliashiria Yuda kuwa mchafu. Mungu aliichagua Yuda iwe ni watu wa haki na uadilifu. Badala yake watu waliishi maisha ya dhambi.[183]

Katika **Ezekieli**, Mungu aliishutumu Israeli kama taifa la waasi wasumbufu; "walioasi kinyume changu."[184] Badala ya kumtii Mungu mtakatifu, Israeli iliishi kama mataifa ya kipagani. "Kwa maana hamuendi katika amri zangu, wala hamkuzishika hukumu zangu, bali mmetenda mambo kama hukumu za mataifa wanaowazunguka."[185] Israeli haikuwa tena yenye maadili na haki.

Wakati wakiwa uhamishoni, **Danieli** alikiri kwamba watu waliokuwa wamechaguliwa kumheshimu Mungu mbele ya mataifa wamefanyika kuwa ni "aibu ya wazi."[186] Kwa nini?

> Naam, Israeli wote wameihalifu sheria yako, kwa kugeuka upande, wasiisikilize sauti yako; basi kwa hiyo laana imemwagwa juu yetu, na uapo ule ulioandikwa katika sheria ya Musa, mtumishi wa Mungu; kwa sababu tumemtenda dhambi.[187]

---

[181] Ezekieli 28:25
[182] Isaya 59:6-7
[183] Yeremia 13:1-11
[184] Ezekieli 2:3
[185] Ezekieli 11:12
[186] Danieli 9:7

Manabii wadogo waliilaumu Israeli kwa dhambi yake. **Hosea** aliishutumu Israeli kwa "kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini;"[188] **Mika** aliwahubiri watu "wanaochukia mema, na kuyapenda mabaya."[189]

**Zephania** alikuwa ni wa ukoo wa Hezekia. Alikuwa ni wa familia iliyokuwa na nguvu sana katika Yuda, lakini hakusita kuilaumu Israeli kwa dhambi yake.

> Wakuu wake walio ndani yake ni simba wangurumao; makadhi wake ni mbwa-mwitu wa jioni; hawasazi kitu cho chote hata siku ya pili. Manabii wake ni watu hafifu, wadanganyifu; makuhani wake wamepatia unajisi patakatifu, wameifanyia sheria udhalimu.[190]

Kuanzia kwenye watawala wa kisiasa hadi viongozi wa dini, Israeli ilitenda dhambi kinyume na sheria za Mungu. Tatizo lilikuwa ni nini? Israeli ilisahau kwamba utakatifu ni kitu cha ndani mno kuliko kawaida *(taratibu)* za dini. Israeli ilibadilisha uadilifu na haki ya kweli kuwa sherehe tupu.

## Utakatifu ni zaidi ya Kawida za Dini na Taaluma

Kusudi mojawapo la sheria ilikuwa ni kuifundisha Israeli ijielewe kwamba yeye ni mali ya Mungu. Kwa bahati mbaya, Israeli katika muda mfupi sana ilisahau maana halisi ya sheria. Watu walifuata kawida za dini zilizokuwa sahihi lakini mioyo yao haikuwa mitakatifu. Taifa hili lililokuwa limetengwa na Mungu lionekane ni sura yake sasa limekuwa chafu *(najisi).* Vitabu vya Manabii vinafundisha kwamba kuwa mtakatifu inamaanisha kuwa mwenye uadilifu na haki ndani na nje yako.

Ezekieli alipelekwa Babeli mwaka wa 597 K.K. Wakati Ezekieli akiwa na miaka thelathini, Mungu alianza kuzungumza naye kupitia mfululizo wa ndoto. Ezekieli aliwaona viongozi wa Yuda wakiabudu sanamu katika Patakatifu pa Patakatifu.[191] Mungu akaamuru malaika kushusha hukumu hadi ua za ndani za hekalu zilipojaa miili iliyokufa. Utukufu wa Mungu uliondoka katika hekalu.[192] Hekalu pamoja na taratibu zake za kidini zilikuwa hazina maana yeyote kwa sababu watu walikuwa sio watakatifu.

### Maisha ya utakatifu ni zaidi ya Kawida za Kidini

Israeli ilijinasibu kwamba ni takatifu, lakini ilikuwa ni yenye dhambi na najisi. Watu walifuata kawaida za utakatifu, lakini hawakuishi maisha ya haki na uadilifu ya utakatifu. "Wamemwacha Bwana, wamemdharau yeye aliye Mtakatifu wa Israeli, wamefarakana

[187] Danieli 9:11
[188] Hosea 4:2
[189] Mika 3:2
[190] Zephania 3:3-4
[191] Ezekieli 8
[192] Ezekieli 10

naye na kurudi nyuma."[193] Watu walifuata kwa usahihi taratibu za dini, lakini wakaishi maisha ya dhambi. Manabii walifundisha kwamba taratibu za kidini zilikuwa hazina maana yeyote kama watu wa Israeli wataishi maisha ya dhambi. Utakatifu ni zaidi ya matamasha na dhabihu.

**Isaya** alisema kwamba Mungu amezikataa dhabihu za Yuda kwa sababu ya kutoishi maisha ya uadilifu na haki.

> Msilete tena matoleo ya ubatili…. siyawezi maovu hayo na makutano ya ibada. Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia; mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua.[194]

Akiwa amesimama mbele ya hekalu, **Yeremia** alitangaza, "Msitumainie maneno ya uongo, mkisema, 'Hekalu la Bwana, Hekalu la Bwana, Hekalu la Bwana ndiyo haya.'"[195] Hekalu lilikuwa siyo takatifu tena. Kwa nini? Kwa sababu watu wa kuabudu katika hekalu hawakuwa na maisha yenye haki na maadili tena. Mungu alionya, "Wafungapo, mimi sitasikia kilio chao; na watoapo sadaka za kuteketezwa na sadaka ya unga, sitazitakabali."[196] Mungu anahitaji zaidi ya taratibu za ibada zilizo tupu.

Mungu alimwamiba **Hosea**, "Nataka fadhili wala si sadaka; na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa."[197] Israeli ilitoa dhabihu, lakini ikavunja maagano yake na Mungu. Sadaka za kuteketezwa bila ya maisha ya haki na uadilifu hayana maana yeyote. Pamoja na Israeli kutoa dhabihu, Mungu "ataukumbuka uovu wao, na kuwapatiliza dhambi zao."[198] Kwa nini?

> Hapana neno ila kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu.[199]

**Amosi** alihubiri kwenye ufalme wa kaskazini muda mfupi kabla ya kutekwa na Waashuru. Amosi aliwapa nafasi ya mwisho ya kutubu. Amosi alikabiliana na Israeli kwa dhambi yake. "Watu wa Mungu" waliokuwa na nadhiri na Mungu walikuwa wenye hatia ya kila dhambi kuanzia kwenye mambo ya ajabu katika jamii hadi kwenye matendo ya aibu ya zinaa. Matajiri wa Israeli waliwatoza watu faini zisizo za haki, na kutumia fedha hizo kununulia mvinyo kwa ajili ya sherehe za kidini.[200] Kwa kuwa maisha yao yalishakuwa ya dhambi, ibada zao zilikuwa hazina chochote.

[193] Isaya 1:4
[194] Isaiah 1:13-14
[195] Jeremiah 7:4
[196] Jeremiah 14:12
[197] Hosea 6:6
[198] Hosea 8:13
[199] Hosea 4:1-2
[200] Kutoka 22:26; Amosi 2:8

> Mungu alisema: “Mimi nazichukia sikukuu zenu, nazidharau, nami sitapendezwa na makutano yenu ya dini. Naam, ijapokuwa mnanitolea sadaka zenu za kuteketezwa na sadaka zenu za unga, sitazikubali; wala sitaziangalia sadaka zenu za amani, na za wanyama walionona. Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu.”[201]

Hata baada ya kutoka uhamishoni, Yuda ilijaribu kufanya mbadala wa kawaida za kidini kugeuka kuwa utiifu kamili. Mwaka 516 K.K. watu walianza kulijenga upya hekalu. Ingawaje walikuwa wanaifanya kazi ya Kanisa, mioyo yao haikuwa mitakatifu. **Hagai** aliwakumbusha watu kwamba kuhani anayekamata kitu kilichokufa anafanyika kuwa najisi. Kwa jinsi hiyo hiyo, uchafu unaosababishwa na dhambi za watu kumeifanya kazi yao katika hekalu kuwa najisi.[202] Kawaida za dini bila haki na uadilifu ni ishara zilizo tupu; Utakatifu ni zaidi ya kawaida (taratibu) za kidini.

**Malaki** alionya kwamba Mungu ameikataa ibada ya Yuda. “Sina furaha kwenu, asema Bwana wa majeshi, wala sitakubali dhabihu yo yote mikononi mwenu.”[203] Mungu alikataa kupokea dhabihu ya Yuda kwa sababu ya dhambi za watu wake.

Vitabu vya Manabii vinaelezea waziwazi kwamba: Utakatifu ni zaidi ya kawaida za ibada. Mtu asiyeishi maisha ya uadilifu na haki, siyo mtakatifu. Hatuwezi tukamwabudu Mungu kwa mikono michafu.

### Maisha ya utakatifu ni zaidi ya kuliita Jina la Mungu

Mungu aliwakataa watu waliokuwa wakiliitia jina lake kwa sababu walikataa kuachana na dhambi zao. Katika Agano Jipya, Yesu alionya:

> Si kila mtu aniambiaye, “Bwana, Bwana,” atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, “Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?” Ndipo nitawaambia dhahiri, “Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”[204]

Utakatifu ni zaidi ya kulikiri jina la Mungu. Utakatifu ni haki ya ndani inayojidhihirisha katika tabia ya nje. Mungu anahitaji moyo mtakatifu na mioyo mitakatifu.

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

“Bwana mwenye upendo,
Nipe moyo imara uliotulia
Nipe moyo usioweza kushindwa;
Nipe moyo ulio mwadilifu.
Nipe ufahamu wa kukuelewa wewe,
Bidii ya kukutafuta wewe,
na uaminifu wa kukukumbatia wewe.”
- Kutoka Thomas Aquinas

---

201 Amosi 5:21-23
202 Hagai 2:10-14
203 Malaki 1:10
204 Mathayo 7:21-23

Kwa sasa, kama ilivyokuwa wakati wa **Yeremia,** Mungu anazungumza na wachungaji wanaojijengea majumba ya kifahari kutokana na sadaka za watu maskini. "Ole wake aijengaye nyumba yake kwa uovu. Na vyumba vyake kwa udhalimu."[205]

Kwa sasa, kama ilivyokuwa wakati wa **Amos,** Mungu anazungumza na waimbaji makanisani ambao wanaishi katika maisha ya dhambi. "Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu."[206]

Kwa sasa, kama ilivyokuwa wakati wa **Mika,** Mungu anazungumza na wafanyabiashara wanaojinadi wanaliitia Jina la Yesu lakini wanawadanganya wateja. "Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako."[207]

Utakatifu ni zaidi ya taratibu za dini au taaluma. Leo, kama ilivyokuwa wakati wa manabii, Mungu hutazama tabia yenye haki na uadilifu.

## Utakatifu ni Haki na Uadilifu

Moyo mtakatifu huonekana katika tabia ya uadilifu. Moyo mtakatifu huonekana katika mikono safi. Israeli isingeweza kujinasibu kwamba ni takatifu wakati inaishi maisha machafu yaliyokosa maadili na haki.

Kwa kuwa Mungu ni mwenye haki, watu wake ni lazima wawe na haki hiyo. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa na tabia ya Mungu wao. Wale wanaoabudu miungu wanachukua tabia ya asili ya miungu yao; wale wanaomwabudu Yehova wanapaswa wachukue tabia ya asili ya Yehova. Kusudi la Mungu ni kutengeneza watu watakatifu wenye uadilifu na haki.

Isaya alielezea asili ya Mungu. "Bwana ametukuka; kwa maana anakaa juu; amejaza Sayuni **hukumu na haki**."[208] Katika ujumbe huo huo, Isaya anamwelezea mtu mwenye haki na uadilifu anayeweza kuishi mbele za Mungu.

> Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao; ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele? Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili; ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma; akung'utaye mikono yake asipokee rushwa; azibaye masikio yake asisikie habari za damu; afumbaye macho yake asitazame uovu.[209]

Ni mtu yule mwenye haki na tabia njema ya Mungu anayeweza kuishi mbele ya uwepo wa Mungu. Watu wa Mungu hutenda kama Mungu anavyotenda; wanaakisi asili ya Mungu mtakatifu.

---

[205] Yeremia 22:13
[206] Amosi 5:23
[207] Mika 6:8
[208] Isaya 33:5
[209] Isaya 33:15

**Utakatifu ni Haki na Uadilifu wa ndani: Moyo**

Haki na uadilifu. huanzia ndani ya moyo. Manabii walitambua vizuri sana kwamba kawaida za sheria zenyewe zilikuwa hazijitoshelezi. Utiifu wa nje pasipo haki na maadili ya ndani huo ni unafiki. Haki na uadilifu huanzia moyoni.

Israeli iliikataa sheria kwa sababu ilimkataa Mungu ambaye aliwapa hiyo sheria. Kukosa utiifu kunaanzia ndani ya moyo. Israeli ilivunja amri za Mungu kwa sababu "mioyo yao iliandama vinyago vyao."[210] Mungu akaona kwamba mioyo yao ilikuwa ya hatia.[211]

Kutokutii kunaanzia ndani ya moyo; haki na maadili huanzia ndani ya moyo. Mungu alizungumza kupitia Isaya, "Nisikilizeni, ninyi mjuao haki, watu ambao mioyoni mwenu mna sheria yangu."[212] Wanaoijua haki ni wale ambao sheria ya Mungu iko ndani ya mioyo yao.

Yeremia na Ezekieli waliingalia siku ambayo sheria ya Mungu ingesimikwa ndani ya mioyo ya watu wa Mungu.

> Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; "Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu."[213]
>
> Nami nitawapa moyo mmoja, nami nitatia roho mpya ndani yao; nami nitauondoa moyo wa kijiwe katika miili yao, nami nitawapa moyo wa nyama; ili waende katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyatenda; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.[214]

Haki na uadilifu huanzia ndani ya moyo. Yoeli aliwaita watu watubu siyo kwa muonekano wa nje tu. Kufunga na kulia kunapaswa kutoke ndani ya moyo wenye toba.

> "Lakini hata sasa," asema Bwana, "nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu." Mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya.[215]

Muonekano wa nje tu hautoshi. Haki na uadilifu vinapaswa vianzie ndani ya moyo.

---

[210] Ezekieli 20:16
[211] Hosea 10:2
[212] Isaya 51:7
[213] Yeremia 31:33
[214] Ezekieli 11:19-20
[215] Yoeli 2:12-13

**Utakatifu ni Haki na Maadili ya nje: Mikono**

Katika Vitabu vya Manabii, tabia ya maadili ndiyo kijiti cha kupimia utakatifu. Utakatifu unahitaji tabia ya haki na mwenendo mzuri. Ufafanuzi rahisi sana katika Agano la Kale kuhusiana na maisha ya haki na uadilifu yanatoka katika kitabu cha Mika. Mika alifafanua mategemeo ya Mungu kwa watu wake.

> Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako?[216]

Hii ndiyo inayomaanisha jinsi ya kuishi maisha ya haki na uadilifu: **haki** na **rehema** kwa watu, na **unyenyekevu** kwa Mungu. Katika Vitabu vya Manabii, haki, rehema na unyenyekevu hufafanua maisha ya haki na uadilifu.

***Haki na Uadilifu ni Haki na Rehema kwa watu wengine***

Baadhi ya watu wanataka kutenganisha moyo na mikono. Wanasema, "Moyo wangu ni mtakatifu, lakini mikono yangu ni ya uovu. Nampenda Mungu kwa moyo wangu wote, lakini siishi maisha ya uadilifu na haki."

Vitabu vya Manabii havitoi mwanya kwa utengano huu. Moyo mtakatifu utaonekana kwa nje katika uadilifu na haki. Moyo msafi utasababisha matokeo ya tabia njema. Watu watakatifu wana mikono safi.

**Zakaria** anafafanua uadilifu na haki kama tabia iliyo safi kwa watu wengine.

> Bwana wa majeshi amesema hivi, ya kwamba, "Fanyeni hukumu za kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma; tena msimdhulumu mjane, wala yatima, wala mgeni, wala maskini; wala mtu awaye yote miongoni mwenu asiwaze mabaya juu ya ndugu yake moyoni mwake."[217]

**Amosi** alihubiri kwa taifa ambalo lilikuwa limesahau uadilifu na haki. Israeli iligeuza "hukumu kuwa uchungu, na kuiangusha haki chini." Nini suluhisho la uasi wa Israeli? "Hukumu na itelemke kama maji, na haki kama maji makuu."[218]

**Isaya** aliishirikisha shauku ya Amosi ya maisha ya uadilifu na haki. Ujumbe wa kwanza wa Isaya kwa Yuda kuhusiana na maisha ya uadilifu na haki:

> Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.[219]

---

[216] Mika 6:8
[217] Zakaria 7:9-10
[218] Amosi 5:7, 24

Mungu alizungumza na **Yeremia** kuitaka Yuda irudi kwenye hukumu na haki:

> Bwana asema hivi, "Fanyeni hukumu na haki, mkamtoe yeye aliyetekwa katika mikono ya mdhalimu; wala msiwatende mabaya mgeni, wala yatima, wala mjane, wala kuwadhulumu, wala msimwage damu ya mtu asiye na hatia katika mahali hapa."[220]

Kiwango cha Mungu kwa watu wake kilikuwa haki, uadilifu na rehema. Mungu aliwataka watu wake waishi maisha ya uadilifu na haki, watende kama Mungu anavyotenda.

### ***Haki na Uadilifu ni Unyenyekevu kwa Mungu***

Mungu huwaangalia watu ambao huwatendea watu wengine kwa haki na rehema; Hii ni lazima iwe msimamo wetu dhidi ya jirani zetu. Mungu anawatafuta watu ambao watatembea mbele yake kwa unyenyekevu; hii ni lazima iwe msimamo wetu na Mungu.

Yuda waliabudu miungu "juu ya mlima mrefu ulioinuka sana." Mungu alijibu kwa kuwakumbusha Yuda kwamba yeye peke yake ndiye aliye juu sana mahali palipoinuka.

> Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; "Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu."[221]

Tunamfikia Mungu aliye juu kupitia roho iliyopondeka na kuvunjika. Haki na uadilifu ni pamoja na unyenyekevu kwa Mungu. Huu ndio utakatifu wa kweli.

Hosea alihubiria taifa lililokuwa limeasi. Nabii alijua kabisa kwamba taifa lingeukataa ujumbe wake. Lakini pamoja na taifa kukataa kutubu, Hosea aliishia na mwaliko kwa kila Mwisraeli binafsi aliyekuwa anamtafuta Mungu. Ingawaje taifa linaweza likamkataa Mungu, mwenye uadilifu na haki bado anaweza kutembea katika njia za Mungu. Mungu atamheshimu mtu atakaye mheshimu yeye. Mungu ambariki mtu anayetembea katika uadilifu na haki.

> Ni nani aliye na hekima, naye atayafahamu mambo haya? Ni nani aliye na busara, naye atayajua? Kwa maana njia za Bwana zimenyoka, nao wenye haki.[222]

## Utakatifu katika Utendaji: Maadili ya Maisha Matakatifu

Utakatifu unaanzia ndani ya moyo, lakini unaonekana kwa tabia za nje. Wakati wa kuliweka hekalu wakfu, Sulemani aliwapa watu changamoto, "Mioyo yenu na iwe kamili kwa Bwana, Mungu wetu, **kuenenda katika sheria zake, na kuzishika amri zake**,

---

[219] Isaya 1:16-17
[220] Yeremia 22:3
[221] Isaya 57:7, 15
[222] Hosea 14:9

kama ilivyo leo."[223] Utakatifu wa ndani huleta matokeo ya utakatifu wa nje; kama ni mtakatifu kwa ndani, utaishi kwa uadilifu na haki katika maisha ya nje.

Manabii walipinga mafundisho ya wale waliokuwa katika Israeli zamani wakifundisha kwamba watu wa Mungu walikuwa hawana ulazima wa kutii sheria za Mungu. Manabii wanapinga wale walioko katika kanisa la leo wanaofundisha kwamba Wakristo hawawezi kutimiza maagizo yote ya Mungu kwa ajili ya kuishi maisha matakatifu.

Wahubiri wengi wa leo wanafundisha, "Sheria za Mungu zinasema tuishi maisha ya uadilifu na haki, lakini anajua kwamba huwezi ukatimiza sheria zake." Huo haukuwa ujumbe wa manabii. Manabii walisema, "Sheria ya Mungu inatutaka tuishi maisha ya uadilifu na haki; hivi ndivyo anavyotaka Mungu. Watu wa Mungu watatii amri za Mungu."

Mfano kutoka Amri za Musa utaonyesha jinsi moyo mtakatifu unavyogusa maisha yetu ya kila siku. Mungu alisema, "Usimdhulumu jirani yako, wala kumnyang'anya mali yake; ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi."[224] Katika ulimwengu wa zamani, mfanyakazi alikuwa analipwa kila mwisho wa siku. Hakukuwa na akaunti za hundi au kadi za mikopo. Malipo ya Jumatatu ndiyo ya kununulia chakula cha Jumanne. Kushindwa kumlipa mfanyakazi kila siku kuliwaletea changamoto ya kujinunulia chakula. Sheria ikasaema, "Mlipe mfanyakazi wako kila mwisho wa siku. Mfanya biashara mwenye uadilifu na haki atawatendea wafanyakazi wake kwa haki."

Tumeona msisitizo juu ya maadili, haki na rehema kutoka kwa manabii. Katika Agano Jipya, Nyaraka za watu wote zinashirikisha ujumbe unaofanana. Hii inaonekana kwa uwazi sana katika Waraka wa Yakobo. Yakobo aliandika kwa wale waliokuwa wakijinadi kwamba ni watoto wa Mungu, lakini hawakuishi maisha ya haki na uadilifu. Anaonyesha kwamba utakatifu wa kweli unaonekana katika kuishi maisha ya haki na uadilifu.

- Watu watakatifu wana zaidi ya kufanya kuliko wanaokiri utauwa; wanaishi maisha ya kimungu. "Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu."[225]
- Watu watakatifu wanaonyesha huruma kwa yatima na wajane. "Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."[226]
- Watu watakatifu hawana upendeleo kwa maskini au matajiri. "Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji."[227]

---

[223] 1 Wafalme 8:61
[224] Mambo ya Walawi 19:13
[225] Yakobo 1:22
[226] Yakobo 1:27
[227] Yakobo 2:9

- Watu watakatifu wanatawala kunena kwao. "Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu."[228]
- Wafanya biashara watakatifu watawatendea wafanyakazi wao kwa uadilifu na haki. "Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliozuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi."[229]

> "Utakatifu inamaanisha
> msafi kabisa ninapotembea kwa miguu,
> msafi kabisa ninapoongea kwa ulimi wangu,
> msafi kabisa ninapotafakari kwa akili zangu –
> kila undani wa maisha chini ya uchunguzi wa Mungu."
> - Oswald Chambers

Utakatifu huleta mabadiliko katika kila eneo la maisha tunayoishi, ikijumuisha biashara na kazi zetu. Mtu mtakatifu ataishi kwa uadilifu na haki. Tukiwa watakatifu mbele za Mungu, tutafanya yaliyo sahihi kwa watu wengine. Ujumbe wa manabii na mitume uko wazi: Moyo mtakatifu hubadilisha matendo yetu. Watu watakatifu watakuwa wenye haki na uadilifu katika maeneo yote ya maisha yao. Kusudi la Mungu ni kuwafanya watu wawe waadilifu na wenye haki kwa pamoja katika mioyo na maisha yao ya kila siku.

Haki na uadilifu vinaonekanaje katika maisha yako ya kila siku? Utakatifu unaonekanaje katika mwingiliano wetu wa kila siku na dunia inayotuzunguka? Tuangalie mifano halisi. Mifano yote hii inatokana na watu waliojinasibu kwamba wao ni watakatifu. Majina yamebadilishwa, lakini kwa masikitiko historia zote ni za kweli.

Mchungaji Tom ni mjenzi. Kazi yake ya ujenzi huisaidia huduma yake ambayo yeye ni mchungaji katika kanisala Holiness. Tom alinunua chombo cha kujengea cha $100. Alikitumia kujengea nyumba yake na baadaye akawa hakihitaji tena. Alipokuwa tayari kuuza kile chombo alimwambia mnunuzi kwamba, "Kilipokuwa kipya, nilikinunua kwa bei ya $200. Sasa nitakiuza kwa bei ya $150."

Mchungaji Tom anasema, "Hii ni biashara nzuri. Nilipata faida kwa kuikuza ile bei niliyonunulia. Hahitajiki mtu kujua. Hata hivyo, nitaitumia hiyo fedha kwa ajili ya kazi ya Mungu." Mungu anasema, "Watu watakatifu ni waaminifu wanaposhughulika na biashara zao." Paulo aliandika:

> Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake.[230]

Jane ni karani wa biashara. Wakati mchungaji wake alipomtembelea nyumbani, alisema, "Kama utahitaji vifaa kutoka ofisini kwangu, ninaweza kukupa. Huwa ninaleta kalamu za

---

[228] Yakobo 3:2
[229] Yakobo 5:4
[230] Wakolosai 3:9

penseli, vifaa vya kuandikia, na vifaa vingine vya ofisi kutoka kazini kuja nyumbani. Hakuna mtu anayegundua."

Jane anasema, "Hicho ni kitu kidogo sana." Mungu anasema, "Watu watakatifu ni waaminifu hata kwenye vitu vidogo." Paulo aliandika kwamba, "wale wote walioumbwa kwa mfano wa Mungu katika haki, uadilifu na utakatifu" wataishi kwenye njia nyingine nyeupe:

> Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.[231]

Bill anaendesha biashara. Ni lazima aweke kumbukumbu na kulipa mapato kila mwisho wa mwaka. Mwaka jana, Bill alitengeneza faida ya $50,000 kutoka katika biashara yake, lakini alipokwenda kulipa mapato, alitoa taarifa ya kupata faida ya $40,000. Mara nyingine hutoa rushwa kwa maafisa wa serikali ili apate mikataba mizuri.

Bill anasema, "Ninajua ni namna gani biashara zinafanyika katika nchi yangu. Ni lazima 'nitie mafuta kwenye magurudumu' kwa ajili ya biashara yangu. Kando ya hayo, ninalipa zaka na kutumia fedha zangu kwa ajili ya madhumuni mengine." Mungu anasema, "Watu watakatifu ni waaminifu wanapohusika na serikali yao." Paulo aliandika kwa wenyeji wa Dola la Kirumi kwamba, "Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu."[232]

Linda haifurahii kazi yake. Anataka autumie muda wake kwa kufanya kazi za kanisani. Badala yake, ana kazi ya kufanya usafi kwenye majumba ya watu matajiri. Analipwa mshahara kwa kufanya kazi kuanzia saa 8 asubuhi hadi saa 11 jioni, lakini mara nyingi hurejea amechelewa sana na huondoka alfajiri sana. Linda akamwambia mchungaji wake, "Ningependa niweze kutumia muda wangu asubuhi kwa kuomba na niende kazini nimechelewa. Ningependa nitoke mapema kazini ili nije kanisani jioni. Sijali kama nitafanya kazi katika masaa yote ninayolipwa kazini au laa."

Linda anasema, "Tajiri yangu hawezi kujua kama sifanyi kazi masaa yote." Mungu anasema, "Watu watakatifu ni waaminifu katika maadili ya kazi. Wanafanya kwa uzuri wote popote pale Mungu anapowaweka." Paulo aliandika:

> Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo.[233]

---

[231] Waefeso 4:24, 28
[232] Warumi 13:1
[233] Wakolosai 3:22-24

Arthur ni mmishenari. Anampenda Mungu na anafanya kazi kwa bidii sana, lakini ulimi wake ni mwepesi sana. Mara nyingi, watu wa karibu naye wamekuwa wakiumizwa na maneno yake makali.

Arthur anasema, "Ninasema kile ninachokifikiri! Inabidi unikubali jinsi nilivyo. Mungu anasema, "Watu watakatifu hutawala midomo yao." Yakobo aliandika:

> Nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu.… Kwa huo twamhimidi Mungu Baba yetu, na kwa huo twawalaani wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haifai mambo hayo kuwa hivyo.[234]

► Katika mila yako, ni maeneo gani yenye majaribu ya kimaadili kwa Waristo? Ni maeneo gani Wakristo wana majaribu mengi yanayoonyesha kukosa uaminifu katika maisha yao ya kila siku? Ni kwa jinsi gani ujumbe wa maisha ya utakatifu yanagusa haya maeneo ya majaribu?

## Aliipata Siri - Chiune Sugihara

Chiune Sugihara alikuwa Mkristo wa Japani akifanya kazi katika Wizara ya mambo ya Nchi za nje Manchuria. Mwaka 1939, alipelekwa Lithuania kuwa balozi wa Japani katika nchi hiyo. Akiwa kule alikutana na dada wa Kiyahudi na akapata kuelezwa jinsi serikali ya Wanazi ya Kijerumani ilivyokuwa inawatendea Wayahudi.

Sugihara aliwasiliana na serikali ya nchi yake akiomba ruhusa ya kuwapa visa wakimbizi wa Kiyahudi waliokuwa wanaikimbia Ujerumani na Poland. Serikali ya Japani ililikataa ombi la Sugihara.

Kwenye majira ya joto ya mwaka 1940, Sugihara alitambua kwamba alipaswa kudhihirisha haki na rehema. Alimwambia mke wake, "Sitaki kuacha kuwa mtiifu kwa serikali yangu, lakini *siwezi* kukosa utiifu kwa Mungu. Nitaifuata dhamira yangu."

Sugihara alianza kutengeneza visa za kutoka za wakimbizi. Inakisiwa kwamba, aliweza kuokoa maisha ya zaidi ya Wayahudi 10,000 ambao walikuwa hatarini kuuawa na Hitla. Baadaye, Sugihara alikamatwa na jeshi la Warusi na akatumikia miezi kumi na nane katika jela za Urusi. Alipoachiwa kutoka jela na kurudishwa Japani, Wizara ya Mambo ya nchi za nje ilimfukuza kazi kwa sababu alikiuka maagizo yao.

> "Watu wote wa Mungu ni watu wa kawaida ambao wanafanywa kuwa siyo wa kawaida kwa ajili ya makusudi yaliyotengwa kwa ajili yao."
> - Oswald Chambers

Baada ya kuwa amefukuzwa kazi, Sugihara alikuwa hana njia nyingine ya kuishi. Alipata matatizo makubwa hata namna ya kuinunulia familia yake chakula. Wakati wazaliwa wa

[234] Yakobo 3:6-10

Kiyahudi aliowaokoa walipokuja kumtafuta baadaye, serikali ya Japai ilikanusha kwamba kamwe haijawahi kufanya kazi naye. Mwishowe, katika mwaka 1968, manusura mmoja wa Kiyahudi alimpata Sugihara na akampeleka Israeli.

Sugihara alitambuliwa kidogo sana na dunia kwa jinsi alivyojitoa sadaka, lakini alimtii Mungu kwa sababu alikuwa mwenye haki. Sugihara alitambua kwamba mtoto wa Mungu ni lazima aishi kwa uadiifu na haki. Hakuweza kuvumilia kuona mateso ya wale waliokuwa wanamzunguka. Alijua kwamba kuwa mwadilifu na mwenye haki ni lazima uweze kutenda haki, kupenda rehema na kutembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu. Chiune Sugihara aliishi maisha ya utakatifu.

**Agizo la kutii ninaye - Charles Wesley**

Agizo la kutii ninaye, Mungu wa kumtukuza
Roho ya kuokoa isiyokufa kamwe, na kuiweka kwa ajili ya mbingu.

Kutumika wakati huu, kuutimiza wito wangu:
Oh, naomba nguvu zangu zote zitumike kwa ajili ya kufanya mapenzi ya Bwana!

Nilinde kwa ulinzi wenye wivu, na uweponi mwako niishi;
Oh, na kwa mtumishi wako, Bwana, andaa maelezo ya kutiisha niyatoe!

Nisaidie jinsi ya kukesha na kuomba, na nikutegemee wewe.
Kwa uhakika, kama nitasaliti utii wangu, nitakufa milele.

**Tafakuri ya Somo la 6**

(1) Kuwa mtakatifu ni kuwa mwenye haki na uadilifu, kwa pamoja nje na ndani.

(2) Israeli iliruhusu ibada na taaluma kuwa badala ya uadilifu na haki.

(3) Bila maisha ya uadilifu na haki, kawaida za ibada na taaluma hazina maana yeyote.

(4) Haki na uadilifu ni lazima utoke ndani – lazima iwe ni utii kutoka moyoni.

(5) Haki na uadilifu lazima zionekane kwa nje – lazima ziweze kuleta mguso kwa wale walio karibu nasi.

(6) Manabii walifundisha kwamba Mungu anahitaji mambo matatu ya mtu mwenye haki na uadilifu:

- Haki kwa watu wengine
- Rehema kwa watu wengine
- Unyenyekevu kwa Mungu

(7) Nyaraka za Agano Jipya zinajirudia-rudia katika ujumbe wake wa kuishi maisha ya haki na uadilifu. Mtu mtakatifu anapaswa aishi maisha yenye maadili na haki.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Andika insha yenye kurasa 2-3 kuhusiana na "Haki na uadilifu katika dunia ya sasa." Chukua eneo moja ambalo dhambi ya maadili imekubalika kama jambo la kawaida, na uoneshe Biblia inafundishaje katika eneo hili la dhambi. Toa maelekezo ya vitendo kwa ajili ya watu unaowahudumia.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Mika 6:8.

# Somo la 7
# Utakatifu ni Kumpenda Mungu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Atathamini uzuri wa uhusiano wa upendo pamoja na Mungu.

(2) Kufuata mfano wa Yesu kama alivyompenda Baba kwa ukamilifu wote.

(3) Kutambua kwamba ulimwengu na sheria kwa pamoja ni dalili na sababu kuu za uharibifu.

(4) Kukariri Marko 12:29-31.

## Ayubu: Mtu aliyempenda Mungu

Ayubu alikuwa amepoteza kila kitu. Utajiri wake ulitoweka. Watoto wake waliuawa kwa upepo wenye nguvu. Afya yake iliharibiwa. Alikaa kwenye majivu akikuna majipu yaliyomtoka mwilini kwa kigae. Mke wake alimtaka amlaani Mungu ili afe. Marafiki zake walimlaumu kwamba ni mwenye dhambi za kutisha. Wale waliokuwa wanamheshimu siku za nyuma sasa wakaanza kumdhihaki.

Katika mateso yake, Ayubu haombi kwamba, "Mungu rudisha utajiri wangu," au "Mungu niponye mwili wangu." Badala yake Analia, "Laiti ningejua mahali niwezapo kumwona, Nifike hata hapo anapokaa!"[235] Ayubu Analia kwa sababu hamwoni tena Mungu aliyekuwa amekaa naye kwa ukaribu sana. "Tazama, naenda mbele, wala hayuko; Narudi nyuma, lakini siwezi kumwona; Na mkono wa kushoto, afanyapo kazi, lakini siwezi kumwona; Hujificha upande wa kuume, hata nisimwone."[236]

Ayubu anakumbuka siku za nyuma: "Hapo siri ya Mungu ilipokuwa hemani mwangu."[237] Lakini sasa:

> Yeye amenibwaga topeni, Nami nimekuwa kama mavumbi na majivu. Nakulilia wewe, wala huniitikii; Nasimama, nawe wanitazama tu. Wewe umegeuka kuwa mkali kwangu; Nawe waniudhi kwa uweza wa mkono wako.[238]

Hiki ni kilio cha mtu anayejisikia kusalitiwa na rafiki yake wa karibu sana. Ni kilio cha mtu aliyempenda Mungu.

---

[235] Ayubu 23:3
[236] Ayubu 23:8-9
[237] Ayubu 29:4
[238] Ayubu 30:19-21

Kisa hiki cha Ayubu hakijaishia kwa kukata tamaa. Baada ya Mungu kumjibu Ayubu kutoka katika upepo wa kisulisuli, Ayubu alimjibu, "Nilikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio; Bali sasa jicho langu linakuona."[239] Ayubu alifarijiwa siyo kwa kurejeshewa kwa mali zake, afya, au hata familia yake, bali kwa kurejea tena uwepo wa Mungu. Ayubu alifarijika alipomwona Mungu. Ayubu alikuwa mtu mtakatifu; Ayubu alimpenda Mungu.

## Utakatifu ndani ya Vitabu Vya Mashairi: Kumpenda Mungu

► Inamaanisha nini kumpenda Mungu? Ni kwa vipi kumpenda Mungu kwa uthabiti kunaweza kugusa vipaumbele vyako vya muda na fedha? Ni kwa vipi kumpenda Mungu kunaweza kugusa mtazamo wako wa maagizo yake?

Kitabu cha Ayubu na cha Zaburi vinarudia ujumbe tuliouona kwenye Vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia: utakatifu ni mahusiano na Mungu. Sisi tunafanyika watakatifu tu pale tunapokuwa kwenye mahusiano na Mungu. Kuwa mtakatifu maana yake ni kumpenda Mungu kwa ukamilifu wote.

Henoko, Nuhu, na Ibrahimu walikuwa watakatifu kwa sababu walitembea na Mungu. Kwa namna hiyo hiyo, Ayubu na Daudi walikuwa watakatifu kwa sababu walitembea na Mungu. Kitabu cha Ayubu kinaelezea kisa cha mtu ambaye alimpenda Mungu hata kupitiliza. Kitabu ha Zaburi kina maombi na nyimbo za mtu ambaye furaha yake kubwa ilikuwa ni ushirika wa karibu sana uliokuwepo kati yake na Mungu.

### Watu Watakatifu wana furaha Ndani ya Mungu

Watu watakatifu wana furaha ndani ya Mungu; wanaipata furaha yao ya ndani kutoka kwake. Matamanio yanayomtawala mtu mtakatifu ni kumpendeza Mungu.

Kwa wale wanaoupima utakatifu kupitia orodha ya vitu vya "kufanya na kutofanya," inaonekana kama ni rahisi tu. Watu wengi wanafikiri kwamba utakatifu ni jambo tu la kufanya kama wajibu kuliko furaha. Maandiko yanaonesha kwamba watu watakatifu wana furaha ndani ya Mungu. Ayubu hakutaka kitu chochote zaidi ya kurejeshewa uhusiano wake na Mungu. Daudi anashuhudia kuwepo kwa uhusiano wa karibu sana na Mungu. Aliipata furaha yake kubwa ndani ya Mungu.

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Mungu wangu,
Ninaomba kwamba niweze kukujua na kukupenda ili niweze kufurahi katika wewe.
Ruhusu akili yangu iweze kutafakari juu ya uzuri wako.
Achilia ulimi wangu uzungumzie hayo.
Acha moyo wangu uishi kwa hilo.
Acha nafsi yangu ione njaa kwa hilo.
Acha utu wangu wote utamani hilo,
hadi nitakapoingia katika furaha yako."
- Anselimu wa Canterbury

[239] Ayubu 42:5

Nilikuwa nafundisha kwenye jiji moja ambalo maji yake ya kunywa yalikuwa siyo salama. Siku moja ya joto, nilisahau kuchukua chupa yangu ya maji ya kunywa. Wakati nilipomaliza kufundisha, nilikuwa na wazo moja tu, "ninahitaji maji!" Kama ungenipa chaguo la $100 au glasi ya maji masafi, ningelichagua maji. Wakati nilipokuwa na kiu hasa, maji yalikuwa ni muhimu kuliko kitu kingine chochote.

Usiku ule, nilijiulza mwenyewe, "Je, ninayo kiu ya Mungu kama nilivyokuwa na kiu ya maji leo? Je, Mungu ana umuhimu wowote kwangu kuliko kitu chochote katika dunia hii?"

Daudi alimwonea Mungu shahuku. "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu. Nafsi yangu inamwonea kiu MUNGU, Mungu aliye hai."[240] Daudi alilinganisha kiu yake kwa Mungu na ile ya paa anayekimbia. Matamanio makubwa ya paa anayekimbia ni maji; matamanio makubwa ya mtu mtakatifu ni kuwa katika mahusiano ya karibu sana na Mungu. Mtu mtakatifu "ni mwenye njaa na kiu ya haki."[241]

Zaburi inalinganisha furaha ya watenda dhambi na ile ya watakatifu wa Mungu. Watenda dhambi furaha yao ni vita; wanafurahia uongo; wanapenda kulaani.[242] Kwa ulinganifu, watu watakatifu wanapata "furaha tele" mbele ya Mungu; wanapenda "makao ya nyumba yako, Na mahali pa maskani ya utukufu wako."[243] Mtunga Zaburi ameamua, "Wala duniani sina cha kupendeza ila Wewe."[244] Watakatifu huipata furaha yao ya ndani sana ndani ya Mungu.

Zaburi ya 63 inaonyesha uzuri wa kumtafakari Mungu. Daudi alikuwa anakimbia kutoka kwa Sauli. Maisha yake yalikuwa hatarini. Katika hali hiyo, utafikiria nini? Nitajaribiwa kutafakari juu ya hiyo hatari. Daudi anasema, "Ninapokukumbuka kitandani mwangu, Nakutafakari Wewe makesha yote ya usiku." Hata katika hatari, mawazo ya Daudi yalimwelekea Mungu. Alijikuta kutafakari huku kukimridhisha "kama kushiba mafuta na vinono."[245]

Mwimbaji wa Zaburi alikuwa na furaha ndani Mungu; alikuwa na upendo kwa Mungu. Watu wa Mungu hufurahia katika Bwana. Fikiria kidogo: Ni nini kinachokupa kiu? Je, uanayo furaha ndani ya Mungu?

### Watu wa Mungu hufurahi ndani ya Sheria za Mungu

Mtu mtakatifu hufurahi ndani ya Sheria za Mungu. Katika Zaburi inaonesha kwamba sheria za Mungu siyo tishio kwa watu wake; watakatifu huzipenda sheria za Mungu. Daudi

[240] Zaburi 42:1-2
[241] Mathayo 5:6
[242] Zaburi 68:30; 62:4; 109:17
[243] Zaburi 16:11; 26:8
[244] Zaburi 73:25
[245] Zaburi 63:5-6

alisema "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu."[246] Hakuwa na mapambano ya kumwamini Mungu; Alipata furaha katika utiifu wake kwa Mungu.

Furaha katika sheria za Mungu zinaonekana katika kitabu chote cha Zaburi. Zaburi ya 119 ni neno la Mungu. Isikilize furaha ya Daudi:

- Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako.[247]
- Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu, Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.[248]
- Rehema zako zinijue nipate kuishi, Maana sheria yako ni furaha yangu.[249]
- Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.[250]
- Ee Bwana, nimeutamani wokovu wako, Na sheria yako ndiyo furaha yangu.[251]

***Sheria ya Mungu hudhihirisha Upendo wa Mungu.***

"Bwana, dunia imejaa fadhili zako, Unifundishe amri zako."[252] Mungu huonesha upendo wake kupitia sheria zake: "Kama zilivyo rehema zako umtendee mtumishi wako, Na amri zako unifundishe."[253] Watu watakatifu hufurahi katika amri za Mungu kwa sababu wanafahamu kwamba sheria ya Mungu hudhihirisha upendo wa Mungu.

Musa alisema kwamba, utii wa Israeli kwa sheria za Mungu kutafanya mataifa mengine yaone wivu kwa hekima yao!

> Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, "Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili."[254]

Musa akauliza, "Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama Torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo?"[255] Sheria ya Mungu haikuwatumikisha Israeli; sheria ya Mungu iliwabariki Israeli.

> "Tunafikria kwamba chochote kisichopendeza ni jukumu letu! Hicho chochote siyo kama roho wa Mungu wetu? 'Ninafurahia kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu.'"
> - Oswald Chambers

Leo, ni jambo la kawaida kusikia wahubiri wakifundisha kwamba sheria ya Mungu ilikuwa ni mzigo mkubwa ambao isingewezekana kuutii. Baadhi ya Wakristo wanasema kwamba sheria ya Mungu ni "lengo" mbalo hakuna mtu anayeweza kulifikia. Hata hivyo, Musa, Daudi na watakatifu wengine katika Agano la Kale

[246] Zaburi 40:8
[247] Zaburi 119:18
[248] Zaburi 119:72
[249] Zaburi 119:77
[250] Zaburi 119:97
[251] Zaburi 119:174
[252] Zaburi 119:64
[253] Zaburi 119:124
[254] Kumbukumbu la Torati 4:6
[255] Kumbukumbu la Torati 4:8

walifurahia katika sheria za Mungu. Waliamini kwamba ilikuwa ni furaha kuheshimu jina la Mungu na Sabato. Hawakupenda kuiinamia miungu ya sanamu.

Hawakuamini kama wangeweza kuwa na furaha zaidi kwa kutowatii wazazi wao, kufanya mauaji na uzinzi, au kuiba na kusema uongo. Walijua ni vyema mtu kuwa na kitu chake kuliko kuwa na tamaa na alicho nacho jirani yake. Sheria ya Mungu haikuwa mzigo. Mungu alitoa amri yake kutoka ndani ya moyo wa upendo. Sheria iliwaongoza watu watakatifu kwenye mahusiano yao na Mungu. Sheria ya Mungu ilikuwa ni furaha kwa watu wake.[256]

***Sheria ya Mungu hudhihirisha Tabia ya Mungu.***

Kama tukimpenda Mungu, tutaipenda na sheria yake. Mtunga Zaburi alikiri, "Shuhuda zako ni za ajabu, Ndiyo maana roho yangu imezishika."[257] Daudi hakusema, "Sheria yako ni ngumu, lakini nitajaribu kuitii." Hapana. Daudi alisema, "Sheria ya Mungu ni ya ajabu!"

Watu watakatifu hufurahia sheria ya Mungu. Mtunga Zaburi aliipenda sheria ya Mungu kwa sababu alijua kwamba sheria ni zaidi ya msururu wa masharti; Sheria ya Mungu hudhihirisha tabia ya Mungu.

► Soma Zaburi 111 na 112.

Zaburi 111 na 112 ni Zaburi washirika. Kwa pamoja, zinaonyesha umuhimu wa sheria za Mungu kwa mtu mtakatifu. Zaburi ya 111 inaelezea tabia ya Mungu: Mungu ni mwadilifu na mwenye haki, ni wa neema na rehema.

Zaburi ya 112 inaanza, "Heri mtu yule amchaye Bwana, apendezwaye sana na maagizo yake!" Mtu anayefurahishwa na maagizo ya Mungu atabarikiwa. Vipi? Atafanana na Mungu. Atakuwa na "neema, huruma na haki." Hizi ni tabia zile zile zinazomwelezea Mungu katika Zaburi ya 111. Tunapofurahia katika sheria za Mungu, tunafanana zaidi na Mungu.

Vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia vinafundisha kwamba mtu mtakatifu huakisi sura ya Mungu. Zaburi 111 na 112 zinaonyesha kwamba mtu anayefurahia sheria za Mungu hubadilishwa kuwa katika sura ya Mungu. Mtu anyefurahia sheria za Mungu hufanana zaidi na Mungu.

Kama kweli tunampenda Mungu, tutazishika sheria za Mungu. Daudi aliuliza, "Ni nani atakayepanda katika mlima wa Bwana? Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake?" Ni nani atakayekaa katika uwepo wake? "Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe..."[258] Kuishi kwenye uwepo wa Mungu, kunahitaji utii katika sheria za Mungu. Vitabu vya

---

[256] Kimenukuliwa kutoka: Dennis F. Kinlaw, *This Day with the Master* (Grand Rapids: Zondervan, 2004).
[257] Zaburi 119:129
[258] Zaburi 24:3-4

Mashairi vinaonyesha kwamba Mungu anahitaji utiifu kwa wale wanaofikiri kwamba wao wanampenda Mungu.

Vitabu hivi pia vinaonyesha kwamba Mungu hufanya utii kuwa kitu kinachowezekana. Hii ni ahadi ya Mungu kwa wale wanaompenda.

Kisa cha Ayubu kinaanza na, "Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi, jina lake alikuwa akiitwa Ayubu; mtu huyo alikuwa mkamilifu na mwelekevu, ni mmoja aliyemcha Mungu, na kuepukana na uovu."[259] Wakati Elifasi alipomshutumu Ayubu kama mtenda dhambi, Ayubu alijibu:

> Mguu wangu umeshikamana sana na hatua zake; Njia yake nimeishika, wala sikukengeuka. Sikurudi nyuma kuiacha amri ya midomo yake; Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu.[260]

Mtu fulani anaweza kuuliza, "Inawezekanaje Ayubu aseme kwamba hajavunja amri za Mungu? Kila siku mtu anatenda dhambi." Ayubu anajibu, "Ninampenda Mungu na nina furaha ya kuwa mtiifu kwake." Ayubu alitembea kwa ukaribu sana na Mungu. Aliweka "amri kinywani mwake," Je, maisha ya utakatatifu yanawezekana? Ayubu anajibu, "Ndiyo." Ayubu anatambua kwamba Mungu hufanya utii wa kuaminika uwe ni kitu kinachowezekana kwa wale wampendao yeye.

Maisha ya utakatifu hayategemei nguvu zetu; yanakuja kwa kumtegemea Mungu kila iitwapo leo. Ayubu alikuwa mtu asiyelaumika siyo kwa sababu alikuwa na nidhamu ya kawaida. Alikuwa asiyelaumika kwa sababu ya uhusiano wake wa karibu wa kutembea na Mungu. Ayubu alielewa kwamba Mungu anahitaji utii wa kuaminika ***na*** kwamba yeye Mungu hufanya utii wa kuaminika uwe ni kitu kinachowezekana.

Ukweli huu una mguso wa nguvu sana katika maisha ya kila siku ya mwamini. Mungu anahitaji watu wake wawe watakatifu ***na*** Mungu huwafanya watu wake wawe watakatifu. Ni kwa kupitia yeye kwamba tunafanywa watakatifu na wasafi. Mungu anataka utakatifu na Mungu hutoa utakatifu. Mungu hutoa kila kitu ambacho Neno lake huhitaji.

### Wote wanaofurahi katika Bwana wanapokea haja za mioyo yao

Zaburi ya 37 inaonyesha matokeo ya kufurahi katika Bwana. "Nawe utajifurahisha kwa Bwana, Naye atakupa haja za moyo wako."[261]

Baadhi ya wasomaji wanafikiri kwamba Zaburi 37:4 hufundisha, "Kama nitamtumikia Mungu, atanipa kila kitu nitakachoomba. Atanifanya niwe tajiri." Daudi hafundishi injili ya mafanikio inayosema, "Mungu anataka watu wake wawe matajiri." Daudi anazungumzia

---

[259] Ayubu 1:1
[260] Ayubu 23:11-12
[261] Zaburi 37:4

jambo lenye maana na umuhimu mkubwa zaidi: “Kama shahuku yako kubwa ni Mungu, Mungu atajitoa mwenyewe kwako.” Kama unamtamani Mungu, utampata Mungu.

Kama utamfuata Mungu ili uweze kupata afya, utajiri, na umashuhuri, utakatishwa tamaa na andiko hili la Zaburi 37:4. Kama unamfuata Mungu kwa ajili ya baraka za mwilini, utakatishwa tamaa utakapokuja kutambua kwamba zawadi yako ni… Mungu!

Kwa mtu mwenye ubinafsi, kumpokea Mungu siyo zawadi kubwa kwake. Mtu mwenye ubinafsi hana tamanio la kumhitaji Mungu. Lakini kwa mtu anayemtamani Mungu, Zaburi 37:4 ni ahadi kubwa kwake. Kwa mtu mtakatifu, Mungu ni zawadi kubwa kwake inayowezekana.

Kwa wale wanaomtamani yeye, Mungu hujitoa kwa uhusiano wa karibu sana na yeye mwenyewe. Siyo kila wakati kufurahi katika Bwana kunaleta baraka za kifedha au uhuru kutokana na mapito. Watu wanaofurahi katika Bwana wanaweza kuchukizwa na maadui zao. Watu watakatifu mara nyingi ni watu wanaopitia katika mapito makali. Hata hivyo, Daudi na Ayubu waligundua kwamba hata katika nyakati za mapito makali, Mungu anawaheshimu wale wanaofurahia katika yeye

Utakatifu ni kumpenda Mungu. Watu watakatifu hufurahi katika Bwana; na Mungu naye, hujitoa mwenyewe kwa wale wenye njaa na kiu kwa ajili yake.

### Utakatifu ndani ya Vitabu Vya Injili: Kumpenda Mungu

Mwanasheria mmoja wa dini alimwuliza Yesu, “Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?” Yesu akarejea kwenye sheria ya Musa kumjibu, “Imeandikwa nini katika Torati? Wasomaje?”

Mwanasheria alikuwa amenukuu kutoka katika Kumbukumbu la Torati 6:5 na Mambo ya Walawi 19:18. Maandiko haya yanatoa muhtasari wa sheria. “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.” Yesu akamwambia, “Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi.”[262] Utakatifu ni upendo kamili.

Miezi michache baadaye, Yesu alikuwa Yerusalemu. Mwandishi mmoja akamwuliza, “Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?”[263] Mafarisayo waliorodhesha amri zote 613 kutoka katika Agano la Kale. Mara kwa mara walikuwa wakibishana ni amri ipi iliyokuwa kuu na muhimu zaidi kuliko nyingine. Yesu akawajibu:

> Ya kwanza ndiyo hii, “Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa

[262] Luka 10:25-28
[263] Marko 12:28

> akili zako zote, na kwa nguvu zako zote." Na ya pili ndiyo hii, "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi.[264]

Yesu alifafanua utakatifu kama upendo kwa Mungu na upendo kwa watu wengine Utakatifu wa kweli huthibishwa katika upendo. Tunakua katika utakatifu kama tunavyokua katika upendo wa kumfanania Kristo. Kuwa mtakatifu ni kuwa na upendo kama vile naye Yesu alivyokuwa na upendo; huu ni upendo kamili.

Kwenye somo la 5, tuliona kwamba waandishi wa Agano la Kale walitumia neno "mkamilifu" kurejea kwenye moyo ambao haujagawanyika. Kuwa mtu mkamilifu ni kutogawanyika katika kuwajibika kwake kwa Mungu. Waandishi wa Agano Jipya wanatumia neno "mkamilifu" katika maana hiyo hiyo. Yesu aliwaagiza wafuasi wake "kuwa wakamilifu."[265] Kwenye Vitabu vya Injili, tunaona kwamba kuwa mkamilifu ni kuwa na upendo usiogawanyika kwa Mungu au kwa majirani zetu. Kuwa mkamilifu ni kupenda bila kujibakiza. Huu ndiyo upendo kamili.

Ujumbe wa upendo mkamilifu haukuwa mpya kwenye Vitabu vya Injili. Yesu aliikumbusha Israeli kwamba Mungu siku zote anahitaji upendo kwa ajili yake kama Mungu na upendo kwa ajili ya majirani zetu. Kumbukumbu la Torati 6 inaonyesha kwamba upendo ndiyo msingi wa sheria. Utii bila upendo unasababisha ushikiliaji mno wa sheria. Yesu alifundisha kwamba kuwa mtakatifu ni kumpenda Mungu. Kama tukimpenda Mungu, tutamtii yeye. Utakatifu ni kumpenda Mungu kwa moyo wako wote.

Kumpenda Mungu ni zaidi ya kuwa na mhemuko au hisia. John Wesley alifafanua upendo kwa Mungu:

> ….kufurahi katika Bwana, ni kufurahi katika mapenzi yake, kutamani wakati wote kumpendeza yeye, kuomba na kutafuta furaha yetu katika yeye, na kuwa na kiu ya ujazo kamili wa kumfurahia yeye mchana na usiku.[266]

Upendo kwa Mungu huleta mabadiliko kabisa ya mwelekeo wetu wa maisha. Kumpendeza Mungu kunakuwa ndiyo lengo letu la juu na furaha yetu kubwa. Yesu alionyesha inamaanisha nini katika kumpenda Mungu kwa ukamilifu. Ndani ya Yesu, tunaona upendo mtakatifu ambao Mungu anataka uwe kwa kila Mkristo.

### Yesu alidhihirisha upendo kamili kwa Mungu katika maisha yake

Yesu alidhihirisha upendo kamili kwa Baba yake. Yesu aliishi katika furaha ya kujikabidhi kabisa kwa mapenzi ya Baba yake. Kujikabidhi huku hakukuwa kwa kulazimishwa kama mtumwa; ilikuwa ni kujikabidhi kwa upendo kutoka kwa mtoto.

---

[264] Marko 12:29-31

[265] Mathayo 5:48

[266] John Wesley, "On Love." Retrieved from http://wesley.nnu.edu/john-wesley/the-sermons-of-john-wesley-1872-edition/sermon-139-on-love/ December 21, 2019.

***Majaribu yalionyesha upendo wa Yesu kwa Baba***

Kabla hajaanza huduma yake nje, Yesu alikutana na jaribu jangwani. Kila jaribu lilikuwa limelengwa kuharibu uhusiano kati ya Baba na Mtoto.

Shetani alimjaribu Yesu ili avuke mipaka ya Baba yake na ajitengenezee mkate kwa ajili yake mwenyewe. Shetani alimjaribu Yesu aachane na kumwabudu Baba yake ili achukue mamlaka juu ya falme zote za dunia. Shetani alimjaribu Yesu ili amjaribu Baba yake kwa kuruka kutoka juu ya kinara cha hekalu.[267] Kila jaribu lilikuwa ni kipimo cha upendo wa Yesu kwa Baba yake. Yesu alijibu kwa kuonyesha utiifu wake kamili kwa Baba yake wa mbinguni.

Badala ya kugeuza mawe yawe mkate, Yesu alinukuu andiko la Kumbukumbu ya Torati 8:3: "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu,'" Musa aliwakumbusha wana wa Israeli kwamba Mungu ametoa mana jangwani; Israeli imwamini Baba yao mtoaji. Kwa njia hiyo hiyo, Yesu aliamini utoaji wa Baba yake.

Badala ya kumsujudia Shetani, Yesu alinukuu andiko la Kumbukumbu la Torati 6:13; "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Kwa kuwa alimpenda Mungu kwa ukamilifu, Yesu alikataa jaribio lolote la kumtaka amsujudie Shetani.

Badala ya kumjaribu Baba yake kwa kuruka kutoka kinara cha hekalu, Yesu alinukuu andiko kutoka Kumbukumbu la Torati 6:16, "Tena imeandikwa, 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.'" Kwa kuwa alimpenda Mungu kwa ukamilifu, Yesu alikataa jaribio lolote la kutaka kuvunja ahadi ya Baba yake ya ulinzi.

***Utakaso wa Hekalu unaonyesha Upendo wa Yesu kwa Baba yake.***

Hata wakati akiwa mtoto, Yesu aliipenda Nyumba ya "Baba yake."[268] Alimpenda Baba yake, kwa hiyo aliipenda pia nyumba ya Baba yake.

Wakati Yesu alipowakuta wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kwenye hekalu, aliwajibu kwa hasira ya haki.

> Akafanya kikoto cha kambaa, akawatoa wote katika hekalu, na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao.[269]

Kwa nini yesu alikasirika? Ni kwa sababu wafanyabiashara hawakuiheshimu nyumba ya Baba yake. Akawaambia, "msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara."[270] Yesu alimpenda Baba yake na akalipuka kwa hasira ya nyumba ya Baba yake kuvunjiwa heshima.

---

[267] Luka 4:1-12
[268] Luka 2:49
[269] Yohana 2:15
[270] Yohana 2:16

Yesu pia alikuwa na hisia za kawaida za kibinadamu. Mbele ya maovu, alijisikia hasira, lakini bila kutenda dhambi.[271] Utakatifu haukuondoa hisia za Yesu. Badala yake, kwa kuwa alikuwa mtakatifu, hisia zake ziliakisi hisia za Baba yake. Yesu alikuwa na hasira katika mambo ambayo yanamchukiza Baba yake.

### *Kutii kwa Yesu kunaonyesha Upendo wake kwa Baba*

Kwenye ujumbe wake wa kuaga, Yesu aligusia kuhusu utii wake kama ushuhuda wa upendo wake kwa Baba yake. "Lakini ulimwengu ujue ya kuwa nampenda Baba; na kama vile Baba alivyoniamuru; ndivyo nifanyavyo."[272] Yesu aliudhihirsha upendo wake kwa Baba kupitia utii wake wa hiari kwenye mapenzi ya Baba. Huu ni upendo kamili.

Hata alipokuwa katika majaribu, Yesu alikuwa mtiifu kwenye mapenzi ya Baba yake. Yesu alijua anaenda kukutana na kesi ya aibu ikifuatiwa na maumivu yasiyoelezeka ya msalaba. Atatengwa na Baba yake kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu. Yesu aliomba, "Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki..."[273] Yesu wa Nazarethi alikabiliana na jaribu kubwa la utii wake kwa Baba yake.

Katika ubinadamu wake, Yesu aliomba kwa ajili ya ukombozi. Lakini katika ubinadamu wake, Yesu alionyesha utii wake wa hiari kwa kwa Baba. "…Hata hivyo, siyo kwa mapenzi yangu, bali mapenzi yako yatimizwe." Yesu alionyesha upendo kamili kwa ajili ya Baba kupitia utiifu wake kwenye mapenzi ya Baba.

Maisha ya Yesu yanatoa mfano wa kuigwa na watu wengine wa upendo kamili. Kuwa mtakatifu ni kumpenda Mungu kama Yesu alivyompenda Baba yake.

### Yesu aliwafundisha wafuasi wake kumpenda Mungu kikamilifu

Kumpenda Mungu ni zaidi ya kuwa na hisia. Ni kujikabidhi kwa muda mrefu kunakoleta mabadiliko katika masuala muhimu ya maisha yetu. Yesu alifafanua upendo kwa jinsi hii:

> Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. Mtu ye yote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.[274]

Kwa waalimu wa Kiyahudi, neno "chuki" linamaanisha "kupenda kidogo kuliko kitu kingine." Mfuasi wa Yesu ni lazima ampende Yesu kuliko vitu vingine vyote, hata kuliko yeye mwenyewe. Hiyo ndiyo inamaanisha kumpenda Mungu – kumpenda Mungu juu ya vitu vingine vyote.

---

[271] Marko 3:5; Waefeso 4:26
[272] Yohana 14:31
[273] Luka 22:42
[274] Luka 14:26-27

Yesu alisema, "Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu."[275] Upendo ni wa pekee. Kama unampenda Mungu, anachukua nafasi ya kwanza juu ya kila kitu katika maisha yako.

Yesu alifundisha kwamba, uaminifu na utii wa hiari ni kielelezo cha upendo. "Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye." Zawadi ya upendo huu wa hiari ni uhusiano wa karibu sana na Mungu. "naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."[276]

Miaka mingi baadaye, Yohana aliyakubuka maneno ya Yesu katika chumba cha juu. Yohana aliandika, "Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli."[277] Utakatifu ni upendo mkamilifu kwa Mungu. Watu watakatifu kwa hiari yao hujikabidhi kwenye mapenzi ya Baba. Watu watakatifu huiga mfano wa Yesu wa utii.

Wakati tunapompenda Mungu kwa ukamilifu wote, tunafurahia kuyatii mapenzi yake. Tunapompenda Mungu kwa ukamilifu wote, kwa hiari yetu tunakabidhi mapenzi yetu kwenye mapenzi ya Baba. Tunapompenda Mungu kwa ukamilifu wote, tunaomba pamoja na Daudi:

> Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele![278]

Upendo uliokamilika unatupa shahuku kubwa ya kumfurahisha Baba yetu wa mbinguni. Tunakataa kila kitu kinachoweza kuvuruga uhusiano wetu na yeye. Utakatifu ni upendo mkamilifu kwa Mungu.

**Uhusiano kati ya Yesu na Baba ni mfano wa kuigwa kwa Wakristo**

► Soma Yohana 17.

Yesu alitoa picha ya utakatifu kwenye maombi yake ya kikuhani mlimani. Katika Yohana 17, Yesu alijiombea mwenyewe, aliombea wanafunzi wake, na aliombea waamini wote. Yesu alionyesha kwamba uhusiano wake wa karibu na Baba ni mpangilio wa uhusiano kati ya Wakristo na Baba yetu.

---

[275] Luka 16:13
[276] Yohana 14:21
[277] 1 Yohana 2:5
[278] Zaburi 139:23-24

***Yesu alijiombea mwenyewe (Yohana 17:1-5)***

Katika kukabiiana na kifo, Yesu alifurahia kwamba amekamilisha kazi ambayo Baba alimtuma kuifanya. "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye."

Baadaye katika maombi haya, Yesu akasema, "Najiweka wakfu mwenyewe," Neno la Kigiriki kutafsiri "wakfu" ni sawa na neno lililokuja baadaye katika tafsiri la "utakaso" katika aya hiyo hiyo. Yesu aliomba: "Uwatakase (***hagiazo***) kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli; Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni. Na kwa ajili yao najiweka wakfu (*hagiazo*) mwenyewe, ili na hao watakaswe (*hagiazo*) katika kweli."[279]

*Hagiazo linaweza* kumaanisha aidha "kufanya takatifu" au "kutengwa." Kwa kuwa Yesu hakuwa na dhambi, hakuhitaji afanywe mtakatifu. Katika sala hii, "utakaso" inamaanisha "kuwekwa wakfu au kutengwa." Yesu alijitenga ili kuikamilisha kazi ambayo Baba alimpa kuifanya. Yesu alijitakasa mwenyewe kwa ajili ya lile jukumu ambalo Baba alikuwa amemkabidhi.

***Yesu aliwaombea Wanafunzi wake (Yohana 17:6-19)***

Yesu aliomba kwamba wanafunzi watakaswe katika kweli. "Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli." Kama vile Yesu alivyotengwa kwa ajili ya kazi duniani, aliomba kwamba wanafunzi watengwe kwa ajili ya huduma. Uhusiano kati ya mtoto na Baba ulikuwa ni mfano wa kuigwa kwa ajili ya mahusiano kati ya wanafunzi na Baba. Kama wanafunzi walivyofuata mtindo wa Yesu, walitengwa ili kushiriki ukweli wake na dunia.

***Yesu aliomba kwa ajili ya Waamini wote (Yohana 17:20-26)***

Kisha Yesu akaomba kwa wote "wale watakaoniamini kwa sababu ya neno." Aliomba kwamba Wakristo wote washiriki umoja ule ambao yeye na Baba yake waliufurahia. Yesu aliomba kwamba "wawe wamoja waliokamilika." Hili neno ni sawa na lile linalotumika katika Mathayo 5:48: "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Hili neno linaashiria kukamilika kwa lengo lililokusudiwa. Lengo hilo ni upendo mkamilifu, upendo unaoonekana ndani ya Utatu Mtakatifu wa Mungu.

Sisi kama waamini tunaalikwa kushiriki kwenye upendo mtakatifu wa Baba na Mwana. Yesu aliomba, "ili pendo lile (Baba) ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao." Upendo kati ya Yesu na Baba ni mwelekeo wa kufuatwa na kila mwamini. Hii ndiyo maana ya kuwa mtakatifu: kuwa na upendo mkamilifu kama ulivyooneshwa na Yesu.

---

[279] Yohana 17:19

## Utakatifu katika Vitendo: Je, ninampenda Mungu?

George alikuwa na swali kwa mchungaji wake. "Mchungaji, nataka niwe mtakatifu. Kama Ibrahimu, nataka niwe rafiki wa Mungu. Lakini kuna tatizo. Ninafanya mambo ninayojua kwamba ni mabaya. Ninampenda Mungu, lakini sitaki kumtii. Je, ninaweza kuwa rafiki wa Mungu kama sitamtii yeye?"

Yesu alijibu swali la George zaidi ya miaka 2,000 iliyopita. "Mkinipenda, mtazishika amri zangu."[280] Hakuna mahali popote Yesu anaposema, "Ukinipenda, unaweza kuendelea kuishi maisha ya kujitakia ya dhambi." Badala yake, Yesu alisema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Yesu akaendelea kusema, "Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu."[281]

Baadhi ya Wakristo waliokwisha kumkiri Kristo, huzungumzia kuhusu upendo wao kwa Mungu ili hali wanaendelea kuishi katika dhambi za kujitakia. Kwa watu hawa, kumpenda Mungu kupo katika mhemuko tu. Wanadai kumpenda Mungu, lakini hawana mabadiliko katika maisha yao. Hata hivyo, kumpenda Mungu ni zaidi ya mhemuko au kuwa na hisia. Kumpenda Mungu kunahitaji utii katika amri zake.

Sally alikuwa na swali kwa mchungaji wake, "Mchungaji, nataka niwe mtakatifu. Kama Ayubu, nataka nisiwe wa kulaumiwa na niwe na msimamo. Niko makini sana katika kuishika kila sheria ya Mungu. Lakini kuna tatizo. Kiuhalisia simpendi Mungu. Ninamtii kwa sababu ya hofu kwamba anaweza kuwa mwenye hasira kama sitatii. Ninamtii Mungu, lakini simpendi. Je, ninaweza kuwa mtakatifu kama simpendi Mungu?"

Yesu alilijibu hili swali la Sally zaidi ya miaka 2,000 iliyopita. Yesu alitoa ujumbe kwa kanisa la Efeso. Aliwapongeza kwa kazi zao nzuri na kwa kuwa na imani inayokubalika. Aliwapongeza kwa uaminifu wao wakati wa kukabiliana na mateso kwa ajili ya imani yao. Lakini, alisema, "Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza." Yesu alizingatia kwa makini ukosefu wa upendo kiasi cha kuonya kwamba "Nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake," kama hawatataka kutubu na kuurejesha upendo wao wa kwanza.[282]

Baadhi ya Wakristo huamini kwamba wanaweza kuupata upendeleo wa Mungu kupitia utii, lakini utii wao haukamilishwi na upendo. Wanaamini kwamba utakatifu ni suala la kuwa mtiifu kwa baadhi ya sheria. Wamesahau kwamba chimbuko la utakatifu ni upendo kwa ajili ya Bwana.

Moyoni, wote George na Sally wana tatizo moja la msingi linalowasumbua; hakuna hata mmoja anayempenda Mungu. Ukosefu wa upendo kwa Mungu kutoka kwa George

[280] Yohana 14:15
[281] Yohana 14:24
[282] Ufunuo 2:2-5

unaonekana kwenye mambo ya kidunia, "Ninaupenda ulimwengu huu kuliko ninavyompenda Mungu."

Ukosefu wa upendo kwa Sally unaonekana katika kushikilia sheria sana. Kushikilia sheria sana kunasema, "Ninamtii Mungu, siyo katika upendo lakini ni kwa ajili ya matamanio ya kupata upendeleo wa Mungu." Hakuna hata moja katika haya linalochochewa na upendo kutoka kwa Mungu. Majibu kwa haya yote mawili yanafanana – upendo kwa Mungu.

**Jawabu kwa Mambo ya Dunia: Kumpenda Mungu**

Inamaanisha nini kuwa wa kidunia? Mara nyingi, tunafafanua mtu wa kidunia kwa kuangalia mavazi, aina za sherehe, kutamani kuthibitika kwa watu, kujionyesha, au alama nyingine za nje. Hizi zinaweza kuwa ni ***dalili*** za kuwa kidunia, lakini kuwa mtu wa kidunia ina maana ya ndani zaidi. Hili hapa ni swali la kusaidia kufafanua kidunia: "Ni nini kinachoniletea furaha ya kweli?"

Kuwa wa "kidunia" ni furaha ya ulimwengu huu. Mtu wa kidunia hutafuta utoshelevu mkamilifu katika dunia hii. Kuwa kidunia ni kuthamini mambo ya dunia hii kuliko mambo ya Mungu.

Lutu "akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji." Alichagua bonde ambalo macho yake yalimvutia.[283] Lutu alikuwa mdunia; Alifurahia sana starehe za dunia hii.

Dema aliiacha huduma kwa sababu aliipata furaha katika dunia hii. Paulo aliandika, "Maana Dema aliniacha, ***akiupenda ulimwengu huu wa sasa***, akasafiri kwenda Thesalonike," mji wa mafanikio.[284] Dema alikuwa mdunia; aliupenda ulimwengu huu.

Watu wa Mungu hutafuta furaha yao ya ndani kutoka kwa Mungu. Mwimba Zaburi aliandika, "Wala duniani sina cha kupendeza ila Wewe."[285] Mtunga Zaburi alikuwa mtu wa Mungu; alimpenda Mungu.

Jawabu la u-dunia siyo msururu wa amri. Jawabu sahihi la u-dunia ni upendo wa Mungu. Mchungaji mmoja Mskoti wa karne ya 19, Thomas Chalmers, alihubiri somo juu ya "Nguvu ya Kutosha katika Upendo Mpya." Mchungaji Chalmers alisema kwamba kuna mambo mawili tunayopaswa kufanya kama tunataka kuachana na kuipenda dunia:

1. Ni lazima tuachane na kitu fulani. Ni lazima tutambue utupu wa dunia hii. Kama tunavyoona ubatili wa vitu vya dunia hii, upendo wetu kwa dunia hii hupungua. Lakini hilo peke yake haitoshi.

[283] Mwanzo 13:10-11
[284] 2 Timotheo 4:10
[285] Zaburi 73:25

2. Ni lazima tuwe na kitu fulani. Ni lazima tubadilishane upendo wa dunia hii na kitu kingine kinachopendeka zaidi. Tunapoingia kwenye mapenzi na Mungu, upendo wetu mpya hutimulia mbali upendo wa zamani wa dunia.

Tiba ya kuipenda dunia ni kuingia kwenye urafiki na Mungu. Yesu alitoa mfano wa mfanyabiashara mmoja aliyekwenda kuuza alivyokuwa navyo vyote ili aweze kwenda kununua lulu moja ya thamani.

> Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara, mwenye kutafuta lulu nzuri; naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua.[286]

Fikiria kama ungetamka haya kwa huyu mfanyabiashara, "Ninakusikitikia sana. Inasemekana kwamba ilibidi uuze vitu vyako vyote." Mfanyabiashara atakucheka! Atakuambia, "Sadaka? Sijatoa sadaka; mimi ninanunua lulu ya thamani kubwa. Vitu nilivyouza siyo ***chochote*** ukilinganisha na hii lulu nzuri." Mfanyabiashara amepata mpenzi mpya. Ameangukia kwenye upendo mpya ambao umefukuza upendo wa zamani.

Jawabu la kuwa wa kidunia ni kuingia kwenye mapenzi mapya na Mungu. Upendo kwa Mungu utafukuza upendo wetu wa kupenda fedha, wa kupigiana makofi, wa kujisifia na kwa mambo yote ambayo dunia inatumia ili kuwashawishi watu wa Mungu. Watu watakatifu wanampenda Mungu – na kwamba upendo wa Mungu huondosha kabisa kuipenda dunia hii.

**Jawabu la Kushikilia Sheria: Kumpenda Mungu**[287]

Wakati tunapokusudia kwa dhati kuishi maisha matakatifu, tunaweza kujaribiwa kuvuka kiwango cha kanuni za kibiblia kutoka kuwa "Mkristo mkamilifu" hadi "nadharia ya ukamilifu" wa kisheria.

"Mkristo mkamilifu" kwa mujibu wa Biblia ni moyo usiogawanyika unaotafuta kumpendeza Mungu katika maeneo yote. Unatambua kwamba hata moyo wa kweli wa upendo hauwezi kutuleta kwenye utendaji uliokamilika. Sisi tumekuwa na mipaka ya udhaifu wa kibinadamu. Mtu mtakatifu hatapenda kuvunja sheria za Mungu kwa makusudi, lakini aliye mtakatifu ataendelea zaidi kutegemea neema ya Mungu katika maeneo yale ambayo kwa kutokukusudia hujikuta tumepungukiwa na viwango vya Mungu vya mema na mabaya.

"Nadharia ya ukamilifu" kwa upande mwingine, inaniongoza mimi kutegemea utendaji mkamilifu kwenye maeneo yote ya maisha. Nadharia ya ukamilifu inanilenga mimi na

[286] Mathayo 13:45-46
[287] Imechukuliwa kutoka John N. Oswalt, "Dangers to Holiness: Perfectionism and Legalism." Retrieved from https://www.gbs.edu/dangers-to-holiness-perfectionism-and-legalism/ December 20, 2019.

utendaji wangu kama mtu mtakatifu badala ya kumwelekea Yesu na nguvu zake katika maisha yangu.

Nadharia ya ukamilifu huelekeza kwenye juhudi za kisheria za "kupata" upendeleo wa Mungu kupitia kutengwa. Mara nyingi inapima utakatifu kwa misingi ya orodha ya vitu nisivyovifanya (mimi sivuti sigara, sinywi pombe, sivai nguo za aibu,) au mambo ambayo ninayafanya (ninafunga, ninaomba, ninatoa kanisani).

Kama tulivyoona katika somo la 4, mtu mtakatifu ***atataka*** abakie kuwa ametengwa kutoka katika mambo yote yasiyompendeza Mungu. Kwa kusema, "Nampenda Mungu kwa moyo wangu wote" halafu unaishi maisha yanayotafuta kukidhi matakwa ya dunia ni mbaya.

Pamoja na hayo, kamwe tusiruhusu matamanio yetu ya moyo uliotengwa na maisha yaliyotengwa yakatupeleka katika kuamini kwamba tunaweza kupima uhusiano wetu na Mungu kwa orodha za "ninavyovifanya na nisivyovifanya." Utakatifu ni jambo la kwanza la moyo wa uhusiano wa upendo na Mungu. Uhusiano huu huhamasisha tamaa zetu za kuishi maisha matakatifu, yaliyotengwa. Kinyume chake haitanya kazi: Maisha yaliyotengwa peke yake hayawezi kuhamasisha uhusiano wa upendo na Mungu.

Tunatafuta kuwa wakamilifu kama Mungu anavyoamuru. Tusijaribu kupata upendeleo wa Mungu kupitia nadharia ya ukamilifu. Moyo mkamilifu ni moyo unaompenda Mungu kabisa.

► Ni lipi jaribu kubwa katika kanisa lako, mambo ya dunia au ya sheria? Jadili upanuzi wa uwigo wetu wa upendo kwa Mungu unavyoweza kuleta mabadiliko sahihi katika haya matatizo. Jadili hatua za vitendo za kuhamasisha upendo wa Mungu miongoni mwa watu unaowahudumia.

### Ufunguo wa Maisha ya Utakatifu: Kumpenda Mungu

Tunampeda Mungu peke yake kama tutamtii kwa ukamilifu. Tunamtii Mungu peke yake kama kwa ukweli tunampenda yeye. Kama watoto wa Mungu, tunaweza kwenda mbali zaidi kumtumikia Mungu kama wajibu. Tunaweza kufikia mahali ambapo tunaona furaha ya kumtumikia yeye. Furaha hii itapatikana peke yake katika upendo. Mtoto anayemtii baba yake kwa ajili tu ya hofu au kufanyizwa kazi, kamwe haoni furaha katika kutii. Mtoto anayetii kutokana na upendo, atauona utii kuwa furaha.

Wakati mtoto mdogo anapojifunza kupiga violin (fidla), ni lazima afanye mazoezi kila siku. Kwanza, mazoezi haya huonekana kama anafanyizwa kazi badala ya kupata furaha. Lakini baadaye kama mtoto atakuwa mpigaji mahiri, itafikia mahali aanze kujikuta kwamba kupiga fidla ni zaidi ya kufanya kazi. Ni lazima iwe furaha. Kazini wakati mtoto anapofanya mazoezi kwa sababu mama yake anasema, "ni lazima ufanye mazoezi." Furaha ni wakati mtoto anacheza kwa sababu anafurahia kucheza. Mpiga fidla wa kweli huipata furaha wakati wa kufanya mazoezi kama wajibu.

Hali hii ni sawa na ukweli ulio katika maisha yetu ya kiroho. Mtu mtakatifu hulisoma neno la Mungu kwa nidhamu ya kiroho, lakini pia hufurahi katika hilo neno la Mungu. Utii kwa Mungu huja kwa pamoja kama kazi ***na*** furaha.

Fikiria tofauti iliyopo wakati tunapomtumikia Mungu katika furaha kuliko kama kazi. Utii hufanyika furaha, na siyo mzigo. Maombi, neno la Mungu, na taratibu za kinidhamu za maisha ya Kikristo hufanyika furaha. Hii ndiyo maana ya kumpenda Mungu. Watu watakatifu hutii kwa furaha kwa sababu wanampenda Mungu.

George Croly, mhubiri wa Kianglikani wa karne ya 19, aliomba kwamba Mungu "amtoe" kutoka kuipenda dunia na amjaze "shauku takatifu" iliyo safi kwa ajili ya Mungu. Wimbo ufuatao utaendelea kuwa sala muhimu kwa kila Mkristo anayetafuta kumpenda Mungu kwa upendo mkamilifu na usiogawanyika.

### Roho wa Mungu shuka ndani ya Moyo Wangu - George Croly

Roho wa Mungu, shuka ndani ya moyo wangu;
Viondoe duniani, kwa hoja zinazosonga;
Simama kwenye udhaifu wangu, mwenye nguvu Bwana wangu,
Na unifanye nikupende nawe, kama ninavyotakiwa nikupende.

Nifundishe kupenda Bwana wangu kama malaika wanavyopenda,
Shauku yangu moja tu ijaze sura yangu yote;
Ubatizo wa mbinguni ushuke kama njiwa,
Moyo wangu uwe madhabahu, Upendo wako uwe moto.

### Aliipata Siri - John Sung

John Sung alikuwa mmoja wa wainjilisti mashuri sana katika karne ya ishirini. Alikuwa mtoto wa mchungaji wa Kimethodisti katika Jimbo la Fijian, China, na akawa Mkristo akiwa na umri wa miaka tisa.

Sung alikwenda Amerika kusoma akiwa na umri wa miaka kumi na tisa. Akiwa mwanafunzi mwenye kipaji, John Sung alimaliza elimu yake ya shahada ya kwanza, uzamili, na uzamivu katika kemia ndani ya miaka sita tu. Kwa bahati mbaya, katika kipindi hiki, Sung alianza kutilia mashaka mafundisho ya Biblia aliyojifunza kutoka kwa baba yake.

Sung aliamua kuchukua tena mwaka mmoja kusoma katika chuo cha Union Theological Seminary akitaka kutafuta majibu ya maswali yake. Badala ya kupata majibu aliyotaka, maprofesa wapenda mabadiliko ya wastani katika chuo hicho, walizidi kuididimiza imani yake zaidi.

Mwaka 1926, John Sung alihuduria ibada eneo la Harlem. Usiku ule, msichana wa miaka kumi na tano alitoa ushuhuda wa mabadiliko Mungu aliyomfanyia katika maisha yake. Sung alianza kutafuta kuurejesha tena uhusiano wake na Mungu. Maprofesa wa ile

seminari walijiridhisha kwamba John Sung alikuwa mgonjwa wa akili, na raisi wa chuo, Henry Sloan Coffin, akamweka Sung kwenye hifadhi ya watu waliochanganyikiwa akili. Katika muda wa siku 193 alizokuwa amezuiliwa kama aliyechanganyikiwa, aliisoma Biblia mwanzo hadi mwisho mara 40.

Kufuatia kuachiliwa kwake, John Sung alirudi China. Dr. Sung alijua kwamba angeweza kuchukua nafasi ya kufundisha katika chuo chochote nchini China. Hata hivyo, akiwa ndani ya meli, Mungu alikuwa anamwita ayasalimishe zaidi maisha yake. Siku moja, kama alama ya kujisalimisha kabisa, na kwenye kutaka kuondoa mipaka na vizuizi vyovyote vya yeye kufundisha, Dr. Sung alikusanya vyeti vya shahada na stashahada zake zote na zawadi nyingine zote za kitaaluma akazitupa nje ya meli.

John Sung aliwasili China siyo kama "Dr. John Sung, Profesa wa Kemia" bali kama "John Sung, Mtumishi wa Mungu." Sung alianza kuhubiri na aliweza kuwa na huduma kubwa na yenye nguvu ya uinjilisti. Wanahistoria wanakadiria kwamba chini ya huduma ya Jonh Sung, zaidi ya watu laki moja waliokolewa wakati wa kurudi kwake China mwaka 1927 hadi alipofariki mwaka 1944 akiwa na umri wa miaka arobaini na moja.

Maisha ya John Sung yanadhihirisha kwamba kumpenda Mungu ni zaidi ya mhemuko. Kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu, Dr. Sung aliachana na tamanio lake la kuwa na kazi yenye sifa ya kufundisha katika vyuo vikuu vya China, na akaitikia mwito wa Mungu wa kutumika kama mhubiri wa injili. Kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu, Sung alikubali kuachana na marupurupu yake yote ya mtu anayelipwa katika nafasi nzuri ya kazi na akaamua kuishi maisha rahisi, akila vyakula vya watu wa kawaida. Kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu, John Sung alitumia masaa kadhaa kutoka katika muda wake kila siku kwa ajili ya maombi na kujifunza Biblia. Maisha yake yalimezwa na upendo wake kwa Mungu, na kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu, Mungu alimtumia John Sung kuleta maelfu ya watu kwa Kristo

## Tafakuri ya Somo la 7

(1) Kuwa mtakatifu ni kumtii Mungu.

(2) Watu wa Mungu huipata furaha yao kubwa kutoka kwa Mungu.

(3) Kwa sababu wanajua kwamba sheria ya Mungu inaakisi upendo wake, watu wa Mungu hufurahi katika sheria za Mungu.

(4) Wale wote walio na furaha ya Mungu, hujikuta kwamba Mungu amejitoa mwenyewe kwa ajili yao.

(5) Yesu alionyesha mfano halisi wa nini maana ya kumpenda Mungu.

(6) Jawabu kwa maisha ya dunia ni kuwa na upendo wa kina kwa Mungu

(7) Jawabu la kuishi kwa sheria ni kuwa na upendo wa kina kwa Mungu.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Fikiria kwamba Mkristo mpya anakuja kwako na kukuambia, "Nataka niwe na uhusiano wa kina na Mungu. Nampenda Mungu, lakini ni vigumu kujua jinsi ya kukua kwenye uhusiano wangu na yeye. Simwoni Mungu, na inaonekana anakaa mbali sana. Nifanyeje?" Andika insha ya kurasa 2-3 ya kumsaidia huyu muumini mpya aweze kujua ni kwa namna gani anaweza kukua kwenye uhusiano wake na Mungu. Pamoja nayo, uongeze na hatua za vitendo za jinsi ya kusoma Biblia, kuendeleza maisha ya maombi, na kushirikisha Imani yako. Kwenye kipindi kinachofuata cha darasa, kila mwanafunzi atapaswa ayasome majibu yake na hatimaye yajadiliwe na darasa kwa pamoja.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Marko 12:29-31.

# Somo la 8
# Utakatifu ni Kumpenda Jirani Yako

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Amtambue Yesu kama mfano wa kuigwa wa Utakatifu.

(2) Akubaliane na maana ya ukamilifu katika Biblia.

(3) Kufanya ukuaji uendelevu wa upendo mkamilifu.

(4) Achukue hatua za vitendo kuonyesha upendo kwa Wakristo na wasio Wakristo.

(5) Kukariri Mathayo 5:43-48.

## Yesu: Mfano wa kuigwa wa Upendo Halisi

Wakati Yesu alipokuwa akitembea kandokando ya bahari ya Galilaya, alipishana na mtoza ushuru. Kwa kuwa alikuwa anawafanyia kazi Warumi, Lawi alikuwa anakwepwa na viongozi wa dini ya Kiyahudi (*Rabbi*). Kwa mshangao wa wa Lawi, Yesu alisema, "Nifuate." Rabbi wengine walimwona tu mtoza ushuru; Yesu alimwona mtu wa kumpenda.

Baadaye, Yesu aliketi chakulani pamoja na kundi la watoza ushuru wengi na wenye dhambi nyumbani kwa Lawi. Mafarisayo walishtushwa. Yesu alipaswa awe mtakatifu; kwa nini anatumia muda wake na watenda dhambi? Yesu aliposikia aliwaambia, "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."[288]

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Bwana
Nifanye niwe chombo chako cha amani.
Palipo na chuki, nionyeshe upendo;
Palipo na maumivu, Msamaha;
Palipo na mashaka, Imani;
Palipo na kukataa tamaa, matumaini;
Palipo na giza, palete mwanga;
Palipo na majonzi, palete furaha.

Ewe Bwana wa Utukufu,
Kuwa mpaji wangu, ili nisiwe ombaomba;
Nipe kufarijiwa, nami niweze kufariji;
Nipe kueleweka, nami nielewe wengine;
Nipe kupendwa, nami niweze kupenda.

Kwa kuwa katika kutoa, ndipo tunapopokea;
Katika kusamehe, ili nasi tuweze kusamehewa;
Ni katika kufa, tunazaliwa upya katika maisha ya milele."

- Mtakatifu Francis wa Assisi

[288] Marko 2:17

Mfano huu wa Yesu, uliwashangaza wapinzani wake wengi. Mafarisayo walifikiriwa kama watu watakatifu sana wakati wa kipindi cha Yesu. Walisema, "Sisi ni watakatifu, kwa hiyo tunakaa mbali na wenye dhambi." Yesu anasema, "Mimi ni Mtakatifu, kwa hiyo ninautumia muda wangu na wenye dhambi."

Yesu alifurahia kuutumia muda wake na wenye dhambi. Kwa jinsi walivyokuwa wanamfuata Yesu, watu wengi waligeuka kuwa watu watakatifu. Yesu alionyesha mfano halisi wa maisha ya upendo mtakatifu unaoweza kuibadilisha dunia. Utakatifu ni upendo kamili kwa Mungu na upendo kamili kwa watu. Utakatifu wa kweli huubadili ulimwengu wetu.

## Utakatifu wakati wa Dunia ya Yesu

► Ni kwa jinsi gani watu katika ulimwengu wako wanaupima utakatifu? Kiwango hiki unawezaje kukilinganisha na jinsi Yesu alivyoishi?

Watu walioishi kipindi cha dunia ya Yesu waliamini nini kuhusu utakatifu? Walitegemea mtu mtakatifu aishije? Kama tutakavyoona katika majibu ya maswali haya, tutaelewa ni kwa nini watu walishtushwa na maisha na mafundisho ya Yesu.[289]

### Walichokiamini Watu wa Wakati wa Dunia ya Yesu

Watu wa wakati wa Yesu **walijua kwamba Mungu ni Mtakatifu**. Walijua kwamba watu wa Mungu ni lazima wawe watakatifu. Mungu mtakatifu anahitaji watu wawe watakatifu. Mungu aliipeleka Israeli uhamishoni kwa sababu watu wake hawakuwa watakatifu.

Watu wa wakati wa siku za Yesu, **walijua kwamba utakatifu unahitaji kutengwa kutoka kitu chochote ambacho ni najisi.** Wito wa Agano la Kale ni kuwataka watu wa Mungu kukaa mbali na chochote kinachoitwa dhambi.

Watu wa siku za Yesu **walijua ahadi ya Mungu ya kuandika agano jipya ndani ya mioyo ya watu.** Mungu aliahidi kuwapa watu wake "moyo mpya" na "roho mpya" itakayowawezesha kuhifadhi lile agano.[290] Watu wa siku za Yesu walikuwa wanaingojea ahadi hii iweze kutimia.

Watu wa siku za Yesu walijua kwamba **Mungu mtakatifu hutimiza ahadi zake.** Mungu ni mwaminifu katika maagano yake. Ingawaje Israeli imelivunja lile agano, Mungu aliendelea kuwa mwaminifu. Wayahudi waliamini kwamba utukufu wa Mungu ungerejea katika Israeli kama watu wake wangekuwa watakatifu.

[289] Maelezo mengi hapa yanatoka kwa Kent Brower, *Holiness in the Gospels* (Kansas City: Beacon Hill Press, 2005).
[290] Ezekieli 36:26

**Walichokifanya Watu wa Wakati wa Dunia ya Yesu**

Watu wa dini wa wakati wa siku za Yesu waliamini katika kanuni hizi, lakini walishindwa kuishi kulingana na mfano wa Mungu wa utakatifu wa kweli. Hawakuwa na mioyo ya utakatifu.

**Viongozi wa kidini** waliweka Imani yao kwenye hekalu. Waliamini kwamba kama dhabihu zingeweza kutolewa kwa usahihi, utukufu wa Mungu ungerudi. Yesu alijibu, "Nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka."[291] Yesu alionyesha kwamba sadaka peke yake hazitoshi.

Waliokuwa **wanajihesabia haki** waliamini kwamba wangeweza kuwa watakatifu kwa kuishi maisha ya kujitenga kuishi na watu wengine. Walitembelea jamii zilizoishi kuzunguka Bahari Nyeusi. Yesu alijibu, "Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu."[292] "Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."[293] Yesu aliwagusa wenye ukoma; alikula na wenye dhambi. Alionyesha kwamba tunaweza kuwa watakatifu kwenye dunia ya dhambi.

**Mafarisayo** waliamini katika muonekano wa nje wa mambo yaliyohusiana na sheria, lakini walipuuzia usafi wa ndani. Yesu aliwalinganisha Mafarisayo na makaburi: "Nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi."[294] Yesu alionyesha kwamba utakatifu unaanzia kwenye moyo. Huwezi ukawa na mikono mitakatifu kama moyo siyo mtakatifu.

Hawa watu wa dunia ya Yesu waliridhika na utoaji wa sadaka badala ya utakatifu wa kweli. Badala ya kumpenda Mungu, waliupima utakatifu na sheria. Badala ya kuupenda ulimwengu wao, Israeli ilijenga kuta kuzuia dunia iliyokuwa na uhitaji. Yesu anaonyesha kwamba mtu mtakatifu anampenda Mungu na anampenda jirani yake.

## Maisha ya Yesu yalikuwa ni Mfano wa Kuigwa wa Utakatifu

Tunaposoma kuhusu utakatifu katika Agano la Kale, tunaweza kushawishika kusema kwamba, "Hiyo inafanya kuwa ni nadharia nzuri, lakini itafananaje katika uhalisia wa maisha?" Yesu alikuja kutuonyesha utakatifu unafananaje katika maisha ya kila siku. Mtiririko wa Luka wa nasaba (ukoo) ya Yesu unaonyesha kwamba Yesu alikuwa "Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu."[295] Tunapomwangalia Yesu, mwana wa Adamu, tunaona

291 Mathayo 9:13
292 Luka 15:7
293 Mathayo 9:13
294 Mathayo 23:27-28
295 Luka 3:38

mfano halisi wa mtu mtakatifu. Vitabu vya Injili vinaonyesha maisha ya utakatifu ya Yesu wa Nazarethi.

**Utakatifu ni Kutembea na Yesu**

Ndani ya Yesu, tunaona mfano wa kuigwa wa uhusiano wa mtu na Mungu. Maombi ya Yesu yalidhirisha uhusiano wake wa karibu na Baba. Mara kwa mara Yesu alikuwa akijitenga na makundi ili awe peke yake na Baba yake. Yesu alitafuta kuwa na uhusiano wa karibu sana na Baba yake. Alitembea na Mungu.

Labda, picha kubwa ya uhusiano wa Yesu na Baba yake unaweza kuonekana kwenye kilio chake pale msalabani. Alipokuwa amezibeba dhambi zetu pale msalabani, "Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, 'Eloi, Eloi, lama sabakthani?' Yaani, 'Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?'"[296] Kwa kufa badala yetu, na kwa kuichukua adhabu stahili kwa ajili ya dhambi zetu, Yesu alijihisi kuachwa na Baba yake.

Yesu alionyesha uhusiano wa ndani na Mungu. Utakatifu aliokuwa nao Ibrahimu na Daudi ulikamilishwa ndani ya Yesu wa Nazarethi.

**Utakatifu ni Kutengwa**

Kuwa mtakatifu maana yake ni kutengwa kutokana na dhambi na kutengwa kwa ajili ya Mungu. Akiwa katika hali ya ubinadamu, Yesu alionyesha mfano wa kutengwa kutokana na dhambi. "Hakuwahi kufanya dhambi."[297] Mwanafunzi aliyekuwa akikaa karibu sana na Yesu wakati wa huduma yake hapa duniani alitoa ushuhuda kwamba, "wala giza lo lote hamna ndani yake."[298]

Akiwa katika hali ya ubinadamu, Yesu alionyesha mfano wa kutengwa kwa ajili ya Mungu. Aliishi maisha ya kujitoa kwa hiari kwa Baba yake. Yesu alithibitisha, "Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha peke yangu; kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo."[299] Yesu alikuwa ametengwa kwa ajili ya Baba yake.

**Utakatifu ni Sura ya Mungu**

Kuwa mtakatifu ni kuakisi sura ya Mungu. Tunapomwangalia Yesu, tunaona kivuli kamili cha sura ya Baba. "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."[300] Wakati Filipo alipomwuliza Yesu, "Tuonyeshe Baba," Yesu alijibu, "Aliyeniona mimi amemwona Baba."[301] Ndani ya Yesu, tunaona kivuli kamili cha sura ya Mungu.

---

[296] Mathayo 27:46
[297] 2 Wakorintho 5:21
[298] 1 Yohana 3:5
[299] Yohana 8:29
[300] Yohana 1:14
[301] Yohana 14:9

### Utakatifu ni Moyo Usiogawanyika

Mtu mtakatifu ana moyo usiogawanyika; amejikabidhi kabisa kwa Mungu. Katika bustani ya Getsemane, Yesu aliomba. "Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke."[302] Moyo wa Yesu ulijisalimisha kabisa kwa Baba. Yesu alionyesha ni nini maana ya kuwa na moyo usiogawanyika.

### Utakatifu ni Uadilifu na Haki

Utakatifu wa kweli unahitaji tabia ya uadilifu na haki. Mtu mtakatifu hudhihirishwa na haki, rehema na unyenyekevu. Katika maisha ya Yesu, tunaona mfano ulio mkamilifu wa uadilifu na haki.

Picha ya mwisho ya **haki** inaonekana wakati Yesu alipobeba hasira ya Mungu msalabani. Yesu hakuikataa hukumu ya kulipia dhambi; badala yake, aliikubali hiyo adhabu kwa ajili yetu.

Yesu alidhihirisha **huruma** yake wakati aliposhughulika na wenye ukoma, wanawake, watoto, na maskini. Alionyesha huruma kwa mwanawake aliyenaswa katika uzinzi, Zakayo, na kwa yule mwizi pale msalabani. Mara kwa mara, Yesu alikuwa na mwitikio wa huruma kwa wale wote waliokuwa wamekataliwa na watu wengine.

Zaidi ya miaka 700 kabla Yesu hajazaliwa, Isaya alielezea kuhusu **unyenyekevu** wa Masihi. "Yeye hana umbo wala uzuri; Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani."[303] Isaya alitabiri, "Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima."[304]

Yesu alionyesha huduma yake ya umisheni, ya haki, rehema na unyenyekevu katika mahubiri yake ya kwanza hadharani. Katika hekalu la Nazarethi, alisoma unabii wa Isaya wa mtumishi ajaye:

> Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.[305]

Isaya aliona kabla "mwaka wa Bwana uliokubalika," muda wa haki kwa watu wote. Yesu alitangaza kwamba alikuja ili kuitimiliza ahadi: "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu."[306] Huduma ya Yesu hapa duniani ilionyesha mfano mzuri wa uadilifu na haki.

---

[302] Luka 22:42
[303] Isaya 53:2
[304] Isaya 42:2-3
[305] Luka 4:18-19, Isaya 61:1-2
[306] Luka 4:21

## Utakatifu katika Vitabu vya Injili: Kuwapenda jirani zetu

Katika somo la 7, tumeona kwamba kuwa mtakatifu ni kumpenda Mungu kwa upendo usiogawanyika. Kuwa mtakatifu pia ni kuwapenda jirani zetu. Yesu alitoa maagizo haya mawili, "Mpende Bwana Mungu wako" na "Mpende jirani yako" kama muhtasari wa sheria zote."[307]

Upendo wa kweli wa Mungu siku zote huleta upendo kwa watu wengine. Kama tunampenda Mungu, tutawapenda na watu ambao Mungu anawapenda. Utakatifu kamwe siyo wa faragha; maisha ya utakatifu ni pamoja ni uhusiano wetu na majirani zetu. Utakatifu ni upendo mkamilifu kwa Mungu ***na*** upendo mkamilifu kwa watu wengine. Upendo mkamilifu kwa Mungu hauwezi kutenganishwa na upendo wetu kwa majirani zetu.

Yesu aliliweka liwe hivi: "Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."[308] Yohana aliunganisha upendo wetu kwa Mungu na upendo wetu kwa majirani zetu:

> Mtu akisema, "Nampenda Mungu," naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona. Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.[309]

Kutokea kwenye chanzo chake, dhambi ni ubinafsi. Kwenye bustani, Shetani alimwahidi Hawa kwamba anaweza "akafanana na Mungu."[310] Kule Babeli, watu walidhamiria "wajijengee jina."[311] Kinyume na mapenzi ya Mungu, Israeli iliomba ipewe mfalme ili "aweze kufanana na mataifa mengine."[312] Kwenye kila eneo, asili ya dhambi ni ubinafsi.

Kama dhambi ni ubinafsi, basi utakatifu (kinyume cha dhambi) utahusisha kujikita kwa aina nyingine. Kama dhambi inasababisha tutafute mambo mazuri ya kwetu wenyewe, basi utakatifu utasababisha tutafute mambo mazuri kwa watu wengine. Kama dhambi ni kujipenda wenyewe, basi utakatifu ni upendo kwa wengine. Kuwa mtakatifu ni kuwapenda wengine. Amri iliyo kuu inayorudiwa mara kwa mara kwenye Agano Jipya ni ile ya upendo. Neno upendo limerudiwa mara hamsini na tano.

Yesu alifundisha kwamba utakatifu ni kuwa na upendo wenye huruma. Yesu alionyesha kwamba mtu mtakatifu atawavuta wengine kuja kwa Mungu takatifu kupitia maisha ya upendo mtakatifu.

---

[307] Marko 12:29-31
[308] Mathayo 25:40
[309] 1 Yohana 4:20-21
[310] Mwanzo 3:5
[311] Mwanzo 11:4
[312] 1 Samweli 8:5

Utii katika sheria ya Mungu ya kuwa mtakatifu kwa sababu Mungu naye ni mtakatifu kunatuhitaji sisi tuwapende jirani zetu. Yesu aliudhihirisha upendo kamili kwa wengine na aliwafundisha wafuasi wake kuwapenda kwa ukamilifu watu wengine.

**Yesu aliudhihirisha upendo kamili kwa wengine**

Mwanzoni mwa huduma ya Yesu, Yohana Mbatizaji alituma wanafunzi wake kuulizia, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?"[313] Farisayo angetegemea Yesu ajibu kwa kujinyooshea kidole cha maisha yake ya kutengwa na mafundisho yake ya hekima. Badala yake, Yesu anagusa huduma yake ya upendo kwa wengine:

> Nendeni mkamweleze Yohana hayo mliyoyaona na kuyasikia: vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, maskini wanahubiriwa habari njema.[314]

Utafiti uliofanywa katika miujiza aliyoifanya Yesu inadhihirisha ukamilifu wa upendo kamili kwa watu wengine. Akida mmoja wa Kirumi alimwomba Yesu amponye mtumishi wake. Makuhani wengi wa Kiyahudi wangelilikataa ombi hili. Yesu siyo tu kwamba alimponya yule mtumishi, bali pia alisifia imani ya yule mmataifa.[315]

Hata wakati miujiza yake ilipoleta upinzani, Yesu aliendelea kutumika kwa upendo. Wakati yule mwanamke kilema alipokuja kwake kwenye siku ya Sabato, alimponya. Ingawaje hakukuwa na sheria yeyote ya kuweza kuzuia uponyaji huu, Mafarisayo hawakuruhusu uponyaji ufanyike siku ya Sabato. Kwa ajili ya upendo, Yesu alisababisha hasira kwa wakuu wa dini.[316]

Yesu alionyesha upendo hata kwa wale waliokuwa wanapitia katika mateso kama matokeo ya matendo ya dhambi zao wenyewe. Yesu alionyesha upendo kwa mwanamke Msamaria aliyeishi maisha ya uasherati.[317] Alimlinda mwanamke aliyekamatwa kwa uzinzi. Yesu hakukataa kwamba hana dhambi; alimwamuru aende, "Enenda zako; wala usitende dhambi tena."[318] Yesu alijua kwamba utakatifu unahitaji mtu atengwe kutokana na dhambi, lakini alijua pia kwamba upendo una nguvu kuliko nguvu ya dhambi.

Masaa machache kabla ya kifo chake, Yesu aliudhihirisha upendo kwa wengine. Mtumwa wa Kuhani Mkuu alifuatana na bwana wake kwenda kumkamata Yesu kwenye bustani ya Getsemani. Wakati Simoni Petro alipolikata sikio la mtumwa wa Kuhani Mkuu, Yesu

[313] Luka 7:19
[314] Luka 7:22
[315] Mathayo 8:5-13
[316] Luka 13:10-21
[317] Yohana 4
[318] Yohana 8:11

alimkemea Petro na akamponya yule mtumwa.[319] Yesu alionyesha ni nini maana ya kumpenda adui yako.

Wakati Yesu akiwa pale msalabani, mwizi aliyekuwa na yeye ametungikwa msalabani alimwomba Yesu rehema. Huyu mwizi alistahili adhabu ya kifo. Alikuwa mhalifu wa ujambazi wa kutumia nguvu. Yesu aliyekuwa anateseka lakini siyo kwa makosa aliyoyatenda, bali kwa ajili ya dhambi za wengine, alimpa ahadi yule mwizi aliyekuwa anangojea kufa.[320] Pamoja na uchungu aliokuwa akiupitia, bado Yesu alimpenda mtu aliyeonekana hawezi kabisa kupendwa.

### Yesu alifundisha wafuasi wake kuwapenda watu wengine kwa ukamilifu

Yesu aliwafundisha wafuasi wake ni nini maana ya kupenda kwa ukamilifu. Yesu alionyesha kwamba upendo mkamilifu ndiyo kiwango cha maisha katika ufalme wa mbinguni.

#### *Yesu alifundisha upendo mkamilifu kwenye Hotuba ya Mlimani*[321]

Agizo hili, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" ndiyo kiini kikuu cha hotuba ya Yesu Mlimani. Agizo hili linafuatiwa na mfululizo wa mifano ya upendo kwa wengine. Kuwa "wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" ni kuishi maisha ya upendo binafsi dhidi ya watu wengine.

Kama utakatifu usingemaanisha kutengwa na dhambi za nje; Mafarisayo wangekuwa ni watakatifu kuliko watu wengine wote. Waliitwa "Waliotengwa." Yesu alitaka zaidi ya huku kutengwa kwa Mafarisayo. "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."[322]

Kwenye ulinganifu na haki waliyokuwa nayo Mafarisayo, Yesu alionyesha kwamba watu wa ufalme wake ni watu wa upendo. Tabia za nje ambazo haziendani na utakatifu wa ndani ni unafiki na siyo utakatifu. Ni lazima tuwe na mioyo mitakatifu na mikono safi.

Mtu mwenye upendo mkamilifu huenda zaidi ya agizo kwamba. "Usiue." Upendo hutafuta upatanisho na ndugu aliyekukosea. Mtu mwenye upendo mkamilifu ataenda hata zaidi ya agizo kwamba, "Usizini." Upendo unakataza hata kumwangalia mwanamke ili kuridhisha matamanio ya mwili.

Mtu mwenye upendo mkamilifu hatafuti sababu za kuachana kwenye ndoa. Anampenda mkewe kiasi cha kutafuta haja za moyo wake. Mtu mwenye upendo mkamilifu huzungumza bila ya kupindisha ukweli. Mtu wa upendo mkamilifu hatafuti kulipiza kisasi.

---

[319] Mathayo 26:50-52
[320] Luka 23:39-43
[321] Mathayo 5-7
[322] Mathayo 5:20

Yesu alihitimisha kwamba:

> Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.[323]

Kupenda kama Mungu anavyopenda ni kuwa na upendo kwa adui zako. Yesu hajawahi kupunguza mahitaji ya utakatifu; bali ***ameyaongeza*** mahitaji ya utakatifu. "Haki yenu ni lazima izidi" haki ya nje ya waandishi na Mafarisayo.[324] Badala ya kuamua kuwa na tabia za nje peke yake, Mungu huubadilisha moyo. Unapokuwa na upendo kama Mungu alivyo na upendo, unakuwa "mkamilifu kama Baba wa mbinguni alivyo mkamilifu."

***Yesu alifundisha upendo mkamilifu kwenye mfano wa msamaria mwema*.**[325]

Mwanasheria mmoja wa dini alimwuliza Yesu, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Yesu akamwambia, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?" Mwanasheria alikuwa anajua jibu sahihi akamjibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako."

Mwanasheria hakutaka kugusia mahitaji ya upendo. Alitafuta kisingizio cha kukwepa kuiweka imani yake kwenye vitendo. "Naye akitaka kujidai haki, alimwuliza Yesu; 'Na jirani yangu ni nani?'" Yesu alimjibu kwa kutumia mfano wa Msamaria mwema.

Yesu alifundisha kwamba hatupaswi kuwapenda majirani zetu kwa maneno tu, bali pia kwa matendo. Kama ilivyokuwa kwa Msamaria mwema, Wakristo wanaopenda kwa ukamilifu hutafuta fursa ya kuwatumikia wengine – hata aliye adui kwake. Tukiwapenda majirani zetu, tutakuwa na fursa ya kuwahudumia. Yakobo alieleza:

> Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, "Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba," lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?[326]

Upendo mkamilifu unaonekana katika vitendo, na siyo maneno peke yake. Watu watakatifu hupenda kama Yesu alivyopenda. Kupenda kwa ukamilifu ni kupenda kwa kujitoa mhanga.

---

[323] Mathayo 5:44-45
[324] Mathayo 5:20
[325] Luka 10:25-37
[326] Yakobo 2:15-16

***Yesu alionyesha upendo mkamilifu kwa kuosha miguu ya wanafunzi.***[327]

Kwenye usiku wa kukamatwa kwake, Yesu alifundisha somo kuu sana kuhusiana na upendo mkamilifu. Walipokuwa wakila chakula, yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa.

Yesu alijibu: "Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani, au yule atumikaye? Siye yule aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye."[328] Ndipo alipochuka taulo akaanza kutawadha miguu ya wanafunzi wake, kazi ya mtumishi. Yesu alipiga magoti akaosha miguu ya kila mtu aliyekuweko katika chumba kile – hata miguu ya Yuda Iskariote.

Baada ya kuwa amemaliza kuwatawadha, Yesu akawauliza, "Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea?" Alitaka awafundishe hawa wanafunzi wake wanaopigania ukubwa somo la msingi sana:

> Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo hivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.[329]

Katika dakika zake za mwisho za kuwa na wanafunzi wake, Yesu alifundisha kwamba upendo ni kujinyenyekeza. Upendo mkamilifu hautafuti madaraka; bali unatafuta fursa za kutumika. Utakatifu ni upendo mkamilifu.

## Maisha ya upendo mtakatifu

Yesu alisema, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu."[330] Watu wengi wanapinga kwamba, "hakuna mtu mtakatifu!" Hata hivyo, hatuwezi kupuuzia agizo la Yesu la "Kuwa wakamilifu." Hii inamaanisha nini? Je, inawezekana Wakristo wa kawaida wakatii hili agizo la Yesu?

### Inamaanisha nini kuhusu "Kuwa Mkamilifu"?

Mambo mawili yatatusaidia kuelewa alichokuwa anamaanisha Yesu. Kwanza, tunaangalia **tafsiri** ya neno la Kigiriki lililofasiri "kuwa mkamilifu" katika Mathayo 5:48. ***Teleios*** inamaanisha "kuwa kamili." *Teleios* inatokana na nomino inayomaanisha "lengo" au "kusudi." Kuwa mkamilifu maana yake ni kufikia lengo.

Agano la Kale linaonyesha kwamba mtu mkamilifu ana moyo usiogawanyika kwa ajili ya Mungu. Wazo hili linaendelea hadi kwenye Agano Jipya. Lengo la Mungu kwa watu wake ni "upendo mkamilifu," upendo unaotoka katika moyo usiogawanyika. Je, kutenda kwa

[327] Yohana 13:1-20
[328] Luka 22:27
[329] Yohana 13:13-15
[330] Mathayo 5:48

kamilifu kunawezekana kwa nguvu zetu wenyewe? Hapana. Je, upendo mkamilifu usiogawanyika kwa ajili ya Mungu unawezekana? Yesu alisema, "Ndiyo."

Pili, angalia **muktadha** ulioko katika Mathayo 5:48. Aya iliyo kabla na baada ya Mathayo 5:48 zinaonyesha kwamba kuwa mkamilifu ni kumpenda Mungu na jirani zetu upendo mkamilifu. Agizo la Yesu linabeba muhtasari wa maisha ya upendo kwa Mungu na kwa jirani zetu.

Agizo la, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu" linafuatiwa na mifano ya upendo kwa jirani zetu katika Mathayo 5:21-47. Badala ya mauaji, uzinzi, talaka, kuvunja ahadi au kulipiza visasi, watu watakatifu huishi kwa upendo. Amri iliyo kuu kuliko zote ni "Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."[331] Watu watakatifu huwapenda hata wale wanaotaka kuwaletea madhara. Kuwa mkamilifu maana yake ni kupenda kama Mungu anavyopenda.

Mara tu baada ya agizo hili, Yesu alitoa mfano wa inamaanisha nini katika kumpenda Mungu katika kweli kabisa katika Mathayo 6:1-18. Wanafiki huwa wanawasaidia maskini kwa ajili ya kutafuta kuonekana na kuheshimiwa na watu wengine; lakini wale wanaompenda Mungu kwa ukamilifu wanatoa ili waonekane na "Baba yao aonaye sirini."

Wanafiki "hupenda kusimama na kuomba ndani ya mahekalu yao na pembezoni mwa barabara ili waweze kuonekana na watu wengine." Wale wanaompenda Mungu kwa ukamilifu "wanaenda chumbani kwako, wanafunga mlango, wanaomba na wewe omba kwa Baba yako aliyeko sirini." Wanafiki hufunga ili kuvutia watu wengine; "wanabadilisha sura za nyuso zao ili waonekane na wengi." Wale wanaompenda Mungu kwa ukamilifu wote watapenda waonekane tu na "Baba yao aonaye sirini."

Paulo aliwaagiza waumini wa Kolosai kuishi maisha ya utakatifu. Anaelezea maisha ya upendo na msamaha: "Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa Rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu..."[332]

Juu ya mambo haya yote ni upendo. "***Zaidi ya hayo yote*** jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu."[333] Kuwa mkamilifu ni "kuuva upendo." Yesu aliposema "kuweni wakamilifu," alituagiza sisi "tuuvae" upendo kwa ajili ya Mungu na jirani zetu. Upendo mkamilifu ni upendo unaotoka katika moyo usiogawanyika.

### Upendo mkamilifu ni kamilifu kwa kiasi gani?

Katika hali ya kawaida mara nyingine tunatumia neno "kamilifu" katika ufahamu kamili. Tunatumia neno "Kamilifu" kumaanisha kitu ambacho hakiwezi kuongezwa au kupunguzwa. Tukifikiria "ukamilifu" kama kiwango kamilifu cha kupimia mafanikio,

[331] Mathayo 5:44
[332] Wakolosai 3:12-13
[333] Wakolosai 3:14

tutaupima utakatifu kwa matendo yetu. Kama Mafarisayo, tutauona utakatifu kama kijiti cha kupimia.

Watu wengi huupeleka mtazamo huu kwenye maisha ya utakatifu. Kama Mafarisayo, wana msururu wa mambo ya kufanyia ukaguzi. Kama mambo yote yatawekwa alama ya vema, wanaonekana ni "wakamilifu."

- "Je, amri ninazifanyia kazi?
- "Je, ninavaa nguo nzuri?
- "Je, ninanena maneno sahihi?


Katika Biblia, neno "mkamilifu" halina mipaka. Halikatai ukuaji endelevu. Ayubu alikuwa "mkamilifu,"[334] lakini aliendelea kukua katika mahusiano yake na Mungu kwa uzoefu aliokuwa ameupata.

Katika Biblia, kuwa "mkamilifu" kunamaanisha "kuwa kamili" katika kila eneo la ukuaji. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliwaandikia Wakristo ambao hawakuwa wakamilifu katika hatua za ukuaji wao. Walikuwa wameshindwa kukua katika eneo la kukua kiroho.

> Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima (*teleios*), ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.[335]

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania hajajaribu kushauri kwamba waumini waliokua kiroho (au wakamilifu) hawahitaji tena chakula cha kiroho. Badala yake anawasogeza zaidi kwenye kuendelea kukua, **ili waweze kula chakula cha kiroho kilicho sahihi katika umri wa maisha yao ya kiroho.** Kuwa mkamilifu ni kukua vyema katika hatua za uzoefu wa ukristo wetu. Kuwa mkamilifu ina maana kwamba tumekamilika kwa ujumla wote, na tuko kama Mungu anavyotutaka tuwe.

Badala ya kijiti cha kupimia, picha ya kibiblia ya "ukamilifu" ni mduara. Mduara uko mkamilifu na hauwezi kufanywa ukawa mduara zaidi. Hata hivyo, mduara mkamilifu unaweza kukuzwa umbo lake ukawa mkubwa, na ukapanuka. Ni mkamilifu, lakini bado unaongezeka.



**Mduara mkamilifu** **Mduara mkamilifu** **Mduara mkamilifu**

[334] Yobu 1:1
[335] Waebrania 5:12-14

Mtu mtakatifu amejazwa na upendo mkamilifu kwa ajili ya Mungu na jirani zake. Jinsi tunavyokua, uwezo wetu wa upendo unaongezeka. Mduara unazidi kupanuka. Jinsi tunavyokua, pendo letu linazidi "kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote."[336] Katika kila hatua ya ukuaji, Mungu anasema, "Mtu huyu ananipenda kwa moyo mkamilifu wa upendo. Ni mtakatifu."

Mtu aliyetembea na Mungu kwa miaka arobaini ana uelewa mkubwa zaidi wa kuonyesha upendo kwa jirani zake kuliko mtu ambaye ametembea na Mungu kwa mwaka mmoja tu. Lakini wote wanaweza kuwapenda majirani zao kutoka katika moyo usiogawanyika. Wote wanaweza kuonyesha upendo mkamilifu.

Wakati mtoto wa miaka mitano anavyochora picha ili kumwonyesha baba yake, husema, "Asante, imekamilika." Hamaanishi kwamba mchoro wake hauwezi kuwa mzuri. Kwenye umri wa miaka kumi na tano mtoto huyu anaweza akachora picha nyingine nzuri na bora zaidi.

"Imekamilika!" maana yake, "Picha hii imetoka katika moyo wa upendo. Ni sahihi katika hatua yake ya kukua."

Upendo mkamilifu siyo kipimo cha utendaji. Upendo mkamilifu ni upendo usiogawanyika kwa ajili ya Mungu na kwa watu wengine. Upendo mkamilifu ni kufuata mfano wa Yesu, aliyekuja kudhihirsha upendo mkamilifu katika maisha ya kila siku.

**Je, upendo mkamilifu unawezekana kwa waumini wa kawaida?**

Katika karne ya kumi na saba, watu waliokuwa wasafi wakati ule walitoa kanuni moja ya tafsiri ya Biblia. Walisema kwamba maagizo ya Biblia ni "ahadi zilizofunikwa*."* Hawa Wasafi walimaanisha kwamba maagizo ya Biblia *"ni ahadi zilizojificha."* Agizo la Biblia inamaanisha ni Ahadi ya Biblia. Kama Mungu akiagiza jambo, atafanya na utii uwezekane. Analolitaka Mungu kwa watu wake, atalifanya kwa watu wake.

Mfikirie baba wa duniani anayempa kijana wake maagizo ambayo hayatekelezeki. "Mwanangu, kama unataka unifurahishe, lazima ukimbie maili moja kwa dakika mbili." Kwa muda kidogo, kijana anaweza kujaribu kufikia hilo lengo, lakini mategemeo ya baba yake hayawezekani. Mwishowe, huyu kijana atakata tamaa sana na hata kuwa na hasira. Je, huyu ni baba mzuri? Hapana!

Mungu ni Baba mwema. Hawafanyi watoto wake wachanganyikiwe kwa maagizo yasiyowezekana. Wakati Yesu anatuagiza "tuwe wakamilifu kama Baba wa mbinguni alivyo mtakatifu," anatuwezesha tuweze kutii maagizo yake.

Hotuba ya Mlimani inaonyesha maisha katika ufalme wa Mungu. Hii siyo sheria mpya inayoleta utumwa mkubwa kuliko sheria ya zamani. Siyo seti ya mawazo yasiyofikiwa ya

---

[336] Wafilipi 1:9

kutuonyesha tuko wapi katika kufikia maagizo ya Mungu. Ni picha ya maisha ya kila siku katika ufalme wa Mungu. Hakuna mahali popote Yesu anasema, "Hili ni agizo langu, lakini hamtaki kutii!" Badala yake, Yesu anasema, "Hivi ndivyo mnavyotakiwa muwe."

Kama tutayaangalia maagizo ya Yesu kwa jicho la kawaida la kibinadamu, haiwezekani. Kwa nguvu ya kibinadamu, hatuwezi kutimiza maagizo ya Mungu ya kuwa wakamilifu. Kwa nguvu ya kibinadamu hatuwezi agizo la "mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote." Hata hivyo, kwa nguvu za Mungu, tunaweza kutii maagizo ya Mungu. Upendo mkamilifu unawezekana kwa neema ya Mungu.

Kijana mmoja tajiri alimwendea Yesu akamwuliza, "Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele?" Yesu alimjibu kwa kuorodhesha maagizo:

> Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie Uongo, Waheshimu Baba Yako Na Mama Yako, Na, Mpende Jirani Yako Kama Nafsi Yako.[337]

Wakati yule kijana alipojibu, "Haya yote nimeyashika." Yesu akaongezea amri nyingine, "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate." Kuwa mkamilifu kunamaanisha kumpenda Yesu kuliko mali.

Yule kijana alipolisikia neno lile, "akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi." Kijana tajiri hakupenda jirani zake kikamilifu; hawezi kuuza mali zake kisha awape maskini. Hakumpenda Mungu kikamilifu; na hawezi kuondoka nyumbani amfuate Yesu. Huyu kijana alikuwa na moyo uliogawanyika. Alimhitaji Mungu, lakini pia alizihitaji "mali zake nyingi."

Walipoona matakwa ya uanafunzi, "walishangaa mno, wakisema, 'Ni nani basi awezaye kuokoka?'" Jibu la Yesu linajibu swali hili, "Je, ukamilifu unawezekana kwa mwamini wa kawaida? Yesu akasema, "Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu mambo yote yawezekana."

Kwa nguvu ya mwanadamu, upendo mkamilifu kwa Mungu na jirani zetu haiwezekani. "Bali kwa Mungu yote yawezekana." Baba mwenye upendo hawezi kuwafadhaisha watoto wake kwa maagizo ambayo hayawezekani kutekelezwa. Maagizo ya Maandiko yanafuatana na neema ya kutii maagizo hayo. "Iweni wakamilifu kama na Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu," siyo sheria halali ya kuwaongoza Wakristo katika kukata tamaa. Ni ahadi ya neema ambayo Mungu anaweza kufanya ndani yetu kile ambacho kamwe tusingeweza kufanya sisi wenyewe.

Je, inawezekana kutii maagizo ya Yesu ya kuwa mkamilifu? Kutokana na Hotuba ya Yesu pale Mlimani, jibu ni la kupendeza "Ndiyo!" Kuwa mkamilifu kwenye ufalme wa Mungu ni

---

[337] Mathayo 19:16-26

kuwa na moyo wenye upendo mkamilifu. Kuwa mkamilifu kwenye ufalme wa Mungu ni kuwa na upendo mmoja tu kwa Mungu na jirani yetu. Je, hili linawezekana? Kwa mujibu wa Yesu, upendo mkamilifu pande zote inawezekana na ni muhimu. Upendo mkamilifu ni lengo kuu la Mungu kwa watu wake.

### Utakatifu katika vitendo: Upendo unatimizaje sheria?

Huang anasema, "Ninampenda Mungu kwa moyo wangu wote, na ninawapenda watu wengine pia. Lakini siwezi nikawapenda watu weusi. Nadhani watu weusi wote ni wavivu."

Rafiki yake na Huang akajibu, "Lakini Wakristo wanatakiwa wampende kila mtu! Wakristo hawawezi kuwahukumu watu wengine bila uhalali." Huang alijibu, "Sitegemei kama Mungu ana nia katika mambo madogo kama haya. Je. kwani siyo jambo la kawaida kuepukana na watu walio tofauti na sisi?"

Mungu anasema, "Watakatifu hushughulika na watu wote – ikiwa ni pamoja na wale wote walio tofauti nasi - walio na huruma na rehema."

> Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama ilivyoandikwa, "Mpende jirani yako kama nafsi yako," mwatenda vema. Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji.[338]

Kipimo kimoja cha tabia yako ni jinsi unavyowatendea wale ambao hawana lolote la kufanya kwa ajili yako. Ni rahisi kuonyesha tofauti na heshima kwa watu wenye nafasi wanaotupatia fedha, kazi, au mamlaka. Upendo unaheshimu wale ambao hawawezi kufanya lolote kwa ajili yetu: maskini, wazee, watoto, na wale wote ambao hawana nafasi katika eneo lolote. "Sheria ya kifalme" ya upendo inagusa jinsi tunavyomtendea kila mtu. Upendo huikamilisha sheria.

### Upendo huikamilisha sheria

Dhamira ya upendo mkamilifu ndio kiini kikuu katika ujumbe wa maisha matakatifu. Katika somo la 7, tuliona kwamba upendo kwa ajili ya Mungu ni zaidi ya hisia. Upendo kwa ajili ya Mungu hubadilisha kabisa mwelekeo wa maisha yetu. Sasa tunataka tumfurahishe Mungu zaidi kuliko tunavyotaka tujiurahishe wenyewe. Kwa njia hiyo hiyo, upendo kwa jirani zetu hubadili mwelekeo wa ubinafsi na umimi kwanza kwa ajili ya wengine.

Paulo anawaadikia kanisa la Rumi:

> Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, "Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani" na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili: "ya

---

[338] Yakobo 2:8-9

> kwamba, mpende jirani yako kama nafsi yako." Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.[339]

Kila Mkristo anawiwa na deni la upendo. Paulo anatuhakikishia kwamba kama tutatimiza vigezo vya vya upendo, tutakuwa pia tumetimiza vigezo vyote vya sheria. Kama tutawapenda watu wengine, hatutafanya uasherati, uuaji, wizi, tamaa na kadhalika. Kigezo cha sheria kitakuwa kimetimizwa nitakapompenda jirani yangu kama ninayojipenda mwenyewe.

Katika sura za mwisho za kitabu cha Warumi, Paulo anaonyesha jinsi upendo unavyokamilisha sheria. Wale wote waliojazwa na upendo wa Mungu:

- Watatumika kwa ajili ya mwili wa Kristo na siyo kwa ajili yao wenyewe (Warumi 12:3-5).
- Watachukia maovu na kuambatana na yaliyo mema (Warumi 12:9).
- Watawatanguliza wengine kwa kuwaonyesha heshima (Warumi 12:10).
- Watajali mahitaji ya wengine (Warumi 12:13).
- Watakuwa na amani na watu wote, hata na wale walio maadui zao (Warumi 12:14-21).
- Watatii mamlaka zinazotawala (Warumi 13:1-7).
- Wataheshimu misimamo ya waumini wengine (Warumi 14:1-23).
- Watachukuliana madhaifu yao kama Kristo alivyofanya (Warumi 15:1-3).

Upendo kwa ajili ya Mungu hubadili mwelekeo wa moyo kutoka kwenye ubinafsi na kuwa kwa ajili ya Mungu. Upendo kwa ajili ya jirani zetu hubadili mwelekeo wa ubinafsi kwa ajili ya kuwajali wengine. Yote haya ni sehemu ya yale yanayoonyesha ni nini maana ya mtu mtakatifu.

John Wesley alifanya majumuisho ya nini maana ya ukamilifu wa Mkristo:

> Upendo ni zawadi ya hali ya juu kutoka kwa Mungu; unyenyekevu, upole, upendo unaovumilia. Maono yote, unabii wote, au karama zote ni mambo madogo sana ukilinganisha na upendo. Hakuna kitu chochote cha hali ya juu katika dini; kama unatafuta chochote kilicho zaidi ya upendo, unatafuta kisichoeleweka na unatoka nje ya sheria ya kifalme.
>
> Huwa unawauliza wengine, "Umeshapokea Baraka hii au ile?" Kama unawauliza ukimaanisha chochote na siyo upendo, unamaanisha vibaya, unawapeleka nje ya njia, na kuwaweka kwenye harufu mbaya. Jifikirie ndani ya moyo wako, kwamba

[339] Warumi 13:8-10

> tangu wakati ule Yesu alipokuokoa kutokana na dhambi zote, hujalenga kwenye lolote zaidi ya ule upendo ulioko katika 1 Wakorintho 13. Huwezi kwenda zaidi ya hapo.[340]

### Kumpenda jirani yako

Maeneo mawili yanaweza kuelezea jinsi upendo mkamilifu unavyoonekana kwa Wakristo wengine.

#### *Upendo huheshimu mitazamo ya waamini wengine*

Akiwaandikia Wakristo wa Korintho, Paulo anazungumzia kuhusu uhuru wa Kikristo. Nitawajibikaje kwa muumini mwingine ambaye atakuwa ameumizwa kiroho na uhuru wangu? Paulo aliandika kwa Wakristo "wenye uwezo" waliokuwa wakisema, "Tunatambua kwamba sanamu siyo chochote. Kula vyakula vya kutambikia havina matatizo yeyote kwetu." Paulo alijibu:

> Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! Dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. Hivyo, mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo. Kwa hiyo, chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu.[341]

Paulo angeacha kula nyama maisha yake yote kuliko kusababisha ndugu yake Mkristo dhaifu kuanguka. Upendo mkamilifu unamaanisha kwamba anajali zaidi wokovu wa ndugu yake Mkristo kuliko haki zake. Baadaye, Paulo anasema, "bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo."[342]

Wakorintho walisema, "Tuko huru kufanya lolote tunalolipenda. Hatuhitajiki kufikira kuhusu mahitaji ya waumini wengine." Paulo akasema, "Niko huru kuhudumia mahitaji ya waumini wengine. Mimi siyo mfungwa wa matamanio na haki zangu mwenyewe. Niko huru kuwapenda wengine." Huu ndio upendo mkamilifu ambao Mungu anataka kumpa kila Mkristo.

► Soma Warumi 14.

Katika kanisa la Roma, kulikuwa na Wakristo "dhaifu" waliokuwa wakila mboga za majani tu. Hawa inawezekana walikuwa ni Waristo wa Kiyahudi walioendelea kufuata sheria za vyakula, na hawakuwa tayari kula vyakula ambavyo havikuwa safi kwao. Kulikuwa pia na

---

[340] Kimenukuliwa kutoka John Wesley, *A Plain Account of Christian Perfection* (Kansas City: Beacon Hill Press, 1966), 99.
[341] 1 Wakorintho 8:10-13
[342] 1 Wakorintho 9:12

Wakristo “wenye uwezo” waliokuwa na ufahamu zaidi, na wakijua kwamba sheria za vyakula hazikuwa kikwazo tena kwa Mkristo.

Paulo alionyesha kila kikundi ni nini maana kupenda kama Kristo naye alivyopenda. Wakristo “dhaifu” wasiwahukumu wenzao wanaokula nyama. Upendo hauhukumu.

Hata hivyo, Mkristo “mwenye uwezo” asimnyanyase Mkristo “dhaifu” na asiutumie uwezo wake kudharau imani ya yule mdhaifu. Badala yake, Mkristo mwenye nguvu, aachane na haki zake ili aweze kuzuia kuharibika kwa imani ya yule muumini dhaifu. Kwa nini? Kwa ajili ya upendo:

> Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake.[343]

Hii ndiyo maana ya kumpenda jirani yako mkristo. Tunapaswa kupenda kama Kristo naye alivyopenda. Aliyatoa maisha yake kwa ajili ya huyu ndugu mdhaifu; kwa hakika, Paulo anasema, tunaweza kuacha kula nyama ingawaje ni haki yetu.

► Jadili eneo ambalo waamini wa kweli na wa Mungu wanatofautiana. Maeneo ambayo hayako wazi kutokana na mafundisho ya Biblia; maeneo ambayo yanaonyesha tofauti za mitazamo. Tumia kanuni za Paulo kutoka Warumi 14 katika suala hili. Ni kwa jinsi gani makundi haya mawili – Wakristo “dhaifu” na “wenye uwezo” wanaweza kushughulikia eneo hili?

### *Upendo huwajali wakristo wanaoanguka katika dhambi*

Jane ni Mkristo aliyetapeliwa katika biashara yake na mshirika mwenzake wa kanisa. Ivani alimwuzia gari lililokwisha tumika, akijua kwamba gari hilo lilikuwa na matatizo makubwa ya kiufundi. Ivani alimdanganya Jane kwamba, “gari hili limeshakaguliwa na fundi magari, na kwamba limethibitishwa liko katika hali nzuri sana. Unaweza kuniamini. Mimi ni Mkristo.”

Baada ya siku mbili tu baada ya kuwa gari lile limenunuliwa, Jane aligundua kwamba mfumo wa usambazaji umeme kwenye lile gari ulikuwa mbovu – na kwamba Ivani alikuwa analijua tatizo hilo.

► Jane atafanya nini?

Je, umejibu, “Jane atamwonya kila mtu kwamba Ivani siyo mwaminifu”? Je, umejibu, “Jane hatasema lolote katika kujizuia asimdhalilishe Mkristo mwenzake”? Tuangalie jibu la Yesu.

► Soma Mathayo 18:15-17.

---

[343] Warumi 14:15

Yesu alitoa hatua nne ambazo zinaonyesha upendo mkamilifu unavyoshughulika na mtu aliyeanguka katika dhambi. Tafadhali fahamu kwamba mfano huu unahusiana na tabia ya dhambi. Yesu hapa hazungumzii kuhusu tofauti binafsi za mawazo. Hajasema, "Ondokeni, nendeni mkashughulike na matatizo ya kila mtu." Yesu anaelezea hali ambayo ndugu mkristo amemkosea mkristo mwenzake. Tuziangalie hatua hizi:

1. **Nitaenda kwa yule ndugu mimi mwenyewe**. Upendo mkamilifu "haufurahii udhalimu."[344] Hautafuti nafasi ya kueneza udhalimu. Badala yake, mtu wa upendo hujaribu kulishughulikia tatizo kwa ukimya yeye mwenyewe. Mtu wa upendo hushughulika na ndugu "aliyeghafilika katika kosa lolote… kwa roho ya upole."[345] Lengo ni kumrejeza upya ndugu huyo. Kama hakutakuwepo na kutubu…

2. **Nitachukua mtu mmoja au wawili pamoja nami kama mashuhuda**. Hapa pia lengo kuu ni kurejeza upya. Mashahidi hawa ni lazima wawe viongozi wa kiroho wa kanisa wanaoweza kutoa ushauri mzuri wa kuleta urejezo upya.[346] Kama hakutakuwepo na kutubu…

3. **Nitaileta dhambi hiyo kwenye kusanyiko la kanisa**. Hapa pia lengo kuu ni kurejeza upya. Lengo hapa siyo kulipiza kisasi au kumdhalilisha mtu hadharani. Lengo la Kanisa kuadabisha lazima liwe ni kuleta kutubu na kumrejesha ndugu. Kama mtu huyu ataasi na akakataa kutubu…

4. **Kanisa lichukue hatua za nidhamu dhidi ya huyu mbaya**. Kanisa la Korintho lilikuwa na mshirika wa kanisa aliyetenda dhambi ya uzinzi. Paulo aliliagiza kanisa limchukulie hatua za kinidhamu mtu huyu. "Mwondoeni yule mbaya miongoni mwenu."[347] Hatuwezi kupuuzia matendo ya dhambi katika mwili wa Kristo.

Hata hivyo, tafadhali angalia haya maneno ya Yesu: "Na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru."[348] Ni kwa jinsi gani wakristo wanatakiwa kuwatendea watu wa mataifa na watoza ushuru? Kwa upendo. Hadi hapa, bado lengo ni kurejeza upya. Katika 2 Wakorintho, Paulo analezea hali ya muumini ambaye anapewa nidhamu na kanisa na ametubu kweli. Paulo anasema,

> Yamtosha mtu wa namna hii adhabu ile aliyopewa na walio wengi; hata kinyume cha hayo, ni afadhali mumsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. Kwa hiyo nawasihi kumthibitishia upendo wenu.[349]

Katika 1 Wakorintho, Kanisa lilivumilia dhambi za wazi na halikutaka kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale waliitenda dhambi hizo. Paulo akawakumbusha kwamba **Upendo wa**

---

[344] 1 Wakorintho 13:6
[345] Wagalatia 6:1
[346] Ibid.
[347] 1 Wakorintho 5:13
[348] Mathayo 18:17
[349] 2 Wakorintho 2:6-8

**Mungu** unataka watu wote watenda dhambi dhidi ya mwili wa Kristo wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Katika 2 Wakorintho, Kanisa lilichukulia hatua za kinidhamu dhidi ya mtu aliyetenda dhambi, lakini wakati mtu huyu alipotubu, kanisa halikutaka kumsamehe. Paulo akawakumbusha kwamba **upendo kwa ajili ya jirani yako** unahitaji tuwasamehe wale wote wanaotubu.

Lengo la kuchukua nidhamu kwa kanisa lazima siku zote liwe ni toba na marejezo upya. Upendo mkamilifu hautafuti kulipa visasi.

### Kumpenda jirani asiyeamini

Ni kwa njia gani tunaweza kuonyesha upendo mkamilifu kwa watu ambao hawajaamini, zaidi sana wale ambao wanatuchukia kwa sababu tu sisi ni Wakristo? Yesu alisema,

> Mmesikia kwamba imenenwa, "Umpende jirani yako, na, umchukie adui yako," lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni.[350]

Unapowapenda wale wanaokusababishia wewe mateso, uko "mkamilifu kama Baba yako wa mbinguni alivyo mkamilifu." Watu watakatifu wana upendo kama Baba wa Mbinguni alivyo na upendo. Hii ndio maana ya kuwa mkamilifu.

Watu watakatifu, "hudhihirisha upendo wao kwa watu wote, siyo tu kwa waamini wenzao, bali pia kwa wale wote ambao siyo waamini wenzao, wale wanaotupinga, na wale wote wanaojihusisha na matendo ya uovu." Tunapaswa tuwajibike kwa wale wanaotupinga kwa huruma, polepole, kwa uangalifu na unyenyekevu. Mungu anakataza kuanzisha ugomvi, kulipiza visasi, vitisho, au kujitafutia haki mwenyewe. Ingawaje Mungu anatuamuru tuachane na matendo ya dhambi, tunapaswa kumpenda na kumwombea mtu yeyote anayejihusisha na tabia hizi."[351]

Wakristo siku zote wamekuwa wakiishi katika ulimwengu unaoipinga Injili. Paulo aliwataka watu wa Rumi kuheshimu mamlaka zilizopo na kulipa kodi zao – kwa serikali iliyokuwa inawauwa Wakristo na muda siyo mrefu itamuuwa na Paulo.

Petro aliwaagiza Wakristo, "Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme."[352] Huyu pia ni mfalme anayetakiwa apewe heshima, lakini muda siyo mrefu naye atamuuwa Petro. Lakini Petro alitaka sana Wakristo wawapende adui zetu. Kwa kuwapenda hata maadui zetu, tunakuwa mashuhuda wa ukweli wa Injili. "Kwa

---

[350] Mathayo 5:43-45
[351] Kutoka: *Discipline of the Bible Methodist Connection of Churches*, 2014.
[352] 1 Petro 2:17

sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu."[353]

Yoshua ni Mchungaji kutoka Nigeria katika eneo moja la Kaskazini ambako kuna Wakristo wengi lakini wamekuwa wakiteswa vikali na mashambulizi ya wanajeshi wa Kiislamu. Wanajeshi hawa wamekuwa wakichoma makanisa, kuuwa Wakristo, na kuwateka wasichana wadogo wa kike kwa ajili ya kuwauza kama watumwa. Mara ya mwisho nilipoitembela tena Nigeria, Yoshua alinionyesha picha za miili ya marehemu waliokuwa washirka wa kanisa lake waliokuwa wameuawa na washambuliaji wa Kiislamu.

Kisha Yoshua akanionyesha picha zinazoonyesha hatua zilizochukuliwa na kanisa lake baada ya mauaji hayo. Kanisa lake lilijenga shule katika kijiji cha Waislamu; walichimba kisima cha maji kwa ajili ya wanakijiji; walitoa viti vya magurudumu kwa ajili ya Waislamu waathirika wa ukoma; na sasa wanajenga kituo cha zahanati kwa ajili ya kijiji hicho. Wanaonyesha upendo kwa maadui zao.

Mchungaji Yoshua alisema, "Waislamu wengi wanakuja kwa Kristo kwa sababu wanauona upendo wa Mungu kupitia Wakristo. Tunawapata siyo kwa kutumia mitutu ya bunduki au kulipiza kisasi; bali tunawapata kupitia kuishi kwetu sawa na andiko la Mathayo 5:43-48." Haya ni matokeo ya maisha ya upendo mkamilifu tunayoyaishi kwa sasa duniani.

► Kuna changamoto gani kubwa katika kuwapenda jirani ambao hawajaamii katika dunia yako? Orodhesha baadhi ya hatua za kivitendo za kuonyesha upendo kwa watu ambao hawajaamini katika jumuiya yako.

Mwandishi wa Kirusi Leo Tolstoy aliandika makala fupi kuonyesha nini maana ya kuishi maisha ya upendo mkamilifu. Martini alikuwa maskini mtengenezaji wa viatu aliyempenda Mungu kwa kiwango kikubwa sana.[354] Siku moja usiku, Martini akiwa anasoma Biblia alipitiwa na usingizi akalala. Akawa anaota kwenye ndoto Yesu akisema kwamba, "Kesho, nitalitembelea duka lako."

Siku iliyofuata, Martini alikaa akiwa anamngojea Yesu. Watu wengine walikuja dukani kwa Martini, lakini Yesu hakutokea. Askari mmoja wa zamani, mzee, alikuwa amesimama nje akitetemeka kwa baridi. Martini alimkaribisha huyu mzee dukani kwake apate kikombe cha chai ya moto. Mwanamke mmoja maskini naye akawa anapita karibu na duka hilo, akijaribu kumfunika mwanae kwa ajili ya kumpatia joto. Martini alimnunulia supu na blanketi kwa ajili ya kumlinda mtoto na baridi. Baadaye Martini alinunua chakula kwa ajili ya kijana aliyekuwa na njaa.

Martini alikata tamaa kwa kuwa Yesu ilikuwa aje, lakini akasema, "Ilikuwa ni ndoto tu. Ilikuwa ni ujinga mimi kufikiria kwamba Yesu angeweza akaja kwenye duka la viatu."

---

353 1 Petro 2:15

354 Leo Tolstoy, "Where Love Is, There God is Also."

Usiku uliofuata, Martini akiwa anasoma Biblia, alisikia usingizi akalala. Aliota ndoto kwamba aliwaona watu wakiwa wamesimama dukani kwake. Yule askari akamwuliza, "Martini unanikumbuka? Mimi ni Yesu." Mwanamke aliyekuwa na mtoto naye akamwambia, "Martini, mimi ni Yesu." Kijana aliyekuwa na njaa akasema, "Mimi ni Yesu." Martini aliamka na kuanza kusoma:

> Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia…. Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.[355]

Katika karne ya pili, kundi moja la Wakristo liliitwa "Genge la wacheza Kamari" kwa sababu walihatarisha maisha yao kwa kuwatunza watu waliokuwa wanakufa kwa magonjwa ya kuambukiza. Hili kundi liliwatembelea wafungwa, kuwahudumia wagonjwa, na kuokoa watoto wadogo waliokuwa wametupwa na wazazi wao. Genge la wacheza Kamari lilidhihirisha upendo kamili.

Katika mwaka 252 B.K. ugonjwa wa tauni ulitokea katika jiji la Carthage. Madaktari waligoma kuwatembelea wagonjwa; familia zilitupa miili ya wapendwa wao waliofariki barabarani, jiji lilikuwa katika taharuki kubwa. Cyprian, askofu mkuu wa Carthage, aliwakutanisha waumini wake. Aliwakumbusha kwamba Wakristo wameitwa kuonyesha upendo mkamilifu. Wakristo wa Carthage wakaanza kuwazika waliokufa, kuwaganga waliokuwa wagonjwa, na wakaukoa mji wao kutokana na uharibifu. Walikuwa watu wa upendo kamili; walikuwa "wakamilifu" kama Baba yao wa mbingini alivyo mkamilifu.

## Aliipata siri - Esther Ahn Kim

Esther Ahn Kim[356] alikuwa mwalimu wa muziki aliyeishi katika nchi ya Korea wakati wa utawala wa Wajapani kuanzia mwaka 1937. Wajapani walimtaka kila mkaazi kuinamia sanamu ya mungu jua katika milima ya Namsan. Mwaka 1939, Esther aliamriwa kusujudu kwenye hekalu la mungu jua. Adhabu ya kukataa kusujudu ilikuwa ni kufungwa jela pamoja na mateso makali.

Baadhi ya Wakristo walishaamua kwamba, "Kwa nje tutasujudu, lakini dhamira yetu ya ndani itamwabudu Kristo." Esther alidhamiria kabisa kwamba hawezi kumsujudia Mungu wa uongo. **Alimpenda Mungu** kwa moyo usiogawanyika. Siku hiyo, alikataa kusujudu.

Mwishoni mwa mwaka 1939, baada ya kuwa mafichoni kwa miezi kadhaa, Esther Ahn Kim alikamatwa. Kwa miezi yote hiyo aliyokuwa mafichoni alikuwa anajiandaa kwenda jela. Alifunga na kuomba, alikariri Maandiko, na alijiandaa kiakili na kimwili katika kukabiliana na mateso ya jela.

---

[355] Mathayo 25:34-40
[356] Ilichukuliwa kutoka: Esther Ahn Kim, *If I Perish* (Chicago: Moody Press, 1977).

Kim alitumikia kifungo cha miaka sita jela. Alisulubiwa mara kwa mara kwa mateso lakini alibakia kuwa mwamiifu kwa sababu alimpenda Mungu. Lakini Kim alijitambua kwamba alikuwa ameitwa **kumpenda jirani yake**. Akiwa kule jela, Esther alianzisha kuomba kila siku asubuhi, "Mungu ni mtu gani unataka umpende leo kupitia mimi?" Wakati mwingine alitoa chakula chake cha mgao kwa siku kadhaa kwa mama mmoja aliyekuwa amehukumiwa kunyongwa kwa kosa la kumuua mume wake. Kupitia upendo wa Esther Kim, huyu mama alimpokea Kristo kabla hajafa.

Esther Ahn Kim alikutana na uzoefu ambao Thomas Chisholm aliandika kwenye wimbo wake: "Oh! niwe kama wewe… mvumilivu wa mambo ya ukatili ya kuumiza, aliye tayari kuteseka, kuwatumikia wengine."

### Oh! Niwe kama wewe - Thomas Chisholm

Oh! Niwe kama wewe, Mkombozi uliyebarikiwa,
Hii imekuwa siku zote ni nia yangu kubwa na maombi;
Kwa furaha nitasalimisha yote ya hazina za dunia,
Nifanane kabisa na yeye.

Oh! Niwe kama wewe, mwingi wa huruma,
Upendo, msamaha, upole na mwema.
Unayewasaidia wasiojiweza, unayewafariji wanaozimia,
Unayetafuta wenye kutangatanga dhambini wakapatikana.

Oh! Niwe kama wewe, mnyenyekevu katika roho,
Mtakatifu usiyekuwa na maadhara, mvumilivu na mjasiri;
Usiyekuwa mwingi wa hasira, mwenye subira wakati watu wanapokuwa wabaya
Uliye tayari kuteseka, ili watu wengine wapate kuokolewa.

Oh! Niwe kama wewe, Oh! Niwe kama wewe,
Mkombozi uliyebarikiwa, msafi kama wewe;
Njoo kwangu kwa uzuri wako, njoo kwangu katika ukamilifu wako;
Nifanye niwe kama wewe, ndani kabisa ya moyo wangu.

## Tafakuri ya Somo la 8

(1) Watu katika wakati wa dunia ya Yesu waliamini kile kilichofundishwa na Agano la Kale kuhusu utakatifu. Hata hivyo, walishindwa kuishi kwenye mpangilio wa Mungu kwa ajili ya watu watakatifu.

(2) Mfano halisi wa kuigwa wa utakatifu unaonekana katika maisha ya Yesu wa Nazarethi. Alifuata kila kanuni ya utakatifu kutoka katika Agano la Kale

(3) Kumpenda jirani yetu kwa ukamilifu ni kupenda kama Yesu alivyopenda – kwa kujitoa na unyenyekevu.

(4) Kuwa mkamilifu maana yake ni kuwa kamili. Kuwa mkamilifu haina maana kwamba hakuhitajiki kukua tena.

(5) Agizo au amri, "ni ahadi zilizojificha." Kama Mungu akiagiza jambo, atafanya liwezekane. Utakatifu unakamilishwa siyo kwa nguvu za kibinadamu bali kwa neema ya Mungu.

(6) Upendo ni ukamilifu wa sheria. Tunapopenda kama Mungu anavyotutaka tupende, tunatimiza matakwa ya sheria.

## Kazi ya Kufanya

(1) Andaa andiko kuhusu "Kumpenda adui yako wa karne ya ishirini na moja." Tumia Mathayo 5:43-48 kama andiko lako. Onyesha inamaanisha nini kumpenda adui yako katika dunia yetu. Hakikisha unajumuisha na habari njema za kile Mungu alichokifanya kupitia Kristo hata kuweza kumpenda adui yako liwe jambo linalowezekana.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Mathayo 5:43-48.

# Somo la 9
# Maisha matakatifu ni kuishi katika ukamilifu wa Roho

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kutambua mabadiliko ambayo Upentekoste ulileta katika kanisa la mwanzo.

(2) Kutambua nguvu ya Roho Mtakatifu katika kuleta mabadiliko kwa waamini wakati wa sasa.

(3) Kuona tunda la Roho Mtakatifu katika maisha ya kila siku kama tabia ya maisha yaliyojazwa nguvu za Roho.

(4) Kukariri Wagalatia 5:22-25.

## Petro: Jiwe Lililokuwa Kikwazo na Likaja Kufanyika Mwamba

Yesu aliwauliza wanafunzi wake, "Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?" Petro alijibu, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Yesu akajibu akamwambia, "Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."[357] Hii ilikuwa ni moja ya siku zilizowahi kung'ara sana katika maisha ya Petro.

Muda mfupi baadaye, Yesu akawaambia wanafunzi wake kwamba atakufa huko Yerusalemu. Wakati Petro alipoanza kumkemea Yesu, alimjibu akamwambia, "Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu."[358] Neno "kikwazo" lina maana ya "jiwe lililo kizuizi." Kwa mara ya kwanza Yesu alimwita Petro "mwamba," lakini mara hii anamwita "jiwe lililo kizuizi." Hakuna wakati ambao Petro aliwahi kujikuta yuko gizani katika maisha yake kama siku hii.

> **Sala kwa ajili ya Utakatifu**
>
> "Puliza ndani yangu, Roho Mtakatifu,
> ili kwamba niweze kufikiria utakatifu ni nini.
> Niwezeshe, Roho Mtakatifu,
> ili kwamba niweze kufanya lililo takatifu.
> Nipendezeshe, Roho Mtakatifu,
> ili kwamba niweze kupenda kilicho kitakatifu.
> Niimarishe mimi, Roho Mtakatifu,
> ili kwamba niweze kulinda kilicho kitakatifu.
> Nilinde mimi, Roho Mtakatifu,
> ili kwamba niweze kuhifadhi kilicho kitakatifu."
>
> - Agustino wa Hippo

[357] Mathayo 16:15-18
[358] Mathayo 16:23

Kisa cha Petro kinazidi kumweka gizani zaidi siku ambayo Yesu alikuja kukamatwa usiku. Baada ya kuwa ameahidi kwamba hatamwacha Bwana wake, Petro alimkana Bwana wake na kukimbia kwa ajili ya hofu. "Mwamba" ulishindwa wakati wa saa ya majaribu.

Baada ya anguko hilo, mtu anayesoma vitabu vya Injli anaweza akahisi kwamba Petro hatakaa aweze kuchukua jukumu lolote la Kanisa. Kwa mshangao wetu, Petro anakuwa kiongozi katika kanisa la mwanzo. Ni nini kilicholeta hata hayo mabadiliko ya ghafla na haraka kiasi hicho? Jibu ni Pentekoste.

Baada ya kufufuka kwake, Yesu alitoa ahadi hii kwa wanafunzi wake, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."[359] Ahadi hii ilitimia katika kitabu cha Matendo 2. Wanafunzi wakajazwa nguu za Roho Mtakatifu wakaanza kuhubiri. Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, zaidi ya watu 3000 waliamini katika Pentekoste ya kwanza.

Petro alibadilishwa na nguvu ya Pentekoste. "Jiwe lililokuwa kizuizi" limegeuka kuwa "Mwamba" ambaye aliliongoza Kanisa katika nyakati zake muhimu sana za mwanzo. Simoni Petro alihubiri kwenye eneo lote la Dola ya Kirumi, aliandika barua mbili za Agano Jipya, na hatimaye alisulubiwa kwa sababu ya imani yake.

Ni nini kilileta mabadiliko haya? Kupitia uwezo wa kubadilisha wa Roho Mtakatifu, mtu mmoja mvuvi Mgalilaya akawa kiongozi katika karne ya kwanza. Petro alijifunza kwamba kuwa mtakatifu inamaanisha kuishi ndani ya ukamilifu wote wa Roho Mtakatifu.

► Waombe wanafunzi wako watoe ushuhuda wa jinsi gani Roho Mtakatifu ameweza kuleta mabadiliko katika maisha yao. Ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu anakupa nguvu kwa ajili ya huduma, ushindi dhidi ya maovu, na furaha katika maisha yako ya Ukristo?

## Roho Mtakatifu na Pentekoste

Petro hakuwa mwanafunzi peke yake aliyebadilishwa wakati wa Pentekoste. Kila mwanafunzi alibadilishwa na Roho Mtakatifu. Hata Thomaso wa mashaka alifanyika kuwa mmishenari mwaminifu sana. "Mwana wa ngurumo" akawa "Mtume wa Upendo." Wafuasi wa Yesu walibadilishwa kutoka wanafunzi wenye hofu hadi kuwa jeshi lenye nguvu kwa ajili ya Injili. Kitabu cha Matendo kinaonyesha matokeo ya Roho Mtakatifu dhidi ya hawa waamini wa kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa na ufanisi sana siyo kwa sababu ya karama zisizokuwa za kawaida za mitume, bali ni kwa sababu ya karama zisizokuwa za kawaida za Roho Mtakatifu. Wanafunzi walijifunza kwamba maisha matakatifu yako ndani ya ukamilifu wa Roho Mtakatifu.

---

[359] Matendo ya Mitume 1:8

## Ahadi Iliyoahidiwa ya Roho Mtakatifu

Kwa hakika, hili lilikuwa ni jambo moja la kushangaza sana ambalo wanafunzi walikuwa hawajawahi kulisikia kutoka kwa Yesu: "Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke."[360] Hawa wanafunzi walikuwa wameacha vyote wakamfuata Yesu. Hebu fikiria mshtuko wao wakati Yesu aliposema, "Kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu."

Kwenye Chakula cha Mwisho, Yesu alielezea jinsi Roho Mtakatifu atakavyowahudumia waamini. Roho Mtakatifu:

- Atakuwa Msaidizi (Yohana 14:16-17)
- Atakuwa Mwalimu (Yohana 14:26)
- Atakuwa shuhuda wa Mwana (Yohana 15:26)
- Atauthibitishia ulimwengu (Yohana 16:7-11)
- Atasema kweli yote (Yohana 16:13-15)

Baada ya kufufuka, Yesu alirudia ahadi yake ya kutuma Roho Mtakatifu:

> Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, "ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache… Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."[361]

Huduma ya Yesu hapa duniani haikuishia tu msalabani, au kwenye kaburi, au hata kwenye kupaa kwake mbinguni. Huduma ya Yesu ilikamilishwa wakati wa Pentekoste. Alama ya utambulisho wa huduma ya Yesu ilikuwa kwamba, "atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto."[362] Karama za Roho Mtakatifu zilikuwa ni kilele cha huduma ya Yesu hapa duniani.

## Kupokelewa kwa Roho Mtakatifu

Kwenye kitabu cha Matendo, Roho amelipa nguvu Kanisa kwa ajili ya huduma. Wakati wa Pentekoste, ahadi ya kupelekewa Msaidizi ilitimia. Baada ya Pentekoste, Roho Mtakatifu aliendelea kuwepo katika kanisa. Alama zilizoambatana na ujio wa Roho Mtakatifu zilithibitisha huduma yake kwa waamini.

Kwanza, "kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu."[363] Hii inaonyesha ujio wa nguvu ya Roho Mtakatifu. Katika Matendo, tunaona nguvu za Roho

[360] Yohana 16:7
[361] Matendo ya Mitume 1:4-8
[362] Luka 3:16
[363] Matendo ya Mitume 2:2

Mtakatifu zikitenda kazi kupitia kwa waamini. Baada ya Pentekoste, kanisa lilihudumu kwa nguvu mpya na ufanisi mkubwa. Roho Mtakatifu amekuwa akitenda kazi duniani hata kabla ya Pentekoste.[364] Lakini baada ya Pentekoste, nguvu ya Roho imekuwepo wakati wote katika huduma za kanisa.

Pili, "kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja."[365] Katika maandiko, siku zote moto unawakilisha usafi. Alama ya Roho Mtakatifu ilikuwa usafi wa moyo. Petro alitoa ushuhuda wake kwenye Baraza la Yerusalemu kuhusu kazi ya Mungu miongoni mwa Mataifa:

> Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi, wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, **akiwasafisha mioyo yao kwa Imani**.[366]

Tatu, wale waliokuwa katika chumba cha juu "wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."[367] Hii iliwawezesha wanafunzi kushuhudia kwenye mataifa yote. Kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, wanafunzi waliweza kutekeleza Agizo Kuu la Kristo. Katika Babeli, Mungu aliihukumu dhambi yao kwa kuwachanganya katika lugha zao wasiweze kuelewana. Wakati wa Pentekoste, Mungu aliruhusu kila msikiaji kuisikia injili "katika lugha yake mwenyewe." Wakati wa Pentekoste, Mungu alianza kugeuza mtawanyiko wa athari za dhambi lugha zilizojitokeza wakati wa Pentekoste ziliwakilisha ahadi ya Mungu kwamba Injili itawafikia watu wa mataifa yote kupitia nguvu za Roho mtakatifu afanyaye kazi kupitia Kanisa.

Wakati wa Pentekoste, mwishowe wanafunzi walikuja kutambua kile Yesu alichokuwa amemaanisha aliposema, "Yawafaa ninyi mimi niondoke." Roho Mtakatifu hakuwa mbadala wa "pili bora" kwa Yesu Kristo. Wakati Yesu aliyefanyika mwili asingeweza kuwa mahali popote kwa wakati mmoja tu, Roho Mtakatifu yuko mahali popote kwa wakati mmoja. Roho Mtakatifu aliwawezesha wanafunzi kutekeleza Agizo Kuu la Yesu. Roho Mtakatifu huwawezesha Wakristo kuishi maisha matakatifu yanayoweza kuwa ushuhuda kwa ulimwengu wote.

### Utakatifu katika kanisa la mwanzo: Maisha katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu

Kitabu cha Matendo kinaonyesha kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya kila mwamini. Kwa sababu ya nguvu ya Roho Mtakatifu, Wakristo walikuwa na nguvu ya kushuhudia,[368] ujasiri mbele ya upinzani,[369] ushindi dhidi ya dhambi za kujitakia,[370] na karama za roho

---

[364] Mifano ya kazi za Roho Mtakatifu katika Agano la Kale: Mwanzo 1:2; Mwanzo 6:3; Kutoka 31:3; Hesabu 11:25-29; Waamuzi 3:10; 6:34; 13:25; 1 Samweli 10:6-10; 2 Mambo ya Nyakati 28:12; Nehemia 9:20; Isaya 63:10-14; Zakaria 4:6-9.

[365] Matendo ya Mitume 2:3

[366] Matendo ya Mitume 15:8-9

[367] Matendo ya Mitume 2:4

[368] Matendo ya Mitume 1:8

[369] Matendo ya Mitume 4:31

kwa ajili ya huduma.[371] Waamini wa mwanzo walikuwa watakatifu kwa sababu waliishi katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu.

Kitabu cha Matendo kinaonyesha kanisa la mwanzo likitimiza wito wa Yesu wa kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi, wito wake wa "mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu," na ahadi yake kwamba "kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo (wewe) utafanya." Hii ilifanyika kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Kitabu cha Matendo kinaonyesha uwepo wa Roho Mtakatifu katika maisha ya waamini hawa wa mwanzo.

### Nguvu kwa ajili ya Huduma

Kama vile Yesu alivyokuwa "amejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu" alipokabiliana na Shetani,[372] Petro alikuwa "amejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu" alipokabiliana na mamlaka za Kiyahudi.[373] Luka anaelezea maisha ya Petro kwa maneno yale yale aliyotumia kuelezea maisha ya Yesu. Kazi ya Roho Mtakatifu inayoonekana katika maisha ya Yesu Kristo duniani yalikuwa sasa ni heshima kwa waamini wote.

Katika siku ya Pentekoste, waamini zaidi waliongezeka kwenye kanisa kuliko wakati mwingine wowote wa huduma ya Yesu hapa duniani. Kupitia Nguvu ya Roho Mtakatifu, mitume walihudumu kwa nguvu na mamlaka. Miujiza ya uponyaji ilidhihirisha nguvu za Mungu kwa ulimwengu usioamini. Watu walikuwa "wamejazwa kwa mshangao na kustajaabu," na watu wote "wakawakusanyikia."[374] Kwa jinsi mitume walivyokuwa wakihudumu katika ukamilifu wa Nguvu ya Roho Mtakatifu, huduma zao zilionekana kujaa nguvu ya kimungu. Kupitia Nguvu ya Roho Mtakatifu, mitume waliweza kutekeleza Agizo la Yesu la "kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi."[375]

### Ujasiri wa Kiroho

#### *Wanafunzi walikuwa wajasiri katika kutangaza Injili*

Nguvu ya kubadilisha ya Roho Mtakatifu inaonekana wazi katika kitabu chote cha Matendo ya mitume. Mitume ambao kwa miezi michache iliyopita walikuwa wamekimbia katika tukio la kukamatwa kwa Yesu, sasa wanahubiri kwa ujasiri mkubwa.

> "Hatujazwi Nguvu ya Roho Mtakatifu kwa ajili ya kufanya kazi yeyote maalumu, lakini tu ni kumruhusu Mungu afanye kazi kupitia sisi."
> - Oswald Chambers

Muda mfupi baada ya Pentekoste, wakuu wa dini waliwakamata Petro na Yohana. Ni wiki chache tu zimepita, Petro alikuwa amemkana Kristo. Sasa,

---

370 Warumi 8:2
371 Matendo ya Mitume 2:17-18; 1 Wakorintho 12:7-11
372 Luka 4:1
373 Matendo ya Mitume 4:8
374 Matendo ya Mitume 3:10-11
375 Mathayo 28:19

"Petro, akiwa amejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu" alihubiri kwa ujasiri mkubwa. Wakuu wa dini "walishangaa" kwa maneno ya hawa "watu wa kawaida ambao walikuwa hawana elimu yeyote."[376]

Kupitia ujazo wa Roho Mtakatifu, mitume walikuwa wajasiri katika kuhubiri kwa nguvu na upako. Kutoka kundi la watu waoga, wavuvi, watoza ushuru, na wafanyakazi wa kawaida, wanafunzi sasa wamekuwa ni watu ambao "wameupindua ulimwengu."[377]

### *Wanafunzi walikuwa wajasiri mbele ya mateso*

Walipokabiliwa na upinzani, mitume hawakuomba kwa ajili ya kuachiwa kutoka kwenye mateso, bali kwa ajili ya ujasiri wa kumhubiri Kristo bila kujali mateso. "Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote…" Mungu alijibu maombi yao. "Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri."[378]

Alama isiyokuwa na dosari yeyote ya kazi ya Roho Mtakatfu kwa kanisa ilikuwa ni ile ya ujasiri wa kuitangaza Injili mbele ya upinzani. Hadi mwisho wa karne ya kwanza, Injili ilikuwa imeenea kutoka watu 120 kutokea chumba cha juu hadi kwenye majiji yote ya Dola ya Kirumi.

## Maisha ya Ushindi

Katika kila kizazi, Wakristo wamekabiliwa na jaribu la kuwa "Wakristo wa Jumapili," – watu ambao wanahudhuria makanisani lakini maisha yao hayaonyeshi mabadiliko ya ndani na mwisho unaoeleweka. Kanisa la mwanzo lilibadilika katika kila eneo la maisha kwa Nguvu ya Roho Mtakatifu.

Katika Agano la Kale, tunaona juhudi za watu waliotaka kushikamana na agano, lakini wakijikuta hawawezi kufanya hivyo kwa sababu mioyo yao ilikuwa imegawanyika. Mtunga Zaburi aliwaelezea watu wa Israeli kwamba: "Mioyo yao haikuwa thabiti kwake. Wala hawakuwa waaminifu katika Agano lake." [379]

Kupitia Ezekieli, Mungu aliahidi siku ambayo watu wake wangebadilishwa.

> Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.[380]

---

[376] Matendo ya Mitume 4:2-13
[377] Matendo ya Mitume 17:6
[378] Matendo ya Mitume 4:29-31
[379] Zaburi 78:37
[380] Ezekieli 36:26-27

Kabla ya Pentekoste, mitume walifuata mwelekeo uliokuwa unafanana na ule wa wana wa Israeli. Walikuwa wanataka kumfuata Kristo, lakini wakishindwa siku zote. Walikuwa na mashaka; walipigania nafasi; walikimbia kwa hofu. Wakati wa Pentekoste, ahadi ya Ezekieli ilitimia. Mitume walipewa uwezo na Roho Mtakatifu wa kuishi maisha ya ushindi. Badala ya kuwa na moyo wenye kutii nusu nusu, walitembea katika kutii kwa furaha sheria ya Mungu. Kupitia Roho Mtakatifu, maisha ya ushindi yakawa ni jambo la kawaida kwa watu wa Mungu.

### Mwongozo wa Huduma

Kabla ya Pentekoste, tamaa na hofu vilitawala maisha ya mitume. Juhudi zao za kumtumikia Yesu zilikwamishwa na kushindwa kwao wenyewe. Baada ya Pentekoste, Roho Mtakatifu aliwaongoza mitume kwenye huduma zilizokuwa na ufanisi.

Roho Mtakatifu aliliongoza Kanisa katika maamuzi magumu yaliyoathiri mahusiano kati ya Wayahudi na mataifa waliogeukia Ukristo.[381] Roho Mtakatifu aliongoza uchaguzi wa viongozi wa Kanisa.[382] Roho Mtakatifu alimwongoza Paulo katika safari yake ya Makedonia.[383] Roho Mtakatifu alimwongoza Paulo katika safari yake ya kurejea Yerusalemu mbali na hatari iliyokuweko ya kukamatwa.[384] Huduma za kanisa la mwanzo ziliongozwa na Roho Mtakatifu.

### Umoja

Labda ushahidi muhimu sana unaoweza kukumbukwa wa kazi za Roho Mtakatifu kwa Kanisa la mwanzo ni umoja miongoni mwa waamini wake. Katika maombi yake ya Mchungaji Mkuu pale mlimani, Yesu aliombea umoja wa Kanisa. Aliomba:

> …ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.[385]

Ombi la Yesu lilijibiwa wakati wa Pentekoste. Matendo 2:42 inaonyesha umoja huu katika maisha ya Kanisa: uwajibikaji katika mafundisho ya mitume, ushirika, usherehekeaji wa Chakula cha Meza ya Bwana, na maombi. Ushirika huu ulionekana kwa kanisa kuwajibika kwa mtu na mtu mwingine. Luka alitoa ushahidi kwamba, "Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji;" kwa sababu Wakristo walijali mahitaji ya kila mmoja wao.[386]

---

[381] Matendo ya Mitume 10-11; 15
[382] Matendo ya Mitume 13:2-3
[383] Matendo ya Mitume 16:6-10
[384] Matendo ya Mitume 19:21; 20:22-23
[385] Yohana 17:22-23
[386] Matendo ya Mitume 4:34

Mara sita, Luka anatumia neno "kwa moyo mmoja" kuelezea umoja wa Kanisa. Hii haimaanishi kwamba Wakristo walikubaliana kwa kila jambo. Masuala magumu yalitishia kuligawa Kanisa. Wayahudi na mataifa waliogeukia Ukristo hawakukubaliana kuhusu Sheria za Musa![387] Paulo na Barnaba hawakukubaliana kuhusiana na Yohana Marko.[388] Lakini pamoja na tofauti zao, Kanisa liliunganishwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Jinsi waamini walivyofuata mwongozo wa Roho Mtakatifu, Kanisa lilifungwa pamoja "kwa moyo mmoja."

Kama mimi na wewe tungeweza kuwaona wale mitume siku chache kabla ya Yesu kukamatwa, kamwe tusingeweza kufikiria kama watu hawa wangeweza kuja kuwa na ufanisi mkubwa kiasi hicho katika huduma. Walikuwa na hofu, wivu wa wenyewe kwa wenyewe, na wenye mashaka yaliyopitiliza. Miezi michache baadaye, watu hawa wamebadilika kabisa. Ni nini kilichotokea?

Kabla ya Pentekoste, Mitume walijaribu kuishi maisha yanayomfanania Kristo kwa nguvu zao wenyewe, na mara kwa mara walishindwa. Baada ya Pentekoste, mitume waliishi chini ya uwezo wa Roho Mtakatifu. Hii ndiyo siri ya maisha ya utakatifu na huduma yenye ufanisi.

### Utakatifu leo: Tutakuwa watakatifu tu kama tutajazwa na Roho Mtakatifu

Wakristo wengi wamejaribu kuishi maisha ya utakatifu kupitia nguvu zao wenyewe – na wameshindwa. Kupitia nidhamu ya kibinafsi inawezekana kwa kipindi kifupi tu kudumisha ushindi dhidi ya dhambi za nje. Kwa nguvu zetu wenyewe, inawezekana kuwapenda jirani zetu kwa muda tu. Hata hivyo, kwa muda mfupi tutashindwa pamoja na kutumia nguvu zetu wenyewe.

Ni kwa nini tunapambana? Ni kwa sababu tunajaribu kuishi maisha ya utakatifu kwa nguvu zetu wenyewe. Inachosha sana kujaribu kuishi maisha ya Kikristo kwa nguvu zetu wenyewe. Tunapambana tukiwa na tabia za dhambi; tunapambana tukiwa hatuna upendo mkamilifu; tunapambana tukiwa na moyo uliogawanyika. Kwa ulinganifu, maisha katika Roho ni ushindi tosha kwa Maisha ya ushindi.

Mungu hajatupangia sisi tuishi maisha ya utakatifu kwa nguvu zetu wenyewe. Ametufanya sisi tuishi kwenye uwezo wa Roho Mtakatifu. Katika Kanisa la mwanzo, maisha ya utakatifu yaliwezekana tu kwenye uwepo wa uwezo wa Roho Mtakatifu. Katika Kanisa leo, maisha matakatifu yanawezekana tu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Tabia zile zilizoacha alama kwa kanisa la mwanzo, zitaacha alama pia kwa kanisa la leo kama tutaishi katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu. Kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu, tunaweza kuwa na moyo mtakatifu na mikono mitakatifu.

[387] Matendo ya Mitume 15:1-29
[388] Matendo ya Mitume 15:39-40

Nguvu katika huduma, ujasiri wa kiroho, ushindi dhidi ya dhambi, na umoja miongoni mwa waamini – yote yanatokana na uwepo wa Roho Mtakatifu. Tunapokuwa tumejazwa na Nguvu za Roho Mtakatifu, tunakuwa tumepewa uwezo wa kuishi maisha ya Kikristo ya utoshelevu ambayo Mungu amekusudia kwa watu wake.

Nyaraka za Paulo zinaonyesha kwamba kuwa mtakatifu ni kumfanania Kristo. Kuwa mtakatifu ni kufikiri, kuongea na kufanya kama ambavyo Kristo angefanya. Huu ni mtazamo mzuri, lakini kwa haraka tunakuja kutambua kwamba kwa nguvu zetu wenyewe hatuna uwezo wa kufikiri, kuongea au kufanya kama ambavyo Kristo angefanya.

Baadhi ya Wakristo huvaa nembo ya **YAN** kwenye nguo zao. YAN inasimama badala ya **"Yesu Atafanya Nini?"** Inatukumbusha kwamba tumeitwa tuishi kama Kristo alivyoishi. Hata hivyo, ni rahisi zaidi kuvaa nembo ya YAN kuliko kuishi katika mfano halisi wa Yesu. Mbali na nguvu ya Roho Mtakatifu, hatuna uwezo wowote wa kufanya kwa mfululizo yale ambayo Yesu angeweza kufanya.

**Maombi ya Mkristo Mchanga**

"Roho Mtakatifu, naomba unijaze hadi nifurike. Siwezi nikaubeba ujazo mwingi sana, lakini ninaweza nikajazwa kwa kiwango changu kinachonitosha."
- Imenukuliwa na Dr. David Bubb

Mimi nina urefu wa inchi 6 na uzito wa paundi 200. Mimi siyo mkimbiaji. Jaribu kufikiri umeniambia, "Ili uwe mchezaji mzuri ni lazima ucheze kama Michael Jordan. Kabla ya kutupa mpira wowote, ni lazima ujiulize, 'Michael Jordan atafanya nini?'" Ushauri huu hautanisaidia mimi. Sina uwezo kama alio nao Michael Jordan.

Hata hivyo, jaribu kufikiria kwamba ningepewa vipawa vyote alivyonavyo Michael Jordan. Fikiria kwamba ningeweza - kupitia roho ya Michael Jordan – kufanya kila kitu ambacho Michael Jordan anafanya. Sasa ingewezekana mimi kuiga mambo makubwa ya mcheza kikapu huyu.

YAN (Yesu Atafanya Nini?) haitatosha. Ndani yetu wenyewe, hatuna uwezo wa kumuiga Yesu. Hata hivyo, Roho Mtakatifu aliyeifanikisha huduma ya Yesu anapatikana kwetu leo. Kupitia ujazo wa Roho Mtakatifu, wewe na mimi tunaweza kumfanania Kristo. Huu ni mguso wa Roho Mtakatifu katika maisha ya mwamini.

Roho Mtakatifu alimpa Yesu nguvu kwa ajili ya maisha ya ushindi na huduma yenye matunda; Ujazo wa Roho Mtakatifu ilikuwa siri ya maisha ya ushindi na huduma zenye kuzaa matunda za mitume; ujazo wa Roho Mtakatifu ndiyo siri ya maisha ya ushindi na huduma zenye matunda leo.

Paulo aliandika, "Basi nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. "[389] Kuna chaguzi mbili tu: Kutembea katika Roho au kutimiza tamaa za mwili. *Hatuwezi* kwa nguvu zetu wenyewe kushinda tamaa za mwili. Ndiyo, tunaweza kuwa

[389] Wagalatia 5:16

washindi kwa siku au wiki moja, lakini njia pekee ya kupata ushindi wa muda mrefu juu ya tamaa za mwili ni kujitoa kwa Roho Mtakatifu.

► Soma Warumi 8:1-17.

Katika muhtasari wake mkubwa wa maisha ya kujazwa Roho katika Warumi 8, Paulo alilinganisha njia mbili za kuishi - maisha kwa kufuata mambo ya mwili na maisha yanayoongozwa na Roho wa Mungu.

> Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi. Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.[390]

Katika Warumi 7, Paulo anaonyesha juhudi zake za huko nyuma jinsi alivyokuwa anatekeleza sheria za Mungu kwa juhudi zake mwenyewe. Juhudi hizo zilishindwa. Kwa nini? Kwa sababu "mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi."[391]

Katika Warumi 8, Paulo anafurahia kwamba, "hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Tuko huru na hukumu ya adhabu siyo kwa sababu Mungu ameamua kupuuzia dhambi zetu; bali ni "**Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."** Tuko huru na hukumu ya dhambi kwa sababu sasa tunaishi katika Roho.

Paulo anaonyesha kwamba kuna njia mbili za kuishi. Njia ya kwanza ni kuishi "katika mwili." Hii ni akili ya kimwili tu. Akili ya kimwili ni "adui kwa Mungu." Ni vigumu sana kwa mtu anayeishi katika mwili kumpendeza Mungu. Aina hii ya maisha ya kimwili mwisho wake ni kifo: "Kwa kuwa kuiweka akili kwenye mambo ya mwili ni kifo."

Njia ya pili ya kuishi ni pamoja na akili ambayo "imeshikamanishwa na Roho." Mtu anayeishi kwa misingi ya Roho hufanikisha "mahitaji ya haki yanayotakiwa na sheria" Tuna "maisha" na "amani" kwa sababu "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu."

Katika Warumi 6, Paulo alifundisha kwamba ni lazima tuishi maisha yaliyo juu ya dhambi ya makusudi. "Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?"[392] Kwa nguvu zetu wenyewe, haiwezekani kuishi maisha yaliyo juu ya dhambi ya makusudi. Tumezaliwa tukiwa na hali ya kutamani kufanya dhambi na kuwa mbali na Mungu. Tutawezaje kutimiza matakwa ya Warumi 6? Jibu linapatikana katika Warumi 8. Kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu "tunaweza kuyazika matendo yetu ya mwili." Tunaweza kuishi maisha ya utakatifu kwa sababu Roho wa Mungu anafanya kazi ndani yetu.

---

[390] Warumi 8:13-14
[391] Warumi 7:25
[392] Warumi 6:2

Robert Coleman aliandika:

> Kuishi katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu ni kama upendeleo wa wafuasi wa Kristo leo kama wa wale mitume wa mwanzo ambao walikaa katika chumba cha juu…. Ukweli unaofunika wote, utakatifu wa Roho Mtakatifu aliokuwa nao Kristo ndiyo msingi wa Ukristo wa Agano Jipya.[393]

Nguvu ya Roho Mtakatifu ndani ya mtu aliyeyatoa mapenzi yake yote kwa Mungu inafanya maisha ya utakatifu yawezekane. Pasipo Roho Mtakatifu, kumfafanania Kristo hakutawezekana. Roho Mtakatifu hufanya iwezekane kwa sisi kuishi maisha ya utakatifu.

Nabii Zakaria aliona maono ya kinara cha taa pamoja na miti miwili ya mizeituni. Bakuli lilikuwa la kugawa mafuta bila kikomo kwa ajili ya taa saba. Malaika alifafanua maana ya yale maono. Zerubabeli, mtawala wa Yuda, alikuwa amepewa jukumu la kulijenga upya hekalu. Kazi hii kubwa ilionekana kama ni mlima kwake. Mungu alimwahidi kwamba kazi hii ni lazima itamalizika aliposema, "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu." Kupitia Roho wa Bwana, mlima utageuka kuwa nchi tambarare.[394]

Kwa njia ile ile, Wakristo leo ni lazima wawe na ujazo endelevu wa Roho Mtakatifu. Paulo aliwaagiza Wakristo wa Efeso "wajazwe Roho."[395] Agizo hilo ni la wakati uliopo; hii inatakiwa iwe mfumo wa mara kwa mara wa maisha. Maisha yetu ya kila siku ni lazima yaongozwe na yeye. Tunazoeshwa furaha ya maisha ya utakatifu kwa kadri tunavyoendelea kuishi katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu..

## Uzoefu wa Utakatifu: Sifa za Maisha ya Utakatifu

Fikiria kwamba ulikuwa na uwezo wa kuepuka aina zote za dhambi katika maisha yako. Fikiria kwamba ulikuwa huru na vitendo vyote vya dhambi na tabia zote za dhambi. Hakuna mtu yeyote anayeweza kukunyooshea kidole kwa lolote baya. Je, hii itatimiza kusudi la Mungu la maisha ya utakatifu?

Hapana! Utakatifu ni zaidi ya kuepuka dhambi. Utakatifu ni pamoja na kuzaa matunda. Utakatifu siyo njia mbaya au ya kisheria iliyo kinyume na maisha. Utakatifu ni uhusiano wa furaha na Mungu. Utakatifu unaonekana pale Roho Mtakatifu anapotengeneza matunda yake katika maisha yetu.

### Tunda la Roho

► Soma Wagalatia 5:13-26.

Katika Wagalatia 5, Paulo anatoa ulinganifu wa maisha katika Roho na maisha katika mwili. Hadi kufikia hapa katika Wagalatia, Paulo amekuwa akiwaonya waamini wa Galatia

---

[393] Robert E. Coleman, *The Mind of the Master* (CO: Waterbrook Press, 1977), 35-36
[394] Zakaria 4:6-7
[395] Efeso 5:18

kuhusu hatari iliyopo ya kuachana na uhuru wao katika Ukristo na kurejea kwenye utumwa wa mila na sheria za Kiyahudi. Wamekombolewa kutokana na juhudi zao za kuutafuta wokovu kupitia matendo yao mema, na kwamba hawapaswi kurejea tena kwenye utumwa huo.

Hata hivyo, Paulo anagundua uwepo wa hatari nyingine tena. Wakati mtu anapowekwa huru kutokana na dhambi, anaweza kujaribu kuutumia uhuru mpya uliopatikana ili kujihusisha na tamaa zake mwenyewe. Kwa hiyo Paulo anawaonya waamini wa Galatia, "Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo."

Paulo anafanya ulinganifu wa nia mbili za kuishi. Mfano mmoja wa maisha ni "kutimiza tamaa zote za mwili," na mwingine ni "kutembea katika Roho." Paulo anatoa mifano hii miwili ya ulinganifu kuonyesha "tunda" la kila kipengele katika maisha.

Kwanza, Paulo anaonyesha "kazi za mwili." Haya ni matokeo ya asili ya mwanadamu ambayo hayako chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Kazi za mwili ni pamoja na:

- Dhambi za ngono: uasherati, uchafu, ufisadi.
- Dhambi za kidini: ibada ya sanamu, uchawi.
- Dhambi za kijamii: uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda.
- Dhambi za shahuku: ulevi, ulafi

Anahitimisha kwamba, "Ninawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya hapo mwanzo kwamba, watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu."

Kisha Paulo anaonyesha "tunda la Roho." Hili ni matokeo ya maisha mtu aliyoishi chini ya uongozi na nguvu ya Roho mtakatifu. Hili ni "tunda moja" na siyo mchanganyiko wa "matunda". Katika 1 Wakorintho 12, Paulo anaorodhesha kundi la "karama" na anasema kila Mkristo atapewa kutoka katika karama hizo na "Roho, kama apendavyo yeye mwenyewe." [396] Katika Wagalatia, hata hivyo, kuna tunda moja tu, linalokua kwa asili katika moyo wa kila mtu anayetembea katika Roho.

Tunda la Roho siyo orodha ya sifa tunazoweza kuzitengeneza kwa nguvu zetu wenyewe. Hili ni tunda ambalo kwa asili linakua wakati mtu anapokuwa amejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu. Hivi ndivyo maisha ya utakatifu yanavyoonekana. Ni matokeo ya asili ya moyo mtakatifu.

Paulo aliorodhesha "kazi za mwili" kumi na tano. Anaorodhesha mambo tisa kuhusiana na tunda la Roho:

[396] 1 Wakorintho 12:5-11

- Tunda linalohusiana na Mungu: upendo, furaha, amani
- Tunda linalohusiana na watu: uvumilivu, utu wema, fadhili
- Tunda linalohusiana na tabia ya ndani: Uaminifu, upole, kiasi

Chanzo cha sifa hizi zote ni upendo. Upendo, "ndio kifungo cha ukamilifu."[397] Upendo "hutimiza sheria" na hutoa mwanya wa hili tunda kukua na kustawi.

**Kuenenda kwa Roho**

Tunda la Roho ni ongezeko la asili la maisha tunapokuwa tumejazwa nguvu za Roho. Huu ni msisitizo wa msingi wa Paulo kwa Wagalatia alipokuwa akisema na watu waliojaribu "kukuza" hili tunda kwa nguvu zao za utii kwa sheria. Paulo anawataka waelewe kwamba hawawezi kulipata hili tunda; ni matokeo ya maisha ndani ya Roho.

Ukweli huu kila siku umekuwa wa uwiano kwa Paulo kwa kumbukumbu kwamba Roho Mtakatifu yuko kwa kumaanisha. Utakatifu siyo wa bahati mbaya; ni lazima "tuifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu."[398] Katika Kolosai, inaonekana kwamba waamini wengi walidhania wanaweza kuendelea katika mfumo wao wa maisha ya zamani. Hapo, Paulo anasisitiza juhudi zinazohitajika ili kuweza kuishi maisha ya utakatifu. Kwa Wakolosai, Paulo anaandika kuhusu "kujivika" sifa za maisha matakatifu. Hii inaelekeza nidhamu endelevu inayohitajika kwenye utakatifu:

> Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, **jivikeni** moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote **jivikeni** upendo, ndio kifungo cha ukamilifu.[399]

Kwa jinsi hiyo hiyo, Paulo hataki Wakristo wa Galatia wafikirie tu kirahisi kwamba maisha matakatifu yanaweza kuendelea bila nidhamu binafsi na juhudi. Katika majibu yao kuhusu sheria, hawapaswi kuwa wazembe. Paulo anasema,[400]

- "Enendeni kwa Roho." Kutembea ni kitendo kinachohitaji juhudi.
- "Kuongozwa na Roho." Nikiongozwa, nitafuata. Kitendo kinachohitaji juhudi.
- "Tukiishi kwa Roho." Kuishi ni chaguo na hatua. Kitendo kinachohitaji juhudi.
- "Kutembea hatua kwa hatua na Roho." Hii ndiyo yenye nguvu kuliko vitenzi vinne hapa juu. Ni neno la kijeshi linaloashiria askari akitembea kwenye mstari. "Kutembea kwenye mstari na Roho" kunahitaji juhudi na nidhamu.

---

397 Wakolosa 3:14
398 Wafilipi 3:12
399 Wakolosai 3:12-14
400 Wagalatia 5:16-25

Kama Wakristo tuliojazwa na Roho, kamwe tusifikiri kwamba tumekua sana Kiroho kiasi kwamba hutuwezi kuangukuia kwenye "tamaa za mwili."[401] Hata hivyo, kamwe tusimruhusu Shetani atushawishi kwamba hatuwezi kuwa huru kutokana na kujitawala dhidi ya tamaaza mwili ***kupitia nguvu za Roho Mtakatifu***. Tunavyozidi kupiga "hatua za kutembea na Roho Mtakatifu" tunatengeneza tunda la Roho ndani ya maisha yetu.

► Baada ya kuwa tumejifunza kuhusu nguvu ya mguso wa Pentekoste kwa mitume wa mwanzo na baada ya kupitia kuhusu tunda ka Roho, jadili ni kwa jinsi gani maisha ya kujazwa Roho Mtakatifu yanaweza kuonekana leo. Ni kwa jinsi gani ujazo wa Roho Mtakatifu unagusa mitazamo yetu, kutembea na Kristo kila siku, na juhudi katika huduma?

### Waliipata Siri - Jonathani na Rosalind Goforth

Jonathani na Rosalind Goforth walikuwa wamishenari wa Kanisa la Kipresibiteri la Kanada kwa ajili ya China kuanzia mwaka 1888-1933. Bibi Goforth alijaribu kufuata mfano wa Yesu katika maisha yake, lakini mara kwa mara alishindwa. Baada ya miaka ishirini ya kujitahidi, Rosalind Goforth alijifunza kwamba siri ya ushindi wa maisha ya Ukristo ni Roho Mtakatifu aishiye ndani yetu ambaye anatengeneza tabia ya Yesu katika maisha yetu. Bibi Goforth alitoa ushuhuda kwamba maisha yake baada ya muda huo aliweza kuyaweka katika neno moja, "Mapumziko."

Kwa jinsi walivyoweza kuruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi kupitia wao, hawa akina Goforth walimwona Mungu akitenda kwao miujiza mikuu. Jonathani Goforth alijibidiisha kwa miezi kadhaa kujifunza lugha ya Kichina. Alipojaribu kuhubiri kwa Kichina, wasikilizaji wachache sana waliweza kumwelewa. Siku moja alipokuwa akihubiri, Ghafla alijikuta anaweza kuwasiliana kwa ufasaha, akitumia misamiati ambayo kamwe alikuwa hajawahi kuwa na ujuzi nayo. Baadaye alikuja kutambua kwamba kundi la wanafunzi kutoka Kanada walikuwa wameitumia siku hiyo kwa ajili ya kuiombea huduma yake. Kuanzia siku hiyo, Jonathan Goforth aliweza kuwa na uthibiti kamili wa lugha ya Kichina. Kile ambacho Goforth hakuweza kukifanya, Roho Mtakatifu alikifanya kwa ajili ya mtumishi wake aliyejisalimisha kwake.

Mungu aliwaongoza hawa akina Goforth ndani ya maeneo ya China ambayo kamwe yalikuwa hayajawahi kuguswa kwa Injili. Maelfu waliweza kubadilishwa kupitia huduma hii ya mtu na mkewe Goforth. Ufunguo wa mafanikio yao siyo uwezo wao mkubwa waliokuwa nao; bali ni katika kuishi ndani ya ukamilifu wa Roho Mtakatifu

Kwenye mazishi yake, Mchungaji wa kanisa la Kipresibiteri la Knox alitoa siri ya mafanikio ya Jonathani Goforth. "Alikuwa mtu aliyemuelewa Mungu – aliyejisalimisha kabisa kwake,

[401] Wagalatia 5:17

na aliyejiweka wakfu kwake. Alikuwa amebatizwa kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. Alijazwa Roho Mtakatifu kwa sababu ubinafsi ulishaondolewa katika nafsi yake."[402]

Jonathani na Rosalind Goforth walielewa umuhimu wa kutembea katika Roho siku hadi siku. Walielewa maombi yaliyokuwa katika wimbo aliouandika Edwin Hatch: "Niwekee pumzi, Pumzi ya Mungu, hadi moyo wangu utakasike." Wakati moyo wangu umetakaswa, nitakapokuwa mtu, ninataka kile Mungu anachotaka.

### Niwekee pumzi, Pumzi ya Mungu - Edwin Hatch

Niwekee pumzi, Pumzi ya Mungu,
nijaze maisha mapya,
Ili niweze kupenda kama Mungu anavyopenda,
na niweze kufanya kama Mungu anavyfanya.

Niwekee pumzi, Pumzi ya Mungu,
hadi moyo wangu uwe umetakaswa.
Hadi pamoja nawe, nitakapokuwa mtu,
wa kufanya na kuvumilia.

[402] Ilichukuliwa kutoka Wesley L. Duewel, *Heroes of the Holy Life* (Grand Rapids: Zondervan, 2002), 52-64.

**Tafakuri ya Somo la 9**

(1) Kuwa mtakatifu ni kuishi maisha yenye ukamilifu wa Roho Mtakatifu.

(2) Katika maisha yake duniani, Yesu alihudumu akiwa na Nguvu za Roho Mtakatifu. Yesu aliahidi nguvu hii kwa wafuasi wake. Kwa sababu ya ahadi hiyo, aliwahakikishia mitume wake kwamba, "Mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke."

(3) Wakati mitume walipojazwa na Nguvu za Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste, maisha yao yalibadilishwa. Alama tatu zilidhihirisha utendaji huu mpya wa Roho Mtakatifu:

- Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, inadhihirisha nguvu za ujio wa Roho Mtakatifu
- Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao kuliambatana na Roho Mtakatifu
- Uwezo wa kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka kuliwavika mitume uwezo wa kwenda kushuhudia kwa mataifa yote.

(4) Jinsi kanisa la mwanzo lilivyoishi katika Nguvu za Roho Mtakatifu, walipata uzoefu huu:

- Ongezeko la nguvu kwa ajili ya huduma
- Ujasiri wa kuitangaza Injili
- Ujasiri kwenye nyakati za mateso
- Maisha ya ushindi
- Uongozi kwa ajili ya huduma
- Umoja mongoni mwa waamini

(5) Kama vile mitume walivyokuwa watakatifu tu kupita Roho Mtakatifu, nasi tutakuwa tu watakatifu katika nguvu za Roho Mtakatifu. Pasipokuwa na ujazo wa Nguvu za Roho Mtakatifu, hatutakuwa na uwezo wa kufuata mfano wa Yesu Kristo. Ni katika nguvu za Roho Mtakatifu peke yake tunapoweza kuishi maisha yanayofanana na ya Kristo.

(6) Tutakavyoendela kuishi ndani ya Roho Mtakatifu, maisha yetu yataonesha tunda la Roho kama zao la asili la maisha ya utakatifu.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Andika barua kwa Mkristo mchanga anayekueleza kwamba, "Ninajijua mimi ni Mkristo, lakini ninaendelea kupambana na mitazamo ya kimwili na maeneo mengine ninayojua ni mdhaifu wakati wa kukabiliana na majaribu." Msaidie Mkristo huyu mchanga kuelewa umuhimu wa kuwa mtu aliyejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Wagalatia 5:22-25.

# Somo la 10
# Utakatifu ni Kumfanania Kristo

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kutambua kiini cha utakatifu katika nyaraka za Agano Jipya.

(2) Kufurahia utoaji wa Mungu wa kuwafanya watu wake wamfananie Kristo.

(3) Kutambua uwiano uliopo kati ya kile ambacho Mungu tayari ameshatufanya tuwe watakatifu na kile Mungu anachoendelea kukifanya jinsi tunavyoendelea kukua katika utakatifu.

(4) Kukubaliana na uwezekano wa maisha yenye ushindi endelevu juu ya dhambi ya makusudi.

(5) Kukariri Wafilipi 2:1-5.

## Kuishi na Akili ya Kristo

Ni mapema Jumapili asubuhi karibia miaka thelathini tangu kupaa kwa Yesu mbinguni. Kundi la Wakristo wamekusanyika kwa ajili ya kumwabudu Mungu kwenye nyumba moja ya binafsi katika mji wa Filipi. Wana msisimko kwa sababu wamepata barua kutoka kwa Paulo, Mchungaji wao.

Kiongozi anaanza kuisoma ile barua ya Paulo. Paulo anaandika kutoka katika moyo uliojawa na furaha. Ingawaje yuko kizuizini katika gereza la Rumi, anamfurahia Kristo. Paulo hajui kama ataachiliwa huru au atafungwa, lakini ana Amani. Kwa nini? "Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida."[403]

Akiwa ni baba yao wa kiroho, Paulo anawatia moyo Wakristo wa Filipi waendelee kukua katika imani ya Kikristo. Anataka awaone hawa waamini wakikua kama watu watakatifu ambao Mungu

**Sala kwa ajili ya Utakatifu**

"Siko tena mwenyewe, bali ni wako.
Niweke katika lolote unalotaka,
nipe cheo chochote unachotaka.
Niweke katika kutenda,
Niweke katika mateso.
Naomba niajiriwe na wewe
Au niwekwe akiba kwa ajili yako.
Niinuliwe kwa ajili yako,
Au nishushwe chini nawe.
Nifanye nijae,
Nifanye niwe mtupu.
Nifanye niwe na kila kitu,
Nifanye nisiwe na chochote.
Kwa uhuru na kwa moyo wangu natoa
vitu vyote kwako
Kwa furaha yako na uwazi wako.
Na sasa, Ewe Mungu wa utukufu na
Baraka, Baba, Mwana na Roho
Mtakatifu, wewe ni wangu,
nami ni wako."
- John Wesley

[403] Wafilipi 1:21

amewaita wawe hivyo. Paulo anaandika, "Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo,"[404] Mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili? Hili linawezekanaje?

Jibu la Paulo ni kwamba: "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu." [405] Kama Wakristo wa Filipi wana akili ya Kristo, watakuwa kama Kristo. Siri ya maisha matakatifu ni kuishi na akili ya Kristo. Utakatifu ni kumfanania Kristo.

## Ujumbe wa Nyaraka: Wakristo wawe Watakatifu

### Nyaraka za Agano Jipya zinawaita Wakristo wawe Watakatifu

Kila Mkristo anaitwa awe mtakatifu. Mungu "alituchagua sisi ndani yake [Kristo] kabla ya kuwepo misingi ya dunia ili kwamba tuwe watakatifu na tusiolaumika mbele zake."[406] Kusudi la Mungu la milele katika wokovu ni kutufanya tuwe watu watakatifu.

Hakuna Mkristo wa Kiyahudi wa karne ya kwanza aliyeshangaa kusoma kwamba wanatakiwa wawe watakatifu. Mungu aliamuru utakatifu katika kitabu cha Walawi. Wayahudi Wakristo walitambua kwamba Mungu aliwategemea watu wake wawe watakatifu.

Hata hivyo, Mataifa walizidi kuabudu miungu ya kipagani ambayo haikuwa mitakatifu. Ujumbe wa utakatifu kwa wapagani ulikuwa mgeni kabisa. Petro aliwaandikia Wakristo waliotoka kwenye upagani ambao si muda mrefu umepita tangu "kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu."[407] Watu hawa wamekuwa wapagani bila dhana ya kuwepo kwa haki ya kweli, lakini Petro aliwaita waje kwenye maisha ya utakatifu.

Mitume walifundisha mataifa waliobadilishwa jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu. Walifundisha ujumbe chanya: "Hili ndilo unalopaswa kufanya." Walifundisha ujumbe hasi: "Hili ndilo hupaswi kufanya."

Mara arobaini, Mitume waliwaita waamini "watakatifu." Mtakatifu wa Agano Jipya siyo mtu aliyekufa zamani za kale na anayechukuliwa kama kioo cha rangi cha Hekalu kubwa la Ulaya. Mtakatifu ni mtu yeyote anayeishi kama Mungu alivyowataka watu wake waishi. Kila Mkristo ameitwa kuwa mtakatifu; kila Mkristo anatakiwa awe mtakatifu.

### *Mitume waliwaagiza waamini kufuatilia utakatifu*

Paulo aliwakumbusha waamini wa Korintho kwamba wao ni "hekalu la Mungu aliye hai."[408] Hekalu lilikuwa sehemu takatifu ya kuabudia. Kwa kuwa sisi ni hakalu la Mungu, "na

[404] Wafilipi 1:27
[405] Wafilipi 2:5
[406] Efeso 1:4
[407] 1 Petro 1:18
[408] 2 Wakorintho 6:16

tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu."[409]

Watu wa Mungu mmeitwa "mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu."[410] Paulo aliandika kwamba, Kristo "alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema."[411] Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliwaelekeza wasomaji wake: "Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao."[412] Watu wa Mungu wameitwa wawe watakatifu.

***Mitume waliomba Wakristo, waweze kuwa watakatifu***

Paulo aliomba kwamba watu wa Mungu wafanywe kuwa watakatifu.

► Soma 1 Wathesalonike 1:2-10. Elezea Wakristo wa Thesalonike wakati wa mwanzo wa barua ya Paulo.

Watu waliopokea barua ya Paulo katika kanisa la Thesalonike walikuwa ni Wakristo wa kweli. Walijulikana kwa Imani yao, upendo wao, uthabiti wa matumaini yao. Walikuwa ni "ndugu waliopendwa na Mungu." Injili ilikuja kwao "siyo kwa maneno tu, bali kwa nguvu na kwa Roho Mtakatifu na kwa uhakika kamili." "Walilipokea neno na mateso mengi kwa furaha ya Roho Mtakatifu." "Walikuwa mfano kwa waamini wengine wote katika Makedonia na Akaia." "Wamegeuka kutoka waabudu sanamu hadi kuwa watumishi wa Mungu wa kweli."

Hata hivyo, hawa Wakristo bado walihitaji uzoefu mzito zaidi na Mungu. Walikuwa watakatifu. Walipozaliwa upya, Mungu alianza kuwafanya watakatifu. Hata hivyo, Paulo aliwaombea:

> Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.[413]

Maombi haya yalikuwa ni muhimu sana kwa Paulo. Alikuwa akiomba, "usiku na mchana tunapoomba kwa juhudi tupate kuwaona nyuso zenu, na kuyatengeneza mapungufu ya Imani yenu."[414] Watu hawa walikuwa ni Wakristo wa kweli; lakini Paulo alijua kwamba kuna kitu kimepungua. Hii haimaanishi kwamba walikuwa Wakristo wenye "mabaya," Paulo alikuwa tayari ameshawapongeza kwa uzoefu wao mzuri katika Ukristo wao.

---

[409] 2 Wakorintho 7:1
[410] Efeso 4:22-24
[411] Tito 2:14
[412] Waebrania 12:14
[413] 1 Wathesalonike 5:23
[414] 1 Wathesalonike 3:10

Hakukuwa na "ubaya" wowote kwenye uzoefu wao wa Ukristo, lakini Paulo alijua kwamba wanahitaji kukua zaidi. Walikuwa wametakaswa, lakini Paulo anawaombea Mungu ***"awatakase kabisa."*** Aliomba kwamba Mungu awafanye watakatifu zaidi na zaidi. Aliomba Mungu awasafishe "mwili, nafsi na roho."

**Mitume waliahidi kwamba Wakristo wanaweza kuwa watakatifu**

Wakati alipoomba kwamba Waefeso "wapate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" Paulo alikuwa na uhakika kwamba Mungu atajibu maombi yake kwa sababu alikuwa anaomba kwa Mungu "yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu…."[415] Wito wa Mungu kwa moyo mtakatifu siyo agizo lisilowezekana. Wito wa Mungu ni kwa ajli ya kila mwamini.

Wakati alipoomba kwa kwa Wakristo wa Thesalonike, alikuwa na uhkika kwamba Mungu angejibu maombi yake, Paulo aliifuatilia sala yake, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa" kwa ahadi kwamba, "Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, ***naye atafanya***."[416] Mitume wanaahidi kwamba ***tunaweza kuwa watakatifu***.

## Utakatifu ni Kumfanania Kristo

Kwenye Agano la Kale, Mungu alifunua ujumbe wa moyo mtakatifu na mikono mitakatifu kupitia Sheria na mitume. Katika maisha ya Yesu Kristo, Mungu alitoa mfano wa upendo mkamilifu. Katika kitabu cha Matendo, Wakristo wa mwanzo walionesha kwamba ni jambo linalowezekana kwa mwamini wa kawaida kuishi maisha ya utakatifu kwa uweza wa Nguvu za Roho Mtakatifu. Katika Nyaraka za Agano Jipya, ujumbe wa utakatifu unatumika katika maisha ya kila siku ya mwamini.

**Utakatifu ni Moyo na Akili vinavyomfanania Kristo**

Nyaraka za Agano Jipya zinafundisha kwamba utakatifu ni kumfanania Kristo. Waamini wanapaswa wafanane na Kristo. Kuwa mtakatifu ni zaidi ya tabia ya nje. Utakatifu unaanzia moyoni. Kuwa mtakatifu ni kuwa kama Kristo ndani ya mioyo yetu na akili zetu.

Paulo hasemi kwamba, "*Utaigiza* kama Yesu Kristo." Anasisitiza kwamba, "*Utakuwa* kama Yesu Kristo." Haitoshi kumwigiza Yesu kwa nje; tunatakiwa tufanane na yeye kwa ndani. Mpango wa Mungu ni kuwabadilisha kabisa watu wake wawe katika mfano wa Kristo. "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake.[417] Kusudi la Mungu la milele ni kutufanya sisi tuwe kwenye mfano wa Kristo. Hii ndiyo maana ya kuwa mtakatifu.

Mfano mmoja unaoshangaza sana wa wazo hili unapatikana kwenye barua ya Paulo kwa Wakorintho. Kanisa hili lilikuwa na matatizo mengi sana, lakini bado Paulo aliwataja kama

---

[415] Waefeso 3:20
[416] 1 Wathesalonike 5:24
[417] Warumi 8:29

“watakatifu” na akawataka wageukie maisha matakatifu. Inawezekanaje kundi hili la waamini wachanga, linalopigania kuachana na tabia zao za zamani za kipagani, litegemee kuwa takatifu? Paulo alijibu, “Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.”[418]

Kwa kuwa Kristo alikuja kwa ajili ya dhambi zetu, tunaweza tukawa “wenye haki wa Mungu.” Katika Agano la Kale, dhabibu kwa ajili ya dhambi zilifunika wingi wa dhambi kwa wale waliomwendea Mungu kwa Imani. Hata leo, damu ya Kristo inafunika wingi wa dhambi kwa wale wote wanaomwendea kwa Imani. Lakini Paulo anaahidi jambo lingine lililo zaidi ya kufunika. Siyo kwamba tu “tunafunikwa,” bali tunabadilishwa. “Kwa kuwa tumepatanishwa na Mungu,” tumefanyika “wenye haki wa Mungu.” Paulo anaandika:

> Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo.[419]

Yesu hakufa ili kufunika uovu wetu unaoendelea dhidi ya Mungu. Kupitia Kristo, sisi ni uzao mpya. Sisi siyo waasi tena; ni viumbe vipya ambavyo vimepatanishwa na Mungu mtakatifu.

Hali hii ya kubadilishwa inaenda mbali zaidi kuliko tabia ya nje peke yake. Paulo aliomba kwa ajili ya Wathesalonike:

> Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.[420]

Neno “Kabisa” linabeba wazo la kufanywa mtakatifu katika maeneo yote yanayohusika. Aya hii inaweza kutafsiriwa kama “utakaswe wewe kila eneo.” Paulo aliomba kwamba hawa waamini wabadilishwe kwenye hali zao zote za “nafsi, mwili, na roho.” Aliahidi, “Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.”[421]

Mabadiliko haya huathiri maeneo yote ya maisha. Kwa Wafilipi, Paulo anaandika kuhusu njia mpya yakufikiri. Anaiita “Akili ya Yesu.” Paulo anaelezea juu ya kujitoa kwa Kristo kwa hiari yake mwenyewe na kwa ajili ya mapenzi ya Baba. Yesu “alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.”[422]

Paulo hajasema, “Unyenyekevu wa Kristo ndio njia nzuri ya kuishi, lakini bila shaka haiwezekani kwa wewe na mimi.” Badala yake anasema, “Iweni na nia iyo hiyo ndani

[418] 2 Wakorintho 5:21
[419] 2 Wakorintho 5:17-18
[420] 1 Wathesalonike 5:23
[421] 1 Wathesalonike 5:24
[422] Wafilipi 2:8

yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu."[423] Wazo hili ni lako; unaweza kumfanania Kristo!

Tunaweza kuwa na roho ileile ya kupenda kujitoa kama ilivyomwongoza Yesu kujitoa kwa ajili ya mapenzi ya Baba yake. Tunaweza kuwa na ufahamu wa Kristo. Tunaweza kuyaangalia maisha kupitia macho ya Yesu Kristo. Hii haitokei kupitia maazimio mazuri, bali kupitia mioyo iliyobadilishwa. Tunaitwa tuwe kama Kristo, siyo kwa matendo peke yake bali kutoka ndani ya moyo. Tunaitwa tuwe na akili ya Kristo.

**Utakatifu ni Tabia inayomfanania Kristo**

Watu wengine wanaweza wakanena, "Moyo wangu unamfanania Yesu, lakini matendo yangu sivyo. Kwa ndani, nia zangu ni njema, lakini kwa nje siishi kama Kristo." Mitume hawakuweza kukubaliana kuhusu huu mgawanyiko wa asili yetu ya ndani na ya nje. Asili yetu ya ndani itadhirishwa kwenye matendo yetu ya nje. Kuwa mtakatifu maana yake ni kuwa kama Kristo katika tabia zetu.

Ujumbe huu unaonekana kwenye Nyaraka zote za Agano Jipya. Paulo alizungumzia kwamba Kristo alijitoa mwenyewe kwa ajili ya Kanisa "ili makusudi alitakase." Kristo alijitoa mwenyewe ili amfanye bibi harusi wake mtakatifu. Kristo anamwandaa bibi harusi. Analiandaa Kanisa "apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa."[424]

Je, unaweza kufikiria bibi harusi wa duniani amwambie mume wake, "Sitakuwa mwaminifu kwako kwa mwili wangu, lakini moyo wangu utakuwa safi?" Kwa hakika haiwezekani! Hata Paulo hawezi kufikiria bibi harusi wa Kristo aseme, "Moyo wangu ni msafi, lakini matendo yangu hayatakuwa masafi." Kanisa linaitwa liwe bibi harusi "liwe takatifu lisilo na mawaa."

Paulo aliandikia Wakristo wa Thesalonike. Kanisa hili lilikuwa na mchanganyiko wa waamini waliotokana na Wayahudi na waamini wapya waliobadilishwa kutoka madhehebu ya kipagani ya Wathesalonike. Waamini waliotokana na Wayahudi walizijua amri za Agano la Kale kuhusiana na tabia ya utakatifu, lakini wapagani wamekuwa wakiishi katika mazingira ya uasherati.

Paulo aliwafundisha hawa waamini wapya ni nini maana ya kuishi maisha ya utakatifu. Aliomba Mungu ili, "apate kuifanya imara mioyo yenu iwe bila lawama katika utakatifu mbele za Mungu."[425] Waamini hawa wapya walipaswa wawe watakatifu ndani ya mioyo yao, na walitakiwa wawe watakatifu katika tabia zao. "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu." Utakaso haugusi mioyo yao tu, bali unasababisha watu kuishi katika hali tofauti:

---

[423] Wafilipi 2:5
[424] Waefeso 5:26-27
[425] 1 Wathesalonike 3:13

- “Mwepukane na uasherati”
- “Kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu.
- “Mtu asimpunje ndugu yake wala kumkosa katika jambo hili.”[426]

Kuwa mtakatifu ni kuwa na moyo unaomfanania Kristo na ambao unahamasisha tabia inayomfanania Kristo. Kuwa mtakatifu ni kufanana na Kristo.

**Utakatifu ni Upendo unaomfanania Kristo**

Vitabu vya Injili vinaonyesha kwamba utakatifu ni upendo kwa Mungu na kwa jirani zetu. Paulo anaunganisha tabia inayomfanania Kristo na Upendo unaomfanania Kristo. Anawapa changamoto Wakristo wa Efeso, “mfuateni Mungu, kama watoto wanaopendwa.” Watamfuataje Mungu? Kwa kuishi katika upendo unaomfanania Kristo. “Mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato.”[427]

Wanapokuwa wakitembea kwenye maisha ya upendo wa kujitoa bure, Wakristo wanadhihirisha sura ya Mungu. Kuwa mtakatifu ni kupenda kama Kristo alivyopenda. Katika Warumi 14, Paulo anadhihirisha kwa vitendo upendo huu unaomfanania Kristo. Anawataka waamini kujitoa dhabihu ya uhuru wa dhamira yao kwa ajili ya ndugu aliye mdhaifu. Kwa nini? Kwa sababu, “Ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula, umeacha kwenda katika upendo.”[428] Kama uhuru wangu utasababisha ndugu yangu *(katika Kristo)* kuanguka, nitakuwa sitembei katika upendo. Kristo alisalimisha uhuru wake kwa sababu ya upendo kwa ajili ya wengine; tumeitwa ili kusalimisha haki zetu kwa sababu ya upendo kwa wengine. Huu ndio upendo unaomfanania Kristo.

Ufafanuzi muhimu sana wa Paulo wa nini maana ya kupenda kama Kristo uko katika 1 Wakorintho 13. Kwa kanisa lililokabiliwa na mgawanyiko, tabia za kujiona, wivu, na majivuno, Paulo aliandika:

> Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli.[429]

Katika kitabu cha 1 Yohana, mtume anasisitiza mambo ya vitendo kuhusu upendo unaomfanania Kristo. 1 Yohana inaonesha upendo unaomfanania Kristo ukoje.

- Upendo huhitaji utiifu. Kama tunampenda Mungu, **tutamtii yeye**.[430] Hatuwezi kutenganisha upendo na utii.

---

[426] 1 Wathesalonike 4:3-6
[427] Waefeso 5:1-2
[428] Warumi 14:15
[429] 1 Wakorintho 13:4-6

- Upendo unahitaji nia moja. Kama tunampenda Mungu, **hatutaupenda ulimwengu**. "Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." [431] Hatuwezi kwa wakati mmoja kumpenda Mungu na huku tunataka kuupenda ulimwengu ambao unapingana na Mungu. Mtu mtakatifu anampenda Mungu kwa moyo usiogawanyika.
- Upendo unahitaji mahusiano. Kama tunampenda Mungu, **tutawapenda na Wakristo wengine.** "Yeyote anayempenda Mungu anapaswa pia kumpenda na ndugu yake." Hakika, "Mtu akisema, 'Nampenda Mungu,' naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo…."[432] Yohana anafundisha kwamba haiwezekani mtu ampende Mungu wakati akiwa anamchukia ndugu yake wa Kikristo.

Ni nini matokeo ya huu upendo wa kumfanania Kristo? Ni kuwa na Imani na Mungu. "Tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu."[433] Upendo huu mkamilifu unatupa "tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu," na "huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu."[434]

Tutauishije huu upendo mkamilifu? "Kwa kuwa tunajua kwamba maisha yetu katika dunia hii, ni maisha yake tunayoyaishi ndani yetu."[435] Tunaweza peke yake kuwa mfano wa upendo unaomfanania Kristo kwa kupitia Kristo aishiye ndani yetu.

## Maisha ya Utakatifu: Wewe ni mtakatifu; fuata utakatifu

Tommy alikuwa na hamu ya kuwa mtu mtakatifu. Kwa bahati mbaya, uelelewa wa Tommy kuhusu utakatifu ulikuwa zaidi kwenye msingi wa mihemuko na hisia kuliko Maandiko. Kwa sababu ya hilo, Tommy alivuka kiwango cha fundisho moja hadi lingine.

Kwa muda, Tommy alifunga mara kadhaa, aliomba kwa masaa, na alijaribu kujiweka katika nidhamu ya utakatifu yeye mwenyewe. Alikuwa na uhakika kwamba tunakuwa watakatifu kwa kupitia nidhamu yetu wenyewe.

Tommy baadaye alivunjika moyo na akaachana na juhudi hizo. Akaanza kuukulia uzembe katika nidhamu ya utakatifu na kurudia kwenye dhambi. Nipomwuliza kuhusu eneo la dhambi linalomsumbua, Tommy alisema, "Ninaishi kwa neema na sihitaji kuwa na nidhamu. Mungu atanifanya niwe mtakatifu atakapokuwa tayari."

Kwa wakati mwingine, Tommy akaomba sana kwa ajili ya kipawa cha kiroho cha ajabu. Aliamua kwamba utakatifu ni juu ya vipawa vya kiroho na nguvu za nje.

---

[430] 1 Yohana 2:5; 5:3
[431] 1 Yohana 2:15
[432] 1 Yohana 4:20-21
[433] 1 Yohana 4:12
[434] 1 Yohana 4:17-18
[435] 1 Yohana 4:17, *New Life Version*

Utafiti wa Tommy kuhusu utakatifu uliwekwa kwenye msingi wa mhemuko kuliko usomaji kwa makini wa Maandiko. Hakusoma Biblia ili aweze kuelewa jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu kila siku.

Nyaraka za Agano Jipya zinafundisha mambo ya ukweli na muhimu yanayohusiana na maisha ya utakatifu. Kama tutazisahau kanuni hizi, tutakuwa hatuna msimamo katika uelewa wetu kuhusu utakatifu. Mitume waliandika kutuonyesha jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu kila siku ambayo Mungu ametuitia.

**Ulifanywa kuwa mtakatifu; Unafanywa kuwa mtakatifu**

Wakati Paulo alipowaandikia "watakatifu," alikuwa anasema, "wewe ni mtakatifu." Mtakatifu ni mtu ambaye tayari ni mtakatifu, lakini Paulo aliwaandikia hawa watakatifu akiwaambia, "Ni lazima muwe watakatifu." Ninyi ni watakatifu, mnapaswa muendelee kuukulia utakatifu.

Uwiano huu unaonekana ukijirudia-rudia katika hizi Nyaraka. Kama Waamini, tayari sisi ni watakatifu, lakini tuendelee kukua katika utakatifu na kutembea na utii kwa Mungu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaonyesha kwamba tulifanywa watakatifu kwa kifo cha Yesu. "Hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu."[436] Tumetakaswa kupitia kifo cha Yesu.

Mwandishi anaendelea, "Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa."[437] Aya hii inahusisha maneno mawili yaliyofanana kwa ajili ya mandhari ya utakatifu, Kupitia kifo chake, Kristo "amewakamilisha" *(teios)* wale wote ambao "wametakaswa" *(hagiazo).* Aya hii inatuambia kwamba:

***Tulifanywa kuwa Watakatifu; "Alitufanyia ukamilifu kwa nyakati zote..."***

Kristo alikufa ili tuweze kuwekwa huru kutokana na nguvu ya dhambi. "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango."[438] Kusudi la Mungu kuwafanya watu wake wawe watakatifu lilitimilika kupitia kifo cha Yesu. Tumefanywa kuwa wakamilifu.

***Tumefanywa kuwa Watakatifu: "Wale Ambao Wanatakaswa"***

Kifo cha Yesu kimekamilisha kusudi la Mungu la utakaso kwa nyakati zote, lakini ukuaji wetu katika utakatifu unaendlea katika maisha yetu yote. Ni ukuaji ulio endelevu. Kupitia kifo cha Yesu, sisi ni watakatifu; kupitia kifo cha Yesu, sisi tunafanywa kuwa watakatifu.

Ushuhuda binafsi wa Paulo unaelezea kanuni hii. Katika Wafilipi 3, Paulo anaandika kwamba yeye bado hajawa ***mkamilifu***, lakini katika aya nyingine baadaye anasema, anajirejea mwenyewe kama ambaye ***amekamilika*** ("wale wote miongoni mwetu ambao

[436] Waebrania 10:10
[437] Waebrania 10:14
[438] Waebrania 13:12

wamekua”). Maneno yaliyokuzwa kwa weusi katika dondoo ifuatayo, kwa pamoja yanatokana na *teleios.* Maneno yote mawili yanaweza kitafsiriwa kama “mkamilifu.”

> Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa **mkamilifu** *(teleios)*; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu… Basi sisi tulio **wakamilifu** *(teleios)* na tuwaze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lo lote, Mungu atawafunulia hilo nalo.[439]

Paulo anasema, “Mimi bado siyo mkamilifu.” Kisha anaendelea, “Wale miongoni mwetu walio wakamilifu.” Paulo bado hajafikia kwenye malengo yake; anakua katika utakatifu wake. Kwa hali hiyo, bado hajawa mkamilifu. Lakini, Paulo anajaribu kukaza kila msuli ili aweze kulifikia lengo. Amejipanga kumaliza mbio. Kwa ufahamu huu tayari Paulo ni mkamilifu. Paulo anaweza kusema “Bado mimi siyo mkamilifu” na “Mimi ni mkamilifu” katika ibara hiyo moja.

Kuwa mkamilifu haina maana kwamba tumepanda ngazi ya kazi inayotufanya sisi tuwe wakamilifu. Badala yake, ina maana kwamba tumejisalimisha kwa neema ya Mungu katika maisha yetu. Ni kwa wakati huo huo kwamba kuna wakati ambao Mungu anaelekeza mioyo yetu kuelekea upande wake. Ni mchakato kwamba nyendo zetu kumwendea yeye zitaendelea katika maisha yetu yote.[440]

Mfikirie mchezaji wa golfu anayepiga mpira kuelekea kwenye shimo; ni shuti kamili. Shuti haliwi kamili tu mpira unapotua kwenye shimo. Unapokuwa angani ukienda, shuti hilo tayari ni kamilifu; ukiwa kwenye mkondo wa kuelekea shimoni. Shuti hilo liko kamilifu tangu wakati mchezaji alipoupiga mpira.[441]

Kwa njia hiyo hiyo, Paulo alikuwa anaelekea kwenye lengo la mwisho. Alishaanda mwelekeo wake na alikuwa akisonga mbele kukaribia lengo lake kwa moyo usiogawanyika. Alikuwa bado hajawa mkamilifu, lakini alikuwa kwenye njia ya kufikia kwenye lengo lake. Hakuwa bado amekamilika, lakini tayari alikuwa mkamilifu.

Kama waamini, ni watakatifu “watakatifu” ambao wamekubalika na Mungu kupitia kwa Kristo, lakini tumeitwa tujitoe wenyewe kama “dhabihu iliyo hai” inayoendelea kukua kila siku katika utii na kujisalimisha. [442] Tayari tumeshafanyika watakatifu; tunaendelea kufanywa watakatifu.

**Ninyi ni Watakatifu; Lazima muishi kama Watakatifu**

Paulo aliandika kwa “watakatifu” walioshi Korintho. 1 Wakorintho imeelekezwa kwa watu watakatifu, “waliotakaswa katika Kristo.”[443] 2 Wakorintho imeelekezwa kwa “Kanisa la

[439] Wafilipi 3:12-15
[440] Timothy C. Tennent. *The Call to Holiness* (Franklin: Seedbed Publishing), 2014), 54-55
[441] Maelezo yanatoka katika: T.A. Noble, *Holy Trinity: Holy People* (Eugene: Cascade Books, 2013), 23.
[442] Warumi 12:1
[443] 1 Wakorintho 1:2

Mungu lililoko Korintho, likiwa na watakatifu wote wa eneo lote la Akaya."[444] Walikuwa watakatifu – lakini walikuwa na mengi ya kujifunza jinsi ya kuishi kama watakatifu.

Kuna njia mbili ambazo Wakristo wanashindwa kuelewa ukweli. Kwanza, baadhi ya Wakristo husema, "Ninaitwa mtakatifu kwa sababu Mungu anaona haki ya Kristo ndani yangu kuliko anavyoiona dhambi yangu. Utakatifu wangu ni 'uongo wa kisheria.' Kamwe siwezi kuwa mtakatifu katika dunia hii, lakini hata hivyo, Mungu ananiita niwe mtakatifu." Kitabu cha Warumi 6 kinaweka wazi kwamba hili jibu haliwezi kabisa kukubaliwa na Paulo. Watu watakatifu ni lazima wayaishi maisha matakatifu.

Pili, Wakristo wengine husema, "Mimi ni mtakatifu. Kamwe sishuki kwenye viwango vya chini vya Mungu alivyoweka kwa ajili ya kuwa mkamilifu. Kamwe situbu kwa sababu mimi sina makosa. Mimi ni mtakatifu!" Paulo anakataa msimamo huu wa pili kama pia alivyokataa msimamo wa kwanza. Paulo aliandika kuwafundisha "watakatifu" wa Korintho kuishi maisha matakatifu. Wanachokosa ni ufahamu na ukuaji wa kiroho, kwa hiyo Paulo anawafundisha hawa watakatifu jinsi ya kuishi kama watakatifu. Watu watakatifu ni lazima wayaishi maisha matakatifu.

Jiji la Korintho lilijulikana sana kwa tabia chafu zisizo za kimungu kwa wakazi wake. Paulo anawataka waamini waishio katika jiji hili la maovu wawe na tabia ya utakatifu. Wajiepushe na tabia ya uasherati kwa sababu "miili yao ni viungo vya Kristo."[445] Paulo anaorodhesha tabia chafu ambazo hazitakiwi kabisa kwenye ufalme wa Mungu:

> Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.[446]

Baada ya orodha hii ya dhambi, Paulo anahoji, "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii." Paulo anawaandikia watu wake ambao wameshiriki sana kwenye haya matendo ya dhambi. Kama waamini, Paulo anawategemea waachane na mfumo wa maisha ya zamani! Inapokumbukwa hali yao ya dhambi ya zamani, je, watu hawa wanawezaje kuishi maisha masafi? Paulo anatoa jibu:

> Lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.[447]

Dhambi za 1 Wakorintho 6:9-10 zimefutwa kwa mabadiliko ya 1 Wakorintho 6:11. Mabadiliko haya siyo ya utaratibu wa kisheria; hakuna mahali popote Paulo anapendekeza kwamba, "Mtaendelea kutenda dhambi hizi, lakini Mungu ataendelea kuwahesabia haki hata pamoja na madhaifu yenu ya tabia." Hapana! Anasema, "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa." Wakristo wa Korintho kamwe hawatarejea kwenye

---

[444] 2 Wakorintho 1:1
[445] 1 Wakorintho 6:15
[446] 1 Wakorintho 6:9-10
[447] 1 Wakorintho 6:11

dhambi zao za zamani. Paulo anasema, "Ninyi ni watakatifu. Fanyeni kama utakatifu unavyowataka mfanye!" Walikuwa wameoshwa; walikuwa wametakaswa; walikuwa wamefanywa watakatifu. Ni watakaifu; ni lazima waishi kama watakatifu.

Wakati kijana anavyojiunga na jeshi, anapewa sare ya jeshi inayomtambulisha kwamba yeye ni mwanajeshi. Wakati huo huo, anapewa mwongozo ambao unaelezea Msimbo wa Maadili ya Jeshi. Sare peke yake haitoshi; ni lazima aweze kuishi kulingana na msimbo wa maadili.

Inachukua muda mrefu zaidi kujifunza msimbo/kanuni za maadili kuliko kuvaa sare. Mwanajeshi mpya ni lazima ajifunze kuishi katika mazingira yanayoendana na ile sare ya jeshi aliyovaa. Ni lazima aweze kukomaa kama mwanajeshi. Mara nyingi, huyu mwanajeshi mpya inabidi akumbushwe kuhusu sheria za kijeshi. Je, utendaji wake ni mkamilifu? Hapana. Lakini, dhamira yake ya kuwa mwanajeshi iko kamilifu? Ndiyo. Kwenye siku ya kwanza jeshini, yeye ni mwanajeshi; lakini atachukua siku nyingi akijifunza jinsi ya kuishi kama mwanajeshi.

Jaribu kumfikiria kijana anayesema, "Nataka niitwe mwanajeshi, lakini sitataka nifuate Msimbo wa Maadili." Ananunua sare ya kijeshi, lakini haishi kwa mujibu wa Msimbo wa Maadili. Je, huyu ni mwanajeshi wa kweli? Hapana. Anajifanya tu kuwa mwanajeshi lakini sivyo.

Nyaraka za Agano Jipya zimendikwa kwa waamini ambao "wamemvaa Kristo." Sasa wanajifunza jinsi ya kuishi maisha matakatifu. Katika Waefeso 4-6 tunajifunza maisha ya utakatifu yakoje kwenye mahusiano ya kifamilia, mahusiano na kanisa, na katika maadili ya biashara. Katika Wagalatia 5, tunajifunza tunda la maisha yaliyofuatana na hatua za Roho Mtakatifu. Katika 1 Petro, tunajifunza jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu wakati wa kukabiliana uso kwa uso na mateso. Tunaposoma kitabu cha Yakobo, tunajifunza jinsi mtu mtakatifu anavyopaswa kuutawala ulimi wake.

Paulo aliandika kwa waamini wa Kolosai, "Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Waamini hawa walikuwa wamekufa katika dhambi; wako hai katika Kristo; siyo watumwa wa dhambi tena; ni watakatifu. Lakini Paulo anaendelea, "Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi."[448] Mmekufa katika dhambi; achilieni dhambi zife. Mmekuwa watakatifu; lazima muishi kama watakatifu.

> "Paulo alisema, 'Nimesulubiwa pamoja na Kristo....' Hajasema, 'Nimefanya maamuzi ya kumuigiza Yesu Kristo,' au, 'Kwa hakika nitafanya juhudi za kumfuata Yeye' — lakini 'Nimekubaliwa na yeye katika mauti yake.'"
> \- Oswald Chambers

Kanuni imeelezwa mwanzoni mwa ibara.

[448] Wakolosai 3:3, 5

> Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.[449]

Paulo anasema, "Siku hadi siku, endelea kutafuta vitu vya mbinguni. Siku hadi siku, endelea kuweka akili yako kwenye mambo ya Mungu." Msingi wa maisha ya utakatifu ni kuweka akili yako kwenye mambo ya Mungu. Umefanywa kuwa mtakatifu ("umeinuliwa na Kristo"), kwa hiyo kuwa mtakatifu, ("weka akili yako kwenye mambo yaliyo juu").

Ni nini matokeo ya haya maisha matakatifu? "Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu."[450] Maisha ya utakatifu yanakuandaa wewe ukaishi milele na Mungu aliye mtakatifu. "Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa."[451] Kutembea kwa utakatifu katika dunia hii kulimwandaa Henoko kwa ajili ya maisha ya umilele na Mungu. Kutembea na Mungu kwenye utakatifu katika ulimwengu huu kunatuandaa sisi "kuonekana na Kristo katika utukufu."

Nyaraka katika Agano Jipya zimeandikwa kwa ajili ya watakatifu. Tumefanywa watakatifu kupitia damu ya Yesu Kristo. Tumemvua mtu wa kale na kumvaa mtu mpya. Sasa tunajifunza siku hadi siku ni nini maana ya kuwa mtakatifu. Tunabadilishwa siku hadi siku kuwa katika sura ya Mungu. Je, utendaji wetu ni mkamilifu? Hapana. Je, ahadi yetu ya kuwa watakatifu iko kamili? Ndiyo. Sisi ni watakatifu. Tunajifunza kuishi kama watakatifu.

### Mungu anakufanya uwe Mtakatifu; Lazima ufuate Utakatifu

Katika kitabu cha Walawi, Mungu anasema, "Jitakaseni basi, iweni watakatifu." Hili ni agizo ambalo kila mtu alipaswa kulifuata. Katika aya inayofuata, Mungu anaahidi, "Mimi ndimi Bwana niwatakasaye ninyi."[452] Hii ilikuwa ni ahadi ya Mungu ya kile ambacho angefanya. Kuuelewa utakatifu, ni lazima tuweke kwenye uwiano kweli mbili zifuatazo:

1. Utakatifu ni zawadi kutoka kwa Mungu. Mungu huwafanya watu wake wawe watakatifu.
2. Utakatifu ni agizo la Mungu; Mungu anawaagiza watu wake "wafuate utakatifu."

Mafarisayo walikumbuka tu, "Ni lazima kufuata utakatifu." Waliamini kwamba wanaweza kuwa watakatifu kwa nguvu zao wenyewe. Majibu ya Nyaraka za Agano Jipya, "Mungu anawafanya kuwa watakatifu."

Baadhi ya Wakristo katika Kanisa la mwanzo walikwenda kinyume tena mbali zaidi. Waliamini, "Kama Mungu anataka kutufanya sisi tuwe watakatifu, atafanya. Sisi hatuna la kufanya." Majibu ya Nyaraka za Agano Jipya, "Lazima kufuata utakatifu."

---

[449] Wakolosai 3:1-2
[450] Wakolosai 3:4
[451] Mwanzo 5:24
[452] Walawi 20:7-8

Kujisalimisha na kufuata yote kwa pamoja ni muhimu katika utakaso. Mungu anatufanya tuwe watakatifu; lazima kufuata utakatifu. Tunajisalimisha kwa Mungu na kumruhusu atubadilishe, lakini tunakaza mwendo, tuifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu kwetu.[453] Paulo alielewa kwamba kuziamini ahadi za Mungu haina maana kwamba hatupo tena katika kukaza mwendo ili tuifikie ile mede ya thawabu. Tumepewa nguvu za kufuata utakatifu kwa sababu Mungu anatufanya tuwe watakatifu.

Wakati watoto wangu walipokuwa wadogo, walikuwa wanaweza kusoma Andiko kwa sauti kwenye kipindi chetu cha maombi ya familia. Siku moja, msichana wetu akautana na andiko la Wafilipi 2:12. Kwa hamasa kubwa, Stacey (binti yetu) akapaaza sauti, "Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka!" Alikuwa amevutiwa sana na agizo hili la "utimizeni wokovu wenu wenyewe." Lakini Paulo anaendelea, "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu." **Kazi yetu imekamilika** kwa sababu ya **kazi ya Mungu.**

Kinyume na Imani ya Wakristo wengi, Kazi ya Mungu inakamilishwa wakati "tunapoufanyia kazi wokovu wetu." Ina maana kwamba tunapata utakatifu kutokana na kazi zetu? Hapana kabisa! Paulo anaendelea, "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."[454] Ni Mungu atoae hamu ya (kutaka kutenda); ni Mungu anayeiwezesha kazi. Bila Mungu afanyaye kazi ndani yako, kazi zetu ni bure. Hatuwezi kujifanya wenyewe watakatifu, lakini Mungu hatatufanya tuwe watakatifu mbali na ufuatiliaji wetu wenyewe wa utakatifu.

Paulo aliwakumbusha Wakorintho juu ya ahadi za ajabu za Mungu. "Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike."[455] Kisha akawaagiza kuishi maisha ya utakatifu. "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu."[456] Kwa sababu ya ahadi za Mungu "tunajitakasa nafsi zetu na uchafu wote." Ahadi za Mungu za kutufanya tuwe watakatifu zinatupa uhakika wa kufuata utakatifu.

Akiwaandikia Wakristo wa Thesalonike, Paulo aliomba kwamba Mungu "aifanye mioyo yenu isiwe ya lawama ndani ya utakatifu."[457] Hii ni kazi ya Mungu. Kisha, Paulo akaanza kufundisha, "Jinsi gani utembee na kumpendeza Mungu." Kwanini? "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu."[458] Mungu alikuwa anawafanya Wakristo wa Thesalonike kuwa watakatifu, kwahiyo ni lazima wafuatilie maisha matakatifu.

---

[453] Wafilipi 3:13
[454] Wafilipi 2:13
[455] 2 Wakorintho 6:18
[456] 2 Wakorintho 7:1
[457] 1 Wathesalonike 3:13
[458] 1 Wathesalonike 4:1, 3

Kitabu cha Wagalatia kimeandikwa kwa waamini waliokuwa wanajaribu kurejea kwenye wokovu kwa matendo ya sheria. Paulo aliwakumbusha kwamba "mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa Imani ya Kristo Yesu; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki."[459] Kama kuhesabiwa haki kwa Imani ndiyo mwisho wa injili, huu ungekuwa waraka sahihi kwa Paulo kwa kusema, "Mmethibitishwa kwa imani. Kwahiyo sasa mnaweza kuishi kama mpendavyo na mtaingia mbinguni. Sehemu yako mbinguni ni ya uhakika." Lakini Paulo hasemi hivyo, badala yake anasema:

> Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.[460]

Kuweka hatua, maana yake ni "kutembea bega kwa bega na kiongozi." Inaelekeza nidhamu na kujitawala binafsi. Inaelekeza kuishi kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu na siyo kwa matamanio yetu. Mungu aliwafanya Wagalatia wawe watakatifu, lakini ni lazima waendelee kufuata utakatifu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliandika kwamba Mungu "huturudi kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake." Huu ni ukweli wa kushangaza! Mtu aliyeanguka anaweza kushiriki kwenye utakatifu wa Mungu. Huu siyo aina ya muungano wa siri kama ilivyo kwa ibada za kipagani. Haya ni mafundisho kamili ya kimatendo kuhusiana na nidhamu ya kiroho. Anaandika kuhusu "tunda la haki," kuhusu amani, na kuhusu dhambi kama vile uchungu na uasherati.[461] Haya siyo mafundisho ya kumfikia Mungu kwa mafumbo, bali ndiyo Ukristo wa kawaida. Mungu anawaita watoto wake wawe watakatifu; anawategemea watoto wake washiriki katika utakatifu wake.

Tunawezaje kushiriki katika utakatifu wa Mungu? Tunashiki utakatifu wa Mungu pale tunapokuwa "washirika wa tabia ya asili ya Uungu."[462] Petro anaonyesha kwa pamoja nguvu za Mungu za kutufanya tufanane naye na juhudi zetu za kukulia katika sura ya Mungu.

Kwanza, Petro anaahidi kwamba tunaweza kuwa washirika wa tabia ya Uungu:

> Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya asili ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.[463]

---

[459] Wagalatia 2:16
[460] Wagalatia 5:24-25
[461] Waebrania 12:10-16
[462] Maelezo haya yametoka kwa Dr. A. Philip Brown, "Divine Holiness and Sanctifying God: A Proposal," unpublished paper.
[463] 2 Petro 1:3-4

Mungu anatufanya tuwe watakatifu. "Uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote" vipasavyo kwa ajili ya "maisha na utauwa." Utauwa siyo ndoto isiyowezekana; Mungu "alishatupa ahadi zake za thamani na kubwa mno." Moja ya ahadi hizi ni kwamba "tutakuwa washirika wa tabia ya asili ya Uungu." Ahadi kwamba tunaweza kufanana na baba yetu wa mbinguni kwa ajili ya kila mtoto wa Mungu. Jambo hili halitimizwi kupitia juhudi zetu wenyewe; utauwa ni zawadi inayotokana na neema ya Mungu. Kupitia uwezo wa Mungu, tunaweza kuishi kwa upatanifu na tabia ya Mungu. Mungu anatufanya watakatifu.

Kisha, Petro anaendelea:

> Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika Imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.[464]

Kwa kuwa nguvu ya Uungu ya Mungu imetufanya sisi tuwe washirika wa tabia ya asili ya Uungu, inatupasa "tufanye kila jitihada" kukua katika wema, maarifa, kiasi, utauwa, upendano wa ndugu, na upendo. Kwa sababu ya yale ambayo Mungu ametenda, tunapaswa kufuata utakatifu.

Petro hajajaribu kutushauri kwamba tujifanye wenyewe watakatifu kwa "kufanya kila jitihada." Hapa hafundishi ushikiliaji mno wa sheria. Hatupati upendeleo wa Mungu kupitia nguvu zetu wenyewe. Hata hivyo, Petro anatutaka sisi tuelewe kwamba hatuwezi kuyaishi maisha ya utakatifu pasipo nidhamu binafsi.

Tunafuata utakatifu kwa sababu ya neema ya Mungu. Neema yake inatuwezesha katika kufuata maisha ya utakatifu. Kwa sababu ya Uweza wake wa Uungu (2 Petro 1:3-4), "tunafanya kila jitihada" kukua (2 Petro 1:5-8). Kufuata kwetu utakatifu siyo takwa la kisheria; ni hamu ya asili ya moyo uliobadilishwa. Kama sisi kwa ukweli ni watoto wa Mungu tutapenda tukulie ndani ya utakatifu. Kama kweli sisi ni watoto wa Mungu, tutapenda kuona kusudi la Mungu likitimia katika maisha yetu.

### Nitayaishije Maisha ya Utakatifu? "Siyo Mimi, Bali Kristo"

Akiwaandikia Wakristo wa Filipi, Paulo anamlenga Yesu kama mfano wa tabia wanayopaswa kuionyesha. "Kristo akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."[465] Paulo alitaka hawa waamini waelewe kwamba njia ya watoto wa Mungu ni njia ya unyenyekevu, na siyo njia ya kujikweza. Tunapaswa kuwa na "akili ya Kristo."

[464] 2 Petro 1:5-8
[465] Wafilipi 2:8

Inawezekana tukashawishika kusema, "Ni kweli, Yesu aliishi maisha ya utakatifu. Alikuwa ni Mwana wa Mungu. Hiyo hainisaidii mimi. Mimi siyo Yesu!" Lakini tunawezaje kufuata mfano wa Yesu? Paulo alifundisha kwamba Roho wa Kristo huishi ndani ya mwamini.

Paulo aliandika kwa Wakristo wachanga, "Ninyi hamuufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."[466] Tunaishi maisha matakatifu siyo kwa nguvu zetu bali kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Ushuhuda wa Paulo mwenyewe unaonyesha ushuhuda wa mabadiliko yake. Paulo anayaona maisha yake yaliyopita kama ya Mfarisayo anayejaribu kutimiza maagizo ya sheria kwa nguvu zake mwenyewe. Anakumbuka wakati ambao alikuwa na nia ya kufanya yaliyo mema, lakini hakuwa na uwezo wa kutenda mema. Anasema, "Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu."[467] Jitihada za Paulo za kuwa mwenye haki kwa nguvu zake mwenyewe ziliongozwa na kushindwa.

Baada ya kukutana na Kristo, ushuhuda wa Paulo ulibadilika kutoka "siyo mimi, bali dhambi" hadi kwenye "siyo mimi, bali Kristo."[468] Paulo ataweza kuishi maisha ya Kikristo ya ushindi kwa sababu sasa Kristo anaishi ndani yake.

Paulo aliwatia moyo Wakorintho, "Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu?"[469] Tunaweza kumfanania Kristo kwa sababu anaishi ndani yetu. Mtheolojia wa Kilutheri aitwaye Dietrich Bonhoeffer aliliweka hivi: Kuwa Mkristo inamaanisha kwamba "nafasi ambayo wakati mmoja ilikuwa imekaliwa na mzee, sasa imekaliwa na Yesu Kristo."[470]

Kristo anaishi ndani yetu, au kuelezea kanuni hii kwa njia nyingine inayofanana na hiyo, "Tunaishi ndani ya Kristo." Mojawapo ya maneno ambayo Paulo amekuwa akitumia sana katika huduma yake ni "ndani ya Kristo." Paulo anatumia fasiri nyingine ya "ndani ya Kristo," "ndani yake," "ambaye" na "ndani ya mwana" zaidi ya mara 150 katika nyaraka zake. Paulo akirudia mara kwa mara huelekeza kuhusu sehemu yetu ndani ya Kristo kama siri kwa maisha ya Mkristo. Ushindi wa kila siku unakuja kwa sababu tuko ndani ya Kristo.

Maisha yetu ya zamani yalikuwa "ndani ya Adamu" kwenye anguko la nafsi yetu ya dhambi. Maisha yetu mapya yako "ndani ya Kristo," katika nguvu ya Bwana aliyefufuka ambaye anatupa ushindi wa kila siku dhidi ya dhambi.

- Ndani ya Adamu, tulitembea katika giza; ndani ya Kristo tunatembea katika nuru.
- Ndani ya Adamu, tulikuwa watumwa wa dhambi; katika Kristo sisi ni watumwa wa uadilifu na haki.

[466] Warumi 8:9
[467] Warumi 7:17
[468] Wagalatia 2:20
[469] 2 Wakorintho 13:5
[470] Dietrich Bonhoeffer, *Ethics* (New York: Macmillan, 1965), 41

- Ndani ya Adamu, tulifurahi katika dhambi za mwili; ndani ya Kristo tulivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba."[471]

Uelewa huu ni muhimu sana kwa ajili ya maisha ya ushindi. Tunapojiona tuko ndani ya Adamu ("watenda dhambi waliosamehewa" wanaoishi kwenye kifungo cha dhambi), tutaendelea kuangukia kwenye majaribu. Tunapojiona wenyewe ndani ya Kristo ("Watakatifu waliobadilishwa" ambao wana nguvu kupitia Kristo), tutaishi kwa ushindi dhidi ya dhambi. Paulo aliwaambia Wakristo wa Kolosai siri iliyoko ya maisha ya utakatifu: "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye."[472] Jinsi tunavyotembea na Kristo, tunafanywa kuwa watakatifu.

Watu wengine wanadhani kwamba utakaso ni kama dozi ya mafua anayokupa daktari ili kuzuia ugonjwa. Wanafikiri kwamba, tunapomwomba Mungu atufanye watakatifu, anatupa "dozi takatifu" ya kutuzuia tusiwe watenda dhambi. Wanaamini kwamba baada ya Mungu kuwa ametutakasa, tunaishi maisha ya utakatifu kwa nguvu zetu wenyewe.

Hakuna mahali popote Biblia inapotoa picha kama hii. Badala yake, tunaishi "ndani ya Kristo." Sisi ni watakatifu "ndani ya Kristo." "Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."[473] Sisi ni wale "waliotakaswa katika Kristo Yesu."[474] Hatufanywi watakatifu kupitia majaribio yetu ya kukata tamaa ya kumuigiza Yesu kwa nguvu zetu wenyewe. Tunakuwa watakatifu kwa kumruhusu Yesu aishi ndani yetu. Kwahiyo, "Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana."[475]

Paulo alishuhudia,

> Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika Imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.[476]

> "Siri ya maisha ya utakatifu haiko katika kumuigiza Yesu, bali katika kuachilia utakatifu wa Yesu ujidhihirishe wenyewe ndani yangu."
> - Oswald Chambers

Ushuhuda wa Paulo unaweza kutafsiriwa kama ifuatavyo: "Maisha ninayoishi kwa sasa katika mwili ninaishi kwa Imani ndani ya Yesu Mwana wa Mungu." Paulo haahirishi mwito wa utakatifu hadi kifo. Paulo anashuhudia kwamba anaishi maisha ya utakatifu "sasa." Anaishije maisha ya utakatifu? Kwa Imani ndani ya Mwana wa Mungu. Paulo aliyaishi maisha ya utakatifu kwa sababu "wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu."

[471] Wakolosai 3:10
[472] Wakolosai 2:6
[473] Warumi 8:2
[474] 1 Wakorintho 1:2
[475] 1 Wakorintho 1:31
[476] Wagalatia 2:20

Lugha ya Paulo inaendana sambamba na mafundisho ya Yesu katika Yohana 15.

> Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.[477]

Utakatifu siyo kitu cha kupokea mbali na maisha yetu ndani ya Kristo; utakatifu ni uhusiano unaotakiwa udumishwe. Sisi tuko hai kwa ule muda wote ambao tutakuwa tumebaki tumeunganika na mzabibu. Tunaishi maisha ya utakatifu peke yake kupitia maisha yetu ndani ya Kristo. Mungu mtakatifu anakaa ndani yetu na tuko watakatifu tunapotembea naye.

"Kwa maana mlikufa, ***na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu***."[478] Maisha ya utakatifu hayapatikani kwa nguvu zetu; maisha matakatifu "yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Tunaishi maisha matakatifu kwa kuishi kila siku na akili ya Kristo. Jinsi tunavyotembea "ndani ya Kristo" tunayo nguvu ya kuishi maisha matakatifu katika dunia hii yenye dhambi. Tunazo nguvu za kuwa watakatifu katika maisha yetu ya kila siku. Hii ndiyo maana yaku mtakatifu.

## Utakatifu katika Vitendo: Kuishi Maisha ya Ushindi

Ujumbe wa maisha matakatifu ni ujumbe mzuri. Hata hivyo, Imani ambayo haiwezekani kuiishi katika maisha ya kila siku ni ya thamani ndogo sana kivitendo. Je, inawezekana kuishi maisha ya ushindi dhidi ya dhambi za kukusudia, au je, ujumbe wa maisha matakatifu ni ndoto tu?

### Je, ushindi dhidi ya dhambi inawezekana?

Paulo aliahidi kwamba "katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda."[479] Kwa hakika, ahadi hii ya maisha ya ushindi katika Kristo inahusisha pamoja na mambo mengine, ushindi juu ya nguvu ya dhambi. Kama inawezekana kuishi maisha ya ushindi wa kila siku dhidi ya dhambi za kukusudia, kwa nini Wakristo wengi sana wanashindwa kuishi kwa ushindi? Kuna sababu gani za kushindwa kiroho?

#### *Tutashindwa kama hatutaamini kwamba maisha ya ushindi yanawezekana*

Ninaridhika kwamba baadhi ya Wakristo hawaishi maisha ya ushindi kwa sababu wamejiridhisha kwamba maisha ya ushindi hayawezekani. Wamesikia mafundisho yakinena kwamba mara kwa mara ni lazima kuanguka kwenye dhambi za kukusudia – na wamekata tamaa ya ushindi wowote dhidi ya dhambi. Kama tunataka tuishi maisha ya ushindi dhidi ya dhambi, ni lazima tuchukue kwa kumaanisha wito wa Yohana: "Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi."[480] Yohana aliwaandikia Wakristo kwa

---

477 Yohana 15:5
478 Wakolosai 3:3
479 Warumi 8:37
480 1 Yohana 2:1

uhakika kwamba ilikuwa inawezekana kwao kuishi maisha ya ushindi. Ni lazima tukiri tumaini hili kwa Imani ili kutupa uhakika wa ushindi wakati wa kukabiliana na majaribu.

### *Tutashindwa kama tutang'ang'ania uzoefu wa zamani wa kiroho au hadhi ya kanisa*

Watu wengine wanayaona maisha ya utakatifu kama ni uzoefu wa maramoja tu ambao hauhitaji nidhamu au juhudi endelevu. Wanaamini kwamba wakishashuhudia tu kwamba, "Mungu amenitakasa moyo wangu na kunifanya msafi" hakuna kitu kingine tena kinachotakiwa kifanyike. Hata hivyo, kama Paulo alivyoonyesha, ni lazima tuendelee "kukaza mwendo katika kuifikilia mede ya thawabu." Ushindi dhidi ya dhambi unahitaji nidhamu endelevu katika maisha. Nitaendelea kusema "hapana" kwa dhambi na "ndiyo" kwa Mungu.

Baadhi ya mafundisho yanayohusu kujaribiwa kwa Yesu yanamalizia na ushindi wa Yesu dhidi ya majaribu ya Shetani. Hata hivyo, Luka anamalizia maelezo yake kwa kauli muhimu sana ya kuhitimisha kwamba, "Basi alipomaliza kila jaribu, Ibilisi akamwacha akaenda zake kwa muda."[481] Hii haikuwa ni mara ya mwisho Yesu kujaribiwa. Ingawaje vitabu vya Injili havijanakili taarifa kamili ya kumbukumbu za majaribu ya mwisho, Luka anabainisha kwa uwazi kwamba Shetani alipanga kumjaribu tena Yesu.

Kamwe hatupaswi kuwa na dhana kwamba tumefikia kilele cha kukua kiroho ambacho hatuwezi kuanguka tena. Badala yake, tunatakiwa tuendelee kujilinda mwili na akili zetu. Shetani anapenda sana kufanya mashambulizi wakati tunapotoka kwenye ulinzi wetu. Maisha ya utakatifu yanahitaji sana umakini wa tahadhari.

Wachungaji na viongozi wa makanisa wanaweza kuingia kwenye majaribu ya kutumainia hadhi zao katika jamii ili kupata ushindi wa kiroho. Tunaweza kuwa na dhana hiyo kwamba kwa sababu tunahubiri ukweli na kujisikia kuwa na upako wa Mungu kwamba hatuwezi kuanguka. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa kuhubiri ibada ya Jumapili na kuanguka kesho yake Jumatatu. Kamwe tusikae tukitumainia uzoefu wetu wa nyuma au nafasi zetu katika kanisa.

### *Tutashindwa kama tutajaribu kuishi maisha ya Kikristo kwa nguvu zetu wenyewe*

Maisha ya ushindi hayaji kwa nguvu zetu wenyewe bali kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Maisha ya utakatifu tunayaishi ***kila siku*** kwa nguvu endelevu za Roho Mtakatifu. Hatuwezi kufikia kiwango ambacho kwa nguvu zetu wenyewe tunaweza kuyashinda majaribu ya Shetani. Petro alijisifu, "Hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi…Ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe."[482] Alijiamini sana kwamba angeweza akakabiliana na mashambulizi ya Shetani kwa nguvu zake mwenyewe. Haikuchukua muda alishindwa.

---

[481] Luka 4:13
[482] Marko 14:29-31

Hata hivyo, tunavyoishi ndani ya nguvu za Roho Mtakatifu, anatupa ushindi dhidi ya majaribu. Kwa njia hiyo hiyo ambayo Yesu alifikwa na majaribu akiwa na nguvu za Roho Mtakatifu, nasi pia tunaweza kukabiliana na majaribu tukiwa na nguvu za Roho Mtakatifu.

Hali kadhalika, wachungaji na viongozi wa makanisa wanaweza kujaribiwa kutegemea nguvu zao wenyewe. Tunapoongoza maombi ya hadhara, tunaweza tukajikuta tunashindwa kuchukua muda binafsi wa maombi na Mungu. Tunapojifunza na kulihuburi Neno la Mungu hadharani, tunaweza kushindwa kuchukua muda wa kumsikiliza Mungu akisemanasi binafsi kupitia Neno lake. Hatupaswi kabisa kuruhusu juhudi zetu katika huduma zetu zidumaze kutembea kwetu binafsi na Mungu pamoja na Roho Mtakatifu kwa ajili ya ushindi wa kiroho.

**Kama tukishindwa**

Yohana aliwataka waamini waishi maisha ya utakatifu dhidi ya dhambi. "Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi."[483] Kuna uwezekano mkubwa wa kuishi bila ya kuwepo kushindwa kiroho. Hata hivyo, Yohana alitoa angalizo kwa wale wanaoangukia kwenye dhambi, "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki."[484] Uwiano huu ni muhimu - lakini mara nyingi ukipuuzwa.

Kwa upande mwingine, kuna wale wanaowekea mkazo sehemu ya kwanza tu ya aya hii: "Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi." Wanafundisha kwamba tunaweza kuishi maisha ya uhuru bila dhambi za kukusudia. Hata hivyo, hawana ujumbe kwa ajili ya wale wanaoshindwa katika dhambi wakati wa kipindi cha madhaifu.

Kwa upande mwingine pia, kuna wale wanaowekea mkazo tu kwenye sehemu ya mwisho ya aya hii: "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki." Wanamaanisha kuwa maisha ya ushindi hayawezekani, kwa hiyo tutaendelea kushindwa katika dhambi.

Yohana anatoa uwiano sahihi. Kwanza, **maisha ya ushindi yanawezekana;** Siwezi kujiachilia tu kwenye majaribu. Lakini la pili, nikianguka katika nyakati za majaribu, **ninaye wakili wa kunitetea**. Sihitaji kuachana na msimamo wangu wa Kikristo. Sihitaji kukata tamaa. Ndiyo, Mungu ataniadabisha. Lakini ananiadabisha kama Baba wa upendo anavyomuadabisha mtoto – ili kusudi "kuwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani." Yeye "anatuadabisha kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. "[485]

Shetani hutaka kuwashawishi Wakristo watumainie utendaji wao kama njia ya kumfurahisha Mungu. Anataka tujisahau kwamba sisi tulishapatanishwa na Mungu na kwamba sisi sasa ni watoto wake. Tulipokuwa watenda dhambi, "tulipatanishwa na Mungu

[483] 1 Yohana 2:1
[484] Ibid.
[485] Waebrania 12:10, 11


kwa mauti ya Mwana wake." Kisha tafakari kwamba, "zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake." [486]

Kama watenda dhambi, hatukupata kibali cha Mungu; alitupatanisha sisi na yeye mwenyewe kwa kifo cha mwanae. Sasa Paulo anasema, "zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake!" Baadhi ya Wakristo wametokea kuamini kwamba, "Nimeokolewa kwa neema kupitia Imani, lakini ninabakia kuwa nimeokolewa kwa kuwa mzuri sana kustahili upendo wa Mungu."

Hii ni sawa na mzazi anayesema, "Ndiyo, Nilikupenda sana kiasi cha kukuleta wewe duniani – lakini kwa sasa upendo wangu utaupata kupitia utendaji wako wa kila siku." Huyu siyo mzazi mwenye upendo! Na huyu siyo Baba yetu wa mbinguni mwenye upendo.

Badala yake, kama nilivyotegemea kwa mara ya kwanza neema ya Mungu inilete kwenye maisha ya kiroho, ninategemea pia neema iiweke hai hali yangu ya kiroho. ***Na kama*** nitaanguka, ni lazima nitegemee tena neema ya Mungu inirejeshe upya kwenye afya ya kiroho.

## Aliipata Siri - Hudson Taylor



Hudson Taylor ni mmoja kati ya wamishenari wa zama za kisasa aliyekuwa na ushawishi mkubwa sana, na alikuwa mwasisi wa shirika la kimisheni la China Inland Mission.[487] Taylor aliongoka akiwa na umria wa miaka 17 kupitia maombi ya mama yake wa Kimethodisti. Alijifunza udaktari na alisafiri kwenda China kama mmishenari katika umri wa miaka 21.

Alipokuwa na umri wa miaka 28 alirejea Uingereza kwa sababu ya ugonjwa wa kisukari. Miaka mitano baadaye iliyofuata, alitafuta sana uongozi wa Mungu, na akiamini kwamba Mungu alimtaka aajiri kundi la wamishenari kwa ajili ya kwenda kufanya uinjilisti katikati ya nchi ya China. Akiwa na umri wa miaka 34, Hudson na Maria Taylor na watoto wao walisafiri pamoja na kundi la wamishenari kumi na sita, likiwa ni kundi la kwanza la wamishenari kutoka katika shirika hilo la China Inland Missionary.

Moja ya misemo maarufu sana ya Hudson Taylor ilikuwa, "Kazi ya Mungu inayofanyika katika mpango wa Mungu kamwe haiwezi kukosa mahitaji." Mara nyingi tunatafsiri kauli hii kwamba ni kuhusiana na fedha, lakini kwa Taylor ilikuwa ni zaidi ya hapo. Yeye aliamini kwamba Mungu atatoa fedha, uhakikisho, Imani, nguvu, na chochote kile ambacho kingehitajika kutimiza mapenzi yake. Kwa muda wote wa kipindi cha miongo mitano akiwa kiongozi wa China Inland Mission, Hudson Taylor aliiona ahadi hii ya Mungu ikitekelezwa mara nyingi zisizohesabika.

---

[486] Warumi 5:10

[487] Image: "HudsonTaylorin1893", *The Story of The China Inland Mission* (1893), retrieved from https://commons.wikimedia.org/wiki/File:HudsonTaylorin1893.jpg, public domain.

Mwaka 1869, Taylor alijikuta kwenye mgogoro mkubwa katika maisha yake ya kiroho. Amepambana na majaribu na kushindwa. Alimwandikia mama yake, "Sikuwa nimejua nilikuwa na moyo mbaya wa aina gani." Lakini pia aliandika, "Ninajua kwamba ninampenda Mungu na kazi yake, nina tumaini la kumtumikia yeye peke yake na katika mambo yote. ***Mungu anisaidie katika kumpenda yeye zaidi na kumtumika vyema."***

Mnamo Septemba 4, 1869, Hudson Taylor alitoa ushuhuda kwamba Mungu alimimina Roho wake kwa njia mpya katika maisha yake. Taylor alimwandikia mtumishi mwenzake, "Mungu amenifanya kuwa mtu mpya!" Msingi wa uhakikisho wa uwepo wa Mungu katika maisha mapya ya Taylor ulikuwa ni sentensi moja katika barua aliyoandikiwa na mmishenari mwenzake John McCarthy. Taylor alikuwa akitafuta kwa nguvu zake mwenyewe kuongeza Imani yake na uhakika wa uwepo wa Mungu. McCarthy aliandika, "Ni kwa jinsi gani Imani yetu inapata kuimarishwa? Siyo kujitahidi kuipata Imani, bali kutulia kwa huyo aliye Mwaminifu."

Taylor alimwandikia dada yake,

> Jinsi ninavyosoma, ninaona yote hayo! "Kama tusipoamini, yeye anabakia kuwa mwaminifu." Nilimwangalia Yesu nikaona, (na nilivyoona, uh, furaha yangu ilibubujikaje)! kwamba alishasema, "Kamwe sitamwacha yeye."
>
> "Ah, kuna mapumziko!" niliwaza. "Nilijisumbua bure kutaka kukaa kwake. Sitajisumbua tena. Kwa kuwa hajaahidi kuacha kushikamana nami – wala kuniacha, wala kunifanya nishindwe." Na mpendwa wangu, hafanyi hivyo.
>
> Sijaona tu kwamba Yesu kamwe hataniacha, bali kwamba na mimi ni mmoja wa mwilli wake, nyama yake, na mifupa yake. Mzabibu siyo mzizi tu, bali ni vyote – mizizi, shina, matawi, vitawi, majani, maua na matunda. Na Yesu siyo mwenyewe tu - Yeye ni udongo, nuru, hewa, manyunyu, na yuko mara elfu kumi zaidi kuliko tunavyomwazia, tunavyomtakia au tunavyomhitaji. Uh, hii ndiyo furaha ya kuuona ukweli! Ninaomba kwamba macho yetu ya kuona pia yawe na ufahamu na yaangaziwe nuru, ili tuweze kujua na kufurahia utajiri tunaopewa bure katika Kristo.

Kwa wakati huu, Taylor anaelewa kwamba kumfanania Kristo hakupatikani kwa juhudi binafsi bali kupitia muunganiko wa mzabibu ambao unatoa uhai. Unakuja kupitia kutambuliwa na Kristo. Mtoto wake baadaye aliandika kwamba, "Kwa muda mrefu alijua ni nini kujisalimisha, lakini kwa hili ilikuwa ni zaidi; ilikuwa ni kukubali kwa upya, furaha na kukabidhi bila kubakiza ubinafsi na vitu vyote kwake."

Hii haikuwa ni kwa muda mfupi tu wa uzoefu wa mhemuko. Miaka thelathini baadaye, Taylor alirejea nyuma na kuandika, "Kamwe hatutasahau baraka tulizopokea kutoka katika maneno, Yohana 4:14, 'walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele.' Tulikuja kutambua kwamba Kristo alimaanisha kila alichokisema kwa ufasaha – kwamba 'hataona' anamaanisha *hataona*, 'milele' anamaanisha *milele*, na 'kiu' anamaanisha *kiu* – mioyo yetu ilifurikwa na furaha mno ***kwa kupokea kipawa***

***hicho*.**" Angalia maneno haya, "kwa kupokea kipawa hicho." Taylor alielewa kwamba neema ya Mungu inayotakasa ni karama inayopaswa kupokelewa, na siyo mafanikio ya kuchuma.

Uzoefu wa neema ya Mungu, haukufanya maisha yaliyobakia ya Taylor kuwa rahisi. Mwaka uliofuata ulikuwa ni mwaka mgumu kwake kuliko miaka mingine yote katika maisha yake. Katika mwaka huo, watoto wake wawili walikufa na Maria alikufa akiwa na miaka 33. Baadaye, Taylor akaliongoza shirika la kimisheni la China Inland Mission katikati ya vitisho vya mashambulizi ya waasi. Wamishenari wapatao sabini na tisa kutoka katika shirika hilo waliuawa katika siku hizo za kutisha sana.

Lakini pamoja na kupitia mambo haya yote, Taylor alibakia na uhakika wa utii wake kwamba Mungu ataendelea kumpatia mahitaji yote yaliyohitajika. Mhubiri mmoja askofu aliyemtembelea Taylor katika nyakati zile ngumu kwake aliandika. "Hapa kuna mtu mwenye umri unaokaribia miaka sitini, akibeba mizigo mizito ya ajabu, lakini bado alikuwa mtulivu na asiyetaabika." Kwa nini? Kwa sababu alikuwa ni kitu kimoja na Mzabibu na alikuwa ametulia ndani ya Kristo. Alikuwa, "mmoja wa watu ambao wamehudumu kwa nguvu kubwa ambayo Mungu alimpa - ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo."[488]c

Uzoefu huu haukua ndio mwisho wa kukua kiroho kwa Taylor. Hata "kupumzika kwake chini ya Kristo" haimaanishi kwamba hakukuwa na juhudi zilizofanyika. Kila asubuhi, bila kujali shinikizo la huduma, Taylor alitumia masaa mawili ya maombi na kujifunza Biblia kabla ya kuanza kazi za siku. Yeye na Paulo walielewa kwamba, "ni lazima kusonga mbele katika kufikia malengo." Lakini hii ni juhudi ambayo inategemea nguvu za Mungu, na siyo za Hudson Taylor. Taylor alitambua kwamba hata nguvu inayomwezesha kuondoka kitandani kwenda kuanza kujifunza Biblia ilikuwa karama ya neema ya Mungu yenye kuwezesha. Angemfanania Kristo kwa ***sababu alikuwa 'ndani ya Kristo.'***

Mtoto wa Taylor alikumbuka maisha yake ya maombi na Neno. Kutulia ndani ya Kristo hakuna maana kwamba Taylor alipuuzia umuhimu wa nidhamu ya Kiroho.

> Kwake yeye, siri ya kushinda ilikuwa katika masaa ya kila siku ya ushirika na Mungu; na kwa hili, aligundua, lingeweza kudumishwa kwa maombi ya siri na kujilisha kwa Neno ambalo Mungu hujidhihirisha mwenyewe kwa nafsi inayongojea. Haikuwa rahisi kwa Bwana Taylor, katika maisha yake yaliyobadilishwa, kuwa na muda wa kufanya maombi na kujifunza Biblia, lakini alijua kwamba ni muhimu.
>
> Mara nyingi katika chumba kimoja kikubwa, wangetenga pembe moja kwa ajili ya baba yao, na pembe nyingine kwa ajili yao wenyewe, kwa mapazia tofauti; kisha baada ya kulala pakawepo na ukimya, watasikia njiti ya kiberiti ikiwashwa na wataona nuru ya mshumaa, ikiashiria kwamba Bwana Taylor, hata kama amechoka kiasi gani, alikuwa anafungua Biblia yake tayari kuanza kuyatafakari maneno ya

[488] 1 Petro 4:11

> Biblia. Kuanzia saa 8 hadi 10 alfajiri ulikuwa ndio muda wake wa maombi; muda ambao alikuwa na uhakika wa kutokuwepo na usumbufu wowote wakati wa kumngojea Mungu…. Sehemu ngumu sana katika huduma ya umishenari aliyoiona Bwana Taylor, ni kudumisha mara kwa mara maombi ya kujifunza Biblia. "Shetani mara zote atakutafutia wewe kitu cha kufanya," Atakusemesha, "wakati ule ambao ndio unataka kuzama" kwenye maombi na kujifunza Maandiko.

Hadi sasa, wamishenari 1600 wanafanya kazi katika shirika la umisheni la OMF International, mrithi wa shirika la China Inland Mission. Mamilioni ya waamini wa China walioongozwa kumwamini Kristo wanatokana na huduma ya shirika hili la umisheni. Haya ni matunda ya mtu aliyeishi katika umoja na Kristo. [489]

## Upendo wa Mungu - Charles Wesley

Upendo wa Mungu, unaozidi zote, furaha ya mbinguni kuja duniani shuka chini;
Turekebishe ndani yetu makao yako ya unyenyekevu;
utuvike kwa uaminifu rehema zako zote!
Yesu, wewe ni wa huruma, msafi, usiyekuwa na upendo wenye mipaka;
Tutembelee kwa wokovu wako; ingia kwenye kila moyo unaotetemeka.

Malizia basi, uumbaji wako; tuwe wasafi na tusiokuwa na doa'
Acha tuuone wokovu wako mkuu ukirejeshwa kikamilifu ndani yetu,
Tukibadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu mwingine,
hadi tutakapochukua nafasi zetu mbinguni.
Hadi tutakapopata taji zetu mbele yako, kwa maajabu, upendo na sifa.

[489] Maelezo yanatokana na Dr. na Bibi Howard Taylor, *Hudson Taylor's Spiritual Secret*

**Tafakuri ya Somo la 10**

(1) Mitume walimtaka kila Mkristo awe mtakatifu.

(2) Kuwa mtakatifu ni kufanana na Kristo.

- Kuwa mtakatifu ni kuwa na moyo wa utakatifu:moyo na akili vinavyomfanania Kristo.
- Kuwa mtakatifu ni kuwa na mikono mitakatifu: Tabia inayomfanania Kristo.
- Kuwa mtakatifu ni kuwa na upendo unaomfanania Kristo.

(3) Mitume walionyesha utakatifu unavyotakiwa uwe kwenye maisha ya kila siku.

- Umefanywa kuwa mtakatifu; unaendelea kufanywa mtakatifu.
- Ninyi ni watakatifu; lazima muishi kama watakatifu.
- Mungu anawafanya muwe watakatifu; lazima kufuata utakatifu.

(4) Tumepewa uwezo wa kuyaishi maisha matakatifu kupitia Roho wa Kristo aishiye ndani yetu.

(5) Tunaishi maisha matakatifu tukiwa "ndani ya Kristo." Maisha yetu ya kale yalikuwa "ndani ya Adamu." Maisha yetu mapya tunayaishi "ndani ya Kristo."

(6) Maisha ya Utakatifu yako kwenye msingi endelevu wa uhusiano na Mzabibu.

**Kazi ya Kufanya**

(1) Andaa fundisho kuhusu "Maisha yanayomfanania Yesu." Linganisha njia mbili za kuishi: Maisha yetu ya zamani ndani ya Adamu na maisha yetu mapya ndani ya Kristo. Onyesha jinsi ambavyo kuwa "ndani ya Kristo" kunatuwezesha sisi kuwa washindi juu ya dhambi.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Wafilipi 2:1-5.

# Somo la 11
# Utakatifu ni Ushirika usiovunjika na Mungu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kufurahia ukamilikaji wa ahadi za kinabii za Mungu.

(2) Kutambua kwamba ushirika katika kanisa  ni maandalizi ya ushirika wa mbinguni.

(3) Kuwajibika kwa vitendo katika kanisa linalohamasisha ukuaji wa utakatifu.

(4) Kukariri Ufunuo 21:2-3.

## Yohana: Mtu Aliyeshuhudia Ukamilikaji wa Ahadi ya Mungu.

Tusafiri kuelekea katika kisiwa cha Patmo kwenye bahari ya Aigea.  Siyo kisiwa kizuri sana katika bahari ya Karibeani au kisiwa cha Pasifiki ya Kusini. Ni kisiwa na gereza la wafungwa. Patmo ni kisiwa kitupu na cha upweke. Hapo utamkuta Yohana, Mwanafunzi aliyependwa sana, akiishi uhamishoni/kifungoni.

Yohana sasa ni mzee. Amemtumikia Mungu kwa uaminifu na amekuwa mfano wa kuigwa wa maisha ya utakatifu. Amehudumu katika kanisa la Efeso, akimhudumia mama mjane wa Yesu, na akihubiri katika Asia ndogo yote.

Akiwa katika umri ambao angekuwa anapaswa kufurahia heshima ya kuwa mwanafunzi wa mwisho wa Yesu aliye hai, Yohana alikuwa amefukuzwa kwenye nchi yake na kupelekwa katika kisiwa cha Patmo. Yuko mwenyewe mpweke na anaweza kuwa anawaza kwamba yeye hana manufaa tena kwenye kazi ya Mungu. Lakini Jumapili moja asubuhi karibia miaka sitini baada ya Yesu kupaa mbinguni, Yohana alikuwa "katika Roho, siku ya Bwana," akasikia sauti kuu nyuma yake, kama sauti ya baragumu.

Wakati Yohana alipogeuka nyuma ilikotokea sauti, alimwona Kristo aliyekuwa amemtolea maisha yake. Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu; na macho yake kama mwali wa moto; na miguu yake ilimeremeta kama shaba iliyosuguliwa sana, na sauti yake kama sauti ya maji mengi, na sauti yake kama sauti ya maji mengi, na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake. Yohana aliuona "utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."[490]

Katika kitabu cha Ufunuo, tunatembea na Yohana hadi Mbinguni ili tukaone kutimizwa kwa mpango wa Mungu. Watu watakatifu, wataishi kwenye umilele katika ushirika usiovunjika na Mungu aliye mtakatifu.

---

[490] Yohana 1:14

## Neno Kamili

### Neno kamili lililopotea

Kwenye somo la ufunguzi la kozi hii, nilikutaka ufikirie kuhusu bustani ya Edeni wakati wa uumbaji. Ilikuwa ni dunia iliyokuwa imekamilika. Maua, miti, na matunda vilikuwa kila mahali. Ilikuwa ni dunia ambayo haikuwa na dhambi. Ilikuwa ni dunia bila maumivu, machozi, au kifo. Jambo la muhimu zaidi, ilikuwa ni dunia iliyokuwa kwenye mahusiano kamili kati ya Mungu na mwanadanu. Hakuna kilichoweza kumtenganisha mwanadamu na muumba wake.

> **Sala kwa ajili ya Utakatifu**
>
> "Ee Bwana, tulete tena kwenye
> uamsho wa mwisho katika nyumba na
> lango la mbinguni,
> kuinga katika lango hilo na kuishi
> katika nyumba hiyo,
> Mahali ambapo hakutakuwepo na giza,
> Bali mwanga mmoja tu;
> Hakuna kelele bali muziki mmoja tu;
> Hakuna mwisho wala mwanzo,
> bali umilele mmoja tu;
> Kwenye makao ya utukufu na
> utawala wako,
> ulimwengu usiokuwa na mwisho."
>
> - Imenukuliwa kutoka kwa
> John Donne

Kwa masikitiko makubwa, dhambi iliiharibu dunia iliyokuwa kamilifu. Magugu yaliota katikati ya maua. Wanyama waliokuwa hawana matatizo wakafanyika kuwa viumbe hatari. Mwanadamu akaishi kwa mateso, maumivu, na kifo. Kubwa na muhimu kuliko hilo, mahusiano kati ya Mungu na mwanadamu yaliharibika. Kwa sababu ya dhambi. Mwanadamu alifukuzwa kutoka katika bustani ya Eden na akazuiliwa katika kuufikia tena Mti wa Uzima. Ilionekana kwamba Shetani amelishinda kusudi la Mungu alilokuwa nalo kwa ajili ya watu wake.

### Ulimwengu kamili ulioahidiwa

Lakini hii haikuwa mwisho wa mambo yote. Katika Maandiko yote, Mungu anaonyesha mpango wake wa kuwafanya watu wake wafanane na yeye; anakusudia kuwafanya watu wake wawe watakatifu. Manabii wa Agano la Kale walitabiri kwamba siku moja Mungu atawafanya watu wake wawe watakatifu na kuwarudisha katika eneo la utakatifu. Akirudia mara kwa mara, Yohana mwona Mafunuo anaonyesha kutimizwa kwa ahadi hizo.

Ezekieli aliiona siku ambayo Mungu atakaa katikati ya watu wake watakatifu:

> Tena maskani yangu itakuwa pamoja nao, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Na mataifa watajua ya kuwa mimi **ndimi Bwana, mimi niwatakasaye Israeli**, patakatifu pangu patakapokuwa katikati yao milele.[491]

Mungu ataitakasa Israeli; atawafanya watu wake kuwa watakatifu. Ataishi katikati ya watu wake. Utabiri wa Ezekieli 37:27 unatimizwa katika Ufunuo 21:3:

[491] Ezekieli 37:27-28

> Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu. Naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao kama Mungu wao.

Kusudi kuu la Mungu litakuwa limetimia wakati atakapokaa katikati ya watu wake watakatifu. Kama Ezekieli, Zakaria naye aliiona siku ambayo kusudi la Mungu kwa watu wake litatimia. Mungu aliahidi, "Nitakaa kati yako."[492]

Kitabu cha Zakaria 3 kinaonyesha mpango wa Mungu kwa ajili ya watu wake. Katika maono ya Zakaria, Kuhani mkuu alikuwa amevaa nguo chafu sana ikiwakilisha uchafu wa Israeli. Siku moja Mungu atawatakasa watu wake; mavazi machafu ya Israeli na kubadilishiwa hariri mpya.

> Na malaika akasema na wale waliokuwa wamesimama mbele yake, "Mvueni nguo hizi zenye uchafu." Kisha akamwambia yeye, "Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi."[493]

Aya za mwisho katika kitabu cha Zakaria kina picha ya mitazamo mingi ya utukufu katika Agano la Kale.

> Siku hiyo katika njuga za farasi yataandikwa maneno haya, "WATAKATIFU KWA Bwana." Navyo vyombo vilivyomo ndani ya nyumba ya Bwana vitakuwa kama mabakuli yaliyoko mbele ya madhabahu. Naam, kila chombo katika Yerusalemu, na katika Yuda, kitakuwa kitakatifu kwa Bwana wa majeshi, nao wote watoao dhabihu watakuja kuvitwaa vile vyombo, na kutokosa nyama ndani yake….[494]

Katika njuga za farasi yataandikwa maneno kutoka katika kilemba cha ya Kuhani mkuu.[495] Sufuria za kawaida zitakuwa takatifu kama zilivyo "bakuli takatifu mbele ya madhabahu." Yerusalemu utakuwa kama Mungu alivyoukusudia uwe; jiji lote litakuwa mahali pa Bwana pa kukaa.

Mungu atatimiza kusudi lake; atakuwa na watu watakatifu watakaoishi katika jiji hilo. Maono ya Zakaria yanatimilika katika Ufunuo 21 na 22. Watu wa Mungu wataishi kwenye uwepo wake. "Naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake."[496]

### Ulimwengu kamili Uliorejeshwa

Biblia inaanza kwa kuelezea juu ya ulimwengu kamili uliopotea kwa sababu ya anguko la dhambi. Inamalizia kwa kuelezea juu ya ulimwengu ambao unawangojea wale waliomruhusu Mungu atimize mpango wake katika maisha yao. Mji Mtakatifu unaandaliwa kwa ajili ya watu wa Mungu watakatifu.

---

[492] Zakaria 2:10-11
[493] Zakaria 3:4
[494] Zakaria 14:20-21
[495] Kutoka 28:36-38
[496] Ufunuo 21:3

Kama ilivyokuwa kwa Bustani ya Edeni, Mji Mtakatifu ni ulimwengu uliokamilika kwa maua, miti, matunda mazuri ya kula kila mahali. Kila kitu ni kizuri:

> Kisha malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo, katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.[497]

Kwa sababu ya dhambi, mwanadamu alifukuzwa kutoka katika bustani ya Eden na Mti wa uzima. Katika kitabu cha Ufunuo ule mti wa uzima kwa mara nyingine tena unapatika kwa mwanadamu.

Huu utakuwa ni ulimwengu usiokuwa na dhambi. Wasomaji wengi hufadhaishwa na sura za katikati za kitabu cha Ufunuo. Sura hizi huelezea juu ya hukumu zitakazoiangukia dunia. Wasomaji wengi huwa wanapenda kukimbilia kwenye sura za mwisho za kitabu cha Ufunuo zinazozungumzia uzuri wa mbinguni. Hata hivyo, hatuwezi kupuuzia kilichoko katikati ya kitabu hiki. Ili watu watakatifu waweze kuishi katika ushirika usiovunjika na Mungu mtakatifu, nguvu ya dhambi ni lazima ivunjwe.

Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha chuki ya Shetani dhidi ya wana wa Mungu. Yohana aliona "mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba."[498] Huyo mnyama "akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda."[499] Kwa muda, inaonekana kwamba uovu unawashinda watakatifu wa Mungu. Hata hivyo, huyo mnyama kwa vyovyoye vile ni lazima atashindwa.[500] Watu wa Mungu hawana budi kushinda. Kusudi la Mungu litakuwa limekamilika.

Popote katika historia, watu wa Mungu wanaamini kwamba Mungu mtakatifu atafanya kilicho sahihi. Utakatifu wa Mungu ulimpa uhakika mtunga zaburi wakati alipolia kwa ajili ya haki. "Maana huwi Mungu apendezwaye na ubaya; Mtu mwovu hatakaa kwako."[501] Katika kitabu cha Ufunuo, Yohana alisikia kilio cha wafia Imani, "Ee Mola, Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?"[502]

Utakatifu wa Mungu unawahakikishia watu wa Mungu kwamba haki itashinda. Yohana aliwaandikia Wakristo waliokuwa wanagandamizwa na utawala wa Kirumi. Aliwaahidi kwamba, mhukumu wa dunia "aliye mtakatifu na mwenye haki" siku moja anakuja kuleta haki kwa watu wake. Kitabu cha Ufunuo kinawataka watu wa Mungu kutulia wakiwa waaminifu, wakijua kwamba Mungu mtakatifu atalipiza kisasi kwa ajili ya watu wake.

[497] Ufunuo 22:1-2
[498] Ufunuo 13:1
[499] Ufunuo 13:7
[500] Ufunuo 15:2
[501] Zaburi 5:4
[502] Ufunuo 6:10

Kitabu cha Ufunuo kinaangalia muda ambao Shetani atashindwa, na watu wa Mungu wataishi kwa amani.

Mbinguni ni mji mtakatifu. Ni mji mtakatifu usiokuwa na dhambi au na madhila ya dhambi. Ni mji usiokuwa na maombolezo, wala machozi, wala maumivu, na hakuna mauti. Mungu, "atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita."[503]

Lakini bado kuna kitu kingine cha ajabu zaidi. Sehemu kubwa ya Bustani ya Edeni ilikuwa ni sehemu kamilifu ya ushirika kati ya Mungu na mwanadamu. Adamu na Hawa walitembea katika bustani hii na Mungu. Walitembea pamoja naye uso kwa uso. Hakuna kilichoweza kumtenganisha Mungu na mwanadamu. Mbinguni, tutaishi katika ushirika mtakatifu na Mungu. Hakuna cha kuweza kutenganisha watu watakatifu kutoka kwa Mungu mtakatifu.

> Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, "Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao."[504]

Yohana anailezea mbingu kuwa ni sehemu isiyokuwa na maombolezo, wala maumivu, wala mauti. Vitu vyote vilivyoleta maombolezo katika ulimwengu wa zamani (utajiri usiojulikana kwenye bahari, hatari za usiku, tishio la magonjwa), vyote vitatoweshwa. Amani hii ya mwisho itategemea sana uwepo wa Mungu mwenyewe.

> Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.[505]

Watu watakatifu wamekuwa mara zote wakitamani kumwona Mungu. Musa aliomba amwone Mungu, lakini hakuweza kuuona uso wake.[506] Daudi aliomba, "Lini nitakapokuja nionekane mbele za Mungu?"[507] Yesu aliahidi kwamba, heri wenye moyo safi; maana hao "watamwona Mungu."[508] Ahadi hii inatimilika katika kitabu cha Ufunuo. "Nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao."[509]

---

[503] Ufunuo 21:4
[504] Ufunuo 21:3
[505] Ufunuo 22:3-5
[506] Kutoka 33:18-20
[507] Zaburi 42:2. Tafsiri nyingine ya maombi haya inasoma, "Lini nitakuja niuone uso wa Mungu?" (Tanbihi ya *English Standard Version*).
[508] Mathayo 5:8
[509] Ufunuo 22:4

Dallas Willard alisimulia kuhusu mtoto mdogo aliyefiwa na mama yake. Usiku mmoja, akiwa mwenye mashaka na peke yake, kijana aliomba alale kwenye chumba cha baba yake. Kwenye usiku wa manane, kijana aliamka na kumwuliza baba yake, "Je, umeugeuzia uso wako kwangu?" Baba akamjibu, "Ndiyo, uso wangu umekugeukia wewe." Hii ilitosha, kijana akalala kwa amani. Mbinguni, watu watakatifu watauona uso wa Mungu. Uso wake utakuwa umegeuziwa kwetu milele; tutakuwa na amani.

Mpango wa Mungu utakuwa umetimilizwa! Bustani ya Edeni itarejeshwa tena. Watu walio na mioyo na mikono mitakatifu wataishi milele na Mungu mtakatifu. Huu ni mpango wa Mungu kwa watu wake.

### Utakatifu ni ushirika pamoja na Mungu usiovunjika

Yohana aliona maono kuhusiana na mpango wa Mungu kwa ajili ya watu wake. Ni maono ya watu watakatifu wanaoishi katika mji mtakatifu. Mara tatu katika kitabu cha Ufunuo Yohana anaelezea maskani yetu ya milele ya kuishi kama "mji mtakatifu." [510] Hapa ndipo nyumbani pa Mungu Mtakatifu, malaika watakatifu, na watu watakatifu. Mji huu mzuri sana ni mahali pa utakatifu mkamilifu. Ni watu watakatifu tu watakaoishi pale.

Katika Ufunuo sura ya 21 inatoa picha nzuri sana ya kulivyo mbinguni, lakini pia inatoa tahadhari ifuatayo:

> Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.[511]

Mbinguni ni mji mtakatifu. Mungu hawezi kuruhusu dhambi iharibu usafi wa mji huo. Wahubiri wa zamani walisema, "Mbinguni ni mahali patakatifu palipoandaliwa kwa ajli ya watu watakatifu." Ni watu watakatifu peke yake watakaoweza ***kufurahia*** kuishi katika huu mji mtakatifu.

Mtu binafsi hataweza kupata furaha ya huu mji ambao ndipo penye kivutio cha Mwana Kondoo wa Mungu. Mtu anayeishi maisha ya kufurahia dhambi hataweza kufurahia kukaa katika mji ambao kila kitu ni kisafi. Mtu ambaye hampendi Mungu atachoka sana kukaa katika mji ambapo kusifu na kumwabudu Mungu ni kwa milele. Mji mtakatatifu umeandaliwa mahususi kwa watu watakatifu tu. Kwa kuwa watu wa Mungu ni watakatifu na wasafi, wataishi na yeye milelle katika mji huo.

Ahadi iliyoko katika kitabu cha Ezekieli 40-48 inatimilizwa katika Yerusalemu Mpya. Hata hivyo, msomaji mara moja anaona tofauti iliyoko kati ya Maono ya Ezekieli na utimilifu wake katika kitabu cha Ufunuo. Kwenye maono ya Ezekieli, hekalu limekaa katikati ya mji. Katika mji mpya hakuna "hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na

---

[510] Ufunuo 21:2; 21:10; 22:9
[511] Ufunuo 21:8

Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake.” [512] Mungu mwenyewe ndiye hekalu! Mji wote sasa ni “ardhi takatifu” iliyotengwa kwa ajili ya Mungu na watu wake.

Ushirika usiovunjika ambao Mungu na mwanadamu walishirikiana katika bustani unarejeshwa. Aibu na maombolezo yaliyosababishwa na watenda dhambi Adamu na Hawa hata kujificha mbele za Mungu yameondoshwa. Tutauangalia uso wa Mungu. Watu watakatifu wataufurahia ushirika usiovunjika pamoja na Mungu mtakatifu.

Katika Agano la Kale, Mungu aliitenga Israeli kama, “ufalme wa makuhani, na taifa takatifu.”[513] Katika kitabu cha Ufunuo, kanisa ni, “ufalme na makuhani kwa Mungu wetu.”[514] Tofauti na taifa la Israeli, ufalme huu ni, “mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha.”[515] Ahadi katika kitabu cha Mwanzo 12:3 inatimilika katika kitabu cha Ufunuo 7:9.

Kama Israeli ingeweza kutimiza ahadi yake ya kuwa ufalme wa makuhani, na taifa takatifu tu kwa kuwa watakatifu, kadhalika Kanisa linaweza kutimiza ahadi yake kama tu litakuwa takatifu. Watu wa Mungu ni lazima wawe watakatifu. Katika Agano la Kale, Walawi walivaa mavazi meupe kama ishara ya usafi. Kwa jinsi hiyo hiyo, Yohana anaonyesha kwamba watakatifu wanatakiwa wawe wasafi.[516] Ni wale tu “wazifuao nguo zao” watakaoingia katika mji huo.[517] Watu watakatifu wataishi kwa Amani pamoja na Mungu mtakatifu.

### Utakatifu katika Mazoezi: Wakati ninapojihisi siyo Mtakatifu

Je, hili ni jambo la kawaida? Unasikia ujumbe unaokupa changamoto ya kuongeza zaidi utakatifu. Unaomba na kujikabidhi mwenyewe kwenye maisha ya utakatifu. Kwa wiki nane zinazofuata, unakuwa katika kiwango chako cha maisha ya kiroho. Unaliona tunda la Roho mtakatifu likiongezeka katika maisha yako ya kiroho. Unajikuta uko kwenye upendo wa ndani na Mungu na jirani yako.

Ghafla, unagonga ukuta. Bado unatembea na Mungu; ukijiagalia unajikuta huna dhambi za kujitakia katika maisha yako; unampenda Mungu na jirani yako. Lakini kutokana na madhaifu ya kimwili, mihemuko ya hisia, au hata shinikizo za huduma, unajigundua kwamba, “*Sijisikii* kama ninakua katika utakatifu. Kuna tatizo gani?”

Ni kwa jnsi gani utaendelea na maisha ya utakatifu wakati hujisikii kuwa mtakatifu? Je, unakata tamaa na kusema, “Utakatifu kamwe hauwezekani”? Je, huwa unarudi madhabahuni? Ni kwa jinsi gani utaendelea kutembea katika utakatifu?

► Je, umeshakutana na changamoto kama hii? Je, uliishughulikiaje?

---

[512] Ufunuo 21:22
[513] Kutoka 19:6
[514] Ufunuo 5:10
[515] Ufunuo 7:9
[516] Ufunuo 3:4-5; 6:11; 19:8
[517] Ufunuo 22:14

**"Wakati ninapojihisi siyo mtakatifu, ni lazima nitembee kwa Imani."**

Katika somo la 2, tumeona kwamba utakatifu ni "kutembea pamoja na Mungu." Ibrahimu alitembea pamoja na Mungu kwenda katika nchi ambayo hakuwahi kuiona. Alitembea pamoja na Mungu kwa utii na Imani. Miaka elfu nne baadaye, bado tunasisimka tunaposoma kuhusu Imani ya Ibrahimu. Lakini hebu vaa kiatu chake – tembea siku hadi siku hadi siku katika ardhi ya mawemawe. Hauoni mwisho, na hata hujui unakokwenda. Je, unadhani kwamba Ibrahimu aliamka kila asubuhi akijihisi kusisimka kwa ajili ya hiyo siku? Sidhani kama ndivyo. Naamini kuna siku ambazo alikuwa akisema, "Sijisikii kutembea leo." Lakini ibrahimu aliendelea kutembea pamoja na Mungu.

Tunasoma kwamba Nuhu "alitembea pamoja na Mungu" katikati ya dunia iliyojaa dhambi. Alikuwa amezungukwa na wapagani waabudu vinyago, na watu ambao kila mara walishauriana njia mpya za kutenda maovu,[518] Nuhu alitembea pamoja na Mungu. Je, unadhani kwamba aliamka kila asubuhi akijihisi kusisimka kwa ajili ya hiyo siku? Ninahisi kwamba mara nyingine alijisikia kuchoka sana na kukatishwa tamaa. Lakini, Nuhu aliendelea kutembea pamoja na Mungu.

Msingi mmoja wa maisha ya utakatifu ni kukumbuka kwamba tulikombolewa kwa neema kwa njia ya Imani; tulitakaswa kwa neema kupitia Imani, na tunaendelea kukua katika utakatifu kwa neema kupitia Imani. Baadhi ya watu wanaelewa kwamba wameokolewa kwa neema kupitia Imani. Hata wamejifunza kwamba wametakaswa kwa neema kupitia Imani. Lakini, baadaye wanaangukia kwenye mtego wa kuamini kwamba kuendelea kwao kukua kunategemea juhudi zao binafsi.

Je, kunayo nidhamu inayohitajika katika maisha ya utakatifu? Kwa hakika ipo! Je, tunahitajika kuendelea "kuvifisha viungo vyetu vilivyo katika nchi"?[519] Ndiyo. Je, ni lazima "kuyachuchumilia yaliyo mbele" na "kukaza mwendo, kuifikilia mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu"? [520] Hakika!

***Lakini*** kamwe usisahau kwamba "kuvifisha viungo vyetu vilivyo katika nchi" "kuyachuchumilia yaliyo mbele" na "kukaza mwendo, kuifikilia mede ya thawabu" hufanyika kwa nguvu za "Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."[521] Huyo ndiye peke yake aliyetufanya tutake sana (mapenzi yake); ndiye anayetoa nguvu (za kazi). Anafanya kazi ndani yetu ili kukamilisha kusudi lake la kutufanya sisi watakatifu. Unapojihisi hauko na utakatifu, unapumzika ndani ya neema ya Mungu ambaye kila siku anatubadilisha tuwe katika mfano wake.

---

[518] Mwanzo 6:5
[519] Wakolosai 3:5
[520] Wafilipi 3:13-14
[521] Wafilipi 2:13

**“Wakati ninapojihisi siyo mtakatifu, ni lazima nipumzike kwenye utakatifu wake.”**

Katika somo la 5, tuliona kwamba ukamilifu siyo kuhusu utendaji usiofaa bali ni kuhusu moyo usiogawanyika katika dhamira yetu kwa Mungu. Katika somo la 7, tulijifunza kwamba agizo la Yesu la “Kuwa mkamilifu” ni agizo kwa upendo usiogawanyika kwa Mungu. Ukristo ulio mkamilifu siyo kuhusu utendaji; bali ni kuhusu upendo.

Sisi ni watakatifu kwa sababu Mungu ni mtakatifu. Utambulisho wetu uko “ndani ya Kristo.” Yeye ndiye anayetufanya tuwe watakatifu. Moja ya kweli za msingi za Injili ni kwamba kwa sasa hatujitaabishi tena kuupata utakatifu kwa juhudi zetu wenyewe. Tuna uhakika katika Kristo. Utambulisho wetu kama Wakristo, utambulisho wetu kama watakatifu, na utambulisho wetu kama watu watakatifu uko ndani yake.

Robert Coleman wakati mmoja alielezea kuhusu ni nini maana ya kumpenda Mungu kwa ukamilifu wakati ambapo hatuwezi kufanya kwa ukamilifu. Dr. Coleman alikuwa anafanya kazi kwenye bustani yake siku moja ya majira ya joto. Kijana wake mdogo alipomwona anatoa jasho kwenye jua, aliamua amletee maji. Alichukua kikombe kilichokuwa kichafu, akakijaza maji kutoka katika birika lililokuwa limejengwa uwani mwa nyumba, akamletea baba yake. Dr. Coleman akasema, ”Kikombe kilikuwa kichafu na maji yalikuwa ya matope. Lakini kinywaji kilikuwa kimekamilika kwa sababu kilikuwa kimetoka katika moyo ulio na upendo.” Hiyo ni taswira ya ukamilifu wetu mdogo. Tunaleta kwa Mungu huduma zetu sizizokamilika na dhaifu, lakini anazikubali kwa sababu zinatoka katika moyo wa upendo.

Mungu huwa anakubali juhudi zetu dhaifu na huzibadilisha ziwe kitu kingine juu ya upeo wetu wa kufikiri – kwa sababu utakatifu wetu ni kitu kidogo tu kutokana na utakatifu wake mwingi usiokuwa na kipimo. Hata upendo wetu mzuri sana unaathiriwa na mapungufu ya kibinadamu. Lakini tunapotulia katika utakatifu wake, tunatambua kwamba kuwa na utii katika maagizo yake ya “Kuwa mtakatifu” kunakamilishwa tu kupitia yeye mwenyewe. Tukiwa na upendo usiogawanyika, tunampelekea glasi yetu ya maji ya matope – na anayabadilisha kuwa kitu kingine kisafi na kinachong’aa. Utakatifu wetu unakamilishwa katika utakatifu wake.

**“Ninapojihisi siyo mtakatifu, napaswa nikumbuke kwamba mimi ni sehemu ya watu watakatifu.”**

Dhamira kuu kabisa ambayo mara nyingi huwa haizingatiwi katika kitabu cha Ufunuo ni Kanisa. Kitabu cha Ufunuo kinaanza na mfululizo wa meseji za ujumbe kwa makanisa saba. Meseji hizi zinaonyesha umuhimu wa jamii katika kanisa la mahali pamoja ndani ya muundo mkubwa wa mwili wa Kristo. Lakini huu siyo mwisho wa msisitizo wa kitabu cha Ufunuo kwa Kanisa.

Jamii ya watu 144,000 iiyokombolewa inaweza kuwa ni uwakilishi wa Kanisa zima, ambalo ni mwili wa Kristo.[522] Baadaye katika kitabu hicho, kanisa linaonekana kama ni bibi harusi wa Mwanakondoo.[523] Kanisa ni kipengele muhimu sana cha kuzingatia katika kitabu cha Ufunuo.

Kama hivi ndivyo kweli, kuabudu kwetu na ushirika kama kanisa hapa duniani ni maandalizi ya kuabudu na kuwa katika ushirika kama kanisa la mbinguni. Hii inamaanisha nini katika maisha yetu kama Kanisa la leo?

► Kama kitabu cha Ufunuo, ni picha ya bibi harusi wa Kristo, ni kwa jinsi gani kuonyeshwa kwa kanisa kutaathiri maisha ndani ya kanisa? Au niulize kwa njia nyingine – Ni kwa njia gani kanisa lako *linafanania* na kanisa lililoko katika kitabu cha Ufunuo? Ni kwa njia gani kanisa lako *halifananii* na kanisa lililoko katika kitabu cha Ufunuo?

Tukio moja la kivitendo la ukweli huu ni kwamba maisha yetu matakatifu yanashabihiana kwa ushirika na kanisa. Katika ulimwengu wa sasa wa mambo ya kibinafsi, Wakristo wengi wanafikiri juu ya wokovu tu katika misingi ya ubinafsi, na uzoefu wa binafsi.

Hata hivyo, wakati kuna mifano ya watu binafsi kama Henoko wakitembea pamoja na Mungu peke yake, kuna mifano mingi ya watoto wa Mungu waliotembea na Mungu ***kama sehemu ya mwili*** wao. Sheria za usafi katika Israeli zilikuwa ni kwa ajili ya "watu wa Mungu." Israeli ilikuwa ni zaidi ya kundi la watu binafsi; ilikuwa ni mwili ulioungana pamoja ukiakisi sura ya Mungu.

Kanisa la Agano Jipya lilikuwa ni zaidi ya kundi la watu binafsi waliotokea kuhusika katika kilabu "moja." Kanisa lilikuwa – na ni - mwili wa Kristo. Watakatifu wa kitabu cha Ufunuo walikumbana na kuifia dini kama sehemu ya mwili wa Kristo. Hata ilipobidi kufa kama mtu binafsi, waljijua kwamba wao ni sehemu ya Kanisa la ulimwenguni kote. Watakatifu wa kitabu cha Ufunuo waliyaishi maisha matakatifu kamasehemu ya mwili wa Kristo. Ni sehemu ya bibi harusi aliye msafi. Hata wakati Yohana alipofungwa katika kisiwa cha Patmo, alijua wazi kwamba yeye ni sehemu ya kanisa la ulimwenguni kote.

Imekuwa ni jambo la kawaida kusikia watu wakisema, "Nampenda Yesu, lakin silipendi kanisa." Hii inategemea kutokuelewana kwa kiwango cha kutisha cha kanisa! Kama Kanisa ni bibi harusi wa Kristo, ni ***lazima*** nilipende Kanisa. (Kama mume wa mtu, sitapendezwa sana na mtu anayeniambia kwamba, "Nakupenda wewe – lakini simtaki mke wako.") Kanisa ni mkusanyiko wa waamini wanaokua pamoja katika mfano wa Mungu.

---

[522] Ufunuo 7:4-8; 14:1-5. Watafsiri wanatofautiana kwenye utambulisho wa watu 144,000. Wengine wanaiona namba hii kama namba ya kawaida ya hesabu ya Wayahudi kabla au baada ya dhiki kuu. Wengine wanaiangalia hii kama alama ya Kanisa. Pamoja na hayo, kwa sasa ni mwili wa Kristo unaojumuisha watu, "Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu" (Ufunuo 7:9).

[523] Ufunuo 19:7-8

> “Wakati mtu anapofikiri kwamba kuyakuza maisha ya utakatifu ni lazima awe peke yake pamoja na Mungu, mtu huyo hawafai tena watu wengine.”
> - Oswald Chambers

Hatujaumbwa ili tuishi peke yetu. John Wesley alisema, “Utakatifu wote ni utakatifu wa Jamii.” Alimaanisha kwamba tunakua kama sehemu ya mwili. Huo ulikuwa ni msukumo kwa makundi ya Wamethodisti; walisaidia katika kuweka msukumo wa ukuaji wa kila mwanachama wao.

Hii inamaanisha nini kwetu leo? Watu watakatifu ni sehemu ya kanisa takatifu. Tunaukulia utakatifu kama sehemu ya mwili ulio mtakatifu. Wakati ninapokuwa katika kujitahidi sana, Mungu humleta kwangu mwenzangu ambaye naye anapambana kuupata utakatifu ili anitie moyo katika yale maeneo ambayo mimi ni mdhaifu. Kwa upande mwingine, wakati Mungu amenipa msaada katika eneo fulani, mimi nami naweza kumtia moyo ndugu ambaye bado ni mdhaifu. Maisha ya utakatifu yanakusudiwa yawe kwenye jamii ya waamini waliojazwa Roho Mtakatifu wanaoufanya upendo wa Mungu udhihirike katika dunia yetu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alilielewa jambo hili vyema:

> Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.[524]

Kuwatia moyo Wakristo wanaoteswa ili waweze kuendelea kudumu katika Imani anasema, “Tukaangaliane sisi kwa sisi” wakati wa kukutanika pamoja na kutiana moyo mmoja kwa mwingine. Toleo la Biblia ya King James linatumia maneno haya, “Kuchochea mtu mwingine kupenda na kufanya kazi njema.” Sehemu kuu ya utendaji ya Kanisa ni kumtia moyo kila mshirika kuzama zaidi kwenye upendo na utakatifu.

Wakati unapojihisi “hauko kwenye utakatifu” mruhusu Mungu akutie moyo wa kuendelea kukua kupitia Mkristo mwenzako katika mwili wa Kristo pale ambapo amekuweka ukae. Wewe ni sehemu ya “Kanisa la ulimwenguni kote” lakini pia ni sehemu ya jumuiya ya kanisa la mahali pamoja pale ulipo. Mungu amekuweka pale kwa makusudi maalumu. Ruhusu waumini wenzako wachochee ukuaji wako katika maisha ya utakatifu.

## Aliipata Siri – Fanny Crosby

Wakati Fanny Crosby[525] alipokuwa na umri wa miezi miwili, alipata upofu wa kudumu kutokana na makosa ya madaktari. Miezi michache baadaye, baba yake alifariki. Mama yake ilibidi aiache familia yake kwa masaa mengi akiwa anafanya kazi kama mjakazi. Fanny aliyajua matatizo ya maisha katika ulimwengu uliolaanika kwa dhambi.

Nyimbo za Fanny Crosby zilidhihirisha uwajibikaji wake kwa Kristo. Alikuwa ameyasalimisha kabisa mapenzi yake kwenye mapenzi ya Mungu. Katika utenzi wake

[524] Waebrania 10:24-25
[525] Image: "Francis Jane Crosby, 1820-1915" by W.J. Searle, retrieved from the Library of Congress Prints and Photographs Division, http://hdl.loc.gov/loc.pnp/cph.3b17084, "no known restrictions."

mzuri, Bi. Crosby aliomba kwamba mapenzi yake yazamishwe ndani ya mapenzi ya Mungu yaliyo makamilfu.

> Niweke wakfu sasa kwenye kazi yako, Bwana.
> Kwa nguvu ya neema yako ya kimungu,
> Ruhusu roho yangu ikuone kwa tumaini lililo thabiti,
> Na mapenzi yangu yashindwe katika wewe.



Fanny Crosby alielewa kwamba utakatifu ni upendo mkamilifu kwa Mungu na kwa jirani yetu. Aliutumia muda wake na fedha zake kwenye umisheni kwa ajili ya walevi na wasio na makazi. Yeye na mume wake walitoa kila kitu ambacho kilikuwa ni muhimu kwa ajili ya wao kuweza kuendelea kuishi. Alimpenda Mungu na jirani zake. Siku hadi siku, Fanny Crosby aliendelea kukua katika kumfanania Kristo na upendo mkamilifu.

Fanny aliiangalia kwa matumaini siku ya ahadi ambayo, "Watauona uso wake" itatimilika. Wakati ikitokea mtu kumwonea huruma katika hali aliyokuwa nayo, Fanny Crosby alikuwa anajibu kwamba anaifurahia hali yake ya kuwa kipofu kwa sababu, "Nitakapoingia mbinguni, uso wa kwanza utakaofurahia kuuona upofu wangu ni ule wa Mwokozi wangu. Nitamwona uso kwa uso."

**Mwokozi wangu kwanza – Fanny Crosby**

Wakati muda wangu wa kazi utakapomalizika,
na nitakapovuka wimbi la maji kujaa na kupwa
Wakati nitakapoiona asubuhi inayong'ara na ya utukufu;
Nitamjua Mkombozi wangu wakati nitakapokuwa nimevuka ng'ambo ya pili,
Kicheko chake kitakuwa cha kwanza kunilaki mimi.

Kupitia katika malango ya jiji na nguo nyeupe isiyokuwa na madoa,
Ataniongoza mimi hadi mahali ambapo hakutakuwa na kulia kwa machozi tena;
Katika wimbo wa furaha wa nyakati zote nitajichanganya kwa furaha;
Lakini matamanio yangu ni kumwona Mwokozi wangu kwanza.

## Tafakuri ya Somo la 11

(1) Utakatifu ni ushirika na Mungu usiovunjika.

(2) Kuanzia kitabu cha Mwanzo 3 hadi Nyaraka za Mitume, Mungu anaahidi kurejesha tena ushirika wa karibu kati ya Mungu na mwanadamu. Ahadi hii imetimilika katika kitabu cha Ufunuo.

(3) Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha watu watakatifu katika ushirika usiovunjika na Mungu mtakatifu.

(4) Ushirika wa Kanisa ni maandalizi ya ushirika wa mbinguni. Kanisa la hapa duniani ni mfano wa kanisa litakalokuwepo wakati wa umilele. Kwa sababu hiyo, ni lazima tutafute sana kuweka maisha ya ushirika wa kanisa la hapa utakaofanana na ule wa kanisa la kule mbinguni.

## Kazi ya Kufanya

(1) Jaribu kufikiria mtu anakuambia, "Nampenda Yesu, lakini siyo Kanisa." Andika barua ya kurasa 1-2 ukimwonyesha huyu mtu kwamba kumpenda Yesu ni lazima kuelekezwe katika kumpenda Bibi harusi wa Bwana Yesu, ambaye ni Kanisa. Onyesha ni kwa jinsi gani moyo wa utakatifu utakavyoweza kuhamasisha upendo kwa ajili ya kanisa la Mungu. Onyesha ni kwa jinsi gani kuwa sehemu ya kanisa kunavyoweza kutusaidia sisi katika kuukulia utakatifu.

(2) Anza kikao kinachofuata cha darasa kwa kunukuu Ufunuo 21:2-3.

# Somo la 12
# Je, Maisha Matakatifu Yanawezekana?

## Malengo ya Somo

Hadi kufikia mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua kwamba agizo la Mungu la utakatifu linatimizwa katika ahadi yake ya kutufanya sisi tuwe watakatifu.

(2) Kujisalimisha kabisa kwa Wito wa Mungu wa utakatifu.

(3) Kujihusisha katika ukuaji wa kila siku katika utakatifu.

(4) Kukariri 1 Wathesalonike 5:23-24.

## Paulo: Mtu aliyeutumainia Utakatifu

Fikiria kuhusu mazungumzo na Sauli, wa Tarso katika mwaka 34 B.K.[526] Uliza, "Je, wewe ni mtakatifu?" Sauli angejibu, "Ndiyo, mimi ni mtakatifu! Nilitahiriwa kwa mujibu wa sheria. Mimi ni Farisayo. Mimi ni mwenye kuishika sheria. Mimi ni mwenye haki." Sauli alijiona kwamba yeye ni mwenye haki kwa sababu ya umakini wake katika kuitii sheria. Alijaribu kupata upendeleo wa Mungu kupitia matendo mema.

Lakini akiwa njiani kwenda Damaskasi, Sauli alikutana uso kwa uso na Bwana mfufuka. Alijifunza kwamba haki yake ni sawa na matambara machafu. Hakupingana na mwalimu ambaye siyo wa uongo, bali Masihi wa kweli. Ameshindwa kutii sheria iliyo kamilifu ya upendo kwa Mungu na jirani yake. Akiwa njiani kwenda Damaskasi, Sauli aliipata njia nyingine ya kumpeleka kwenye utakatifu: "…nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa Imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa Imani."[527]

Tafakari kuhusu mazungumzo na Sauli, mwaka 60 B.K. "Paulo, sasa unajua kwamba njia pekee ya kupata haki ya kweli ni kwa Imaniiliyo katika Kristo. Je, hii haimaanishi kwamba unaweza kuwa mtakatifu? Je, Ina maana kwamba Kristo atakuhesabia mtakatifu hata kama wewe ni mtenda dhambi?"

Paulo angejibu kwa mshituko. "Hilo ni kosa! Haki inapatikana kwa Imani iliyo katika Kristo – lakini Mungu hatuachi sisi katika hali ya dhambi aliyotukuta nayo. Soma ushuhuda wangu. Lengo langu ni 'ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake.' Lengo langu ni kumfanania Kristo. Wokovu kwa Imani hautupi sisi kibali cha kuishi maisha ya dhambi; wokovu kwa Imani unatupa

[526] Wafilipi 3:4-6
[527] Wafilipi 3:9

sisi nguvu ya kumfanania Kristo. Mungu wa upendo huwawezesha watoto wake kuishi maisha ya utakatifu kupitia Roho aliyeko ndani yetu!"[528]

► Fanya mapitio ya mambo ambayo umejifunza kuhusiana na utakatifu. Je, unayo taswira halisi ya uzuri wa utakatifu? Je,unaamini kwamba haya maisha ya utakatifu yameahidiwa kwa wana wa Mungu?

## Je, Maisha ya Utakatifu Yanawezekana?

Katika kozi hii, tumeona wamba Mungu huwaagiza watu wake wawe watakatifu. Lakini watu wengi husoma maagizo ya Mungu kujibu kwamba, "Hilo haliwezekani. Siwezi nikawa mtakatifu." Je, Wakristo wanapaswa kuishi maisha ya kushindwa kila siku na matumaini ya kuchanganyikiwa? Je, tushindwe kufurahia maisha ya utakatifu aliyotupa Mungu? Au je, tunaweza kufurahia kusudi kuu la Mungu kwa ajili ya watu wake?

### Neno la Mungu linathibitisha kwamba Maisha ya Utakatifu yanawezekana

Kutokea wakati wa Henoko hadi kuongoka kwa mataifa wa Thesalonike, Biblia inafundisha kwamba maisha ya utakatifu yanawezekana.

Katika kitabu cha Walawi na kitabu cha 1 Petro, Mungu anaamrisha, "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu."[529] Hakuna mahali popote ambapo Mungu ametoa maagizo akaacha kutoa na maagizo ya utiifu. Mungu ni Baba wa upendo ambaye hawezi kuwachanganya watoto wake na maagizo yasiyowezekana. Wakati tukiwa hatuna uwezo wa kuyatii maagizo yake kwa nguvu zetu wenyewe, neema ya Mungu hutupa sisi nguvu za kutii maagizo ya Mungu.

Profesa Bill Ury anasema, "Amri au maagizo yanaonyesha picha ya Mungu ni nani na ahadi ya jinsi ambavyo tunaweza kuwa."[530] Agizo hili kwamba, "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" inaonyesha kwamba Mungu ni nani; ni Mungu aliye mtakatifu. Agizo hili pia linaonyesha kwamba tunaweza kuwa; na tunaweza kuwa watakatifu.

### Wakristo kwa wakati wote wa Historia wamedhihirisha kwamba Maisha ya Utakatifu yanawezekana

Wakristo katika kila kizazi wamegundua hilo kwamba maisha ya utakatifu ni upendeleo kwa watoto wa Mungu. Watu kutoka katika kila mfumo wa maisha wameiona furaha ya kukaa kwenye uwepo wa nguvu za Roho Mtakatifu. Wameiona amani inayopatikana kwa kumpenda Mungu kwa moyo usiogawanyika na kuwapenda jirani zao kama wanavyojipenda wenyewe.

[528] Wafilipi 3:10
[529] Walawi 19:2; 1 Petro 1:15-16
[530] Mawasiliano ya Email, June 27, 2016

**Njaa ya Mungu kwetu ya Utakatifu inadhihirisha kwamba Maisha ya Utakatifu yanawezekana**

Kila muamini anaona njaa ya ndani sana ya kutembea na Mungu. Wakristo wa kweli wanataka watembee kwa ukaribu sana na Baba yao. Wakristo wa kweli wanataka wawe kama alivyo Kristo. Mungu amepandikiza ndani ya mioyo ya watoto wake njaa ya kutaka mahusiano ya kina na yeye mwenyewe. Tunaweza kuwa na uhakikisho kwamba Mungu wa mbinguni wa upendo hawezi akaleta njaa bila ya kutoa njia ya kuimaliza njaa hiyo. Utakaifu ni upendeleo wa furaha kwa kila muamini.

## Je, Moyo Mtakatifu ni kwa ajili yako?

Miaka mingi iliyopita, kulikuwa na mtu mmoja aliyewania kuivuka bahari kwa njia ya meli. Aliwekeza fedha zake kwa miaka mingi hadi zikafikia kununua tiketi. Baada ya kuwa ameilipia tiketi, alibakiwa na fedha kidogo. Alikuwa amesikia kuhusu vyakula vizuri vitamu vinavyopatikana ndani ya meli za baharini, lakini alijua pia kwamba vyakula hivyo vitakuwa ni vya gharama kubwa. Ili kuokoa fedha, mtu huyu alinunua mkate na siagi akaviweka kwenye mkoba wake wa safari.

Kila siku abiria walipokuwa wakiaenda kwenye chumba cha chakula, mtu huyu alikuwa anaingia chumbani mwake na kula mkate wake na siagi. Alikuwa na furaha kuwepo kwenye meli, lakini mara nyingi alikuwa akitamani kama angeweza kula vile vyakula vizuri vinavyopatikana kwenye kile chumba cha chakula. Kwenye siku ya mwisho ya safari, yule mtu aliamua angalao akale mlo mmoja kwenye kile chumba cha chakula. Alikusanya kila senti aliyokuwa amebakiwa nayo, akitegemea  kwamba zitatosha kulipia mlo mmoja. Kwa mshangao wake, mhudumu aliuliza, "Wewe ulikuwa wapi? Tumekuwa tukikuandalia meza yako kwa wiki yote! Bei ya chakula imeingizwa kwenye bei ya tiketi yako. Bei ni tayari ilishalipwa."[531]

Wakristo wengi wamefanana na huyu mtu maskini. Furaha ya maisha, amani ya kuishi kwa kujisalimisha kabisa kwa Mungu, na ushindi wa kuishi katika nguvu za Roho Mtakatifu – vyote vilishatolewa kupitia kifo cha Yesu pale msalabani. Kristo alilipa gharama zote, lakini tunaishi chini ya viwango vya fadhila hizo.

Kama moyo mtakatifu utapatikana kwa kila mwamini, ni kwa nini Mkristo ashindwa kufurahia fadhila hizi? Mara nyingi tumekuwa tukimruhusu Shetani kutudanganya katika kuyaelewa mafundisho ya Biblia. Uongo wa Shetani umetuondoa katika kufurahia fadhila za Mungu alizozikusudia kwa ajili ya watoto wake.

[531] Kisa hiki kimechukuliwa kutokakitabu cha John N. Oswalt, *Called to be Holy* (Nappanee: Evangel Publishing, 1999), 149-150

**"Moyo wa Utakatifu Hauwezekani"**

Wakristo wengi wanafikiri kwamba moyo wa utakatifu hauwezekani. Wanasoma maagizo na ahadi katika Maandiko, lakini wanafikiri kwamba, "Hiyo ilikuwa ni sawa kwa Ibrahimu, lakini kamwe siwezi kuwa 'rafiki wa Mungu.'"

Baadhi ya wale wanaosema, "Moyo wa utakatifu hauwezekani" wanazungumza kutoka kwenye uzoefu mchungu sana. Wamejaribu kuishi maisha ya utakatifu – lakini wameshindwa. Inawezekana walifuata sheria za nje zilizoambatana na utakatifu; Inawezekana wamejaribu kutawala tabia za dhambi na matendo yanayoharibu nidhamu binafsi; inawezekana hata wametoa ushuhuda wa moyo safi. Kwa sasa, wameamua kwamba haiwezekani "kuwa mtakatifu kama Bwana wetu alivyo mtakatifu."

Tafakari juu ya mtu anayejaribu kujifunza lugha za ndege. Anafanya majaribio hadi atakapoweza kutoa mlio unaofanana na kasuku. Amekuwa mzuri kiasi kwamba jirani atadhania ni mlio wa kasuku. Lakini huyu mtu siyo ndege! Anaweza akaigiza sauti zao, lakini hajui sauti hizo zinamaanisha nini. Ana uwezo uwezo wa kuigiza sauti, lakini hajui ndege anakuwa anajisikiaje anapotoa mlio wake wa sauti. Mtu huyu ana matendo ya nje; hana uhalisia wa kweli wa ndani.

Wakristo wengi wamejifunza lugha na hata matendo ya mtu mtakatifu. Wanayasema maneno, lakini hayana uzoefu ndani ya mioyo yao. Wamefanya matendo ya nje kuwa mbadala wa uhalisia wa mambo ya ndani. Kwa muda mfupi sana huwaongoza kwenye kukataa tamaa na kuchanganyikiwa.

Ni nini jibu la uongo wa Shetani kwamba, "Moyo wa utakatifu hauwezekani"? Tunapaswa tuwe na Imani katika ahadi za Mungu. Tunapaswa kuamini kwamba Mungu wetu wa upendo atatupa nguvu za kuweza kutii maagizo yake.

Ndiyo, wewe na mimi ni viumbe tuliotengwa ambao kamwe hatuwezi kufikia kiwango cha ukamilifu wa Mungu. Lakini Mungu alituagiza, "Iweni watakatifu." Mbali na asili yetu ya anguko, tunaweza kumwamini Mungu wetu mwema kutupa neema na nguvu vitakavyotuwezesha kuyatii maagizo yake.

**"Sina Njaa ya Moyo wa Utakatifu"**

Kwa masikitiko, wako watu wanaodai kwamba wao ni Wakristo lakini kabisa hawana njaa ya utakatifu. Wanadai kuwa Wakristo, lakini wana nia kidogo sana au hawana kabisa nia ya kukua katika mfano wa Kristo.

Jimmy anajishuhudia kwamba yeye ni Mkristo, lakini anaonyesha ana shauku kidogo sana na maisha ya utakatifu. Anaendelea kufanya dhambi za kujitakia; anaishi kama vile alivyokuwa mwanzoni kabla hajamkiri Kristo. Tulipomtembelea, Jimmy alitaja baadhi ya watu ambao walikuwa makini na waangalifu katika maisha wanayoishi. Tabia zao zilikuwa za upendo; matendo yao yanaonyesha nia ya kutaka kumpedezesha Mungu. Walikuwa na mioyo na mikono ya utakatifu.

Jimmy alitoa maoni yake kuhusu njaa yao ya kuutaka utakatifu kisha akasema, “Sijali kuhusu kuwa mtakatifu. Mchungaji wangu aliniambia kwamba, kama nilishatubu dhambi zangu, na kumwamini Yesu kama Mwokozi wangu, nitaenda mbinguni. Kwenda mbinguni ndicho kitu ninachojali tu. Sihitaji kitu kingine zaidi ya hicho!”

Tatizo la Jimmy ni nini? Hana njaa ya utakatifu. Sina shaka kwamba Jimmy ana uelewa mdogo sana kuhusu ni nini maana ya kuwa Mkristo. Mtu yeyote aliyezaliwa mara ya pili atapenda sana kumfanania Kristo. Mkristo wa kweli anapaswa awe na njaa ya moyo wa utakatifu.

Jibu ni nini kama wewe huna njaa ya moyo wa utakatifu? Inawezekana ni kweli umezaliwa mara ya pili, lakini umekuwa ukisumbuliwa na tabia na mazoea ya nyuma, umejichanganya na wanafiki wanaojidai kwamba wao ni watakatifu, au hujawahi kukutana na fundisho la moyo wa utakatifu katika Maandiko. Kama ndivyo, msihi Mungu akupe njaa ya moyo wa utakatifu.

**“Mimi ni Mtakatifu wa Kutosha”**

Labda uongo wa hatari zaidi tunaoweza kujiambia wenyewe ni, “Mimi ni mtakatifu wa kutosha.” Watu wengine wanajiaminisha kwamba wao ni watakatifu kwa sababu ya jinsi wanavyovaa, ushiriki wao katika kanisa, au wawapo na “karama ya kiroho.” Ninapojiridhisha mimi mwenyewe katika hayo kwamba, “Mimi ni mtakatifu wa kutosha,” hakuna ongezeko lingine tena la kukua katika utakatifu.

Alama isiyoweza kukosewa ya kumtambua mtu mtakatifu ni hamu yake ya kutaka kukua katika utakatifu. Sijawahi kuona mfano wowote au mahali popote katika Maandiko au historia ya Kanisa ya mtu mtakatifu anayesema, “Mimi ni mtakatifu wa kutosha.” Jinsi mtu anavyozidi kukua katika kumfanania Kristo, kwa kiwango hicho hicho anazidi kuwa na njaa ya kukua zaidi.

Mwanamume au mwanamke anayetembea karibu na Mungu husema, “Nina furaha katika kutembea kwangu na Mungu, lakini nataka niendelee kutembea naye karibu zaidi!” Mtu mtakatifu hufurahia kuwa na ushirika na Mungu, lakini hutafuta hata na zaidi jinsi ya kuwa na uhusiano wa ndani kabisa na Mungu. Anafurahia anavyozidi kukua katika kumfanania Kristo, lakini pia huomba kwamba Mungu aendelee kumfanya afanane zaidi na Kristo.

Jibu ni nini kwa ukiri dhaifu wa utakatifu? Kama umejidanganya mwenyewe kwa kujiridhisha, jibu ni udhalilishaji mbele ya utakatifu wa Mungu aliye mkamilifu. Kama utauangalia utakatifu wake mkamilifu, kamwe hutakaa uridhike na ukiri dhaifu wa utakatifu. Wakati Isaya “alimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana,” alitambua hitaji lake binafsi la utakatifu:

> Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi![532]

Wakati Isaya alipouona utukufu kamili wa Mungu, alitambua uhitaji wake binafsi wa utakaso. Tiba ya ukiri dhaifu wa utakatifu ni kuwa na uelewa wa kina kuhusu Mungu. Tunapomwona Mungu, tunajiongezea njaa ya kuwa na moyo wa utakatifu. Tunapozidi kumwona Mungu, ndio vivyo hivyo tunavyozidi kuwa na hamu ya kutaka kuwa kama yeye.

## Njia ya Kuuelekea Utakatifu

Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanywa kuwa kama Kristo? Unawezaje, wewe kama mwamini mwenye hamu ya kujazwa na utimilifu wote wa Mungu, karama hii ya ajabu? Njia ya kuelekea kwenye moyo wa utakatifu ni ipi?

Hatuhitajiki kupambana sana katika kutafuta njia ya kuuelekea utakatifu. Neno la Mungu latosha kuonyesha njia ya kuelekea maisha ya utakatifu.

### Utakaso wa Awali

Kuanzia tu unapozaliwa upya, Roho Mtakatifu amekuwa akiishi ndani yako.[533] Kwa papo hapo, ulihama kutoka gizani na kuingia kwenye nuru. Kuanzia hapo, Agano Jipya linakutambua kama "Mtakatifu."

Ingawaje unaweza ukapambana na majaribu, Roho Mtakatifu anakupa ushindi wa kila siku dhidi ya dhambi za makusudi. Watu wanaokuzunguka wameona mabadiliko yako kwa jinsi unavyoishi katika maisha mapya ndani ya Kristo. Furahi kwa kile Mungu alichofanya!

### Kukua katika Utakaso

Kwa jinsi unavyokuwa unamfuata Kristo, Roho Mtakatifu anabadilisha roho yako ya ndani. Jinsi "unavyoenenda kwa Roho," wala "hautazitimiza kamwe tamaa za mwili."[534] Majaribu ya zamani yanasalimu amri juu yako. Utiifu kwa Mungu unakuletea furaha isiyoisha.

Hata hivyo, utakutana na maeneo ya kupambana. Unamtii Mungu, lakini wakati mwingine kuna mapambano kati ya maagizo ya Mungu na matamanio yako ya ndani. Kuna mapambano kati ya kile ambacho Mungu amekuamuru na mapenzi yako ya ubinafsi. Utaona vigumu sana kumpenda Mungu kabisa na kumpenda jirani yako. Unaanza kujitambua kwamba una "moyo uliogawanyika."

[532] Isaya 6:1, 5
[533] Warumi 8:1-2, 9-11
[534] Wagalatia 5:16

## Usafi wa Moyo

Jinsi Mungu anavyodhihirisha maeneo ambayo unayahitaji kwa ajili ya kujiweka msafi kwa kina zaidi, utaanza kusikia njaa ya ahadi iliyoko katika kitabu cha 1 Wathesalonike 5:23. Utatafuta kujua ukweli wa maombi ya Paulo, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase ***kabisa***." Utaanza kumwuliza Mungu, "Je, kunalo jambo la zaidi unalotaka kunifanyia katika maisha yangu? Je, naweza kufanywa kuwa msafi? Je, matamanio yangu ya ndani yanaweza kubadilishwa upya hadi kwenye kiwango ambacho sitaweza kupambana tena katika kukutii wewe kabisa?"

Wakristo kwa nyakati zote za historia wameomba sana Mungu awape moyo ulio msafi. Kulingana na 1 Wathesalonike 5:23, wako wachache waliotumia jina "utakaso wote" kwa ajili ya uzoefu huu.[535] Wengine wameuita "maisha ya kina zaidi." John Wesley alitumia jina "upendo kamili." Bila kujali maneno yaliyotumika hapa, hii ni kiu ya asili ya mtoto wa Mungu anayetaka kukua katika kumfanania Kristo.

Unapokuwa unaomba kwa ajili ya usafi huu wa ndani sana, unawea kukutana na maeneo matatu ambayo Mungu atakuongoza. Hii siyo hukumu kama ile uliyokuwa unajisikia kama mtu asiyeamini; wewe sasa ni mtoto wa Mungu! Badala yake, haya ni maeneo ambayo Mungu anakuitia kwa ajili ya moyo wa utakatifu.

### *Mungu atakuita kwa ajili ya utiifu wote*

Baadhi ya waumini wanapambana kutafuta moyo wa utakatifu kwa sababu bado wanapambana na maeneo mengine ya ukosefu wa utiifu. Hatuwezi kutembea kwenye mahusiano ya karibu na Mungu isipokuwa tumetembea katika utiifu.

Hakuna Mkristo wa kweli anayeishi katika uasi wa kujitakia kinyume na maamrisho ya Mungu. Hata hivyo, Wakristo wengi wamepata upenyo wa kusamehe au kuacha (hata kwa ajili yao wenyewe) maeneo mengine ya uzembe. Hawatakaa waseme, "Mungu, sitakutii wewe," lakini husema, "Mungu, sidhani kama hili ni muhimu sana kulitilia maanani." Kwa kutojali, wanadharau maeneo mengine ambayo wangepaswa kuwa watiifu. Kama tunahitaji kuwa watu watakatifu ambao Mungu anawaita watu wake, ni lazima tumtii Mungu katika ***kila*** eneo**.**

Kama watu tulioanguka, tunajidanganya hata wenyewe kuhusu kina cha uovu wetu. Kwa sababu ya hii, mtunga Zaburi aliomba:

> Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele![536]

---

[535] "utakaso wote" ni maana nyingine ya neno "mkamilifu" neno lililotumika katika 1 Wathesalonike 5:23. Haina maana ya "ukuaji mkamilifu;" ina maana ya usafi uliokamilika na utakaso.
[536] Zaburi 139:23-24

Mtunga Zaburi aliomba kwamba Mungu amchunguze na aujue moyo wake. Alijua kwamba hatuna uwezo wa kuyajua yote yaliyomo katika mioyo yetu wenyewe. Lakini kwa jinsi tunavyoendelea kutafuta "kujazwa na utimilifu wote wa Mungu," tutaomba kwamba Mungu atufunulie kila njia inayohusika na asili yetu ya dhambi.

Daudi aliomba, "Unitakase na mambo ya siri."[537] Alijua kwamba tunaweza kuficha ukweli wa dhambi zetu hata kutoka ndani yetu sisi wenyewe. Ni Mungu peke yake anayeweza kuangazia mwanga ndani ya mioyo yetu kwa ajili ya dhambi za siri zilizojificha humo.

Unapotafuta kuwa na moyo msafi, utaona kwamba Mungu atakufunulia maeneo ambayo tabia zako na matendo yako haziakisi sura yake. Kwa kuwa unataka umfananie Kristo, kwa hiari yako mwenyewe utayakiri maeneo haya na kutii wito wa Mungu wa kuwa mtiifu kabisa.

### *Mungu atakuita uusalimishe moyo wako*

Unapotafuta kuwa na moyo safi, Mungu atakuita usalimishe kila kipengele cha maisha yako. Hii ni zaidi ya kusema "Hapana" kwa majaribu kutoka nje. Hii ni kujitakasa kamili kwako mwenyewe kwa ajili ya Mungu. Ni kujisalimisha mapenzi yako kwa ajili ya mapenzi ya Mungu.

Paulo aliwaita Wakristo pale Roma kujitoa wenyewe miili yao "iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu."[538] Hawa walikuwa ni Wakristo waliokuwa wakiishi kwa kumtii Mungu, lakini Paulo aliwaita kwenye kujisalimisha kabisa kwa Mungu. Paulo aliwaita kwa kusudi la kusema "ndiyo ya milele" kwa Mungu. Aliwaita wajisalimishe kabisa.

Oswald Chambers alionyesha umuhimu wa kujisalimisha kabisa kwa ajii ya kusudi la Mungu.

> Ili kuwa pamoja na Yesu Kristo, mtu hatapaswa tu kuachana na dhambi, lakini pia atapaswa asalimishe mfumo wake wote wa jinsi anavyoyatazama mambo. Kuzaliwa upya na Roho wa Mungu inamaanisha kwamba ni lazima kwanza tuachilie mambo mengine ili kuingiza vitu vingine….
>
> Kwenye kila hatua ya utaratibu huu, tutapaswa tuachane na malalamiko yetu kwa ajili ya haki zetu wenyewe. Je, tuko tayari kusalimisha ufahamu wetu katika vile vyote tunavyovimiliki, matamanio yetu, na kitu kingine chochote katika maisha yetu? Je, tuko tayari kutambuliwa na kifo cha Yesu Kristo?

"Mgogoro mkubwa uliopo kwenye maisha ya Kikristo ni kusalimisha kabisa mapenzi yetu."
- Oswald Chambers

[537] Zaburi 19:12
[538] Warumi 12:1

> …Amua kusonga mbele katikati ya mgogoro, ukisalimisha vyote ulivyo navyo na wewe mwenyewe jinsi ulivyo kwake. Na Mungu atakuwezesha wewe kufanya yale yote anayotaka kutoka kwako.[539]

George Matheson alikuwa mchungaji Mskoti wa kanisa la Presibiteri aliyejitambua kwamba ndani ya moyo wake kulikuwa na upinzani mkubwa dhidi ya mapenzi ya Mungu. Alikuwa na njaa ya moyo usiogawanyika ambao ungejitoa kwa hiari kabisa kwa Mungu. Aliomba maombi haya kwa ajili ya kujisalimisha:

> Nifanye mateka wako, Bwana, na kisha niwe huru. Nilazimishe niachane na upanga wangu, na nitakuwa mshindi. Ninazama kwenye kengele za maisha wakati mimi mwenyewe nimesimama; Nizuie mikononi mwako, na mikono yangu itakuwa na nguvu.[540]

Matheson alitambua kwamba katika kujisalimisha kabisa, tunapata ushindi. Tunapojitoa wenyewe kama mateka kwa Mungu, anatuweka huru kutoka katika vifungo na dhambi. Tunapokuwa wadhaifu, anatujaza nguvu. Tunaupata ushindi wetu mkuu tunapofikia kwenye hatua ya kujisalimisha kabisa kwa Mungu.

### *Mungu atakuita umtii yeye kwa Imani*

Kama umejisalimisha kabisa kwa Mungu, unaweza kumwamini yeye katika "kukusafisha moyo kwa Imani."[541] Tunafanywa watakatifu kwa neema kupitia Imani.

Kama mwenye dhambi, ulikuja kwa Kristo ukiwa huna chochote. Ukajitupa mwenyewe kwenye neema yake. Kwa Imani, ukakubaliana na wokovu wake wa bure, na akakufanya kuwa kiumbe kipya.

Kwa njia hiyo hiyo, utakapokuwa na njaa ya moyo wa utakatifu, ni lazima uende kwa Yesu kwa Imani. Mungu aliyekuita wewe katika utakatifu atakufanya uwe mtakatifu. Unaweza ukaamini kwamba ahadi yake ni kwa ajili yako. Maombi ya Paulo, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa." Inaweza kuwa kweli katika maisha yako. Unaweza ukasadiki ahadi za Mungu. "Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya."[542]

## Isaya 6 – Kisa cha Kutakaswa

"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu," malaika walikuwa wakisema, wakati huo Isaya akiwa anatetemeka! Isaya alihitaji kujiona mwenyewe kama "mchafu" kabla ya Mungu mtakatifu kumwamini kwa ajili ya roho ya taifa.

---

[539] Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (March 8 entry). Accessed from https://utmost.org/the-surrendered-life/ on March 28, 2020.
[540] Imepatikana kutoka https://library.timelesstruths.org/music/Make_Me_a_Captive_Lord/ June 1, 2020.
[541] Matendo 15:9
[542] 1 Wathesalonike 5:23-24

Isaya alipojiangalia moyo wake mwenyewe, alisema kwa sauti, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Aliona undani wa asili yake ya dhambi. Lakini Mungu hakumwacha katika hali hii ya kutisha.

> Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu; akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, "Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa."

Utakaso mara nyingi huwa mchungu. Je, waweza kusikia nyama inayoungua wakati malaika akigusa kinywa cha Isaya kwa kaa la moto? Hii haikuwa neema rahisi; utakaso haupiti bure bila maumivu.

Hata hivyo, kisa hiki kinafundisha ukweli wa ajabu na unaotia moyo. Tukimruhusu, Mungu atatufanya watakatifu. Kusudi la Mungu halikuwa kwa ajili ya kumtesa Isaya. Kusudi la Mungu lilikuwa ni kumtakasa Isaya. Kusudi la Mungu kwa watu wake linaweza likatimia. Tunaweza kufanywa wasafi.

### Ukuaji Endelevu katika Utakatifu

Paulo aliomba, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa." Kisha akaendelea, "nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo."[543] Kukua kwako katika kumfanania Kristo kutaendelea hadi wakati wa "kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo." Utakapokuwa unaendelea kutembea na Mungu, kama vile katika kioo, utabadilishwa ufanane na mfano wa Mungu.[544] Utakomaa katika utakatifu. Utaendelea kujisalimisha kwa furaha kwenye mapenzi ya Mungu. Utakuwa unaendelea kutembea na kujisalimisha kwa uangalifu kwa Mungu.

Jaribu kufikiri juu ya siku yako ya harusi. Kwenye hiyo ndoa, ulitoa ahadi ya maisha. Hujawahi kujiuliza kila asubuhi, "Je, leo nimeoa? Je, agano la ndoa bado linafanya kazi?" Ulifanya tendo la kudumu. Njia pekee unayoweza kuvunja hilo agano ni kugeuka nyuma na kwenda kinyume na nadhiri ulizofanya wakati wa ndoa yako.

Kila siku ya ndoa yako, unaishi kutokana na maagano uliyoahidi kwenye ndoa yako. Unapokabiliwa na kufanya maamuzi, unachagua kufanya kwa upendo kuelekea mwenzi wako. Ile ahadi ya kudumu uliyokiri unaiishi katika maisha ya kila siku.

Hali kadhalika, kujisalimisha kwako kwa Mungu ni tendo la kudumu. Huhitaji kujiuliza kila siku, "Hivi bado nimejisalimisha kwa Mungu hadi sasa?" Badala yake, kila siku unaishi kutokana na ahadi yako uliyofanya wakati ulipojisalimisha kabisa kwa Mungu.

---

[543] 1 Wathesalonike 5:23
[544] 2 Wakorintho 3:18

Mhubiri maarufu Mskoti, Horatius Bonar, aliandika kuhusu kuendelea kukua kwa mtu mtakatifu.

> Maisha ya utakatifu yanatokana na wingi wa mambo madogo madogo. Maneno machache, siyo hotuba ndefu au mahubiri marefu; matendo machache, siyo miujiza, siyo mapigano, au tendo moja la kishujaa au kuifia dini kunakofanya maisha ya Ukristo yawe ya kweli. Ni mambo madogo madogo ambayo kwayo maisha hukamilishwa.[545]

Haya ndio maisha ya kila siku ya utakatifu. Unaishi maisha ya utakatifu ambayo siyo kwa ajili yako mwenyewe, bali ni katika utimilifu wa Roho Mtakatifu. Maisha ya utakatifu ni kuhusu mahusiano ya upendo usiogawanyika pamoja na Mungu. Ni kuwa na shauku kwa ajili yake. Ni kumtaka yeye awe juu ya mambo yote. Matamanio haya yatakuongoza wewe kuingia katika mahusiano endelevu ya ndani sana na Mungu.

Katika historia ya mwanadamu, mtu amejaribu kuishi bila kumtegemea Mungu. Shetani alimjaribu Hawa kwa ahadi kwamba, "Mtakuwa kama Mungu."[546] Katika Babeli, watu waliamua, "na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina."[547] Katika hali yake ya ubinafsi, mtu anataka aishi maisha ya bila kumtegemea Mungu. Kwa ulinganifu, maisha ya utakatifu ni ya kuishi kwa kumtegemea Mungu kabisa.

Utakatifu ni wa Mungu; wewe na mimi ni watakatifu ***tu*** pale tunapoendelea kuishi kwenye mahusiano na yeye. Kamwe hautakaa ufikie kiwango cha kusema kwamba, "Mimi ni mtakatifu kwa nguvu zangu mwenyewe." Badala yake unapaswa kusema, "Leo, Roho Mtakatifu ananiwezesha nguvu za kuishi maisha ya utakatifu. Leo, ninabadilishwa katika sura yake. Leo, ninamtii Mungu kwa moyo ambao unampenda yeye kabisa. Leo, ninampenda jirani yangu kwa neema ya Mungu. Leo, Roho Mtakatifu ananifanya niwe kile ambacho Mungu alitaka niwe wakati aliponiita." Haya ndiyo maisha ya utakatifu.

### Mambo Kumi ya Vitendo ya Kupalilia Maisha ya Kila Siku ya Utakatifu

Maisha thabiti yenye matunda ya utakatifu yanahitaji kipindi katika maisha cha kuyapalilia na kuyatunza.[548] Kutakaswa kwa moyo siyo mwisho wetu wa kufuatilia utakatifu. Sisi ni sawasawa na marubani ambao tumeiweka ndege yetu kwenye usawa wa barabara ya kurukia ndege, lakini tunahitaji kufanya masahihisho mengi kabla ya ndege kutua.

Kifo cha kiroho kwa Wakristo hadi nafsi ni kifo kilicho ***hai*** – kufa mara kwa mara. Dhabihu yetu ya nafsi ni dhabihu iliyo ***hai*** – dhabihu ya mara kwa mara. Maneno kama "kifo cha nafsi" yapo tu kwa ajili ya kutufundisha kweli za kiroho lakini tunapaswa kuwa waangalifu tusitoke nje ya Neno la Mungu. Kuwa na moyo msafi siyo mwisho wetu wa kuutafuta

[545] Horatius Bonar, *God's Way of Holiness* (Chicago: Moody Press, 1970), 125-126
[546] Mwanzo 3:5
[547] Mwanzo 11:4
[548] Sehemu hii imenukuliwa kutoka katika somo la Rev. Timothy Keep.

utakatifu. Moyo msafi na mapenzi binafsi yaliyosalimishwa vinatuwezesha sisi kusonga mbele, lakini tunao muda katika maisha wa kupanda kileleni!

Maisha yaliyojazwa Roho Mtakatifu ni maisha ya kukua na **utakaso endelevu**. Kwa msaada wa Roho wa Mungu "tunabadilishwa toka utukufu hata utukufu."[549] Ufuatao hapa ni ushauri wa vitendo kwa wale wote walio na matamanio ya kuwa na maisha ya ndani kabisa ya utakatifu.[550]

(1) Endelea kubakia uliyepondeka kiroho.

Maisha ya kweli ya utakatatifu ni yale yenye ***toba ya mara kwa mara***,[551] wakati Mungu akiendelea kutuponya madhaifu yetu na kuturejesha kwenye tabia kamili ya mfano wa Kristo. Njia ya kuhifadhi kicheko cha Mungu katika maisha yetu ni kukiri kwa haraka makosa yetu na kutembea kwenye nuru ambayo Mungu ameiweka kwenye njia yetu. [552]

(2) Kukubali kuonywa na Mungu.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaweka wazi kwamba kukubali ***kupokea*** kuliko ***kuyapuuzia*** maonyo ya Baba yetu wa mbinguni kutatuwezesha "tuushiriki utakatifu wake."[553] Hakuna mtu yeyote anayefurahia kukemewa na Mungu, hasa kwa sababu inatokea mara nyingi kwa watu wa kawaida ambao wana matatizo yao ya kushughulikiwa. Kila mmoja wetu ana tabia ya kupuuzia marekebisho machungu hasa inapotokea kwa mwanandoa aliyekosa au viongozi wa kiroho wanaowekwa na Mungu kwenye nafasi za mamlaka juu yetu wanapotenda yasiyofaa. Lakini nidhamu ni mojawapo ya chombo kikuu sana cha Mungu cha kubomoa kabisa maeneo yetu mabovu na kuturejesha tena ndani ya mfano wa Kristo.

Kama itatokea tumefikia mahali ambapo hatuwezi tena kupokea masahihisho, hata kutoka kwa watu ambao kiroho bado ni wachanga, tutakuwa tumeuacha msingi wa njia sahihi ya utakatifu.

(3) Jikabidhi wewe mwenyewe kila siku kama dhabihu kwa Mungu.

Paulo anatukumbusha kwamba tunapaswa kukabidhi miili yetu, pamoja na hamu na tamaa zake zote kwa Mungu kama, "dhabihu iliyo hai."[554] Miili yetu ambayo hapo mwanzo ilikuwa "silaha za dhuluma kwa dhambi"[555] inabadilishwa kwa neema ya Mungu kuwa "silaha za haki."

Paulo anaonyesha hii hatua endelevu ya kujitoa kwa Mungu kama ishara ya alama ya maisha ya Kikristo. Alisema, "Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na

---

[549] 2 Wakorintho 3:18
[550] 1 Wakorintho 6:11
[551] Mathayo 6:12
[552] 1 Yohana 1:7
[553] Waebrania 12:10
[554] Warumi 12:1
[555] Warumi 6:13

Kristo katika Mungu." Kisha akaendelea kwa kutoa maagizo, "Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi."[556] Fanya haya, na utakuwa na uzoefu wa kuzidi na zaidi wa vipimo vya neema ya Mungu.

(4) Yatafakari Maandiko kila siku.

Kutakaswa, na tabia inayomfanania Kristo siyo matokeo ya muda mfupi, bali ni matokeo ya kuwa na muda katika maisha ya kutafakari na utiifu kwa Neno la Mungu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba walifanywa wasafi kupitia Neno. "Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia."[557] Kisha Yesu akaomba kwamba waendelee kuwa watakatifu kupitia Neno. "Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli."[558] Mungu hukamilisha kazi yake ya kututakasa na kutufanya wasafi tunapolitafakari Neno lake mara kwa mara an kulitii.

(5) Kujivalisha mwenyewe kwa Yesu kila siku.

Maisha ya utakatifu yanapatikana kwa kujivalisha wenyewe kwa uangalifu tabia na fadhila za Kristo. "Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo...."[559] Neno "mvaeni" linamaanisha kufikiri kama Yesu, kuiga roho yake, na kuishi kama yeye. Waamini wanapaswa kila siku wachague kuwa kama Yesu katika upendo wake mtakatifu, furaha, amani, msamaha, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi.

(6) Msiuangalie mwili hata kuwasha tamaa zake.

Baada ya kuwa tumemvaa Yesu tunapaswa kuwa waangalifu sana, "msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake."[560] Je, inawezekana tamaa binafsi zikajitokeza nyuma ya mtu ambaye ana moyo uliojazwa Roho Mtakatifu? Kama ingekuwa haiwezekani, Paulo hangetoa angalizo hilo. Kwa muda wote ambao sisi tunaishi, ni lazima tuchague unyenyekevu. Kila mume au mke anayeongozwa na Roho, ameshajifunza kwamba utauwa unaimarishwa tu kwa kuupalilia kwa uangalifu, umakini wa mara kwa mara, na maombi ya ulinzi. Kama mwili hautaendelea kubakia umesulubishwa, utainuka na kusababisha anguko kubwa la kiroho, mfano wa baba mmoja wa Kiafrika aliyefuga mbwa, akashindwa kuwazuia wasimng'ate miguuni kwa sababu alikuwa anawatembelea mbwa wake akiwa ameweka nyama yao mfukoni!

(7) Isitawishe akili yako kila siku.

Akili yako ndio kituo kikuu cha maamrisho cha maisha yako na siri ya mabadiliko yake. "Maana aonavyo mtu nafsini mwake, ndivyo alivyo."[561] Akili yako ina mamlaka juu ya maisha yako kwamba utafanyika kuwa kile ambacho umechagua akili yako ikifanye. Paulo

[556] Wakolosai 3:3, 5
[557] Yohana 15:3
[558] Yohana 17:17
[559] Warumi 13:14
[560] Ibid.
[561] Mithali 23:7

alifundisha, "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."[562]

(8) Vaeni silaha zote za Mungu.

Mpango mkamilifu wa Mungu kwa kila mwamini ni kwamba "mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani."[563] Tunafanya haya kwa kuvaa silaha zote za Mungu – ukweli, haki, utayari, Imani, uhakika wa wokovu, na Neno la Mungu. Vaa silaha zako kwa sababu peke yetu tu, hatuna uwezo dhidi ya adui yetu!

(9) Endelea kuukuza ufahamu wako juu ya Roho Mtakatifu.

Kama unataka kuwa mtakatifu, unapaswa kumwalika Roho Mtakatifu kujaza na kusafisha kila chumba cha maisha yako: sebule yako (chumba ambacho maisha ya kijamii na burudani hufanyikia), chumba cha kulala (chumba chako cha kimaadili na ngono), jiko lako (Chumba chako cha hamu na matamanio), na ofisi yako (chumba chako cha maamuzi ya fedha na kazi mbalimbali). Mara nyingi tunapambana kuwa watakatifu kwa sababu tunashindwa kukuza wakati kwa wakati ufahamu wetu juu ya Roho Mtakatifu na kuuliza kwa dhati "ahadi ya Baba," ambayo Yesu anayo furaha ya kutoa. Inawezekana hofu ni sehemu ya  sababu ya kusita kwetu kuuliza. Hatuhitajiki kuwa na mashaka. Yesu alitoa ahadi hii ya ajabu sana: "Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"[564]

(10) Ishi kwa neema.

Yesu alisema, "Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote."[565] Tumefanywa watakatifu kwa sababu sisi ni mali ya mzabibu. Ni mzabibu ambao unazaa matunda. Tunazaa matunda zaidi na zaidi siyo kwa kujaribu kuwa wazuri bali ni kwa kumng'ang'ania Yesu.

Wakristo wengi wamekuwa wakiumizwa na wasiwasi mkubwa kuhusiana na kutembea kwao na Mungu. Wengine, ambao wamefundishwa kufanya utafiti wa kina wa nafsi, wamekuwa wakijichunguza mno kupita kiasi. Bila kujali viwango vyao vya kukua kiroho, wanakuwa na mashaka kwamba bado wanashindwa kufikia "viwango" anavyotaka Mungu.

Wakristo wengine wamefundishwa kutegemea kupata mihemko maalumu baada ya Mungu kuwa amewatakasa mioyo yao na kuwafanya watakatifu. Wanajiangalia wenyewe pamoja na mihemko yao kuliko kumwangalia Mungu. Hata hivyo, Biblia inafundisha kwamba

---

[562] Warumi 12:2
[563] Waefeso 6:11
[564] Luka 11:13
[565] Yohana 15:5

utakatifu ni tunda la kushikamana na Kristo. Tunapokuwa tunatembea katika Roho, kudumu katika maombi, kujilisha kwa Neno la Mungu, kushiriki katika kuabudu na ushirika wa Kikristo, kukiri madhaifu yetu, na kutembea nuruni, Mungu anatuumba kwenye sura ya Kristo. Tunaweza tusiyaone maendeleo ya haraka kama tulivyotegemea kwa wiki au mwezi, lakini kama tutaangalia nyuma tulikokuwa mwaka mmoja uliopita au mitano iliyopita, kwa vyovyote tutayaona mabadiliko!

Paulo alimtia moyo kila mwamini kujua kwamba Mungu anayeanza kazi ya kutufanya tuwe watakatifu ataikamilisha kazi hiyo: "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu."[566]

Utakatifu wa moyo na maisha ni safari. Kanuni hizi kumi za kibiblia zitahifadhi nafsi zetu kupita katika mawimbi ya upepo mkali ya taabu na majaribu na kutufanya sisi tukae kwenye mfungamano mmoja na nyumbani kwetu mbinguni.

## Je, Umeipata Siri?

Katika kila somo, tumesoma habari za mtu mmoja kutoka historia ya Kanisa aliyenakisi moyo mtakatifu. Wengine ni Wakristo waliokuwa mashuhuri. Wengine ni watu waliojulikana kidogo sana lakini kwa kimya kabisa wakiishi maisha matakatifu.

Sasa ni nafasi yako. Je, unayo njaa ya kuwa na moyo mtakatifu? Je, unayo matamanio ya kushika urafiki na Mungu? Je, unataka umfananie Baba wa Mbinguni? Unaweza kuwa mtakatifu.

Je, unayo njaa ya kuwa mkamilifu katika Roho? Je, unataka kumtumikia Mungu kwa moyo usiogawanyika? Unaweza "kuwa mkamilifu kama kama Baba yako wa mbinguni alivyo mtakatifu." Unaweza kumpenda Mungu na jirani yako kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu katika maisha yako.

Chaguo ni lako. Je, utajisalimisha kikamilifu kwa Mungu? Kama ndivyo, utapata utimilifu wa utajiri wake utakapokuwa umesogea karibu naye. Utapata furaha wakati Mungu atakapokufanya uwe wa sura yake. Utapata amani ya moyo ambayo ni mali ya Mungu kabisa. Utatembea kwa ushindi kila siku katika ukamilifu wa Roho Mtakatifu. Kwa neema ya Mungu, unaweza kuishi maisha ya utakatifu.

---

[566] Wafilipi 1:6

## Tafakuri ya Somo la 12

(1) Maisha ya utakatifu yanawezekana kwa kila mtoto wa kweli wa Mungu.

- Neno la Mungu linafundisha kwamba maisha ya utakatifu yanawezekana.
- Wakristo katika historia yote wamedhihirisha kwamba maisha ya utakatifu yanawezekana.
- Njaa inayotokana na Mungu ya kutaka utakatifu ni udhihirisho kwamba maisha ya utakatifu yanawezekana.

(2) Neno la Mungu linaonyesha njia ya maisha ya utakatifu.

- Wakati tu wa kuzaliwa kwetu mara ya pili, Mungu anaanza kutufanya watakatifu. Huu ndio mwanzo wa utakaso.
- Jinsi tunavyomfuata Kristo, tunakua katika utakaso.
- Mungu anataka atupe moyo mtakatifu. Mwito kwa ajili ya usafi wa moyo ni pamoja na:
    - Kuitwa kwa ajili ya utiifu uliokamilika.
    - Kuitwa kwa ajili ya moyo uliojisalimisha.
    - Kuitwa kwa ajili ya uaminifu ulio mkamilifu
- Baada ya mioyo yetu kuwa misafi, tunaendelea kukua katika kumfanania Kristo.

(3) Njia ambazo tunaweza kuendelea nazo katika kupalilia maisha yetu ya utakatifu ya kila siku:

- Endelea kubakia uliyepondeka kiroho.
- Kukubali kuonywa na Mungu.
- Jikabidhi wewe mwenyewe kila siku kama dhabihu kwa Mungu.
- Yatafakari Maandiko kila siku.
- Kujivalisha mwenyewe kwa Yesu kila siku.
- Msiuangalie mwili hata kuwasha tamaa zake.
- Istawishe akili yako kila siku
- Vaeni silaha zote za Mungu.
- Endelea kuukuza ufahamu wako juu ya Roho Mtakatifu.
- Ishi kwa neema.

## Kazi ya Kufanya

(1) Soma 1 Wathesalonike 5:23-24.

(2) Katika kila somo, tumeomba maombi ya utakatifu. Mwisho wa somo hili, andika maombi yako mwenyewe kwa ajili ya utakatifu. Andika maombi yako ukimwomba Mungu akuongoze kuendelea kukua katika sura yake. Jisalimishe mwenyewe kabisa kwenye mamlaka na mapenzi yake katika maisha yako. Omba kwa Imani kwamba Mungu aliyekuokoa atalitimiza kusudi la kukubadilisha wewe uwe katika sura yake.

# Mpangokazi wa Mwisho

Utahubiri mahubiri matatu au utafundisha masomo matatu yatokanayo na Biblia kuhusiana na Imani na uzoefu wa maisha ya utakatifu. Mahubiri haya utayaweka kwenye kumbukumbu na kukabidhi kwa kiongozi wa darasa kwa ajili ya andiko lako la mwisho. Utaanda somo moja la mahubiri au la kujifunza Biblia kutokana na vichwa vya somo hapa chini:

(1) Mahubiri au fundisho la kujifunza Biblia katika mojawapo ya vipengele vya kitheolojia kuhusu utakatifu. Chagua kimojawapo katika hivi:

- Utakatifu kama Mahusiano
- Utakatifu kama sura ya Mungu kwa watu wake.
- Utakatifu kama maisha ya kutengwa.
- Utakatifu kama Moyo Usiogawanyika
- Utakatifu kama Maisha ya haki
- Utakatifu kama Upendo kamili
- Utakatifu kama utimilifu wa Roho Mtakatifu
- Utakatifu kama kumfanania Kristo

(2) Mahubiri au fundisho la kujifunza Biblia katika kipengele cha vitendo cha utakatifu. Unaweza ukachagua mada yeyote iliyojadiliwa katika kozi hii, au unaweza kuchagua mada yako mwenyewe. Mada zinazowezekana ni pamoja na:

- Kuutumia muda pamoja na Mungu
- Utakatifu na Utu
- Inamaanisha nini kutengwa kutoka dunia?
- Utakatifu na Biashara
- Utakatifu na Maisha ya familia
- Kuimarisha ushindi dhidi ya dhambi za kujitakia
- Utakatifu na Maisha ya Kanisa

(3) Mahubiri au fundisho la kujifunza Biblia juu ya mtu mwenye tabia ya kibiblia anayedhihirisha utakatifu.

# Vyanzo Vilivyopendekezwa

Vitabu hivi ndivyo msingi wa masomo haya. Vinatumika kwa kiwango kikubwa sana katika masomo haya. Labda kwa ajili ya nukuzi maalumu, sijaonyesha vitabu hivi kwenye rejeo *(tanbihi)* chini ya ukurasa.


Brower, Kent E. and Andy Johnson, ed. *Holiness and Ecclesiology in the New Testament.* Grand Rapids: William Eerdmans, 2007.

Brown, A. Philip, II. *Loving God: The Primary Principle of the Christian Life.* Cincinnati: Revivalist Press, 2005.

Cattell, Everett L. *The Spirit of Holiness* (revised edition). Newberg: Barclay Press, 2015.

Greathouse, William M. *Wholeness in Christ.* Kansas City: Beacon Hill Press, 1998.

Kinlaw, Dennis. *The Mind of Christ*. Wilmore: Francis Asbury Press, 1998.

Kinlaw, Dennis. *This Day with the Master*. Grand Rapids: Zondervan, 2010.

Noble, T.A. *Holy Trinity: Holy People.* Eugene: Cascade Books, 2013.

Oswalt, John N. *Called to Be Holy: A Biblical Perspective*. Nappanee: Evangel Publishing House, 1999.

# Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa (Mazoezi)

Jina la Mwanafunzi ________________________________________

Weka sahihi yako kila wakati kazi iliyofaywa inapomalizika. Kazi zote zilizotolewa ni lazima zimalizike kwa usahihi wake ili kuweza kupata cheti cha kufuzu kutoka *Shepherds Global Classroom*.

| Somo la | Kuandika kazi iliyofaywa | Andiko la kukumbuka |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Andiko la Mwisho | | | |

**Ombi la Kupewa Cheti Kutoka Shepherds Global Classroom**

Maombi ya Cheti cha Kuhitimu kutoka Darasa la Shepherds Global yanaweza kumalizwa katika ukurasa wetu wa www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitapelekwa kwa njia ya digitali kutoka kwa rais wa SGC kwenda kwa walimu na wawezeshaji ambao wamemaliza maombi kwa niaba ya (m)wanafunzi wao.

# Maelezo ya Kozi za Shepherds Global Classroom

### Kuchambua Agano la Kale

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

### Kuchambua Agano Jipya

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

### Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inasoma maisha ya Yesu kama mfano kwa huduma na uongozi katika karne ya 21.

### Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na dhamira kama inavyoelezewa katika vitabu ya Warumi, kujadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa ya kutatanisha katika kanisa.

### Kanuni za Tasfiri ya Kibiblia

Kozi hii inafundisha kanuni na njia za kutafsiri Biblia vizuri ili kuongoza maisha yetu na mahusiano na Mungu.

### Imani za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea mafundisho ya Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, Mwanadamu, Kristo, Wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na Vitu vya Mwisho.

### Eskolojia

Kozi hii inafundisha vitabu vya kibiblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu zingine za maandiko ya kinabii na inasisitiza mafundisho muhimu kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa Mungu wa milele.

### Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

**Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa**

Kozi hii inaelezea ubunifu na mpango wa Mungu kwa kanisa na masomo ya kibiblia kama vile uanachama wa kanisa, ubatizo, ushirika, zaka, na uongozi wa kiroho.

**Historia ya Kanisa I**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyotimiza dhamira yake na kutunza mafundisho muhimu kuanzia kipindi cha kanisa la mwanzo mpaka Matengenezo.

**Historia ya Kanisa II**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyopanuka na lilivyopitia changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo mpaka nyakati za kisasa.

**Uundaji wa Kiroho**

Katika kozi hii wanafunzi wanajifunza kuwa na mitazamo ya yesu, kuwa na Mungu kama Yesu alivyokwa na baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kufanya nidhamu ya kiroho na binafsi ya yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) lililoundwa na Yesu.

**Huduma ya Uongozi**

Kozi hii inahimiza tabia ya Kikristo wakati inafundisha viongozi kuongoza mashirika kupitia mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushirikishana maono, kuweka malengo, kupanga mkakati, kuchukua hatua, na kupitia mafanikio.

**Kanuni za Mawasiliano**

Kozi hii inafundisha theolojia ya mawasiliano, njia za kuzungumza kwa ufanisi, na njia za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

**Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi**

Kozi hii inatoa kanuni za kibiblia ambazo huongoza mbinu za uinjilisti. Inaelezea aina za uinjilisti na kutoa masomo ya kutumia kufundisha wapya waliobadilishwa.

**Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani**

Kozi hii inafundisha misingi ya kisayansi, kihistoria, na kifalsafa kwa mtazamo wa ulimwengu wa Kikristo, na inaonyesha jinsi gani imani ya Kikristo ni thabiti katika hoja na hali halisi.

**Dini za Ulimwengu na Ibada**

Kozi hii huumpa muumini wa kiinjili uelewa wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya dini.

**Utangulizi wa Kuabudu Kikristo**

Kozi hii inaelezea jinsi gani kuabudu huathiri nyanja zote za maisha ya muumini na hutoa kanuni ambazo humuongoza mtu binafsi na mkutano wote mazoezi ya kuabudu.

**Kuishi Kikristo kwa Vitendo**

Kozi hii hutumia kanuni za kiroho kwa utumiaji wa fedha, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na maeneo mengine ya kuishi kwa vitendo.

**Ndoa ya Kikristo na Familia**

Kozi hii inatoa mtazamo wa Kikristo kuhusiana na maendeleo ya binadamu kupitia hatua mbalimbali za maisha na zinatumia kanuni za kimaandiko kwa ajili ya majukumu ya kifamilia na mahusiano.